# Kiswahili

## kwa

## Shule za Rwanda

### Kidato cha 3

### Mwongozo wa Mwalimu

© 2020 Bodi ya Elimu Rwanda
Haki zote zimehifadhiwa.
Kitabu hiki ni mali ya Bodi ya Elimu Rwanda.
Shukrani lazima zitolewe kwa Bodi ya Elimu Rwanda wakati yaliyomo yamenukuliwa.

Chapa ya kwanza 2020.

# DIBAJI

Mwalimu mpendwa,

Bodi ya Elimu Rwanda inayo heshima kwa kutoa mwongozo wa mwalimu kwa kidato cha tatu katika ngazi ya chini ya elimu ya sekondari.

Mwongozo huu ni waraka rasmi utakaoongoza ufundishaji na ujifunzaji kuendana na mtaala uegemeao katika uwezo.

Falsafa ya Elimu Rwanda inalenga kumpatia mlengwa uwezo kwa kila ngazi ya elimu ili kumwezesha kumudu vizuri katika jamii na kumpa fursa ya kujipatia ajira.

Ili kwenda sambamba na juhudi za kuboresha elimu, Serikali ya Rwanda inasisitiza umuhimu wa kufungamanisha ujifunzaji na ufundishaji na zana pamoja na mitaala ili kuwezesha mchakato wa ujifunzaji. Mambo mengi huathiri yale ambayo wanafunzi wanafundishwa, namna nzuri ya kujifunza na uwezo waupatao. Mambo hayo ni pamoja na umuhimu mahususi wa yaliyomo, ubora wa walimu, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, mikakati ya upimaji na vifaa vya kufundishia vilivyopo.

Tumezingatia umuhimu wa mbinu zenye mchakato wa kujifunza ambao unamwezesha mwanafunzi kuendeleza mawazo yake na kufanya ugunduzi mpya wakati wa mazoezi thabiti yawe ya binafsi au katika makundi. Wanafunzi, kwa msaada wa wakufunzi, watapata stadi za lugha zinazofaa zitakazowawezesha kutumia yale waliyojifunza katika miktadha ya maisha halisi. Kwa kufanya hivyo, wataonyesha tofauti siyo tu katika maisha yao binafsi bali pia hata kwa taifa .

Hii inatofautiana na mfumo wa zamani kuhusu nadharia ya ujifunzaji iliyosisitiza mchakato wa kujifunza kama upataji wa maarifa kutoka kwa yule aliyemzidi maarifa na hasa akiwa ni mwalimu.

Katika mtaala uegemeao katika uwezo, ujifunzaji unachukuliwa kama mchakato wa kazi ya kujenga na kuendeleza maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema kutoka kwa mwanafunzi ambapo dhana aghalabu huanzishwa kwa mazoezi, hali na mazingira yanayomsaidia mwanafunzi kujenga maarifa, kuendeleza stadi na upatikanaji chanya wa maadili na mwenendo mwema.

Aidha, kazi ya kujifunza hujishughulisha na wanafunzi kwa kufanya mambo na kufikiri kuhusu yale wanayoyafanya na wanafarijika kuonyesha uzoefu wao halisi na maarifa katika mchakato wa ujifunzaji.

Katika mtazamo huu, ili kutumia kitabu hiki kwa ufanisi, jukumu lako kama mkufunzi litakuwa :

- Kuandaa masomo yako na vifaa vya ufundishaji vinavyofaa,
- Kuandaa majadiliano katika makundi ya ushirikiano ya wanafunzi ukizingatia umuhimu wa ushauri kuwa kujifunza hufanyika kwa ufanisi wakati mwanafunzi afanyapo kazi kwa kushirikiana na watu wanaomzidi maarifa na uzoefu;
- Kushirikisha wanafunzi kwa kupitia kazi za ujifunzaji kama: njia ya uchunguzi, makundi ya mijadala, utafiti, mazoezi ya utafiti na kazi za kibinafsi;
- Kutoa fursa ya usimamizi kwa wanafunzi kwa kuendeleza uwezo wao, kwa kuwapa ushindani tofauti na kutoa majukumu yanayoongeza tafakuri tunduizi, utatuzi wa matatazo, ubunifu na uvumbuzi, mawasiliano na ushirikiano;
- Kutoa msaada na kuwezesha mchakato wa ujifunzaji kwa kutathmini mchango wa wanafunzi katika mazoezi ya darasani;
- Kuwaongoza wanafunzi ili waweze kuoanisha matokeo ya utafiti;
- Kutilia maanani tathmini ya kazi binafsi na kazi za makundi zilizofanyika darasani kwa kutumia mchakato na mbinu za tathmini zinazoegemea katika uwezo wa wanafunzi,
- Kuutumia mwongozo kutakusaidia katika kazi yako ya kufundisha kwani yaliyomo katika mwongozo huu wa mwalimu yanaeleweka kiasi kwamba unaweza kutumiwa kwa urahisi.

Ingawa mwongozo huu wa mwalimu una majibu kwa kila kazi zote zilizotolewa katika kitabu cha mwanafunzi, unaombwa kupitia kila swali na kazi kabla ya kutathmini.

Napenda, kwa moyo wote, kutoa shukrani zangu kwa watu wote walioshiriki kutoa mchango wao wa kuboresha mwongozo huu wa mwalimu, na hasa wafanyakazi wa Bodi ya Elimu Rwanda ( REB/CTLR) walioandaa mchakato wa kazi hii tokea ilipoanzishwa.

Pongezi maalum ziwaendee walimu wa ngazi tofauti kwa msaada wao wa kuendeleza na kukamilisha zoezi hili.

Maoni au mchango wowote wa mawazo unakaribishwa kwa ajili ya uboreshaji wa kitabu hiki kwa matoleo mengine yatakayofuata baadaye.

**Dkt. Irénée NDAYAMBAJE**
**Mkurugenzi Mkuu, Bodi ya Elimu Rwanda**

# SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa hali na mali katika kukiandaa na kukifanikisha kitabu hiki cha mwongozo wa mkufunzi. Kitabu hiki kisingeliwezekana bila kuwepo wadau mbalimbali walioshiriki; jambo ambalo limenifanya nitoe shukrani zangu za dhati.

Shukrani zangu za kwanza ni kwa wafanyakazi wa Bodi ya Elimu Rwanda walioshiriki katika kuandaa na kuandika kitabu hiki. Pia napenda kutoa shukrani kwa walimu wa ngazi zote kwa juhudi zao katika ufanikishaji wa kazi hii ya thamani.

Aidha, natoa shukrani kwa uongozi wa shule mbalimbali nchini Rwanda kwa kuwaruhusu walimu kushiriki katika kukiandaa na hata kukikamilisha kitabu hiki.

**Joan MURUNGI**

**Mkuu wa Idara ya Mitaala, Ufundishaji, Ujifunzaji na Zana ( CTLR)**

# Yaliyomo


Ramani ya yaliyomo ........................................................................................ xiv

Utangulizi ........................................................................................................ xix

Ratiba ya mafunzo ........................................................................................... xxv

Andalio la somo ............................................................................................... xxvi

**SURA YA KWANZA ........................................................... 1**

**Mada Kuu 1:** Lugha na mazingira ………….………................... 1

**Mada Ndogo:** Utalii nchini Rwanda .............................................. 1

**Somo la 1: Ofisi ya utalii ......................................... 6**

**Kipindi cha 1: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati ................ 6**

1.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Mazungumzo kati ya Mpokeaji na Mtalii .................................................................. 7

1.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu utalii ........................................................... 8

**Kipindi cha 2: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza .......... 9**

1.3 ***Matumizi ya lugha:*** Aina mbalimbali za pesa ................ ...................... 10

1.4 ***Kusikiliza na kuzungumza:*** Maigizo ...................................................... 10

**Kipindi cha 3: Sarufi .............................................................. 11**

1.5 Viulizi ‘*nani*’ na ‘*nini*’ ........................................................................................ 12

1.6 Mazoezi ya ziada ......................................................................................... 13

1.7 Majibu ............................................................................................................ 14

**Somo la 2: Mbuga za wanyama.................................... 18**

**Kipindi cha 4: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati ............. 18**

2.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Kifungu kuhusu mbuga za wanyama nchini Rwanda ..................................................... 19

2.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu mbuga za wanyama ............................ 20

**Kipindi cha 5: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza ........ 21**
2.3 ***Matumizi ya lugha:*** Majadiliano na kuandika ufupisho .......................... 22
2.4 ***Kusikiliza na kuzungumza:*** Majadiliano ................................................ 23
**Kipindi cha 6: Sarufi ....................................................................... 23**
2.5 Kiulizi '*lini*' .................................................................................... 24
2.6 Mazoezi ya ziada .............................................................................. 26
2.7 Majibu ............................................................................................. 27

**Somo la 3: Mwelekezaji na Mtalii................................ 31**
**Kipindi cha 7: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati ................ 31**
3.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Mazungumzo kati ya Mwelekezaji na Mtalii ................................................................. 32
3.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu ziara ya kitalii .......................................... 33
**Kipindi cha 8: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza ........ 34**
3.3 ***Matumizi ya lugha:*** Majadiliano ............................................................... 35
3.4 ***Kusikiliza na kuzungumza:*** Maigizo ...................................................... 35
**Kipindi cha 9: Sarufi ........................................................................ 36**
3.5 Viulizi '*wapi*' na '*vipi*' ........................................................................ 37
3.5.1 Kiulizi '*kwa nini*' ............................................................................ 37
3.6 Mazoezi ya ziada .............................................................................. 39
3.7 Majibu ............................................................................................. 39

**Somo la 4: Utamaduni na utalii.................................... 43**
**Kipindi cha 10: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati ............... 43**
4.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Kifungu kuhusu utamaduni na utalii ................. 44
4.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu utamaduni ............................................... 45
**Kipindi cha 11: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza ...... 46**
4.3 ***Matumizi ya lugha:*** Zoezi la msamiati ..................................................... 47
4.4 ***Kusikiliza na kuzungumza:*** Majadiliano ................................................ 48

**Kipindi cha 12: Sarufi ........................................................ 49**
4.5 Wakati wa mazoea, tungo yakinishi ........................................................ 49
4.6 Mazoezi ya ziada ........................................................ 51
4.7 Majibu ........................................................ 52

**Somo la 5: Milima yetu ........................................................ 56**
**Kipindi cha 13: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati .............. 56**
5.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Kifungu kuhusu 'Milima yetu' .......................... 57
5.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu 'Milima yetu' ........................................ 58
**Kipindi cha 14: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza ....... 59**
5.3 ***Matumizi ya lugha:*** Zoezi la jedwali ........................................................ 60
5.4 ***Kusikiliza na kuzungumza:*** Majadiliano ............................................. 61
**Kipindi cha 15: Sarufi ........................................................ 61**
5.5 Wakati wa mazoea, tungo kanushi ........................................................ 62
5.6 Mazoezi ya ziada ........................................................ 64
5.7 Majibu ........................................................ 64

**Somo la 6: Maji yetu ........................................................ 69**
**Kipindi cha 16: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati ................ 69**
6.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Kifungu kuhusu 'maji yetu' ............................. 70
6.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu 'maji yetu' ............................................ 71
**Kipindi cha 17: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza ....... 72**
6.3 ***Matumizi ya lugha:*** Majadiliano ........................................................ 73
6.4 ***Kusikiliza na kuzungumza:*** Majadiliano ............................................. 73
**Kipindi cha 18 Sarufi ........................................................ 75**
6.5 Matumizi ya kiulizi '*-pi*' ........................................................ 76
6.6 Mazoezi ya ziada ........................................................ 78
6.7 Majibu ........................................................ 79

**SURA YA PILI ......................................................... 84**

**Mada Kuu 2:** Lugha na matukio ya kijamii na kitaifa ............. 84

**Mada Ndogo:** Sikukuu na sherehe nchini Rwanda .................... 84

**Somo la 7: Sikukuu na sherehe katika kalenda ............... 88**

**Kipindi cha 1: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati ................. 88**

7.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Kifungu kuhusu sikukuu na sherehe nchini Rwanda ............................................. 89

7.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu sikukuu nchini Rwanda ........................ 90

**Kipindi cha 2: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza ........ 91**

7.3 ***Matumizi ya lugha:*** Majadiliano ............................................................ 92

7.4 ***Kusikiliza na kuzungumza:*** Maigizo ................................................... 92

**Kipindi cha 3: Sarufi ........................................................................ 93**

7.5 Matumizi ya wakati uliopita .................................................................... 94

**Kipindi cha 4: Sarufi ......................................................................... 95**

7.6 Matumizi ya wakati ujao ......................................................................... 95

7.7 Mazoezi ya ziada ....................................................................................... 98

7.8 Majibu ........................................................................................................ 99

**Somo la 8: Maadhimisho mbalimbali nchini Rwanda .... 104**

**Kipindi cha 5: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati ................. 104**

8.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Shairi kuhusu maadhimisho mbalimbali nchini Rwanda ........................................... 105

8.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu maadhimisho mbalimbali ..................... 106

**Kipindi cha 6: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza ........ 107**

8.3 ***Matumizi ya lugha:*** Majadiliano ........................................................... 107

8.4 ***Kusikiliza na kuzungumza:*** Zoezi la mazungumzo ............................ 108

**Kipindi cha 7: Sarufi ....................................................................... 109**

8.5 Vitenzi vya silabi moja ............................................................................. 109

**Kipindi cha 8: Sarufi ........................................................................110**

8.6 Vitenzi vya silabi moja, tungo yakinishi na kanushi ............................ 111

8.7 Mazoezi ya ziada ........................................................................................ 113
8.8 Majibu ........................................................................................................... 114

**Somo la 9: Matumizi ya kalenda ya mwaka .................. 118**
**Kipindi cha 9: Kusoma ufahamu .................................................. 118**
9.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Mazungumzo kuhusu kalenda ya mwaka .....119
**Kipindi cha 10: Kujifunza msamiati .............................................. 120**
9.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu kalenda ya mwaka ................................ 121
**Kipindi cha 11: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza ....... 122**
9.3 ***Matumizi ya lugha:*** Majadiliano ........................................................... 122
9.4 ***Kusikiliza na kuzungumza:*** Maigizo ................................................... 123
**Kipindi cha 12: Sarufi .................................................................. 124**
9.5 Matumizi ya herufi kubwa na alama za uandishi ................................. 124
9.6 Mazoezi ya ziada ........................................................................................ 125
9.7 Majibu ........................................................................................................... 126

**SURA YA TATU ........................................................ 133**
**Mada Kuu 3:** Ukuzaji wa matumizi ya lugha kimazungumzo ...................................................... 133
**Mada Ndogo:** Midahalo na mijadala kuhusu shughuli za maendeleo na uzalishajimali dhidi ya umaskini nchini ..................................................... 133
**Somo la 10: Mdahalo .................................................. 137**
**Kipindi cha 1: Kusoma ufahamu ...................................................137**
10.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Mdahalo kuhusu '*Elimu ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi kuliko biashara*' ...... 139
**Kipindi cha 2: Kujifunza msamiati ................................................ 140**
10.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu mdahalo .............................................. 141

**Kipindi cha 3: Matumizi ya lugha................................................. 141**

10.3 ***Matumizi ya lugha:*** Majadiliano ............................................................ 142

**Kipindi cha 4: Kusikiliza na kuzungumza ..................................... 143**

10.4 ***Kusikiliza na kuzungumza:*** Kuandaa mdahalo .................................. 144

**Kipindi cha 5: Sarufi ...................................................................... 146**

10.5 Wakati uliotimilika, tungo yakinishi ......................................................... 146

10.5.1 Wakati uliotimilika, tungo kanushi ............. .............................. 147

10.6 Mazoezi ya ziada .......................................................................................... 149

10.7 Majibu ........................................................................................................... 150

**Somo la 11: Mjadala ....................................................... 155**

**Kipindi cha 6: Kusoma ufahamu .................................................. 155**

11.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Mjadala kuhusu '*Nafasi ya ukulima katika uzalishajimali dhidi ya umaskini*' ..... 156

**Kipindi cha 7: Kujifunza msamiati ................................................ 157**

11.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu ukulima ................................................ 158

**Kipindi cha 8: Matumizi ya lugha................................................. 159**

11.3 ***Matumizi ya lugha:*** Zoezi la jedwali .................................................. 160

**Kipindi cha 9: Kusikiliza na kuzungumza ..................................... 161**

11.4 ***Kusikiliza na kuzungumza:*** Kuandaa mjadala ................................. 162

**Kipindi cha 10: Sarufi .................................................................... 163**

11.5 Kauli asili na kauli taarifa ......................................................................... 164

11.6 Mazoezi ya ziada ......................................................................................... 165

11.7 Majibu ........................................................................................................... 166

**Somo la 12: Mjadala .................................................... 170**

**Kipindi cha 11: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati ...............170**

12.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Mjadala kuhusu '*Ufugaji kama njia ya kupigana na umaskini nchini*'..........................171

12.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu ufugaji .................................................. 171

**Kipindi cha 12: Matumizi ya lugha ..............................................172**

12.3 ***Matumizi ya lugha:*** Kuunda maneno kamili ...................................... 173

**Kipindi cha 13: Kusikiliza na kuzungumza .................................... 174**

12.4 ***Kusikiliza na kuzungumza:*** Kuandaa mjadala ................................. 175

**Kipindi cha 14: Sarufi ................................................................ 176**

12.5 Mabadiliko ya kauli asili na kauli taarifa .................................................. 177

12.6 Mazoezi ya ziada ............................................................................ 179

12.7 Majibu .......................................................................................... 180

**SURA YA NNE ........................................................................ 187**

**Mada Kuu 4:** Uimarishaji wa stadi ya uandishi na masimulizi kupitia lugha ya Kiswahili ............... 187

**Mada Ndogo:** Utungaji wa insha ................................................ 187

**Somo la 13: Sehemu kuu za insha .................................. 191**

**Kipindi cha 1: Kusoma ufahamu .................................................... 191**

13.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Kifungu kuhusu somo la Kiswahili ................ 192

**Kipindi cha 2: Kujifunza msamiati ................................................ 193**

13.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu sehemu za insha ................................ 194

**Kipindi cha 3: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza ....... 195**

13.3 ***Matumizi ya lugha:*** Majadiliano ......................................................... 196

13.4 ***Kusikiliza na kuzungumza:*** Somo la imla ........................................... 196

**Kipindi cha 4: Sarufi ................................................................ 197**

13.5 ***Sarufi:*** Ngeli ya U-ZI ...................................................................... 198

13.5.1 Ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vya sifa ........................... 199

13.6 Mazoezi ya ziada ............................................................................ 201

13.7 Majibu .......................................................................................... 201

**Somo la 14: Mambo ya kuzingatia katika kuandika insha ............................................ 206**
**Kipindi cha 5: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati ................ 206**
14.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Kifungu kuhusu malezi bora .......................... 207
14.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu uandishi wa insha ............................... 208
**Kipindi cha 6: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza ....... 208**
14.3 ***Matumizi ya lugha:*** Majadiliano .......................................................... 209
14.4 ***Kusikiliza na kuzungumza:*** Majadiliano ............................................ 210
**Kipindi cha 7: Sarufi ........................................................................ 210**
14.5 ***Sarufi:*** Ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi viashiria ............................ 211
14.6 Mazoezi ya ziada ........................................................................................ 212
14.7 Majibu ........................................................................................................ 213

**Somo la 15: Aina mbalimbali za insha ............................ 217**
**Kipindi cha 8: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati ................ 217**
15.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Kifungu kuhusu umuhimu wa adabu ............ 218
15.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusiana na umuhimu wa adabu .................. 218
**Kipindi cha 9: Matumizi ya lugha ................................................. 219**
15.3 ***Matumizi ya lugha:*** Mifano ya insha ................................................... 220
**Kipindi cha 10: Kusikiliza na kuzungumza .................................. 221**
15.4 ***Kusikiliza na kuzungumza:*** Somo la imla ........................................... 222
**Kipindi cha 11: Sarufi ...................................................................... 222**
15.5 ***Sarufi:*** Ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vimilikishi ........................ 223
15.6 Mazoezi ya ziada ...................................................................................... 225
15.7 Majibu ........................................................................................................ 226

**Somo la 16: Aina za insha ............................................ 230**
**Kipindi cha 12: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati ................ 230**
16.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Kifungu kuhusu madhara ya uvivu ................ 231

16.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu madhara ya uvivu ................................ 232
**Kipindi cha 13: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza ....... 233**
16.3 ***Matumizi ya lugha:*** Mifano ya insha .................................................. 234
16.4 ***Kusikiliza na kuzungumza:*** Somo la imla .......................................... 234
**Kipindi cha 14: Sarufi ..................................................................235**
16.5 ***Sarufi:*** Ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vya idadi ........................... 236
16.6 Mazoezi ya ziada ......................................................................................... 237
16.7 Majibu .......................................................................................................... 238

**SURA YA TANO ............................................................ 244**
**Mada Kuu 5:** Lugha na teknolojia ............................................ 244
**Mada Ndogo:** Kiswahili katika teknolojia ya habari na mawasiliano ........................................................ 244
**Somo la 17: Simu ya mkononi ...................................... 249**
**Kipindi cha 1: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati ................. 249**
17.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Kifungu kuhusu matumizi ya simu ya mkononi ........................................................ 251
17.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu simu ya mkononi ................................ 251
**Kipindi cha 2: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza ....... 252**
17.3 ***Matumizi ya lugha:*** Majadiliano .......................................................... 253
17.4 ***Kusikiliza na kuzungumza:*** Majadiliano ............................................ 254
**Kipindi cha 3: Sarufi ................................................................... 254**
17.5 Hali ya kuomba, tungo yakinishi ............................................................... 256
17.6 Mazoezi ya ziada ......................................................................................... 257
17.7 Majibu ...........................................................................................................258

**Somo la 18: Matumizi ya tarakilishi .............................. 261**
**Kipindi cha 4: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati ................. 261**
18.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Kifungu kuhusu matumizi ya tarakilishi .........262

18.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu matumizi ya tarakilishi ........................ 262

**Kipindi cha 5: Matumizi ya lugha .................................................. 263**

18.3 ***Matumizi ya lugha:*** Majadiliano ........................................................ 264

**Kipindi cha 6: Kusikiliza na kuzungumza ..................................... 265**

18.4 ***Kusikiliza na kuzungumza:*** Majadiliano ............................................ 266

**Kipindi cha 7: Sarufi ...................................................................... 266**

18.5 Hali ya kuomba, tungo kanushi ................................................................ 267

18.6 Mazoezi ya ziada ........................................................................................ 268

18.7 Majibu .......................................................................................................... 269

## Somo la 19: Redio na runinga ......................................... 274

**Kipindi cha 8: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati ..................274**

19.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Kifungu kuhusu matumizi ya redio na runinga ...............................................................275

19.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu matumizi ya redio na runinga .............. 275

**Kipindi cha 9: Matumizi ya lugha .................................................. 276**

19.3 ***Matumizi ya lugha:*** Majadiliano .......................................................... 277

**Kipindi cha 10: Kusikiliza na kuzungumza .................................... 278**

19.4 ***Kusikiliza na kuzungumza:*** Maigizo .................................................. 279

**Kipindi cha 11: Sarufi .................................................................... 280**

19.5 ***Sarufi:*** Hali ya kuamrisha, tungo yakinishi............................................. 281

19.6 Mazoezi ya ziada ........................................................................................ 282

19.7 Majibu .......................................................................................................... 283

## Somo la 20: Barua kwa mhariri ..................................... 287

**Kipindi cha 12: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati ............... 287**

20.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Kifungu kuhusu barua kwa mhariri ..................288

20.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu barua kwa mhariri ................................. 288

**Kipindi cha 13: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza ....... 289**
20.3 ***Matumizi ya lugha:*** Majadiliano ........................................................... 290
20.4 ***Kusikiliza na kuzungumza:*** Majadiliano ............................................. 291
**Kipindi cha 14: Sarufi ..................................................................... 292**
20.5 Hali ya kuamrisha, tungo kanushi ............................................................... 293
20.6 Mazoezi ya ziada ........................................................................... 294
20.7 Majibu ........................................................................................................ 295
Marejeleo ........................................................................................................ 300

# Ramani ya yaliyomo

| | **MADA 1: LUGHA NA MAZINGIRA** | **MADA 2: LUGHA NA MATUKIO YA KIJAMII NA KITAIFA** | **MADA 3: UKUZAJI WA MATUMIZI YA LUGHA KIMAZUNGUMZO** | **MADA 4: UIMARISHAJI WA STADI YA UANDISHI NA MASIMULIZI KUPITIA LUGHA YA KISWAHILI** | **MADA 5: LUGHA NA TEKNOLOJIA** |
|---|---|---|---|---|---|
| **IDADI YA VIPINDI** | **18** | **12** | **14** | **14** | **14** |
| **UWEZO WA MSINGI UPATIKANAO KATIKA MADA** | Mwanafunzi aweze kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika kuhusu muktadha wa utalii na kuzingatia matumizi ya sarufi inayohusika. | Mwanafunzi aweze kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika kwa kutumia lugha katika muktadha wa sikukuu na sherehe katika jamii anamoishi. | Mwanafunzi aweze kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika kwa kutumia lugha katika muktadha wa midahalo na mijadala darasani. | Mwanafunzi aweze kusikiliza, kusema, kusoma na kuandika mada juu ya shughuli za ujenzi wa taifa kupitia kwa utungaji wa insha. | Mwanafunzi aweze kutumia lugha ya Kiswahili katika muktadha wa teknolojia ya habari na mawasiliano. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | - Kutaja aina za pesa zitumiwazo mara nyingi katika mazingira ya utalii au biashara. | - Kueleza kwa ufasaha katika maandishi na mazungumzo juu ya sikukuu aliyohudhuria hapo zamani.<br>- Kukumbuka matumizi sahihi ya wakati uliopita kuhusu vitenzi vyenye silabi moja katika hali yakinishi na hali kanushi.<br>- Kuonyesha uelewa wa matumizi ya herufi kubwa pamoja na matumizi ya alama za vituo | - Kukumbuka na kuainisha mabadiliko yanayojitokeza kwenye vitenzi vinapotumiwa katika wakati timilifu hali yakinishi na hali kanushi.<br>- Kueleza mabadiliko yanayojitokeza wakati wa kunukuu maneno yaliyotamkwa na mtu mwingine. | - Kubaini matumizi ya utokeaji wa ngeli ya majina ya ngeli ya U-ZI katika tungo na jinsi yanavyobadilika kufuatana na vivumishi husika. | - Kuonyesha ustadi juu ya namna mbalimbali ya kuwasiliana na watu mbalimbali kwa kutumia njia moja au nyingine za teknolojia ya habari na mawasiliano ya kisasa.<br>- Kubainisha matumizi sahihi ya hali ya kuamrisha katika mawasiliano kwa kutumia neno “tafadhali”. |
| **IDADI YA MASOMO** | 6 | 3 | 3 | 4 | 4 |
| **VIFAA VYA KUJIFUNZIA** | - Picha zinazoonyesha vivutio mbalimbali kama vile: milima, mabonde, mito na maziwa<br>- Vitabu | - Kalenda inayobainisha sikukuu zote nchini Rwanda<br>- Picha za watu wakisherekea sikukuu mbalimbali | - Michoro na picha zinazoonesha watu wakishiriki kwenye mjadala au mdahalo<br>- Vitabu<br>- Midahalo iliyorekodiwa | - Vitabu<br>- Chati yenye mchoro wa umbo la insha.<br>- Wanafunzi wenyewe<br>- Insha zilizorekodiwa | - Ramani ya nchi ya Rwanda inayoonyesha maeneo, vituo na majengo ya teknolojia ya mawasiliano |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | - Vifaa au zana kwa wanafunzi wasiojiweza au wazito kuelewa | - Vitabu<br>- Vifaa au zana kwa wanafunzi wasiojiweza au wazito kuelewa | - Vifaa au zana kwa wanafunzi wasiojiweza au wazito kuelewa | | - Picha za runinga, kompyuta, simu ya mkononi na mezani<br>- Vitabu<br>- Vifaa au zana kwa wanafunzi wasiojiweza au wazito kuelewa |
| **MBINU ZA KUJIFUNZIA NA KAZI** | - Kubuni mazungumzo kati ya mtalii wa kigeni na mtalii wa ndani wakizuru maeneo ya kitalii nchini Rwanda.<br>- Kujadiliana faida za utalii nchini Rwanda.<br>- Wanafunzi kuigiza wakiwa wamepewa majukumu kama vile: watalii, mwongozaji wa watalii, dereva wa utalii na askari wa uhifadhi. | - Kujibu maswali ya usomaji wa kalenda ya mwaka kwa kuegemea katika matukio au sikukuu muhimu za kijamii na kitaifa kama zijulikanavyo katika jamii.<br>- Kusoma au kutamka tarehe, siku na majina ya miezi kwa kuzingatia matamshi fasaha ya Kiswahili. | - Kuchagua mojawapo ya kazi za maendeleo na uzalishaji mali na kuzijadili katika makundi wakionyesha jinsi kazi hizo zinavyoweza kuwasaidia raia kupigana dhidi ya umaskini nchini.<br>- Kuchagua mdahalo au mjadala mmoja uliorekodiwa kuhusu kazi na ajira na kujaribu kuuigiza katika makundi.<br>- Kubadilisha kauli asili iwe kauli taarifa. | - Kushiriki katika kubaini muundo wa aya na kufanya mazoezi ya kuandika aya.<br>- Kubaini sehemu zinazounda insha kwa kuzitaja huku wakionyesha mipaka ya sehemu hizo kwa usahihi.<br>- Kueleza sifa za msingi za kila sehemu ya insha ili kuitofautisha na sehemu nyingine. | - Kujadili katika makundi athari za teknolojia ya mawasiliano katika maisha ya jamii ya kila siku.<br>- Kujaza sentensi fupi kwa kutumia msamiati maalumu unaohusu teknolojia ya mawasiliano.<br>- Kufanya mazoezi ya mawasiliano kwa kutumia aina mbalimbali za nyenzo za teknolojia ya mawasiliano (ujumbe mfupi wa simu, baruapepe, fesibuku n.k). |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | - Kutetea ukuzaji na uhifadhi wa vivutio vya utalii kama mojawapo ya njia ya kujikomboa dhidi ya umaskini.<br>- Kubadilisha pesa za Rwanda kama vile: faranga hamsini na kuzifanya pesa za kigeni kama vile: Yuro, Dola za Marekani, Shilingi za Uganda au Kenya n.k. | - Katika makundi, wanafunzi wazungumzie au kujadili shughuli zinazofanyika kwenye sikukuu fulani nyumbani kwao. | - Kuzungumza na wazazi au watu wengine nyumbani kuhusu sababu za umaskini unaojitokeza katika familia mbalimbali pamoja na hatua zinazoweza kuchukuliwa kama suluhisho kwa umaskini huo. | - Kufanya mazoezi ya kutunga insha kutokana na mada mbalimbali zinazojitokeza maishani (shuleni, nyumbani, afya, urafiki, uchumi, n.k.) na kuzisimulia hadharani.<br>– Kusoma insha tofauti kutoka vitabuni au na kuzitolea muhtasari kwa njia ya masimulizi darasani.<br>- Kubainisha matumizi sahihi ya majina katika ngeli ya U-ZI. | - Kutunga sentensi ambazo zitabeba au zitaonyesha hali ya kumtafadhalisha mtu afanye au asifanye kitu fulani, zinazoonyesha wakati timilifu.<br>- Kutafsiri istilahi za kiteknolojia kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. |
| **UWEZO WA JUMLA** | - Stadi za utafiti<br>- Ubunifu na ugunduzi<br>- Ujifunzaji wa muda mrefu<br>- Ushirikiano na stadi za maisha<br>- Mawasiliano katika lugha rasmi<br>- Tafakuri tanduizi | -Tafakuri tanduizi<br>- Mawasiliano katika lugha rasmi<br>- Stadi za utafiti<br>- Ubunifu na ugunduzi<br>- Ushirikiano, utawala na stadi za maisha<br>- Ujifunzaji wa muda mrefu | - Usuluhishaji wa matatizo<br>- Tafakuri tanduizi<br>- Mawasiliano katika lugha rasmi<br>- Ujifunzaji wa muda mrefu<br>- Utawala binafsi na stadi za maisha<br>- Ubunifu na ugunduzi | - Tafakuri tanduizi<br>- Ubunifu na ugunduzi<br>- Ujifunzaji wa muda mrefu<br>- Ushirikiano, utawala na stadi za maisha<br>- Mawasiliano katika lugha rasmi<br>- Stadi za utafiti | - Tafakuri tanduizi<br>- Mawasiliano katika lugha rasmi<br>- Stadi za utafiti<br>- Ubunifu na ugunduzi<br>- Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha<br>- Ujifunzaji wa muda mrefu<br>- Usuluhishaji wa matatizo |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **MASUALA MTAMBUKA** | - Umoja na uwiano wa kijamii<br>- Usawa na heshima kijinsia<br>- Elimu ya pamoja<br>- Mazingira na mabadiliko ya hali ya hewa | - Amani na maadili mema<br>- Elimu ya pamoja<br>- Usawa wa kijinsia<br>- Mazingira pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa na mwendelezo wake | - Amani na maadili mema<br>- Usawa wa kijinsia<br>- Elimu kuhusu fedha<br>- Mazingira pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa na mwendelezo wake<br>- Elimu ya pamoja | - Amani na maadili mema<br>- Mazingira pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa na mwendelezo wake<br>- Elimu kuhusu fedha<br>- Usawa wa kijinsia<br>- Elimu ya pamoja | - Amani na maadili mema<br>- Elimu ya pamoja<br>- Usawa wa kijinsia<br>- Elimu kuhusu fedha<br>- Mazingira pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa na mwendelezo wake |
| **VIGEZO VYA TATHMINI NA UPIMAJI WA UWEZO WA MSINGI UPATIKANAO KATIKA MADA** | - Uwezo wa kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kufanya mawasiliano kwa kuzingatia muktadha wa sekta ya utalii huku mwanafunzi akizingatia matumizi sahihi ya sarufi aliyoisoma. | - Uwezo wa mwanafunzi kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kufanya mawasiliano kwa njia ya maandishi akizingatia muktadha wa sikukuu na sherehe kwa kutegemea kalenda. | - Uwezo wa mwanafunzi kujitetea akitoa hoja zake hadharani, kusikiliza na kuwasiliana na wenzake katika mdahalo na mjadala.<br>- Utambuzi wa namna ya kubadilisha kauli asili kuwa kauli taarifa.<br>- Ujasiri wa kujieleza kwa ufasaha mbele ya wanafunzi wengine. | - Uwezo wa kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kufanya mawasiliano kwa njia ya maandishi kwa kuelezea shughuli za ujenzi wa taifa huku akizingatia matumizi sahihi ya sarufi aliyoisoma.<br>- Ujuzi wa kutunga sentensi sahihi kwa kutumia majina katika ngeli ya U-ZI katika umoja na wingi. | - Uwezo wa kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kufanya mawasiliano kwa njia ya maandishi kwa kuzingatia teknolojia ya mawasiliano.<br>- Ujasiri wa kujieleza kwa ufasaha mbele ya wanafunzi wengine.<br>- Uwezo wa kutunga sentensi sahihi kwa kuzingatia msamiati wa teknolojia ya mawasiliano. |

# UTANGULIZI

## Nafasi ya Kiswahili katika jamii na mfumo wa elimu

Lugha ya Kiswahili imepewa hadhi kubwa kwa kuteuliwa kuwa mojawapo katika lugha rasmi za Jumuiya ya Afrika. Nchini Kenya na katika nchi ya Tanzania, Kiswahili ni lugha ya taifa na pia lugha rasmi. Nchi za Uganda na Burundi nazo hazijaachwa nyuma kwani lugha ya Kiswahili imeanza kukita mizizi huko na kufunzwa kikamilifu. Nchini Rwanda, Kiswahili ni lugha rasmi.

Nchi nyingine kama Marekani, Ujerumani na mataifa mengi ya Ulaya yameanza kufunza lugha ya Kiswahili katika vyuo vikuu. Wanaelewa kuwa Kiswahili ndiyo lugha inayoweza kuunganisha nchi za ng'ambo na Afrika. Lugha hii huwafaa sana watalii wanaozuru Afrika.

Mipango imefanywa ili kuhakikisha kuwa lugha ya Kiswahili inawekwa katika programu za tarakilishi na kwenye mtandao duniani kote. Ni wazi kuwa Kiswahili kinapiga hatua kwa kasi sana ili kuweza kwenda na wakati.

### Kiswahili katika mfumo wa elimu nchini Rwanda

Somo la Kiswahili limekuwa likifundishwa katika viwango vya elimu vya sekondari nchini Rwanda. Kwa sasa, somo hili linatathminiwa kitaifa.

Lugha ya Kiswahili imepewa nguvu zaidi hasa tukizingatia kuwa wanafunzi wengi hulichukua somo hili katika sekondari na vyuo vikuu na kupata mafunzo katika fasihi na isimu na kufuzu katika somo hili. Tukitilia maanani mambo haya yote, tutaona kuwa wizara ya elimu imeipa lugha ya Kiswahili heshima inayostahili na kuhakikisha kuwa lugha hii inakuzwa.

### Mbinu za kufundisha mada mbalimbali

### a) Ufahamu

Ufahamu ni kipengele muhimu katika lugha ya Kiswahili. Ufahamu umebeba stadi zote zinazoweza kushughulikiwa kama vipengele tofauti tofauti.

Katika kufundisha hatua hii, mwalimu anaweza kuwachangamsha wanafunzi kwa kuwaagiza watazame michoro ya vitabuni na kutaja majina ya wanayoyaona. Pili, wanafunzi waeleze matukio mbalimbali katika michoro hiyo. Kwa mfano: *watalii wakizuru mbuga za wanyama, wanyama wanaopatikana katika mbuga mbalimbali na pesa zinazotumika katika shughuli za utalii.*

Kuwaruhusu wanafunzi kusoma kwa sauti huku wakipokezana kwa zamu ni muhimu. Mwalimu wa Kiswahili anashauriwa awe ameteua kifungu kabla ya kipindi kuwadia. Auchambue msamiati mpya na kuupigia mistari ama kuuandika kwenye daftari la kumbukumbu. Angalau kila mwanafunzi apate fursa ya kusoma sentensi kadhaa. Mwalimu ayakosoe makosa yoyote ya matamshi.

Wanafunzi wasome tena habari hiyo kwa kimya. Watafakari juu ya habari hiyo kisha wajibu maswali kwa kusema kisha kwa kuandika. Katika kiwango hiki cha wanafunzi, mwalimu azingatie na kusisitiza majibu ya sentensi nzima.
*Kwa mfano*:
Kalisa alikuwa akifanya nini? Akipiga wanyama pori picha. (ni kosa)
Kalisa alikuwa akipiga wanyama pori picha. (sahihi)

Mwalimu awaelekeze na kuwaongoza wanafunzi jinsi ya kutunga sentensi fupifupi wakitumia msamiati mpya baada ya kuyafafanua na kuelezea maana na matumizi ya maneno hayo.

**b) Msamiati**

Katika kufunza msamiati, ni jambo la busara endapo mwalimu atatumia vifaa halisi katika kueleza maana na matumizi ya msamiati. Endapo vifaa vingine ni vigumu kuvipata, basi mwalimu anaweza kutumia picha au aandae chati nzuri ili kulifanya funzo hili kueleweka kwa urahisi na pia kulifanya kuwa la kusisimua zaidi. Aidha, mwalimu anaweza kuunda au kubuni vifaa vya kufundisha. Kwa mfano: matumizi ya katoni kuunda mfano wa tarakilishi pale ambapo si rahisi kuipata tarakilishi na kuileta darasani ili kuizungumzia.

Mwalimu anaweza kufunza msamiati kwa njia ya ufahamu. Hapa itambidi mwalimu awaongoze wanafunzi kupata maana kutokana na habari yenyewe. Katika funzo la msamiati, ni bora mwalimu awaambie wanafunzi watunge sentensi wakitumia msamiati waliojifunza.

**ch) Kusikiliza na kuzungumza**

Kusikiliza na kuzungumza ni kipengele muhimu sana katika kujifunza lugha yoyote ile. Ni wazi kuwa mtu ambaye hajapata kusikia neno lolote, yaani alizaliwa kiziwi, kamwe hawezi kuongea. Ataongea akisema nini? Binadamu yeyote alijifunza kuongea kupitia kwa kuwasikiliza watu wengine wakiongea na maneno ya kwanza aliyoyazungumza ni yale aliyoyasikia.

Ni sharti mwalimu akuze stadi hii muhimu ya kujifunza lugha. Wanafunzi wanaweza kujifunza funzo la kusikiliza na kuzungumza kwa kuigiza mchezo wa kuigiza. Kila mwanafunzi apewe sehemu yake ya kuigiza. Mwalimu ajitayarishe

kwa kutunga (endapo ana uwezo) au kuteua mchezo wa kuigiza unaofaa kwa kuzingatia maudhui na kiwango cha wanafunzi. Somo hili huwajenga wanafunzi kuwa na uwezo wa kuongea mbele ya wengine kwa ufasaha bila matatizo yoyote.

Hali kadhalika, wanafunzi wanaweza kujadiliana na wenzao kuhusu mada tofauti tofauti. Wanaweza kuendeleza mijadala kwa kutoa hoja mbalimbali kuhusu mada watakayoteua.

Tathmini katika funzo hili huwa ni maswali ambayo humhitaji mwanafunzi kuyajibu kwa kuongea ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wamepata fursa ya kuongea na kuwasikiliza wengine wakiongea. Itakuwa bora endapo mwalimu ataandaa mara kwa mara vipindi kabambe vya michezo ya kuigiza, midahalo na masimulizi. Aidha, wanafunzi wapewe fursa ya kusikiliza vipindi vya redio na hata inapowezekana, kutazama runinga na kanda za video.

**d) Sarufi**

Sarufi ni mpangilio maalum wa maneno kwa ufasaha kulingana na kanuni zake au kupanga na kutumia maneno vizuri kulingana na mipango au taratibu zilizokubaliwa kuwa ni sahihi. Sehemu muhimu katika sarufi ni ngeli. Mtu yeyote asiyejua na kuzitawala ngeli kamwe hawezi kusema kuwa anaielewa lugha ya Kiswahili. Atakuwa akituhadaa. Sarufi pia hujumuisha sehemu muhimu kama vile: matamshi, majina, vielezi, vitenzi, viambishi, uakifishaji, nyakati, vivumishi na mnyambuliko wa vitenzi.

Mwalimu atumie mbinu mbalimbali katika kuwafunza wanafunzi sarufi. Mwalimu atafute nyenzo zinazofaa na rahisi kupata. Mwalimu asitafute nyenzo ambazo zitagharimu kiasi kikubwa cha pesa. Pia, aunde vifaa vyake ili kuepuka matumizi ya pesa kwa minajili ya kuvinunua.

Mwalimu awatathmini wanafunzi wake ili kutambua iwapo wameelewa yale yote waliyojifunza. Endapo watatokea wanafunzi ambao hawajaelewa, basi mwalimu achukue jukumu la kuwasaidia wanafunzi wake mmoja mmoja kibinafsi kutegemea matatizo yao.

**e) Kuandika**

Wanafunzi katika kiwango hiki wanapaswa kuwa wanajua kusoma kwa ufasaha. Wanaposoma, mwalimu anapaswa kuwa macho kwa sababu wanafunzi wengine huenda wakawa na mbinu mbaya ya usomaji. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi hawasogezi kitabu karibu sana na macho na pia hawatumii vidole kuelekeza macho.

Mwalimu anapaswa kusoma taarifa ambayo anawatarajia wanafunzi kusoma. Achambue maneno magumu ambayo yametumika na kuelewa maana. Awaambie

wanafunzi wasome mmoja mmoja kwa sauti huku akisikiliza kwa makini ili kukosoa makosa yote ya matamshi. Ni bora zaidi mwalimu ayaandike maneno magumu ubaoni. Awaelekeze wanafunzi ili wapate maana ya maneno magumu kutokana na makala waliyoisoma.

Katika kuandika, mwalimu asisitize kuhusu hati nadhifu na inayosomeka kwa urahisi. Kila herufi iandikwe vizuri. Mwalimu aziandike herufi ubaoni na kuwaonyesha wanafunzi jinsi zinavyoandikwa. Mwalimu azungumzie uakifishaji bora. Mwalimu awape zoezi la kuandika na kuhakikisha kuwa wanafunzi wamefuata maagizo.

Mwalimu anaweza kuandaa funzo la imla ambapo anapaswa kuteua sentensi nzuri zenye maneno ambayo huwatatiza wanafunzi wake kisha ayaandike ubaoni na kuwaongoza wanafunzi kuyasoma kwa ufasaha. Mwalimu ayafute kisha awaambie wanafunzi wayaandike jinsi atakavyoyasoma. Njia hii itamwezesha mwalimu kuelewa iwapo wanafunzi wake wameelewa au la. Vilevile, mwalimu anaweza kuyasoma maneno (kwa matamshi sahihi) na kuwaagiza wanafunzi wayaandike.

**Tathmini**

Hii ndiyo sehemu muhimu sana kwa sababu hiki ndicho kigezo kinachomwezesha mwanafunzi na mwalimu kutambua kama malengo ya funzo lake yalitimia.

Mwalimu huwatathmini wanafunzi wake ili:

(a) Kumwezesha kuelewa hatua walizozipiga wanafunzi.
(b) Kuwatia wanafunzi moyo wa kuendelea kujifunza.
(c) Kuelewa maendeleo yake katika kufunza.
(d) Kumwezesha kuelewa kama ametimiza malengo yake vizuri ili aweze kulirudia funzo inapobidi.
(e) Kumwezesha kutambua kama malengo ya funzo lake yalifaulu na kwa kiasi gani.

Aina za tathmini 1. Kuandika muhtasari wa yale wanafunzi walisoma.
2. Kutahini usahihi wa sentensi zilizoandikwa kwenye madaftari.
3. Kuhakiki matamshi kwa kusoma sentensi au vifungu mbalimbali.
4. Kutunga sentensi zilizoendelezwa vizuri.
5. Kuambatanisha maelezo na maneno kwa usahihi.
6. Mazoezi na marudio ya mitihani ya wiki.
7. Maswali ya chemshabongo darasani ambayo humwezesha mwanafunzi kuelewa na kukumbuka aliyoyasoma hapo awali.
8. Mitihani ya kila mwisho wa muhula.

Ni muhimu mwalimu asahihishe kazi za wanafunzi ili aelewe matatizo ambayo yanawakabili wanafunzi na awafunze upya sehemu yenye matatizo. Mwalimu asisitize kuhusu kufanya masahihisho.

Mwalimu awatambue wanafunzi wenye matatizo na kuwapa msaada maalum. Atumie mbinu mbalimbali ili kumwezesha mwanafunzi kuelewa vyema. Mwalimu awe makini sana anaposhughulikia wanafunzi dhaifu ili wasikate tamaa. Daima awatie motisha.

**Nyenzo za kufunzia**

Nyenzo ni muhimu katika somo lolote likiwamo Kiswahili. Mwalimu anatarajiwa kuwa mbunifu na kutumia nyenzo ambazo zinapatikana kwa urahisi. Ni muhimu mwalimu kuhakikisha kuwa hamna gharama inayoweza kuepukika katika funzo lolote lile. Ni vyema mwalimu abuni baadhi ya nyenzo zake.

Mwalimu yeyote ni lazima aende na wakati. Wakati huu ambapo teknolojia imekua sana hasa katika mawasiliano, ni muhimu mwalimu kutumia vifaa vya kisasa. Kwa mfano, ni muhimu mwalimu kutumia vifaa halisi kama rununu na kutumia picha za baadhi ya vyombo ambavyo ama havipatikani katika mazingira ya shuleni au mwalimu hawezi kuvibeba na kwenda navyo darasani kama vile: tarakilishi, runinga, kipepesi n.k.

Ni vyema kwa mwalimu kuyafahamu mazingira ya mwanafunzi wake. Anapofunza kuhusu baruapepe, mtandao, wavuti n.k., somo hili litakuwa rahisi kwa wanafunzi wa mjini na kuwaelezea wanafunzi hao ni rahisi sana. Wanafunzi wale ambao hawajawahi kuona wala kusikia mambo hayo, kwao huenda ikawa ni kioja. Hapo mwalimu anatakiwa awe na nyenzo za kutosha ili kuwafaa wanafunzi wake. Vifaa vingine vinapatikana kwa urahisi na mwalimu anaweza kuwaambia wanafunzi wake walete baadhi ya vifaa hivyo.

Mwalimu asichukulie funzo lolote kuwa rahisi. Utashangaa kugundua kwamba unapofunza kuhusu mimea, wanafunzi wengi hasa wa mijini hawajapata kuiona mimea mingi. Ni bora kwa mwalimu kutumia picha au mimea yenyewe kama inaweza kupatikana.

Mwisho kabisa, ni vyema kwa mwalimu kuelewa kuwa kufaulu au kutofaulu kwa funzo lolote kunamtegemea mwalimu. Ukiwaona wanafunzi wako wakilipenda somo la Kiswahili ujue kuwa aliyefaulu ni wewe. Ukiwaona wanafunzi wakilalamika kuwa lugha ya Kiswahili ni ngumu na inayosinya basi ujue tatizo ni wewe. Ni jukumu la mwalimu yeyote aliyehitimu kuona kuwa wanafunzi wake watakuwa wakilitarajia somo lake na kutaka asitoke darasani. Hapo utakuwa umefaulu. Wewe ndiwe unayewafanya wanafunzi wakuchukie na wewe ndiwe unayeweza kuwafanya wanafunzi wakupende.

**Namna ya kuwashughulikia wanafunzi wa aina mbalimbali**

Mwalimu anapaswa kwenda darasani akifahamu jambo moja kuwa wanafunzi wote wanaweza kufunzwa na kuelewa. Mwalimu ajiepushe kabisa na tabia ya kuwapa wanafunzi wengine majina kuwa ni wajinga. Wanafunzi wote wameletwa

shuleni kuondoa ujinga. Unapomwita mwanafunzi mjinga uelewe kuwa wewe ndiwe uliyeshindwa kuondoa ujinga huo.

Jinsi wanafunzi walivyotoka katika mazingira tofauti ndivyo wanavyotofautiana na ndivyo walivyo tofauti katika kuelewa somo au funzo lolote. Utawapata wanafunzi wenye akili tambuzi kiasi kwamba wakiambiwa kitu huelewa haraka ajabu. Wakipewa zoezi wao hulifanya haraka.

Mwalimu anapaswa kuwa macho na kuwashughulikia vizuri kwa sababu wanaweza kupotoka kwa urahisi. Wanapomaliza zoezi huishia kupiga kelele na kuwasumbua wenzao. Mwalimu anapaswa kuwaandalia mazoezi ya kutosha ili wakimaliza waendelee na mengine.

Mwalimu anapaswa kuwashughulikia barabara wanafunzi wanaochukua muda kuelewa. Akishawapa wengine zoezi, achukue muda huo kuwasaidia wanafunzi dhaifu. Ahakikishe kuwa japo watachukua muda kuelewa, mwishowe watawafikia wale wanaoelewa haraka.

Mwalimu hupata sifa chungu nzima anapowasaidia wanafunzi dhaifu kuwa bora. Kufaulu kwa darasa lolote kunategemea wanafunzi wote. Ni bora kwa mwalimu yeyote kujikwamua katika kutoa sababu kuwa wanafunzi wake ni dhaifu. Swali bado litamrudia, “Umefanya nini kuondoa udhaifu wao?” Umepewa jukumu. Mustakabali wa wanafunzi unakutegemea wewe. Itakuwa ni fahari kubwa utakapowaona wanafunzi wako wakifanikiwa. Wanafunzi pia watamwonea fahari mwalimu wao.

Mwalimu atenge muda wake ili kuwashughulikia wanafunzi wenye matatizo mbalimbali hasa wale ambao si wepesi wa kuelewa. Hali kadhalika, mwalimu anapaswa kuchukua tahadhari ili asiwakere wanafunzi wengine. *Kwa mfano:* katika kusimulia hadithi, anapaswa kutoa hadithi ambazo hazitawadunisha wanafunzi wenye upungufu fulani.

Mwalimu ahakikishe kuwa katika mafunzo yake ameshughulikia usawa wa jinsia. Pasiwe na ubaguzi wa aina yoyote.

**Ratiba ya mafunzo**

Ratiba ni muhimu kwa mwalimu yeyote aliyehitimu. Ni sharti mwalimu awe na mwongozo na taratibu za kufuata ili asisahau mambo muhimu.

Mwalimu aandae ratiba kutokana na silabasi ambayo ndiyo mwongozo unaotoa mwelekeo wa kufundisha. Mwalimu avitumie vitabu bora vilivyoidhinishwa na wizara ya elimu.
Ufuatao ni mfano wa ratiba ya mafunzo katika somo la Kiswahili.

**Andalio la somo**

Huu ni utaratibu anaouandaa mwalimu ili kuliendesha vyema somo lake kuanzia mwanzo hadi tamati. Utaratibu huo humwezesha mwalimu kufuata hatua baada ya

| WIKI | KIPINDI | MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO | NYENZO | ASILIA | MAONI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **1** | 1 | LUGHA NA MAZINGIRA | Utalii nchini Rwanda<br>i) Ufahamu na msamiati | - Kusoma kwa usahihi kifungu cha mazungumzo kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;<br>- Kubaini msamiati unaotumika katika ofisi ya utalii;<br>- Kutambua namna ya kumhudumia mtalii;<br>- Kusoma ramani inayohusu vivutio vya utalii nchini. | - Ramani yenye kuonyesha vivutio mbalimbali<br>- Michoro ya watalii<br>- Picha za wanyama wanaopatikana katika mbuga | Kitabu cha mwanafunzi ukurasa wa 1-4 | |
| | 2 | | ii) Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza | - Kukuza stadi za utafiti za wanafunzi;<br>- Kubaini aina za pesa zinazotumika katika nchi mbalimbali;<br>- Kutamka maneno kwa usahihi na kwa utambuzi wa herufi katika maigizo. | - Michoro ya watalii<br>- Aina za pesa zinazotumika katika nchi mbalimbali | Kitabu cha mwanafunzi ukurasa wa 5-7 | |
| **2** | 3 | | iii) Sarufi - viulizi ‘nani’ na ‘nini’ | - Kubaini matumizi ya viulizi ‘nani’ na ‘nini’ katika sentensi;<br>- Kutumia kwa usahihi viulizi ‘nani’ na ‘nini’ kuulizia maswali. | - Vifaa halisi darasani. Kwa mfano: kalamu, daftari n.k.<br>- Wanafunzi wenyewe<br>- Michoro | Kitabu cha mwanafunzi ukurasa wa 7-8 | |
| | 4 | | Mbuga za wanyama<br><br>i) Ufahamu na msamiati | - Kusoma kwa usahihi kifungu cha habari kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;<br>- Kubaini msamiati unaotumika katika mazingira ya mbuga za wanyama;<br>- Kutumia msamiati wa mbuga za wanyama katika sentensi sahihi. | - Ramani yenye kuonyesha mbuga mbalimbali za wanyama<br>- Michoro ya watalii katika shughuli zao | Kitabu cha mwanafunzi ukurasa wa 9-13 | |

nyingine na kuweza kupata picha ya somo lake mapema. Humwezesha mwalimu kushughulikia masuala yote muhimu katika somo. Kufikia mwisho wa somo, mwalimu huweza kutathmini ili kuelewa kama somo lake limefaulu.

**Mfano wa andalio la somo**

**Jina la shule**: GIKONDO **Jina la mwalimu:** GASIMBA LUKA

| Muhula | Tarehe | Somo | Kidato | Mada | Idadi ya masomo | Muda | Idadi ya wanafunzi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| wa kwanza | 07.08.2017 | Kiswahili | cha tatu | ya 1 | 2 kwa 6 | Dakika 40 | 46 |

| | |
|---|---|
| **Aina ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu pamoja na idadi yao: 1**<br>1. Mwanafunzi mwenye matatizo ya kutembea ( ana mguu mmoja). | |
| **Mada Kuu:** | **Lugha na Mazingira** |
| **Uwezo upatikanao katika mada:** | Mwanafunzi aweze kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika kuhusu muktadha wa utalii na kuzingatia matumizi sahihi ya sarufi inayohusika. |
| **Kichwa cha somo:** | Kifungu kuhusu mbuga za wanyama nchini Rwanda |
| **Malengo ya kujifunza:** | • Kutokana na kifungu cha habari, mwanafunzi atakuwa na uwezo wa kusoma kwa usahihi kifungu cha habari kuhusu mbuga za wanyama nchini Rwanda.<br>• Kutokana na kifungu cha habari, mwanafunzi atakuwa na uwezo wa kutambua kwa urahisi maana ya msamiati katika kifungu kuhusu mbuga za wanyama nchini Rwanda. |
| **Mpangilio wa darasa** | **Mandhari:** Somo linatokea darasani ambamo wanafunzi watatazama ramani yenye kuonyesha mbuga mbalimbali za wanyama na pia kujadiliana. |
| **Zana / Vifaa** | Kitabu cha mwanafunzi, ramani ya mbuga za wanyama nchini Rwanda, ubao, chaki, michoro ya watalii katika shughuli zao za kitalii, wanafunzi wenyewe. |
| **Marejeleo** | Kitabu cha *Kiswahili kwa shule za Rwanda*, kidato cha 3; 2017, *Kamusi ya karne ya 21*,Longhorn Kenya, *Kitabu cha Kiswahili*, kidato cha 3 MK. |

| **Muda na hatua** | **Mbinu za kufundishia na kujifunzia**<br>Kwa njia ya maigizo katika makundi au kati ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi watasoma kifungu cha habari kuhusu mbuga za wanyama. | | **Uwezo wa jumla, masuala mtambuka na maelezo mafupi** |
|---|---|---|---|
| | **Wajibu wa mwalimu** | **Wajibu wa wanafunzi** | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Utangulizi**<br><br>Dakika 5 | - Mwalimu awaamkue wanafunzi kisha awaulize maswali kuhusu mbuga za wanyama ambazo wanazijua.<br><br>- Mwalimu awape wanafunzi fursa ya kueleza wanachokiona kwenye michoro katika vitabu vyao. | - Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu na kutaja mbuga za wanyama ambazo wanafahamu.<br><br>- Wanafunzi wajadiliane kile wanachokiona kwenye michoro kwa sentensi kamili za Kiswahili. | **Uwezo wa jumla:**<br>*i)* ***Kupata stadi za utafiti:***<br>Wanafunzi wahimizwe kufanya utafiti zaidi kuhusiana na mbuga za wanyama nchini Rwanda.<br>*ii)* ***Kuwa na tafakuri tanduizi:***<br>Wanafunzi wataweza kujadiliana kuhusu mbuga za wanyama zilizopo nchini Rwanda pamoja na umuhimu wao kwa uchumi wa taifa.<br>*iii)* ***Kuwa na uwezo wa kushiriki katika mawasiliano kwa lugha rasmi:***<br>Kupitia kwa mazoezi ya kuigiza, wanafunzi wataweza kuwasiliana kwa lugha rasmi ya Kiswahili.<br>*iv)* ***Kuwa na uwezo wa usuluhishaji wa matatizo:***<br>Wanafunzi wajadiliane kuhusu njia za kuhifadhi mazingira kwa ajili ya kuwahifadhi wanyamapori. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Somo lenyewe**<br><br>Dakika 30 | - Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kifungu cha habari kuhusu mbuga za wanyama.<br>- Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili ili watafute na kujadiliana maana za msamiati uliotumika kwenye kifungu walichokisoma.<br>- Mwalimu awape wanafunzi fursa ya kutunga sentensi sahihi za Kiswahili kwa kutumia msamiati waliojadili.<br>- Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kujibu maswali ya ufahamu kwa kuandika majibu sahihi kwenye madaftari yao. | - Wanafunzi wajipange katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha wasome kifungu cha habari.<br>- Wanafunzi wajadiliane katika makundi matumizi na maana za msamiati husika.<br>- Wanafunzi washiriki katika kutunga sentensi sahihi za Kiswahili kwa kutumia msamiati waliopata kwenye kifungu.<br>- Wanafunzi wajibu maswali ya ufahamu. | **Masuala mtambuka:**<br>***i) Mazingira na maendeleo ya kumudu:***<br>Wanafunzi wafahamu kuwa mazingira ya mbuga za wanyama yanapotunzwa vizuri, utalii utaimarika nchini na hivyo nchi itakuwa na mvua ya kutosha.<br>***ii) Mafunzo kuhusu uzalishajimali:***<br>Wanafunzi wafahamu kuwa mbuga za wanyama huwavutia watalii ambao huiletea nchi yetu pesa za kigeni.<br>***iii) Mafunzo kuhusu amani na maadili:***<br>Wanafunzi watambue kuwa nchi ikiwa na amani, shughuli za utalii zitaendeshwa vizuri. |
| **Hitimisho**<br><br>Dakika 5 | - Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kusahihisha maswali ya ufahamu kwa kuwashirikisha kwenye shughuli hiyo. Pia, atilie mkazo pale ambapo wanafunzi wanapata matatizo katika kujibu maswali ya ufahamu. | - Wanafunzi washiriki katika usahihishaji wa zoezi la ufahamu na baadaye wafanye marudio. | |
| **Tathmini ya mwalimu** | Mwalimu achunguze iwapo ameyatimiza malengo ya somo hili au la. | | |

Sura ya Kwanza

# Mada Kuu 1: Lugha na mazingira

## Mada Ndogo: Utalii nchini Rwanda

**Uwezo upatikanao katika mada hii:**
Mwanafunzi aweze, kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika kuhusu muktadha wa utalii na kuzingatia matumizi sahihi ya sarufi inayohusika.

### Malengo ya kujifunza

Mwalimu ahakikishe kwamba katika ufundishaji wake, wanafunzi wanapata maarifa, ufahamu, stadi, maadili na mwenendo mwema ufuatao:

| Maarifa na ufahamu | Stadi | Maadili na mwenendo mwema |
|---|---|---|
| • Kukumbuka msamiati unaotumiwa katika uwanja wa utalii. | • Kutumia msamiati unaohusika na mambo ya utalii katika mazingira mbalimbali ya kimawasiliano. | • Kujali na kuthamini mali ya kibinafsi pamoja na ile ya umma na kutimiza wajibu wa kuitumia vizuri. |
| • Kuonyesha uelewa wa jinsi ya kuuliza maswali kutokana na kifungu ca habari kinacohusika na kuyatolea majibu yanayofaa. | • Kutumia maarifa aliyosoma katika kujibu maswali yanayotokana na kifungu ca habari kwa kuzingatia jinsi yalivyotolewa. | • Kuheshimu mazingira na kuyahifadhi kama inavyostahili. |
| • Kueleza yaliyo katika kifungu ca habari na kuyatolea muhtasari kwa njia ya mazungumzo na maandishi. | • Kutoa muhtasari wa kifungu ca habari alicopewa. | • Kutetea haki za wanyama na kuhifadhi vivutio vya utalii. |
| • Kutoa mifano ya namna ya kuwasiliana kwa usahihi na watu mbalimbali katika sekta ya utalii. | • Kuonyesha jukumu la kutoa huduma kwa mtalii au mtu yeyote katika sekta ya utalii hususan kupitia mawasiliano ya lugha ya Kiswahili | • Kuthamini utamaduni wa mtu binafsi na wa watu wengine. |

| | | |
|---|---|---|
| • Kubainisha matumizi ya wakati wa mazoea katika mawasiliano mbalimbali. | • Kujadiliana katika makundi na kueleza hadharani vivutio vya utalii ncini Rwanda. | |
| • Kutaja aina za pesa zitumiwazo mara nyingi katika mazingira ya utalii au biashara. | • Kutathimini aina mbalimbali za vivutio vya utalii ncini Rwanda na kuweza kueleza sifa za msingi kwa kila kivutio. | |
| | • Kuonyesha ujuzi wa kubadilisha pesa za kigeni na pesa za Rwanda au za nci jirani na Rwanda. | |
| | • Kutumia kwa usahihi wakati wa mazoea katika hali yakinishi na hali kanushi katika mawasiliano mbalimbali. | |

## Maelezo kwa mwalimu

Mwalimu afahamu na awafahamishe wanafunzi kuwa mada hii inahusiana na masomo mengine kama vile ***somo la Jiografia*** kuhusu mada ya utalii na ramani ya maeneo yenye vivutio vya utalii, njia za uhifadhi wa mazingira na vivutio vya utalii, ***somo la Hisabati*** kuhusu aina za pesa zinazotumika katika nci mbalimbali na namna au fomula ya kubadilisha pesa za nci moja na kuwa pesa za nci nyingine.

Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanaelewa kuwa lugha ni combo ca mawasiliano kinacotumiwa katika miktadha mbalimbali inayohusu maisha ya binadamu ambaye huishi katika mazingira ya aina tofauti.

Ili mwalimu atimize malengo yake katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo hili, ni vyema akumbuke kutilia mkazo mbinu ya kuwagawa wanafunzi katika makundi madogo madogo ili waweze kujishughulisha na kazi tofauti kwa kuwacocea kuigiza mazungumzo yaliyopo na yale yatakayobuniwa na wanafunzi.

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kujua vivutio mbalimbali vya utalii na kuonyesha faida za utalii kwa ucumi wa nci. Kwa hivyo, mwalimu atumie micoro, pica na ramani ya Rwanda kuweka wazi maeneo mbalimbali ya utalii yanayozungumziwa katika mada hii ili kuwasaidia wanafunzi kupata ujuzi unaotakikana.

Aidha, utamaduni ni jambo muhimu katika shughuli za kiutalii. Hivyo basi, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuthamini utamaduni wao ili waweze kufahamu jinsi unavyoweza kutumiwa kama njia ya kuleta faida za kiutalii.

Mbali na hayo, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wake wamezifahamu namna mbalimbali za kuuliza maswali. Kwa hivyo, awasaidie wanafunzi kupata ujuzi wa kutosha katika kutunga mazungumzo baina ya watu tofauti wanaouliza maswali kama vile: *Nani atakuja?, Nini kitapikwa?, Lini tutasafiri?, Vipi tutaimba?, Wapi tutazuru?, Kwa nini unalia?* na kadhalika. Ni vyema mwalimu awaweke wanafunzi katika muktadha ambapo wataweza kutambua namna tofauti za kuuliza maswali na jinsi maswali hayo yanavyoweza kujibiwa bila kusita. Vilevile, mada hii inalenga kudhihirisha mwongozo wa kutoa muhtasari au ufupisho wa kifungu ca habari kilicosomwa au kuzungumziwa. Kwa hivyo, kupitia mazoezi yaliyopo, mwalimu awaelekeze wanafunzi ili waweze kupata mbinu muhimu za kuandaa muhtasari wa vifungu vilivyopo kwa kuzingatia mambo muhimu yaliyozungumziwa na kujiepusha kurudia maneno yaliyo katika kifungu ca habari kilicopo.

Kipengele ca kisarufi kinacohusiana na matumizi ya wakati wa mazoea naco kimeandaliwa katika mada hii. Mwalimu awasaidie wanafunzi kufahamu matumizi ya wakati huu kwa kulinganisha na kurejelea nyakati nyingine zilizozungumziwa katika mada tangulizi za mada hii ili waweze kuzitofautisha na kuzitumia kwa njia sahihi.

### Masuala mtambuka

Baadhi ya masuala mtambuka ambayo yatashughulikiwa katika mada hii ni amani na maadili, usawa wa kijinsia, elimu ya pamoja, elimu kuhusu fedha pamoja na mazingira, mabadiliko ya hali ya hewa na mwendelezo wake.

Usawa wa kijinsia utatiliwa mkazo kwa kuwafahamisha wanafunzi kuwa wasicana pamoja na wavulana wana uwezo sawa wa kufaulu katika maisha yao lica ya jinsia zao tofauti. Elimu ya pamoja itaendelezwa kupitia kwa wanafunzi wote kusoma pamoja kwa kuwashirikisha hata na wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali na matatizo mbalimbali. Elimu hii ya pamoja pia itahusisha wanafunzi wote kuwakubali na kushirikiana kwa pamoja na wenzao kutoka katika matabaka mbalimbali ya kijamii. Wanafunzi pia watafundishwa umuhimu wa mazingira yao na namna ya kuyahifadhi. Elimu kuhusu pesa itafundishwa kwa kuwaeleza wanafunzi kuhusu umuhimu wa pesa na namna ya kutotumia pesa vibaya. Amani na maadili yatafundishwa kupitia kwa wanafunzi kushirikiana katika kazi mbalimbali za makundi darasani.

## Uwezo wa jumla

Mwalimu ahakikishe kuwa katika ufundishaji wake, wanafunzi wanapata uwezo wa kuwa na tafakuri tanduizi, usuluhishaji wa matatizo, mawasiliano katika lugha rasmi, stadi za utafiti, ubunifu na ugunduzi, ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha pamoja na ujifunzaji wa muda mrefu.

Wanafunzi wataweza kuwa na tafakuri tanduizi kwa kufikiri kwa undani (kutafakari zaidi) ili kuweza kuyajibu maswali katika mada hii kuhusiana na micoro waliyopewa pamoja na fahamu watakazosoma. Kupitia kwa mazoezi ya kuigiza, wanafunzi watahimizwa kuwasiliana kwa lugha rasmi pamoja na kuwa na utawala binafsi na kuzifahamu stadi mbalimbali za maisha. Stadi za utafiti zitahitajika hapa ambapo wanafunzi watafanya utafiti mbalimbali kuhusiana na vivutio mbalimbali vya utalii vilivyo ncini Rwanda. Ujifunzaji wa muda mrefu uendelezwe kupitia kwa wanafunzi kupata maarifa mbalimbali kuhusiana na nci yao watakayotumia nje ya darasa na katika maisha yao ya kila siku.

## Msamiati maalum

Msamiati maalum na muhimu ambao wanafunzi watapatana nao katika mada hii ni kuhusu utalii ncini Rwanda kama vile:

| | **Msamiati** | **Maana** |
|---|---|---|
| 1. | ***mtalii*** | mtu kutoka ndani au nje ya nci ambaye anatembelea mahali fulani kwa ajili ya kujifunza au kujifurahisha |
| 2. | ***mwelekezaji*** | mtu anayemwongoza mtu au watu mahali fulani kwa kuwaonyesha mazingira ya mahali hapo pamoja na vitu vilivyomo |
| 3. | ***vivutio*** | kitu, mtu au mahali popote penye uwezo wa kuwafanya watalii kwenda kutazama |
| 4. | ***mbuga*** | mahali palipotengwa kwa ajili ya kuwahifadhi wanyamapori |
| 5. | ***wanyamapori*** | viumbe hai ambao huishi msituni |
| 6. | ***ramani*** | pica ya nci au sehemu ya nci inayoonyeshwa kwenye karatasi kwa vipimo mahususi |
| 7. | ***volkano*** | tope, moshi na mawe ambayo hulipuka na kumwagika katika ardhi kutoka kwenye kilele ca mlima mahususi |
| 8. | ***faranga*** | pesa zinazotumika ncini Rwanda |
| 9. | ***dola*** | pesa zinazotumika ncini Marekani |
| 10. | ***mpokeaji*** | mtu anayemkaribisha mgeni au wageni mahali fulani |

## Usuluhishaji wa tatizo

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi yanayotakikana kisha awaombe wacunguze kwa makini mcoro ulio katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 16 kuhusiana na shughuli za utalii. Wanafunzi wote washirikishwe katika shughuli hii. Wanafunzi wacunguze mcoro huo na mwalimu awaulize maswali kama vile: *Mnaona nini kwenye mcoro huu? Ni nini kinaendelea katika mcoro huu?* Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika makundi yao ili waweze kujibu maswali hayo na kuelewa kinacoendelea katika mcoro uliopo. Kwa hivyo, mwalimu acocee uwezo wa wanafunzi wa kupata maarifa kuhusu ubunifu na ugunduzi na tafakuri tanduizi kwa kucunguza na kujibu maswali kuhusu mcoro husika.

## Ushirikishaji wa wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali

Ili kuwashirikisha kwa pamoja wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali, ni vyema mwalimu awe na vifaa maalum vya kuwasaidia wanafunzi wa aina hii katika kusoma kwao. Kwa wanafunzi wasio na uwezo wa kuona, mwalimu ahusishe matumizi ya breli pamoja na vifaa vya kunasia sauti. Kwa wanafunzi wasio na uwezo wa kusikia, mwalimu ahusishe matumizi ya lugha ya ishara. Mwalimu anaweza kuwahusisha watafsiri wa lugha ya ishara. Haya yatawawezesha wanafunzi hawa kusoma kama wenzao bila vikwazo vyovyote. Nafasi ya wanawake na walemavu katika shughuli kama vile za kitalii itiliwe maanani kupitia mcoro uliopo katika *Kitabu ca Mwanafunzi* 16 ili kukuza usawa wa kijinsia na elimu ya pamoja kwa kudumisha ushirikiano na mienendo mizuri miongoni mwa wanafunzi.

## Orodha ya masomo na vipindi

| Mada ya somo | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|
| **Somo la 1:** | Ofisi ya utalii | 3 |
| **Somo la 2:** | Mbuga za wanyama | 3 |
| **Somo la 3:** | Mwelekezaji na Mtalii | 3 |
| **Somo la 4:** | Utamaduni na utalii | 3 |
| **Somo la 5:** | Milima yetu | 3 |
| **Somo la 6:** | Maji yetu | 3 |
| | | **JUMLA: 18** |

# Somo la 1: Ofisi ya Utalii

## Kipindi cha 1: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati

### a) Malengo ya somo

- Kusoma kwa usahihi kifungu ca mazungumzo kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;
- Kubaini msamiati unaotumika katika ofisi ya utalii;
- Kutambua namna ya kumhudumia mtalii;
- Kusoma ramani inayohusu vivutio vya utalii ncini;

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Ramani yenye kuonyesha vivutio mbalimbali vya utalii;
- Micoro ya watalii katika shughuli zao za kiutalii,
- Pica za wanyama wanaopatikana katika mbuga mbalimbali;
- Micoro ya vifaa tofauti vinavyotumiwa na watalii kama vile: hema, magari ya kiutalii, kamera, na vingine;
- *Kitabu ca Mwanafunzi,* ukurasa 1-4*;*
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### c) Maandalizi ya somo

Hili ni somo la kwanza katika masomo mengine yanayohusu utalii cini ya mada kuu ya '*Lugha na Mazingira*'. Kwa hivyo, mwalimu atafute kwanza vifaa vinavyoweza kurahisisha uelewa wa wanafunzi katika somo hili kama vile: ramani ya vivutio vya utalii ncini Rwanda, pica na micoro ya mazingira ya utalii, micoro ya watalii na kadhalika. Kupitia micoro hiyo, mwalimu aandae maswali mbalimbali yatakayowacocea wanafunzi kutambua maana ya utalii, shughuli zinazofanywa katika utalii, watu wanaohudumia watalii, umuhimu wa utalii na hata namna ya kuhifadhi na kutunza mazingira yaliyotengwa kwa shughuli za utalii.

Wakati wa kuendesha somo, mwalimu atambue wakati mwafaka wa kuweka hadharani vifaa alivyovileta kwa kukumbuka kuwa matumizi ya micoro na pica ni mbinu nzuri sana kwa wanafunzi; hasa wale ambao wana matatizo mbalimbali katika kuelewa na kufahamu haraka yale wanayofundishwa darasani

au wale walio na kiwango ca cini katika ujifunzaji wao. Ikiwa kuna wanafunzi wasioweza kuona, ni lazima mwalimu awaombe wao wenyewe kuvigusa vifaa vilivyopo wakivitolea maelezo na wale ambao hawawezi kusikia wavionyeshe kwa kuvigusa huku wakiandika maelezo yake ubaoni. Ili kutimiza malengo yake katika somo hili, ni vyema mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli ya wanafunzi iliyopendekezwa katika *Kitabu ca Mwanafunzi*.

### d) Utaratibu wa somo

### Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu vitu vinavyowavutia kwa maco. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu kisha waendelee kujibu maswali mbalimbali kuhusu vitu vinavyoweza kuvutia maco yao. Mwalimu awacangamshe wanafunzi kwa kuwauliza maswali kuhusu pica na micoro aliyoileta ili kucocea ufahamu wao kuhusu shughuli ya utalii. Wanafunzi wajibu maswali kama walivyoulizwa naye mwalimu aendelee kwa kuwaomba wacunguze mcoro ulio katika *Kitabu ca Mwanafunzi,* ukurasa 1. Wanafunzi wacunguze mcoro huo na mwalimu awaulize maswali kama vile: *Mnaona nini kwenye mcoro huu? Watu hawa wanafanya nini? Wao wanatazama nini?* Mwalimu awaelekeze wanafunzi ili waweze kujibu maswali hayo na kuelewa kinacoendelea katika mcoro uliopo. Kwa hivyo, mwalimu acocee uwezo wa wanafunzi wa kupata maarifa kuhusu ubunifu na ugunduzi, tafakuri tunduizi kwa kucunguza na kujibu maswali kuhusu mcoro huo. Vilevile, usawa wa kijinsia nao ugusiwe kwa kuonyesha nafasi kubwa ya mwanamke miongoni mwa watalii na wahudumu waliopo na jinsi wanavyotekeleza majukumu yao kwa njia nzuri. Mkazo utiliwe kuhusiana na ushirikiano unaojitokeza kati ya wanaume na wanawake, wavulana na wasicana ili waweze kufanikisha shughuli zao za utalii na kupata faida mbalimbali. Vilevile, masuala ya elimu ya pamoja nayo yasisitizwe pale ambapo miongoni mwa watalii na wahudumu waliopo kuna wale wenye ulemavu wa aina tofauti na ambao wanafanya kazi yao kwa njia inayotakikana.

### 1.1 Kusoma na ufahamu: Mazungumzo kati ya Mpokeaji na Mtalii

Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa kimya kifungu ca mazungumzo kinacohusika na kuandika msamiati mpya wanaopatana nao. Baadaye, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wote wamesoma na kuelewa kama alivyowaomba kwa kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu kifungu ca

mazungumzo walicosoma. Kwa mfano, anaweza kuwauliza: *Ni watu gani wanaozungumza katika kifungu hiki? Watu hao wanazungumzia nini?* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu wao kulingana na yale waliyoyasoma katika kifungu hico ca mazungumzo. Kwa mfano: *Watu wanaozungumza ni Mtalii na Mpokeaji; Wao wanazungumzia utalii*. Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa sauti na kwa usahihi baada ya kutambua kwamba wanafunzi wamepata uelewa wa kile kinacozungumziwa katika kifungu ca mazungumzo kilicopo. Kwa hivyo, ni vyema mwalimu akumbuke kusahihisha matamshi ya wanafunzi pale wanapokosea.

Mwalimu awaombe wanafunzi wajibu maswali waliyopewa kama maswali ya ufahamu. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali hayo huku akitoa maelezo yake kwa kutilia mkazo pale ambapo wanatatizika. Mwalimu atilie mkazo maadili na mienendo miema inayomtambulisha Mpokeaji na Mtalii wake wakati wa kuomba huduma na kuhudumiwa.

### 1.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu utalii

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu ili wajadiliane kuhusu maana za msamiati mpya waliopatana nao wakati wao wa kusoma kifungu kinacohusika. Ili kuimarisha stadi za utafiti na kudumisha uwezo wao wa kupata suluhisho kwa matatizo wanayokutana nayo, mwalimu awaombe wanafunzi wacunguze matumizi ya msamiati huo katika kifungu walicokisoma huku wakitumia kamusi pale wanapoihitaji. Mwalimu azunguke darasani akiwaelekeza wanafunzi wanaotatizika. Wanafunzi wajadiliane kwa kuzingatia maelekezo ya mwalimu wao. Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi kujadiliana pia kuhusu sentensi zilizo katika zoezi la 1.1 la msamiati ili waweze kutunga sentensi zao kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mstari. Wanafunzi nao, katika makundi yao ya wanafunzi watatu watatu, wajadiliane kuhusu zoezi hilo. Ili kurahisisha uelewa wa wanafunzi wa zoezi hilo, mwalimu awaombe walinganishe sentensi zilizopo na matumizi ya msamiati uliopigiwa mstari katika kifungu ca mazungumzo walicosoma. Katika kutunga sentensi zao, mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wanapata ujuzi wa mawasiliano katika lugha rasmi, ubunifu na ugunduzi, ushirikiano na hata utawala binafsi na stadi za maisha kupitia sentensi za wanafunzi na zile zilizopendekezwa katika *Kitabu ca Mwanafunzi,* ukurasa 4. Hivyo basi, mwalimu azunguke darasani ili kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika katika utunzi wao wa sentensi na baadaye awashirikishe wote kutoa mcango wao katika kusahihisha zoezi hilo.

**Tathmini ya kipindi ca 1**

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti kwa kurejelea msamiati mahususi uliopatikana katika kifungu ca mazungumzo walicokisoma kama vile: *utalii, kuvutia, ramani, kuelekeza, mbuga za wanyama, kuzuru maeneo ya kitalii, ofisi ya utalii, mgeni, mpokeaji, vivutio* na kadhalika. Kwa hivyo, vifaa na pica zilizotumiwa kujifunzia somo hili zinaweza kutumiwa kucunguza ikiwa wanafunzi wanaweza kurejelea mienendo mizuri na shughuli mbalimbali za kiutalii kama vile: namna ya kuuliza maswali ili uelekezwe kama mtalii au namna ya kumhudumia mtalii anayekuja kutembelea maeneo mbalimbali ya kiutalii.

## Kipindi cha 2: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza

**a) Malengo ya somo**

- Kukuza stadi za utafiti za wanafunzi;
- Kubaini aina za pesa zinazotumika katika nci mbalimbali;
- Kutamka maneno kwa usahihi na kwa utambuzi wa herufi katika maigizo.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Micoro ya watalii katika shughuli zao za kiutalii;
- Aina za pesa zinazotumika katika nci mbalimbali;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 4-6;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Mwalimu atafute vifaa vitakavyoweza kurahisisha uelewa wa wanafunzi katika somo hili kama vile micoro ya watalii katika shughuli zao za kiutalii, aina za pesa zinazotumika katika nci mbalimbali pamoja na combo ca kunasia sauti au breli, ramani ya vivutio vya utalii ncini Rwanda, pica na micoro ya mazingira ya utalii na kadhalika. Kupitia vifaa hivyo, mwalimu aandae maswali mbalimbali yatakayowacocea wanafunzi kutambua maana ya utalii, shughuli zinazofanywa katika utalii, watu wanaohudumia watalii, umuhimu wa utalii na hata namna ya kuhifadhi na kutunza mazingira yaliyotengwa kwa shughuli za utalii pamoja na pesa zinazotumiwa katika nci mbalimbali.

Wakati wa kuendesha somo, mwalimu atambue wakati mwafaka wa kuweka hadharani vifaa alivyovileta kwa kukumbuka kuwa matumizi ya micoro na pica ni mbinu nzuri sana kwa wanafunzi; hasa wale ambao wana matatizo mbalimbali katika kuelewa na kufahamu haraka yale wanayofundishwa darasani au wale walio na kiwango ca cini katika ujifunzaji wao. Ikiwa kuna wanafunzi wasioweza kuona, ni lazima mwalimu awaombe wao wenyewe kuvigusa vifaa vilivyopo wakivitolea maelezo na wale ambao hawawezi kusikia wavionyeshe kwa kuvigusa huku wakiandika maelezo yake ubaoni. Ili kuyafikia malengo yake katika somo hili, ni vyema mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli ya wanafunzi iliyopendekezwa katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 4.

### d) Utaratibu wa somo

### Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi ca 1. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa. Wanafunzi waeleze kuhusu shughuli za utalii walizosoma, vivutio mbalimbali vya utalii ncini pamoja na huduma mbalimbali ambazo watalii hupokea.

### 1.3 Matumizi ya lugha: Aina mbalimbali za pesa

Katika hatua hii, mwalimu alenge kuwaelekeza wanafunzi kupata ujuzi kuhusu stadi za utafiti kwa kuwaomba wanafunzi wabaini aina za pesa zinazotumiwa katika nci tofauti. Mwalimu awaonyeshe wanafunzi aina mbalimbali za pesa zinazotumika katika nci mbalimbali. Mwalimu anaweza pia kuonyesha wanafunzi micoro ya pesa mbalimbali iwapo hakupata pesa halisi. Ni vyema mwalimu kucukua fursa hii kuwaelekeza wanafunzi ili wapate ujuzi kuhusu jinsi pesa hizo zinavyoweza kubadilishwa katika faranga za Rwanda. Ikiwezekana, mtandao utumiwe ili kuwasaidia wanafunzi kupata habari kamili kuhusu thamani ya pesa hizo.

### 1.4 Kusikiliza na kuzungumza: Maigizo

Katika hatua hii, mwalimu awaombe wanafunzi waigize mazungumzo kati ya Mtalii na Mpokeaji katika makundi ya wanafunzi wawili wawili. Mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wanatamka maneno kwa usahihi na kwa utambuzi wa herufi, silabi, neno na sentensi. Ili kuigiza mazungumzo kwa namna inayotakikana, mwalimu awaombe wanafunzi hawa wajitokeze mbele

ya wanafunzi wengine na acunguze pia ikiwa uigizaji wa ishara unaambatana na maana kusudiwa au inayozungumziwa na mhusika. Mwalimu asahihishe makosa ya kimatamshi kila mara yanapojitokeza ili kuwazoesha wanafunzi kutamka maneno kwa usahihi na kudumisha uwezo wao wa kuwasiliana kwa lugha rasmi.

**Tathmini ya kipindi ca 2**

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali kuhusu mambo muhimu waliyojifunza katika matumizi ya lugha pamoja na kusikiliza na kuzungumza. Maswali yake yacunguze uwezo wa wanafunzi wa kutumia msamiati unaojitokeza katika mazungumzo kati ya Mpokeaji wa Mtalii; kubaini namna ya kuhudumia mtalii; kusoma na kutumia ramani inayohusu vivutio vya utalii ncini; kutaja aina za pesa zitumiwazo katika sekta ya utalii pamoja na kuweza kubadilisha pesa za nci moja hadi pesa za nci nyingine.

## Kipindi cha 3: Sarufi (Viulizi 'nani' na 'nini')

**a) Malengo ya somo**

- Kubaini matumizi ya viulizi 'nani' na 'nini' katika sentensi;
- Kutumia kwa usahihi viulizi 'nini' na 'nani' kuulizia maswali mbalimbali.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Vifaa vya darasani kama vile: madaftari, kalamu, rula n.k.;
- Wanafunzi wenyewe;
- Micoro ya watalii katika shughuli zao za kiutalii;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 6-7;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Mwalimu atafute vifaa vitakavyoweza kurahisisha uelewa wa wanafunzi katika somo hili kama vile: madaftari, kalamu, micoro ya watalii katika shughuli zao za kiutalii pamoja na combo ca kunasia sauti au breli na kadhalika. Kupitia vifaa hivyo, mwalimu aandae maswali mbalimbali yatakayowacocea wanafunzi kutambua maana ya viulizi ***nani*** na ***nini*** pamoja na matumizi yavyo katika maongezi na sentensi sahihi.

Mwalimu atambue wakati mwafaka wa kuweka hadharani vifaa alivyovileta. Wanafunzi walio na matatizo mbalimbali katika kuelewa na kufahamu haraka yale wanayofundishwa darasani au wale walio na kiwango ca cini katika ujifunzaji wao wataweza kufaidika kutokana na matumizi ya vifaa mbalimbali katika somo hili. Ikiwa kuna wanafunzi wasioweza kuona, ni lazima mwalimu awaombe wao wenyewe kuvigusa vifaa vilivyopo wakivitolea maelezo na wale ambao hawawezi kusikia wavionyeshe kwa kuvigusa huku wakiandika maelezo yake ubaoni. Ili kuyaafikia malengo yake katika somo hili, ni vyema mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli ya wanafunzi iliyopendekezwa katika *Kitabu ca Mwanafunzi*.

### d) Utaratibu wa somo

### Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi ca 2. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa. Wanafunzi waeleze kuhusu aina za pesa zinazotumika katika nci mbalimbali, vivutio mbalimbali vya utalii ncini pamoja na huduma mbalimbali ambazo watalii hupokea.

### 1.5 Sarufi: Viulizi 'nani' na 'nini'

Katika hatua hii, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili na awaombe wasome sentensi zilizo kitabuni huku wakicunguza maneno yaliyopigiwa mistari. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua na kuelewa matumizi ya maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi walizopewa. Wanafunzi wasome sentensi walizopewa kwa makini ili waweze kufanya zoezi la kwanza ambapo wanatakiwa kuuliza maswali kwa kutumia kiulizi ***'je'***.

Kupitia mfano uliopo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua maneno ambayo hutumiwa kuulizia maswali ambayo ni: *nani, nini* na *je*. Ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wamepata ufahamu wa kutosha katika matumizi ya viulizi hivi, mwalimu awaombe wafanye zoezi la pili ambapo wanatakiwa kujaza nafasi zilizo wazi kwa jibu sahihi kutoka kwa yaliyo kwenye mabano. Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma maelezo muhimu yaliyo kwenye *Kitabu ca Mwanafunzi, ukurasa* 7 na kuyacunguza ipasavyo ili wapate muhtasari wa matumizi ya viulizi *nani* na *nini* katika sentensi.

### Tathmini ya kipindi ca 3

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali yake yacunguze uwezo wa wanafunzi wa kutumia kwa sahihi viulizi *nani* na *nini* kuulizia maswali mbalimbali. Ili kuwasaidia wanafunzi kuendeleza ujifunzaji wao hata na nje ya darasa lao, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kujibu zoezi la 1.5 katika sehemu ya sarufi. Zoezi hili litasahihishwa kabla ya kuanza somo la pili.

**Maelezo muhimu kwa mwalimu**

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kufahamu kuwa:

- ***Viulizi*** ni maneno ambayo hutumiwa kuulizia maswali.

**Kwa mfano:**

1. <u>Nani</u> alikubeba jana?
2. <u>Nini</u> kimekufurahisha?

- Neno ***nani*** huuliza kuhusu mtu aliyetenda kitendo fulani.
- Neno ***nini*** huuliza kuhusu kitu au jambo linalohusika.
- Maneno ***nani*** na ***nini*** hayaongezewi viambishi ngeli vyovyote.

### 1.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Kwa wanafunzi wenye kiwango ca cini katika ujifunzaji, mwalimu awaombe watunge sentensi kwa kutumia maneno au vifungu vya maneno vifuatavyo:

| | |
|---|---|
| 1. kuelekeza | 2. vivutio vya utalii |
| 3. kuzuru | 4. nini |
| 5. mtalii | 6. hoteli |
| 7. nani | 8. mbuga ya wanyama |
| 9. shilingi | 10. mazingira |
| 11. ramani | 12. sokwe watu |

***Kwa mfano:***

*Mtalii huyu anataka mtu wa <u>**kumwelekeza**</u> ili aweze kufika ofisini kwetu.*

### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga.

Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe maneno waliyopewa.

**ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka**

Kwa wanafunzi wenye kiwango ca juu ca uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe waandike masimulizi kuhusu vivutio vya utalii wanavyofahamu ncini Rwanda.

**Kwa mfano:**

*Mimi nimewahi kuzuru mbuga ya wanyama ya Akagera. Huko nilijionea wanyamapori wa kila aina wakiwemo simba, ndovu, pundamilia, swara, sungura pamoja na nyati. Nilifurahi sana.*

# 1.7 Majibu

**Zoezi la makundi, ukurasa 1**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti sentensi zihusiane na mcoro uliopo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 1.

**Kwa mfano:**

1. Mimi ninaona mtalii wa kizungu.
2. Mwelekezaji wa watalii anamwonyesha mtalii ramani ya vivutio vya utalii.
3. Ramani ya nci ya Rwanda iko ukutani.
4. Mimi ninaona watu wawili wakizungumza.

**Maswali ya ufahamu, ukurasa 3**

1. Mtalii anatoka Ujerumani. Yeye anataka kuzuru vivutio mbalimbali ncini.
2. Kuna mbuga za wanyama, mito, milima mizuri na nyumba za kuhifadhi utamaduni miongoni mwa vivutio vingine.
3. Mtalii atatembelea mazingira ya mbuga ya Akagera na maeneo yenye milima mirefu.
4. Wiki mbili ndio muda atakaoucukua Mtalii ncini Rwanda.
5. Mwelekezaji wa watalii ndiye anayemfafanulia mtalii kila jambo kuhusu (vivutio vya utalii) pamoja na kumwelezea wanyama walio mbugani.
6. Watu huingia katika mbuga za wanyama kuanzia saa moja na nusu asubuhi kisha hutoka saa kumi na mbili jioni.
7. Mtalii atatumia nambari za simu kupata huduma za hoteli pamoja na magari ya kutumia katika ziara yake.
8. Siku ambayo ingefuata asubuhi ndiyo Mtalii angeanza shughuli yake ya kuzuru maeneo mbalimbali.

9. Mtalii atatumia magari ya kulipia kusafiri kwenye mbuga za wanyama.
10. Cumba ca kulala, vinywaji, maakuli pamoja na starehe nyingine ndizo huduma zitolewazo na hoteli kwa Mtalii.

**Zoezi la 1.1A, ukurasa 3-4**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi, kwa mfano:

1. **mtalii:** mtu kutoka ndani au nje ya nci ambaye anatembea mahali kwa ajili ya kujifunza au kujifurahisha.
2. **yanavutia:** yanafurahisha, yanapendeza.
3. **kuzuru:** kutembea mahali fulani kwa ajili ya kujifurahisha au kujifunza.
4. **mbuga ya wanyama:** sehemu maalum zilizotengwa kwa ajili ya kuhifadhi wanyamapori.
5. **kivutio:** mahali, mtu au kitu cocote cenye uwezo wa kufanya watalii kwenda kukitazama.
6. **ziara:** shughuli ya kutembelea mahali fulani kwa ajili ya kujifunza au kujifurahisha.
7. **inatarajia:** inatumainia kupata
8. **wanyama wakali:** wanyama wenye uwezo wa kumdhuru binadamu
9. **kitalii:** -a kuhusishwa na shughuli za utalii
10. **mazingira:** eneo linalozunguka makazi ya mtu

**Zoezi 1.1B, ukurasa 4**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti sentensi ziwe sahihi na zenye kutumia msamiati uliopigiwa mistari katika zoezi la 1A.

**Kwa mfano:**

1. *Huyu ni **mtalii** kutoka Ujerumani.*
2. *Maeneo yenye milima **yanavutia**.*
3. *Tutaenda kuzuru **mbuga ya wanyama**.*
4. *Msitu huu ni **kivutio** kikuu kwa watalii.*
5. ***Ziara** ya mji mkuu itatufaa.*

**Zoezi la matumizi ya lugha, ukurasa 4-5**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi ili kuhakikisha wanalinganisha kwa usahihi pesa walizopewa na nci zinakotumika.

**Kwa mfano:**

| Pesa | Nci |
|---|---|
| 1. Faranga elfu tano | Rwanda |
| 2. Shilingi mia moja | Kenya |
| 3. Shilingi elfu moja | Uganda |
| 4. Shilingi mia tano | Tanzania |
| 5. Dola tano | Marekani |

**Zoezi la 1.2, ukurasa 5**

| Sarafu | | Nci |
|---|---|---|
| 1. Faranga | - | Rwanda |
| 2. Yeni | - | Japani |
| 3. Dola | - | Marekani |
| 4. Naira | - | Naijeria |
| 5. Shilingi ya Kenya | - | Kenya |

**Zoezi la 1.3, ukurasa 5**

1. Ubelgiji hutumia yuro ya Ulaya.
2. Uingereza hutumia pauni ya Uingereza.
3. Nci ya Kanada hutumia dola.
4. Nci ya Malawi hutumia kwaca.
5. Nci ya Afrika Kusini hutumia randi ya Afrika Kusini.

**Zoezi la utafiti, ukurasa 6**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi na fomula walizotumia kubadilisha pesa walizopewa.

**Kwa mfano:**

1. Dola hamsini za Marekani = Faranga elfu arubaini
2. Shilingi mia mbili za Uganda = Faranga arubaini na tano
3. Shilingi hamsini za Tanzania = Faranga kumi na nane
4. Yuro tano = Faranga elfu nne, mia tatu na sitini na tisa
5. Naira mia moja za Nijeria = Faranga mia mbili na sitini

**Zoezi la 1.4, ukurasa 6**

Mwalimu atathmini maswali watakayotunga wanafunzi. Sharti maswali yenyewe yahusishe matumizi ya '**je**' pamoja na sentensi walizopewa.

**Kwa mfano:**

1. *Je, ni nani atamaliza wiki mbili ncini Rwanda?*
2. *Je, ni nini kinavutia katika mazingira ya Akagera?*
3. *Je, ni nani aliyempa mtalii maelezo kuhusu hoteli ya kuishi?*
4. *Je, ni nani atarudi mwaka ujao kwa shughuli ya utalii?*
5. *Je, mtalii atalipa nini ili kuzuru mbuga ya wanyama?*

**Zoezi la 1.5, ukurasa 7**

1. Nani
2. Nani
3. Nini
4. Nini
5. Nani

**Zoezi la 1.6, ukurasa 7**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi na zihusishe matumizi ya viulizi '***nani'*** na '***nini'***.

**Kwa mfano:**

1. *Nani ataenda sokoni?*
2. *Nani amecukua kalamu ya mwalimu?*
3. *Nyumba hii ni ya nani?*
4. *Kanisa litasafishwa na nani?*
5. *Nani atatembea shambani?*
6. *Nini kitatumika kunywea maziwa?*
7. *Nini kimekukata kidole?*
8. *Mtoto atavishwa nini?*
9. *Karatasi hii ni ya nini?*
10. *Nini hutendeka sokoni?*

# Somo la 2: Mbuga za wanyama

## Kipindi cha 4: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati

### a) Malengo ya somo

- Kusoma kwa usahihi kifungu ca habari kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;
- Kubaini msamiati unaotumika katika mazingira ya mbuga za wanyama;
- Kutumia msamiati wa mbuga za wanyama katika sentensi sahihi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Ramani yenye kuonyesha mbuga mbalimbali za wanyama;
- Micoro ya watalii katika shughuli zao za utalii;
- *Kitabu ca Mwanafunzi,* ukurasa 8-12*;*
- Combo ca kunasia sauti, breli na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### c) Maandalizi ya somo

Katika maandalizi ya somo hili, mwalimu alenge kumsaidia mwanafunzi kubaini mbuga za wanyama zilizo ncini na wanyama mbalimbali wanaopatikana katika mbuga hizo. Kwa hivyo, mwalimu atafute vifaa vya kutosha kufundishia somo hili kama vile: micoro na pica za mbuga hizo pamoja na za wanyama mbalimbali wanaopatikana katika mbuga hizo. Mwalimu atumie ramani ya Rwanda ili kuonyesha maeneo ambapo mbuga hizo hupatikana. Aidha, mwalimu atafute namna ya kuwaelekeza wanafunzi kutambua umuhimu wa mbuga za wanyama, namna ya kuhifadhi na kutunza wanyama hao katika mazingira mazuri.

### d) Utaratibu wa somo

#### Utangulizi

Katika utangulizi, mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali kuhusu somo lililopita. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu aendelee kwa kuwashirikisha wanafunzi wote kusahihisha zoezi walilopewa katika somo lililopita.

Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi wawili wawili ili wacunguze na kujadiliana kuhusu pica zilizo katika *Kitabu ca*

*Mwanafunzi,* ukurasa 8. Mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamecunguza pica hizo kwa kuwauliza maswali mbalimbali. Kwa mfano: *Mnaona nini kwenye pica hizi?* Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kwa kueleza wanacokiona katika pica hizo. Kwa mfano: *"Mimi ninaona wanyama. Mimi ninaona ndege."* na kadhalika. Kupitia majibu ya wanafunzi, mwalimu acukue fursa ya kuuliza maswali mengine yanayowaelekeza kueleza mbuga za wanyama zilizopo na umuhimu wa mbuga hizo kwa wananci. Kwa mfano: *Wanyama hawa wako wapi? Nani amewahi kufika kwenye mbuga ya wanyama? Hii ni nini?* Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu. Kwa mfano: *Wanyama hawa wako msituni. Wanyama hawa wako katika mbuga zao. Hii ni milima.* na kadhalika. Kwa hivyo, katika sehemu hii ya utangulizi, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wake wanapata ujuzi, ubunifu na ugunduzi kwa kuwaonyesha micoro iliyopo huku akiwaomba kufikiria na kugundua kile kinacoendelea katika micoro hiyo.

### 2.1 Kusoma na ufahamu: Kifungu kuhusu mbuga za wanyama ncini Rwanda

Mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa kimya kifungu ca habari kilicopo huku wakiandika msamiati mpya wanaokutana nao. Wanafunzi wasome kwa kimya kama walivyoambiwa na mwalimu na pia waandike msamiati mpya ulio katika kifungu hico. Baadaye, mwalimu aendeleze somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu kifungu ca habari walicokisoma kwa lengo la kucunguza ikiwa wote wamesoma na kuelewa. Mwalimu awaulize, kwa mfano, maswali yafuatayo: *Rwanda inajitokeza wapi katika bara la Afrika? Ni mbuga zipi za wanyama zilizozungumziwa katika habari hii? Mbuga ya wanyama ya Akagera inapatikana wapi?* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika kifungu hico. Kwa mfano: *Rwanda inapatikana katikati mwa bara la Afrika. Mbuga za wanyama zilizozungumziwa katika habari hii ni mbuga ya wanyama ya Akagera, mbuga ya wanyama ya milima mirefu ya Virunga na mbuga ya wanyama ya msitu Nyungwe. Mbuga ya wanyama ya Akagera inapatikana katika sehemu za Kaskazini Mashariki mwa Rwanda.* Baada ya kumaizi kwamba wanafunzi wamesoma kwa kimya kifungu kilico na kukielewa, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa sauti na kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi. Wanafunzi wasome kwa sauti kama walivyoambiwa na mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa.

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kujibu maswali ya ufahamu katika makundi ya wanafunzi watatu watatu. Hatimaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali hayo huku akitoa maelezo yake kwa kutilia mkazo pale ambapo wanafunzi hutatizika.

## 2.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu mbuga za wanyama

Katika ujifunzaji wa msamiati, mwalimu awapange kwanza wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na awaombe watafute maana za msamiati mpya kwa kucunguza matumizi yake katika kifungu ca habari walicosoma. Ili kucocea wanafunzi kukuza stadi zao za utafiti, tafakuri tanduizi na usuluhishaji wa matatizo, mwalimu awaombe wanafunzi watumie kamusi pale wanapoihitaji na azunguke darasani ili kuwaelekeza wale wanaotatizika. Hali hii iendelezwe kwa kuwaambia wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wawili wawili ili kujibu zoezi la kwanza la sehemu hii ya msamiati. Wanafunzi wafanye zoezi hili na mwalimu awaombe kulisahihisha kwa pamoja mara tu wanapomaliza kujibu katika makundi yao.

Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi wacunguze micoro iliyo katika zoezi la pili kisha awaelekeze katika kuhusisha sentensi zilizopo na micoro hiyo. Baada ya wanafunzi hawa kukamilisha zoezi walilopewa, mwalimu awaombe kulisahihisha pia kwa pamoja. Katika kujibu maswali haya, mwalimu awaelekeze wanafunzi kupata ujuzi kuhusu mazingira ya kitalii yaliyopo na maelezo yake yagusie umuhimu wa mazingira ya aina hiyo kwa maisha ya wananci kwa jumla kama vile: kusaidia kupata hewa safi kwa afya ya watu na wanyama, kupata samaki wa aina tofauti, kusafiri, kupumzika, kuendeleza ucumi wa nci na kadhalika ili kuwawezesha kupata ujuzi wa utawala binafsi na stadi za maisha.

### Tathmini ya kipindi ca 4

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza katika somo hii. Maswali hayo yajikite katika kucunguza ikiwa wanafunzi wanaweza kutaja na kueleza msamiati mahususi kuhusu utalii uliopatikana katika kifungu ca habari walicokisoma. Pia, mwalimu acunguze iwapo wanafunzi wanaweza kutunga sentensi sahihi kwa kutumia msamiati waliojifunza.

- Kutaja aina za wanyama wanaopatikana katika mbuga za wanyama ncini;
- Kubaini mambo muhimu yanayozingatiwa wakati wa kufupisha kifungu ca habari;
- Kufupisha kifungu ca habari kwa kuzingatia urefu uliotakiwa.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Ramani yenye kuonyesha mbuga mbalimbali za wanyama;
- Pica za wanyama wanaopatikana katika mbuga mbalimbali;
- *Kitabu ca Mwanafunzi,* ukurasa 13*;*
- Combo ca kunasia sauti, breli na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Katika maandalizi ya somo hili, mwalimu alenge kumsaidia mwanafunzi kubaini mbuga za wanyama zilizo ncini na wanyama mbalimbali wanaopatikana katika mbuga hizo. Mwalimu atumie ramani ya Rwanda ili aweze kuonyesha maeneo ambapo mbuga hizo hupatikana. Aidha, mwalimu atafute namna ya kuelekeza wanafunzi kutambua umuhimu wa mbuga za wanyama, namna ya kuhifadhi na kutunza wanyama hao katika mazingira mazuri. Katika hali hii, micoro yenye kuonyesha faida za mbuga za wanyama kama vile: kufurahia kutazama mazingira ambapo wanyama hao hupatikana, kustarehe na kupumzika kwa watalii, nci kupata pesa za kigeni na kuweza kujiendeleza na kadhalika.

**d) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Katika utangulizi, mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali kuhusu somo lililopita. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu aendelee kwa kuwashirikisha wanafunzi wote kusahihisha zoezi walilopewa katika somo lililopita.

### 2.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano na kuandika ufupisho

Sehemu hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kuwasiliana kwa lugha rasmi na kupata ujuzi wa kutumia lugha kwa namna tofauti kwa kueleza au kufafanua

jambo husika. Kwa hivyo, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na awaombe wajadiliane kuhusu sifa za vivutio vya utalii vilivyozungumziwa katika kifungu ca habari walicokisoma na vivutio ambavyo wangependa kuvitembelea. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kuwaomba wacunguze maelezo yaliyo katika kifungu hico. Aidha, wanafunzi wajadiliane kwa kubainisha sifa za vivutio vya utalii vilivyojadiliwa katika kifungu ca habari na wacague vile ambavyo wangependa kutembelea huku wakitoa sababu za caguo lao. Katika kujibu swali hili, mwalimu agusie masuala mbalimbali kuhusu utamaduni wa kiusanifishaji ambapo caguo la kivutio ca utalii dhidi ya vingine litatolewa sababu zenye mashiko kulingana na vivutio vingine vinavyopatikana ncini. Kwa mfano, mwalimu anaweza kucunguza vigezo vya usafirishaji wa watalii, huduma zinazopatikana ili kumnufaisha mtalii kama vile: hoteli zilizo katika eneo fulani, na kadhalika. Vilevile, mwalimu awasaidie wanafunzi kutetea caguo lao kwa kudumisha ujuzi kuhusu utawala binafsi na stadi za maisha ambapo wanafunzi watabainisha faida mbalimbali wanazoweza kupata kutokana na caguo lao.

Zoezi la pili (2.3.1) la sehemu hii ya matumizi ya lugha linahusu kuwaelekeza wanafunzi kusoma tena kifungu ca habari walicokisoma hapo awali kwa kubaini mambo muhimu yaliyozungumziwa. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kufanya zoezi hili. Kwa mfano anaweza kuwaambia wanafunzi wasome tena kwa makini kifungu hico huku wakiorodhesha mambo muhimu yaliyozungumziwa katika kifungu hico. Wanafunzi wazingatie maelekezo ya mwalimu wao ili waweze kuandika kwa ufupi habari waliyoisoma kwa kutumia maneno yao wenyewe. Baadaye, mwalimu aombe kila kundi kucagua mwakilishi wao ambaye atajitokeza mbele ya wanafunzi wenzake na kuwasomea muhtasari wao. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote kutathmini ikiwa mambo yote muhimu yaliyozungumziwa katika kifungu ca habari yamejitokeza katika kila muhtasari ulioandaliwa na makundi ya wanafunzi. Mwishowe, mwalimu awaombe wanafunzi kucunguza maelezo muhimu kuhusu namna ya kuandika muhtasari kamili wa kifungu cocote ca habari kwa kuweka wazi hatua mbalimbali zinazozingatiwa katika shughuli hii.

## 2.4 Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano

Katika hatua ya kusikiliza na kuzungumza, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili. Wanafunzi nao wajigawe katika makundi hayo na mwalimu awafafanulie namna ya kufanya zoezi husika. Mwalimu

awaombe wanafunzi wajadiliane na kuandika mambo muhimu waliyojifunza kuhusu mbuga za wanyama zinazopatikana ncini Rwanda. Katika hatua hii mwalimu alenge kuwasaidia wanafunzi kueleza mambo muhimu kwa ufupi miongoni mwa mambo mengi waliyokutana nayo kama mwendelezo wa ujuzi waliopata katika ujifunzaji wa ufupisho au muhtasari.

Baadaye, kila kundi lijitokeze mbele ya wanafunzi wenzao na kuwasomea maelezo waliyoyaandika. Mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wanagusia mambo muhimu waliyojifunza kuhusiana na mbuga za wanyama na acunguze ikiwa wanatamka kwa usahihi silabi, maneno na sentensi wanazotumia katika maelezo yao. Mwalimu asahihishe makosa ya wanafunzi pale yanapojitokeza ili kuimarisha mawasiliano yao kwa lugha rasmi.

**Tathmini ya kipindi ca 5**

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza katika kipindi hiki. Maswali hayo yajikite katika kucunguza ikiwa wanafunzi wanaweza kutaja mbuga za wanyama zinazopatikana ncini, wanyama wanaopatikana katika mbuga hizo, umuhimu wa kutunza wanyama hao na hata umuhimu wa mbuga za wanyama kwa taifa.

## Kipindi cha 6: Sarufi (Kiulizi 'lini')

**a) Malengo ya somo**

- Kubaini matumizi ya kiulizi ***lini*** katika sentensi sahihi;
- Kutumia kiulizi ***lini*** kuulizia maswali mbalimbali.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Ramani yenye kuonyesha vivutio mbalimbali vya utalii;
- Wanafunzi wenyewe;
- Micoro ya watalii katika shughuli zao za kiutalii;
- *Kitabu ca Mwanafunzi,* ukurasa 14-15*;*
- Combo ca kunasia sauti, breli na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Katika maandalizi ya somo hili, mwalimu alenge kumsaidia mwanafunzi kubaini matumizi ya kiulizi ***lini*** katika maongezi na katika utungaji wa sentensi sahihi. Kwa hivyo, mwalimu atafute vifaa vya kutosha kufundishia somo hili kama vile

micoro ya watalii katika shughuli zao za utalii. Ili kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wote, mwalimu afikirie wakati mwafaka wa kuonyesha vifaa hadharani na kuwatumia wanafunzi wenyewe kuelewa somo hili.

### d) Utaratibu wa somo

### Utangulizi

Katika utangulizi, mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali kuhusu kipindi kilicopita kuhusu sarufi ya viulizi ***nini*** na ***nani***. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu aendelee kwa kuwashirikisha wanafunzi wote kusahihisha zoezi walilopewa katika kipindi kilicopita.

## 2.5 Sarufi: Kiulizi 'lini'

Ujifunzaji wa sarufi katika somo hili uzingatie matumizi ya kiulizi ***lini***. Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wawili wawili na kucunguza sentensi zilizo katika umoja na wingi. Wanafunzi wajigawe katika makundi hayo kama walivyoelekezwa na mwalimu wao na wacunguze sentensi hizo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika ucunguzi wao kwa kutilia mkazo matumizi ya kiulizi 'lini' kinacorudiwarudiwa katika kila sentensi kwa kubainisha kuwa kiulizi hiki hakibadiliki katika umoja na katika wingi. Pia, ni wazi kuwa kiulizi hiki hakiongezewi viambishi ngeli vyovyote. Kwa mfano: ***Lini*** *utakuja kwangu? - **Lini** mtakuja kwetu?*

Kwa hivyo, mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kutambua aina ya neno lililopigiwa mstari katika sentensi walizopewa, wajadili mabadiliko ya sentensi hizo katika umoja na wingi kisha watunge sentensi sahihi kwa kutumia kiulizi 'lini'.

Kupitia ucunguzi wa sentensi hizi, mwalimu acocee ubunifu na ugunduzi wa wanafunzi kwa kuwaomba kufanya zoezi la kwanza katika sehemu hii ambapo watatambua matumizi ya kiulizi 'lini' kwa kukitungia sentensi mbalimbali. Katika zoezi la 4, wanafunzi waelekezwe kujaza nafasi zilizo wazi katika sentensi walizopewa kwa kutumia jibu sahihi kutoka kwenye mabano.

Ili kufanikisha ujifunzaji wa kipengele hiki ca sarufi, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma maelezo muhimu yaliyo katika *Kitabu ca Mwanafunzi,* ukurasa 15 hatua kwa hatua huku akiwauliza maswali yanayowasaidia kuelewa kwa namna inayofaa matumizi ya kiulizi 'lini'. Kwa hivyo, mwalimu awaelekeze

wanafunzi kujibu zoezi la 2.5. Ni vyema zoezi hili lisahihishwe kwa kuwashirikisha wanafunzi wote.

### Tathmini ya kipindi ca 6

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kwa lengo la kucunguza iwapo wameelewa matumizi ya kiulizi '***lini***' katika maongezi, sentensi na kuulizia maswali.

Ili kuwasaidia wanafunzi kuendeleza ujifunzaji wao hata nje ya darasa lao, mwalimu awaelekeze wanafunzi namna ya kujibu zoezi la 2.6 la sarufi na kuwaomba walifanye kama kazi ya nje ya darasa. Zoezi hili litasahihishwa kabla ya kipindi ca 7.

**Maelezo muhimu kwa mwalimu**

- Kabla ya kuandika ufupisho au muhtasari ni vyema wanafunzi:

1. Wasome kwa makini kifungu kilichopo na kuandika mawazo muhimu. Wasome mara tatu ili kuelewa vizuri.
2. Wajibu maswali haya:
   - Kifungu cha habari kinahusu nini? (Waandike sentensi moja).
   - Kifungu hiki kina aya ngapi? (Watambue aya zinazojenga kifungu hiki).
   - Waandike wazo moja kutoka kwa kila aya.
3. Waunganishe mawazo waliyoorodhesha na kuandika habari kamili. Ili waandike vizuri ni vyema:
   - Watumie maneno yao wenyewe (wasitumie maneno na sentensi zilizotumiwa katika kifungu cha habari walichokisoma).
   - Watoe maelezo bila kupotosha ujumbe asilia.
   - Wahakikishe kuwa wamerejelea mawazo yote muhimu yanayopatikana katika kifungu cha habari walichokisoma.
   - Wahakikishe kuwa hakuna makosa ya kisarufi.
   - Wahakikishe kwamba wamezingatia urefu unaofaa.
   - Wazingatie matumizi ya alama za uandishi.

Habari hiyo waliyoandika wanafunzi kwa kuzingatia maelekezo hayo hapo juu ni **muhtasari** au **ufupisho** wa habari asilia waliyosoma. Neno '***ufupisho***' linatokana na kitenzi '***fupisha'*** lenye maana ya 'kufanya maelezo kuwa mafupi au kupunguza urefu wake'.

- Neno '***lini***' ni kiulizi cha wakati. Hutumika katika sentensi kuulizia wakati wa kutendeka kwa kitendo fulani.

  ***Kwa mfano:*** Utapanda mahindi ***lini?***

  ***Jibu:*** ***Wiki ijayo.***

  Jibu linalotolewa kwa sentensi iliyo na neno '***lini***' linaonyesha majira mbalimbali ya wakati kama vile: *majira ya siku, saa, siku, wiki, mwezi, mwaka* n.k.

## 2.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Kwa wanafunzi wasioweza kuelewa haraka, mwalimu awape zoezi la ziada lifuatalo ambalo linalenga kuinua kiwango cao ca ujifunzaji.

*Andika wingi au umoja wa sentensi hizi.*

**Kwa mfano:**

**Wingi:** Lini mtakuja kututembelea?

**Umoja:** Lini utakuja kunitembelea?

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. ____________ | Lini mtaondoka kuelekea mashambani? |
| 2. Lini alianza kufanya kazi mjini? | ____________ |
| 3. ____________ | Lini milango iliyonunuliwa iliharibika? |
| 4. Lini kisu kiliconolewa kilipotea? | ____________ |
| 5. ____________ | Lini wazazi waliandikiwa barua na walimu wetu? |

| **Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu** | |
|---|---|
| **Umoja** | **Wingi** |
| 1. *Lini utaondoka kuelekea shambani?* | Lini mtaondoka kuelekea mashambani? |
| 2. Lini alianza kufanya kazi mjini? | *Lini walianza kufanya kazi mijini?* |
| 3. *Lini mlango ulionunuliwa uliharibika?* | Lini milango iliyonunuliwa iliharibika? |
| 4. Lini kisu kiliconolewa kilipotea? | *Lini visu vilivyonolewa vilipotea?* |
| 5. *Lini mzazi aliandikiwa barua na mwalimu wangu?* | Lini wazazi waliandikiwa barua na walimu wetu? |

**ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka**

Kwa wanafunzi wenye kiwango ca juu ca uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe waeleze faida za mbuga za wanyama kwa taifa la Rwanda.

**Kwa mfano:**

*Mbuga za wanyama ni muhimu kwa sababu huhifadhi wanyamapori dhidi ya wawindaji haramu. Wanyamapori hawa huwavutia watalii wengi ambao huja kuwatazama na hivyo kulipatia taifa letu pesa za kigeni na hatimaye kuimarisha ucumi wetu.*

## 2.7 Majibu

**Zoezi la makundi, ukurasa 8**

Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi kwa kurejelea micoro iliyopo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 8.

**Kwa mfano:**

*Micoro hii inaonyesha wanyamapori ambao hupatikana katika mbuga ya Akagera, aina mbalimbali za ndege ambao hupatikana katika msitu wa Nyungwe pamoja na milima ya Virunga na sokwe watu wapatikanao huko.*

**Maswali ya ufahamu, ukurasa 10**

1. Nci ya Rwanda inapatikana katikati ya bara la Afrika.
2. Mito mbalimbali, mbuga za wanyama, misitu ya kiasili, hoteli nzuri, maziwa,

milima mirefu na nyumba za kuhifadhia vifaa vya utamaduni ni vivutio vya utalii ncini Rwanda.

3. Pundamilia, swara, paa, twiga, tembo, vifaru na simba ni baadhi ya wanyama katika mbuga ya Akagera.
4. Mbuga ya Akagera ina mandhari ya kipekee: savana ya kupendeza watu wengi, sehemu kubwa ya majimaji yenye mto mkubwa wa Akagera, maziwa mengi na visiwa mbalimbali.
5. Kaskazini Magharibi mwa Rwanda kuanzia kwenye mpaka wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo hadi mpaka wa Rwanda na Jamhuri ya Uganda ndiko mbuga ya wanyama ya milima mirefu inakopatikana. Milima mirefu minne ni: Kalisimbi, Muhabura, Bisoke, Sabyinyo, Nyamuragira na Nyiragongo.
6. Wanyama wanaoitwa 'sokwe mtu' ndio huipa mbuga hiyo sifa.
   Watu wengi hupenda kuwatazama wanyama hawa kutokana na maumbile yao na tabia zao zinazofanana na za binadamu.
7. Sikukuu ya kuwapa watoto wao majina hufanyika kila mwaka.
8. Mbuga ya wanyama ya msitu wa Nyungwe unajulikana kwa miti yake ya aina mbalimbali pamoja na aina nyingi za ndege wasiopatikana mahali pengi ulimwenguni.
9. Fedha nyingi za kigeni ambazo huendeleza ucumi wa nci ni faida ipatikanayo kutokana na shughuli ya utalii.
10. Vitendo vya kuwinda, kuwaua wanyamapori kiharamu na kufanya biashara za magendo za kuuza pembe za tembo baada ya kuwaua ni mambo yanayostahili kukomeshwa.

**Zoezi la 2.1, ukurasa 11**

1. - I
2. - D
3. - F
4. - J
5. - H
6. - G
7. - C
8. - E
9. - B
10. - A

**Zoezi la 2.2, ukurasa 12**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi kwa kuhakikisha kuwa wanahusisha pica walizopewa na sentensi walizopewa kwa usahihi. Yaani:

1. - C
2. - E
3. - D
4. - A
5. - B

**Zoezi la muhtasari, ukurasa 13**

Mwalimu atathmini muhtasari ambao wanafunzi wataandika. Sharti muhtasari huo uhusishe kifungu ca habari walicokisoma hapo awali. Maneno yasiyozidi mia moja yatumike kwa usahihi. Sarufi iwe sahihi.

**Kwa mfano:**

*Ncini Rwanda kuna sehemu nyingi za kuzuru. Watalii wengi hufurahia maeneo kama vile: mbuga za wanyama, maziwa, milima, nyumba za kuhifadhia vifaa vya utamaduni na misitu. Katika mbuga za wanyama, kuna wanyama wengi kama vile: twiga, pundamilia, swara, simba na vifaru. Mbuga ya wanyama ya milima mirefu ya Virunga ndiyo huwavutia watalii kutoka katika mataifa mengi zaidi. Hii ni mbuga yenye wanyama wengi waitwao 'sokwe mtu' ambao wanapenda mahali penye milima mirefu. Kunao Wanyarwanda ambao huwinda, kuua wanyamapori na kufanya biashara za magendo kwa kuuza pembe za ndovu baada ya kuwaua. Jambo hili limesababisha wito kutolewa ili kukomesha shughuli za aina hii.*

**Zoezi la 2.3, ukurasa 14**

1. Ni kiulizi
2. Hakuna mabadiliko katika umoja na wingi wa kiulizi 'lini'.
3. Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga kwa kutumia kiulizi 'lini'. **Kwa mfano:**
   a) *Utanitembelea lini?*
   b) *Watalii watazuru mbuga ya wanyama lini?*

**Zoezi la 2.4, ukurasa 15**

1. lini
2. lini
3. lini
4. lini
5. lini

**Zoezi la 2.5, ukurasa 15**

1. Nani alizuru mbuga ya wanyama?
2. Nini kitaliwa?
3. Watalii kutoka Marekani watafika lini?
4. Nani atawapeleka watalii mjini Kigali?
5. Nini kitanunuliwa sokoni?

**Zoezi la 2.6, ukurasa 15**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi atatunga kwa kutumia kiulizi 'lini' katika umoja na wingi. Sharti sentensi hizi ziwe sahihi. **Kwa mfano:**

1. *Mtoto atakuja lini?* – *Watoto watakuja lini?*
2. *Lini utasafiri?* – *Lini mtasafiri?*
3. *Mnyama atalishwa lini?* – *Wanyama watalishwa lini?*
4. *Kiatu hiki kitashonwa lini?* – *Viatu hivi vitashonwa lini?*
5. *Mwalimu alienda lini?* – *Walimu walienda lini?*

# Somo la 3: Mwelekezaji na Mtalii

## Kipindi cha 7: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati

### a) Malengo ya somo

- Kusoma kwa usahihi kifungu ca mazungumzo kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;
- Kubaini msamiati unaotumika katika mazingira ya utalii;
- Kutumia msamiati wa mazingira ya utalii katika sentensi;
- Kuwasiliana na mtalii kwa kumwelekeza katika shughuli zake za utalii.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Micoro ya watalii katika shughuli zao za kiutalii;
- Pica za wanyama wanaopatikana katika mbuga zao;
- Micoro ya vifaa tofauti vinavyotumiwa na watalii kama vile: gari la kiutalii, kamera, na vingine;
- *Kitabu ca Mwanafunzi,* ukurasa 16-20*;*
- Combo ca kunasia sauti, breli na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### c) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu mazungumzo au mawasiliano kati ya Mwelekezaji na Mtalii. Kwa hivyo, lengo la kwanza la mwalimu katika somo hili ni kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu mawasiliano na mgeni; hasa katika mazingira ya utalii kwa kuleta pica au micoro inayoweza kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi kufahamu mambo muhimu ambayo watalii hufaa kuuliza ili waweze kujiandaa vizuri katika mawasiliano yao na wageni kwa kutumia lugha rasmi.

Mwalimu alete vifaa mbalimbali vya kujifunzia somo hili ili aweze kuwaelekeza wanafunzi kwa namna inayofaa. Katika hali hii, ni vyema pia mwalimu azingatie wakati unaofaa wa kuonyesha vifaa hivyo hadharani ili wanafunzi waweze kupata ufahamu unaotarajiwa kwa muda unaotakikana. Ikiwa kuna wanafunzi wasioweza kuona, ni lazima mwalimu atumie vifaa hivyo kwa kuwaomba wao wenyewe kuvigusa huku wakitaja majina ya vifaa vyenyewe. Pengine, maelezo yanaweza kuandikwa ubaoni kwa lengo la kuwasaidia wanafunzi wenye

matatizo ya kuelewa haraka au wale wasioweza kusikia. Katika somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamejigawa katika makundi ya idadi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila zoezi linalohusika.

### d) Utaratibu wa somo

### Utangulizi

Katika ufunguzi wa somo hili, mwalimu awaamkie wanafunzi na awaulize maswali mbalimbali kuhusu somo lililopita. Wanafunzi nao, kwa upande wao, wajibu maamkizi ya mwalimu wao na maswali mengine waliyoulizwa. Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi wasahihishe zoezi walilopewa katika somo lililopita ili aweze kuendelea na somo jipya. Wanafunzi wasahihishe zoezi hilo. Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu ili wacunguze mcoro ulio katika *Kitabu ca Mwanafunzi,* ukurasa 16. Wanafunzi wacunguze mcoro huo kwa kuandika sentensi mbalimbali zinazoonyesha kuwa wamefanya ucunguzi wao. Mwalimu azunguke darasani kuhakikisha kuwa wanafunzi wanajadiliana na kuandika sentensi za kuelezea kile wanacokiona katika mcoro huo. Mwalimu awaombe wanafunzi wajitokeze mbele ya darasa ili wawaelezee wenzao mambo muhimu waliyoyapata kutokana na micoro uliopo. Mwalimu acukue fursa hii kuwaelekeza wanafunzi kutafakari na kugundua kile kinacofanywa na wahusika waliocorwa huku akihakikisha kuwa wanafunzi wanapata ujuzi ainasafu kuhusu usawa wa kijinsia, elimu ya pamoja, mazingira kwa kuhusisha micoro ya wanawake, wanaume na hata ya walemavu wanaoshiriki katika shughuli za kiutalii.

### 3.1 Kusoma na ufahamu: Mazungumzo kati ya Mwelekezaji na Mtalii

Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa kimya kifungu ca mazungumzo kinacohusika huku wakiandika msamiati mpya wanaokutana nao. Wanafunzi wasome kwa kimya pamoja na kuandika msamiati huo mpya. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wamesoma kwa kimya kama walivyoambiwa, mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu kifungu hico ca habari. Kwa mfano: *Mtalii alifurahishwa na nini tangu afike ncini Rwanda? Waharibifu hufanya nini?* na kadhalika. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kuonyesha kuwa wamesoma na kuelewa kifungu hico. Kwa mfano: *Mtalii alifurahishwa na huduma nzuri aliyopewa. Mtalii alifurahishwa na usafi. Waharibifu huwinda wanyama na kuwaua.* Baada ya kupata pica ya uelewa wa jumla wa wanafunzi kuhusu kifungu hico ca habari, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa sauti na kwa usahihi kifungu

ca mazungumzo kati ya Mtalii na Mwelekezaji nao wanafunzi wasome kwa sauti kama walivyoambiwa na mwalimu wao. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kusoma kwa lengo la kutambua herufi, silabi na sentensi zilizopo na hata kwa kuzingatia matumizi ya alama na vituo vilivyopo kama vile: nukta, alama ya mshangao, alama ya kuuliza na kadhalika.

Baada ya kusoma, mwalimu awaombe wanafunzi wajibu maswali ya ufahamu yaliyotolewa kwenye *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 18. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote ili wasahihishe maswali hayo. Mwalimu atoe maelezo yake kwa kutilia mkazo pale ambapo wanafunzi wanatatizika kwa kucocea ujuzi wa wanafunzi kuhusu tafakuri tanduizi, usuluhishaji wa matatizo, mawasiliano katika lugha rasmi, ushirikiano, utawala binafsi na hata stadi za maisha kupitia maswali waliyopewa katika sehemu hii ya ufahamu.

### 3.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu ziara ya kitalii

Ujifunzaji wa msamiati katika hatua hii ufanywe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu ambapo watajadiliana kuhusu msamiati mpya waliokutana nao wakati wao wa kusoma kifungu husika. Mwalimu awaombe wanafunzi watafute maana za msamiati huo kwa kurejelea matumizi yake katika kifungu ca mazungumzo walicokisoma huku wakicunguza maana yake katika kamusi. Wanafunzi nao wajadiliane kama walivyoelekezwa na mwalimu naye mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi pale wanapotatizika. Baadaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi kufanya zoezi la 3.1 la msamiati kwa kuwafafanulia kile kinacotakiwa kutimizwa katika zoezi hilo. Wanafunzi wafanye zoezi hilo kama walivyoelekezwa na mwalimu. Mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika huku akilenga waelewe maana ya msamiati husika.

Katika zoezi la 3.2, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kuhusisha micoro waliyopewa pamoja na sentensi zilizopo. Kupitia zoezi hili, wanafunzi wanatarajiwa kupata ufahamu wa kutunza wanyama kwa kugusia waharibifu wa mazingira wanaowasaka na kuwawinda wanyama ili kuwaua. Madhara yanayoweza kujitokeza yabainishwe katika zoezi hili na adhabu wanazopata waharibifu hao. Mwalimu awaombe wanafunzi kuendelea na makundi yao ya wanafunzi wawili wawili ili wacunguze na kujadiliana kuhusu maana za sentensi walizopewa.

### Tathmini ya kipindi ca 7

Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamepata ujuzi kuhusu mambo muhimu waliyojifunza katika kipindi hiki. Mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu huduma inayotolewa kwa mtalii wakati wa kumwelekeza kupata habari za kiutalii na katika shughuli yake ya kiutalii. Kwa mfano, awaulize maswali kuhusiana na mienendo ya mtalii na vitu kadhaa vinavyoweza kuwavutia watalii na faida zinazoweza kupatikana katika kuwaelekeza watalii vizuri.

Mwalimu pia awaulize wanafunzi maswali kuhusiana na msamiati waliojifunza kuhusiana na ziara ya kiutalii katika kipindi hiki pamoja na namna ya kuutumia msamiati huo katika maongezi yao na katika kutunga sentensi sahihi.

## Kipindi cha 8: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza

### a) Malengo ya somo

- Kutaja majina ya wanyamapori mbalimbali;
- Kutambua wanyamapori mbalimbali katika micoro au pica;
- Kuigiza mawasiliano kati ya Mwelekezaji na Mtalii kwa lugha rasmi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Pica za wanyamapori wanaopatikana katika mbuga zao;
- *Kitabu ca Mwanafunzi,* ukurasa 20-21*;*
- Wanafunzi wenyewe;
- Combo ca kunasia sauti, breli na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### c) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu wanyamapori mbalimbali, majina yao pamoja na umuhimu wao kwa binadamu na taifa kwa jumla. Aidha, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi kutazama micoro au pica mbalimbali za wanyamapori mbalimbali na kuwataja kwa majina yao.

Katika hali hii, ni vyema pia mwalimu azingatie wakati unaofaa wa kuonyesha pica au micoro ya wanyamapori ili wanafunzi waweze kupata ufahamu unaotarajiwa kwa muda unaotakikana. Ikiwa kuna wanafunzi wasioweza kuona ni lazima mwalimu awe amecora micoro hiyo kwenye breli na kuwaomba wao wenyewe

kuvigusa huku wakitaja majina ya yao. Pengine, maelezo yanaweza kuandikwa ubaoni kwa lengo la kuwasaidia wanafunzi wenye matatizo ya kuelewa haraka au wale wasioweza kusikia. Katika somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamejigawa katika makundi ya idadi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila zoezi linalohusika.

### d) Utaratibu wa somo

### Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi na awaulize maswali mbalimbali kuhusu kipindi kilicopita. Wanafunzi nao, kwa upande wao, wajibu maamkizi ya mwalimu wao na maswali mengine waliyoulizwa. Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi wasahihishe zoezi walilopewa katika kipindi kilicopita. Wanafunzi wasahihishe zoezi hilo.

### 3.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha wajadiliane kuhusu wanyamapori ambao wamewahi kuwaona. Wanafunzi waelezane kuhusu:

1. *Majina ya wanyamapori hao.*
2. *Sifa za wanyamapori hao.*
3. *Cakula ca wanyamapori hao.*
4. *Maumbile ya wanyamapori hao.*
5. *Waliwaona wanyama hao wapi?*
6. *Wanyamapori hao wanapenda kuishi katika mazingira ya aina gani?*

Baada ya wanafunzi kujadiliana katika makundi yao, mwalimu anaweza kuwaomba wanafunzi wacace kusimama mbele ya wanafunzi wengine na kuwaeleza waliyojadiliana. Mwalimu ahakikishe kuwa anakosoa makosa yoyote ya kimatamshi pindi yanapotokea. Katika zoezi la 3.3, mwalimu awaelekeze wanafunzi kucunguza micoro ya wanyama mbalimbali iliyo katika *Kitabu ca Mwanafunzi* ukurasa 20-21 kisha wabainishe wanyama wanaofugwa na wanyama wasiofugwa. Majadiliano haya ya makundi yahakikishe kwamba wanafunzi wamepata ujuzi kuhusu mawasiliano katika lugha rasmi.

### 3.4 Kusikiliza na kuzungumza: Maigizo

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kusoma kwa usahihi na kwa utambuzi wa herufi, silabi, neno na sentensi katika kifungu ca mazungumzo kinacohusika. Baadaye, mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili

wawili ambapo mwanafunzi wa kwanza atacukua nafasi ya Mwelekezaji na wa pili nafasi ya Mtalii. Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi hawa wajitokeze mbele ya wanafunzi wenzao ili kuigiza mazungumzo waliyoyasoma kati ya Mwelekezaji na Mtalii. Ni vyema mwalimu asahihishe makosa ya kimatamshi mara tu yanapojitokeza ili kuwazoesha wanafunzi kutamka na kuzungumza kwa usahihi.

### Tathmini ya kipindi ca 8

Mwalimu atambue iwapo malengo ya ufundishaji yametimizwa kwa kiwango kilicotarajiwa. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamepata ujuzi kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Awaulize maswali mbalimbali kuhusu kutaja majina na umuhimu wa wanyama wanaofugwa na wanyama wasiofugwa. Wanafunzi wataje majina na watoe maelezo kuhusu wanyama hao. Maswali mengine yalenge kuwasaidia wanafunzi kupata ujuzi wa kuwasiliana kwa lugha rasmi, ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha kupitia maigizo waliyoyafanya. Aidha, namna ya kutunza mazingira na wanyama nayo igusiwe katika sehemu hii.

## Kipindi cha 9: Sarufi (Kiulizi 'wapi')

### a) Malengo ya somo

- Kubaini matumizi ya viulizi ***wapi, vipi*** na ***kwa nini*** katika sentensi sahihi;
- Kutumia viulizi ***wapi, vipi*** na ***kwa nini*** kuulizia maswali mbalimbali.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Micoro au pica za wanyamapori mbalimbali;
- Ramani ya maeneo mbalimbali yanayowavutia watalii;
- Wanafunzi wenyewe;
- Micoro ya watalii katika shughuli zao za kiutalii,
- *Kitabu ca Mwanafunzi,* ukurasa 21-24*;*
- Combo ca kunasia sauti, breli na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### c) Maandalizi ya somo

Katika maandalizi ya somo hili, mwalimu alenge kumsaidia mwanafunzi kubaini

matumizi ya viulizi ***wapi, vipi*** na ***kwa nini*** katika maongezi na katika utungaji wa sentensi sahihi. Kwa hivyo, mwalimu atafute vifaa vya kutosha kufundishia somo hili kama vile: micoro ya watalii katika shughuli zao za utalii, micoro au pica za wanyamapori mbalimbali na ramani yenye kuonyesha maeneo mbalimbali ya kuwavutia watalii. Ili kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wote, mwalimu afikirie wakati mwafaka wa kuonyesha vifaa hadharani na kuwatumia wanafunzi wenyewe kuelewa somo hili.

### d) Utaratibu wa somo

#### Utangulizi

Katika utangulizi, mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali kuhusu kipindi kilicopita kuhusu sarufi ya kiulizi ***lini***. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu aendelee kwa kuwashirikisha wanafunzi wote kusahihisha zoezi walilopewa katika kipindi kilicopita.

### 3.5 Sarufi

#### Viulizi 'wapi' na 'vipi'

Katika hatua hii ya ujifunzaji wa sarufi, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha awaombe wanafunzi wacunguze sentensi walizopewa pamoja na maswali yaliyo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 21 kwa kutilia mkazo matumizi ya viulizi ***wapi*** na ***vipi***. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kufahamu namna ya kugeuza sentensi zinazotaja mahali fulani au namna ya kufanya jambo fulani na kuwa maswali yanayotumia viulizi ***wapi*** na ***vipi***. Kwa hivyo, mwalimu awaombe wanafunzi wacunguze kila sentensi iliyopo huku wakisaidiwa kutambua namna ya kuigeuza na kuwa maswali yenye viulizi ***wapi*** na ***vipi.*** Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua matumizi ya viulizi ***wapi*** na ***vipi*** katika maongezi na kutunga sentensi sahihi.

Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kufanya zoezi la 3.4 na zoezi la 3.5 ambapo wanafunzi wanahitajika kutunga sentensi kwa kutumia viulizi ***wapi*** na ***vipi***.

Vilevile, mwalimu awaombe wanafunzi kufanya zoezi la 3.6 na zoezi la 3.7 ili kuthibitisha kwamba wameshapata ufahamu wa kutosha katika kipengele hiki ca kisarufi.

### 3.5.1 Kiulizi 'kwa nini'

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili

kisha awaombe wacunguze sentensi walizopewa pamoja na maswali yaliyo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 23 kwa kutilia mkazo matumizi ya kiulizi ***kwa nini***. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kufahamu namna ya kugeuza sentensi zinazotaja sababu ya kufanya jambo fulani na kuwa maswali yanayotumia kiulizi ***kwa nini***.

Kwa hivyo, mwalimu awaombe wanafunzi wacunguze kila sentensi iliyopo huku wakisaidiwa kutambua namna ya kuigeuza na kuwa maswali yenye kiulizi ***kwa nini.*** Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua matumizi ya kiulizi ***kwa nini*** katika maongezi na kutunga sentensi sahihi.

Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kufanya zoezi la 3.8 ambapo wanafunzi wanahitajika kutunga sentensi kwa kutumia kiulizi ***kwa nini***.

### Tathmini ya kipindi ca 9

Mwalimu acunguze iwapo malengo yake ya kufundisha sarufi kuhusu viulizi '***wapi***', '***vipi***' na '***kwa nini***'' yametimizwa.

**Maelezo muhimu kwa mwalimu**

Maneno ***wapi*** na ***vipi*** yanaitwa ***viulizi***.

- Kiulizi ***wapi*** kinatumiwa kuulizia swali kuhusu ***mahali***.
- Kiulizi ***vipi*** kinatumiwa kuulizia swali kuhusu ***namna***.

  **Kwa mfano:**
  - Sentensi: Watalii walizuru ***mji wa Kigali***.
  - Swali: Watalii walizuru ***wapi***?
  - Sentensi: Viongozi walisafiri na kufika ***salama***.
  - Swali: Viongozi walisafiri na kufika ***vipi***?

Maneno ***'kwa nini'*** linatumiwa kuulizia ***sababu ya kufanyika kwa jambo fulani.***

**Kwa mfano:**

- **Sentensi 1:** *Mwanafunzi huyu alipewa zawadi kwa sababu alifaulu katika mtihani wake.*
- **Swali:** ***Kwa nini*** mwanafunzi huyu alipewa zawadi? *(Neno **'kwa nini'** limetumiwa kuulizia sababu ya kupewa zawadi kwa mwanafunzi huyu).*
- **Sentensi 2:** *Waelekezaji walipewa mafundisho ili wajue namna ya kuwaelekeza watalii.*
- **Swali:** ***Kwa nini*** waelekezaji walipewa mafundisho? *(Neno **'kwa nini'** limetumiwa kuulizia sababu ya waelekezaji kupewa mafundisho).*

### 3.6 Mazoezi ya ziada

#### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Ili kufanikisha ujifunzaji wa pamoja, zoezi la ziada litolewe kwa wanafunzi wa kiwango ca cini katika ujifunzaji wao. Kwa hivyo, mwalimu awaombe wanafunzi hawa kujibu maswali haya:

*Tunga sentensi mbili mbili zenye maswali yanayotumia kiulizi 'wapi'. (Andika sentensi na swali lake.)*

**Kwa mfano:**

***Sentensi:*** *Mama alienda sokoni.*

***Swali:*** *Mama alienda **wapi**?*

#### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atathmini sentensi pamoja na maswali ambayo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe kiulizi 'wapi'. Kwa mfano:

1. ***Sentensi:*** *Wewe ulizuru mbuga ya wanyama.*
   ***Swali:*** *Wewe ulizuru wapi?*
2. ***Sentensi:*** *Simba amelala cini ya mti.*
   ***Swali:*** *Simba amelala wapi?*

#### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango ca juu ca uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe waeleze faida za wanyamapori watano na mifugo watano.

**Kwa mfano:**

a) Simba huvutia watalii hivyo kutupatia fedha za kigeni.

b) Ng'ombe hutupatia maziwa, nyama, ngozi pamoja na pembe.

## 3.7 Majibu

#### Zoezi la makundi, ukurasa 16

Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi kwa kurejelea mcoro uliopo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 16.

**Kwa mfano:**

*Mimi ninaona mtalii na mwelekezaji mmoja wakiwa kwenye gari la kiutalii. Pia, ninawaona ndovu, pundamilia, sungura, simba na swara wakiwa mbugani.*

**Maswali ya ufahamu, ukurasa 18**

1. Kwa sababu kuna miti mingi hivyo kuna hewa safi, vicaka hapa na pale na savana ya kuvutia.
2. Huduma nzuri aliyopata, usafi uliopo, hewa nzuri na mazingira ya mbuga za wanyama.
3. Siku iliyokuwa imepita.
4. Baada ya wiki mbili
5. Ndovu, pundamilia, paa, simba, kware, sungura na wengine
6. Ni mpole
7. Sungura na kware hupenda kujifica sana.
8. Mwelekezaji aliwabembeleza.
   Aliwanyemelea na kuwaelekeza kwenye sehemu nyingine ili waonekane.
9. Wakiona mtu aliyebeba silaha.
10. Huwawinda na kuwaua wanyama.

**Zoezi la msamiati, ukurasa 18**

Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, wanafunzi watafute msamiati mpya kutoka kwenye kifungu ca mazungumzo na wautolee maana.

**Kwa mfano:**

1. ***watalii*** *– watu wanaotembelea eneo fulani ili kujifurahisha au kujifundisha*
2. ***huduma*** *– mambo muhimu yanayohitajika kustawisha maisha ya binadamu*

**Zoezi la 3.1, ukurasa 18**

1. - D
2. - E
3. - F
4. - A
5. - H
6. - B
7. - C
8. - G

**Zoezi la 3.2, ukurasa 19-20**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi. Wanafunzi walinganishe sentensi na pica na micoro waliyopewa kwa usahihi. Yaani:

1. - E
2. - B

3. - D
4. - A
5. - C

**Zoezi la matumizi ya lugha, ukurasa 20**

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika majadiliano kuhusu wanyamapori. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanataja majina ya wanyamapori wanaowafahamu na waliowahi kuwaona, sifa zao, cakula wanacokula pamoja na maumbile yao. Wanafunzi pia waeleze walikowaona wanyamapori hao pamoja na mazingira ambamo wanyamapori hao wanapenda kuishi.

**Kwa mfano:**

*Mamba ni mnyama aliye na ngozi yenye magamba mengi. Yeye ni hatari sana na anapenda kula nyama. Nilimwona mamba katika mbuga ya wanyama ya Akagera. Mamba anapenda kuishi katika mazingira ya majini.*

**Zoezi la 3.3A, ukurasa 20**

Mwalimu atathmini iwapo wanafunzi wanahusisha kwa usahihi pica walizopewa pamoja na majina ya wanyama mbalimbali waliyopewa.

Simba - 1
Ng'ombe - 2
Kiboko - 3
Mbuzi - 4
Mamba - 5
Ndovu - 6
Kondoo - 7
Pundamilia - 8
Sungura - 9

**Zoezi la 3.3B, ukurasa 21**

Mwalimu atathmini jinsi wanafunzi watakavyoainisha wanyama wanaofugwa na wanyama wasiofugwa. Yaani:

| Wanyama wanaofugwa | Wanyama wasiofugwa |
|---|---|
| sungura, ng'ombe, mbuzi, kondoo | simba, ndovu, mamba, pundamilia, kiboko |

**Zoezi la 3.4, ukurasa 21**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga pamoja na maswali yake kwa kutumia kiulizi 'wapi'.

**Kwa mfano:**

***Sentensi:*** *Mamba huishi majini.*

***Swali:*** *Mamba huishi wapi?*

***Sentensi:*** *Mtalii alilala hotelini.*

***Swali:*** *Mtalii alilala wapi?*

**Zoezi la 3.5, ukurasa 22**

1. Dereva huyu anatoka **wapi**?
2. Sembare anaingia cumbani mwake **vipi**?
3. Gari la mtalii limesimama **wapi**?
4. Simba anajificha **wapi**?
5. Ndugu yangu anatembea **vipi**?

**Zoezi la 3.6, ukurasa 22**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga katika umoja na wingi kwa kutumia kiulizi 'wapi' na 'vipi'. **Kwa mfano:**

1. *Mtalii anatoka wapi?* – *Watalii wanatoka wapi?*
2. *Gari huendeshwa vipi?* – *Magari huendeshwa vipi?*

**Zoezi la 3.7, ukurasa 23**

1. Kijana mmoja alienda **wapi**?
2. Waziri ataondoka **vipi**?
3. Mtumishi amepotezea ufagio wake **wapi**?
4. Fundi hodari amejenga nyumba yake **vipi**?
5. Mwalimu wetu ameenda **wapi**?

**Zoezi la 3.8, ukurasa 23**

1. Mwalimu hakikishe kuwa wanafunzi wametunga sentensi sahihi.

**Kwa mfano:**

a) *Ninazuru mbuga ya wanyama ili kuwaona ndovu.*
b) *Watalii wamesimama garini ili kupiga pica.*

2. Mwalimu atathmini maswali yatakayotungwa na wanafunzi. Sharti maswali hayo yatumie kiulizi 'kwa nini'.

**Kwa mfano:**

a) *Kwa nini unazuru mbuga ya wanyama?*
b) *Kwa nini watalii wamesimama garini?*

**Zoezi la 3.9, ukurasa 24**

1. Kwa nini mtoto huyu analia?
2. Kwa nini mkulima huyu alicinja mbuzi mmoja?
3. Kwa nini Mukandori anakaa katika nyumba hii?
4. Kwa nini mtu huyu amepelekwa jela?
5. Kwa nini mama na baba wamekaa sebuleni?

# Somo la 4: Utamaduni na utalii

## Kipindi cha 10: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati

### a) Malengo ya somo

- Kusoma kwa usahihi kifungu ca habari kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;
- Kubaini msamiati unaotumika katika mazingira ya utalii;
- Kutumia msamiati wa mazingira ya utalii katika sentensi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Pica za vivutio vya utalii vinavyohusiana na historia na utamaduni wa Rwanda;
- Ramani yenye kuonyesha vivutio mbalimbali vya utalii;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 25-28;
- Combo ca kunasia sauti, breli na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### c) Maandalizi ya somo

Mwalimu atambue kwanza vivutio vya utalii vilivyo ncini na ambavyo vinahusiana na utamaduni na historia ya Rwanda ili viweze kutolewa kama mifano katika kuendeleza somo hili. Micoro ya mambo yenye kuvutia na ambayo yanatumiwa katika sekta ya utalii nayo iandaliwe ili kurahisisha uelewa wa wanafunzi. Kwa mfano, mwalimu anaweza kucora ng'ombe wa kitamaduni '*Inyambo*', vifaa vya kitamaduni kama vile: *viti, kinu na mci wake, mkuki, mishale, njuga, watu waliovaa mavazi mbalimbali ya kitamaduni au mavazi ya zamani, nyumba za kuhifadhi vifaa vya kitamaduni, majabali yenye kubainisha nyayo za Ruganzu na mbwa wake* na kadhalika.

Mwalimu alete vifaa na micoro hiyo na ahakikishe kuwa anavionyesha hadharani wakati unaofaa ili asipoteze muda na wanafunzi wapate ujuzi unaotarajiwa kwa muda uliopangwa. Kama kuna wanafunzi wenye matatizo ya kuona na kusikia, mwalimu akumbuke kuwaomba waguse vifaa alivyovileta au avionyeshe huku akivitolea maelezo kwa sauti na kwa kuandika ubaoni.

### d) Utaratibu wa somo

### Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake na awaulize maswali kuhusu kipindi kilicopita. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu wao kuhusu kipindi hico. Mwalimu acukue fursa hii ya utangulizi ili kuwaomba wanafunzi kusahihisha mazoezi waliyopewa kuhusiana na kipindi kilicopita. Mwalimu aendeleze somo kwa kuwaomba wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi wawili wawili na kujadiliana kuhusu kile wanacokiona au kinacoendelea katika pica zilizo katika *Kitabu ca Mwanafunzi 25*. Wanafunzi wajadiliane kama walivyoambiwa na mwalimu wao kisha baadaye, wajitokeze mbele ya darasa na kuwaelezea wanafunzi wengine kile kinacoendelea katika pica hizo. Wakati wa mawasilisho ya wanafunzi, mwalimu awaelekeze wanafunzi ili watoe maelezo kuhusu pica zilizopo kwa kudhihirisha nafasi ya utamaduni na umuhimu wa vifaa vilivyopo. Kwa mfano, anaweza kuuliza: "*Watu hawa wanafanya nini? Nyumba hii ina umuhimu gani?* na kadhalika. Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu wao kwa kuelezea kile kinacofanywa na watu walio katika pica hizo. Kwa mfano: *Watu hawa wanaimba, nyumba hii inatumiwa kuhifadhi vifaa vya utamaduni* na kadhalika.

Katika sehemu hii ya utangulizi, ni vyema mwalimu awacocee wanafunzi kupata umuhimu wa utamaduni kama njia inayoweza kuisaidia nci kuendeleza ucumi wake ambapo wenyeji na wageni hulipa pesa za kutembelea vivutio mbalimbali vya kitamaduni vilivyo ncini.

### 4.1 Kusoma na ufahamu: Kifungu kuhusu utamaduni na utalii

Katika hatua hii, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa kimya kifungu ca habari kinacohusika huku wakiandika msamiati mpya wanaopatana nao. Baada ya kusoma kwa kimya, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu kifungu hico walicosoma ili kuhakikisha kuwa wameelewa. Kwa mfano, anaweza kuuliza maswali yafuatayo: *Baadhi ya watu hufikiria nini kuhusu utamaduni? Taja vitu unavyoweza kupata katika nyumba ya kuhifadhi utamaduni iliyoko mjini*

*Huye* na kadhalika. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika kifungu hico. Kwa mfano: *Baadhi ya watu hufikiria kuwa utamaduni wetu hauwezi kuleta faida za kiucumi. Baadhi ya watu hufikiria kuwa utamaduni hauna umuhimu. Katika nyumba ya kuhifadhi utamaduni iliyoko mjini Huye, tunaweza kupata aina mbalimbali za mavazi yaliyotumiwa na mababu zetu, ngoma zetu za kitamaduni, viti vya Kinyarwanda, majamvi mazuri* na kadhalika. Hatimaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kusoma kwa sauti kifungu ca habari na wanafunzi wasome kwa sauti mmoja baada ya mwingine. Mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wanasoma kwa usahihi na kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi huku akisahihisha matamshi pale ambapo wanafanya makosa. Vilevile, ni vyema mwalimu acunguze ikiwa wanafunzi wanasoma kwa kuzingatia matumizi ya alama za uakifishaji zilizotumika katika kifungu ca habari kilicopo.

Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi wajibu maswali ya ufahamu yaliyo katika *Kitabu ca Mwanafunzi, ukurasa 26-27*. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali hayo. Mwalimu atoe maelezo yake kwa kutilia mkazo pale ambapo wanafunzi wanatatizika na kwa kucocea ujuzi wa wanafunzi kuhusu tafakuri tanduizi, usuluhishaji wa matatizo, mawasiliano katika lugha rasmi, ushirikiano, utawala binafsi na hata stadi za maisha kupitia maswali waliyopewa katika sehemu hii ya ufahamu.

### 4.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu utamaduni

Katika hatua hii ya ujifunzaji wa msamiati, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na awaombe watafute maana za msamiati mpya waliopatana nao katika kifungu ca habari walicokisoma. Mwalimu awaambie wanafunzi wajadiliane kuhusu maana za msamiati huo kulingana na matumizi yake katika kifungu walicokisoma. Ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wanajadiliana kama walivyoelekezwa, ni vyema mwalimu azunguke darasani na acunguze jinsi ambavyo mijadala ya wanafunzi inaendelea na acukue fursa hii kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika. Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi kujadiliana kuhusu zoezi la 4.1 la msamiati ambapo wanatarajiwa kuhusisha msamiati na maelezo yake sahihi. Zoezi hili lisahihishwe kwa kuwashirikisha wanafunzi katika makundi yao na mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wameelewa maana ya msamiati uliopo kwa kurejelea matumizi yake katika kifungu ca habari walicokisoma. Zoezi hili lilenge kumpatia mwanafunzi ujuzi wa kutosha kuhusu tafakuri tanduizi, stadi za utafiti na ugunduzi kwa kuelekeza

wanafunzi kupata maana iliyokusudiwa wao wenyewe kupitia matumizi ya msamiati husika pamoja na matumizi ya kamusi.

Zoezi la 4.2 la msamiati nalo lifanywe ambapo mwalimu atawaomba wanafunzi wacunguze micoro iliyopo na sentensi walizopewa ili waweze kuzihusisha na micoro hiyo. Ni vyema mwalimu awawezeshe wanafunzi kuwasiliana katika lugha rasmi ambapo watapata ujuzi kuhusu msamiati uliotumiwa kutunga sentensi hizo. Vilevile, zoezi hili lilenge kumpatia mwanafunzi ujuzi kuhusu mienendo mizuri inayomtambulisha mtu katika mazungumzo kati yake na mgeni, amani na maadili kwa kurejelea watu walio katika familia yao kama vile: nyanya na wajukuu wake, mtu na wageni wake na kadhalika. Zoezi hili lisahihishwe pia kwa kushirikisha wanafunzi wote ambapo wanafunzi watahusisha sentensi na micoro sahihi huku wakitoa maelezo ya ziada kuhusu hali halisi ya maisha na kile kinacoendelea katika pica zilizo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 28.

**Tathmini ya kipindi ca 10**

Katika hatua ya kuhitimisha somo hili, mwalimu awaulize wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza ili kuthibitisha iwapo wanaweza kutumia msamiati wa utalii na utamaduni wa Rwanda katika sentensi zao kwa kucocea maadili na stadi za maisha miongoni mwao.

## Kipindi cha 11: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza

**a) Malengo ya somo**

- Kufahamu utamaduni wa Wanyarwanda;
- Kutambua msamiati maalum kuhusu utamaduni na utalii;
- Kujadili kuhusu faida zitokanazo na utamaduni ncini;
- Kudhihirisha nafasi ya utamaduni katika shughuli za kiutalii.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Micoro/pica za nyumba za kitamaduni zipatikanazo ncini Rwanda;
- Micoro/ pica za vifaa mbalimbali vya kitamaduni;
- Pica za vivutio vya utalii vinavyohusiana na historia na utamaduni wa Rwanda;
- Micoro/pica za mavazi ya kitamaduni ya Wanyarwanda;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 29-30;
- Combo ca kunasia sauti, breli na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia

wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### c) Maandalizi ya somo

Mwalimu aandae micoro au pica za nyumba za kitamaduni, mavazi ya kitamaduni pamoja na vifaa na vyombo mbalimbali vya kitamaduni. Mwalimu anaweza kutafuta vifaa hivi vya kitamaduni na kuvileta darasani. Pia, mwalimu anaweza kuwapeleka wanafunzi wake kwenye makavazi yoyote ncini Rwanda ili wanafunzi wajionee wenyewe vifaa hivi. Hili litawasaidia wanafunzi kupata uelewa halisi na kamili wa funzo hili kuhusu utamaduni wa wanyarwanda. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika funzo hili.

Iwapo kuna wanafunzi wenye matatizo ya kuona na kusikia, mwalimu akumbuke kuwaomba waguse vifaa alivyovileta au avionyeshe huku akivitolea maelezo kwa sauti na kwa kuandika ubaoni.

### d) Utaratibu wa somo

#### Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake na kuwauliza maswali kuhusu kipindi kilicopita. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu wao kuhusu kipindi hico. Mwalimu acukue fursa hii ya utangulizi ili kuwaomba wanafunzi wasahihishe mazoezi waliyopewa kuhusiana na kipindi kilicopita.

## 4.3 Matumizi ya lugha: Zoezi la msamiati

Mwalimu alenge kumwezesha mwanafunzi kuufahamu msamiati maalum unaohusiana na utalii na utamaduni wa Wanyarwanda kwa ujumla. Katika hatua hii, mwanafunzi anastahili kuwa na uwezo wa kutambua herufi sahihi za kuundia neno lolote lile kuhusiana na utalii na utamaduni. Maendelezo ya wanafunzi yatiliwe mkazo katika sehemu hii. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuendeleza maneno kwa usahihi. Masahihisho ya maendelezo ya maneno yafanywe panapohitajika.

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha wacunguze msamiati waliopewa katika majedwali ambao una herufi zinazokosekana. Mwalimu awahimize wanafunzi kujadiliana kuhusu msamiati huo kisha waukamilishe kwa usahihi kwa herufi sahihi.

Mwalimu awaeleze wanafunzi kuwa maneno yanayotakiwa kukalimishwa katika zoezi hili ni yale waliyokutana nayo katika usomaji wao wa kifungu walicopewa na ambayo wanapaswa kuyajua na kuyatumia katika mawasiliano

yao ya kawaida.

### 4.4 Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu ili waweze kujadiliana kuhusu utamaduni na utalii. Mbali na kuwazoesha wanafunzi kupata ujuzi katika mawasiliano yao katika lugha rasmi, kutamka kwa usahihi herufi, silabi na sentensi. Zoezi hili lisaidie pia wanafunzi kupata ujuzi kuhusu stadi za utafiti, ubunifu na ugunduzi, maadili na mienendo mizuri, usawa wa kijinsia, elimu ya pamoja na elimu kuhusu fedha.

Kwa hivyo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kuwafafanulia maswali wanayopaswa kujibu katika mjadala wao ambapo utamaduni utafafanuliwa kama njia ya kujithamini na kuthamini wenzao na mambo kadhaa yanayowatambulisha kuwa walivyo. Hivyo basi, kupitia zoezi hili, mwalimu awaelekeze wanafunzi kufahamu misingi ya utamaduni ambapo wasicana, wavulana, wanawake, wanaume, walemavu na wengine wote wanapaswa kudumisha umoja, ushirikiano, kuheshimiana, amani, bidii, uungwana na kadhalika kama vitambulisho vyao mbele ya wageni wanaovutiwa na utamaduni wa Wanyarwanda.

Wanafunzi wajadiliane kwa kujibu maswali yaliyopo na wajitokeze mbele ya darasa ili kuwaeleza yale waliyoafikiana katika mjadala wao. Aidha, ni vyema mwalimu atumie zoezi hili kumsaidia mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu utawala binafsi, stadi za maisha, tafakuri tanduizi na usuluhishaji wa matatizo kupitia maswali yaliyo katika kitabu ca mwanafunzi. Hivyo basi, mwalimu ashirikishe wanafunzi wote ili waweze kutoa maoni yao kuhusu hoja za wanafunzi wa kila kundi na awacocee kutoa mawazo yanayothibitisha kuwa wamepata ufahamu wa namna ya kupanga miradi ya utamaduni inayoweza kuleta faida za kiucumi na ile ya kutunza na kuhifadhi vivutio vya utalii wa utamaduni wa Wanyarwanda.

### Tathmini ya kipindi ca 11

Mwalimu alenge kubaini iwapo malengo ya somo lake yametimizwa. Awaulize wanafunzi maswali ya kupima uwezo wao wa kufahamu utamaduni wa Wanyarwanda kwa kurejelea nyumba za kuhifadhi utamaduni, vifaa vya utamaduni vinavyoweza kuvutia watalii, vivutio vya utalii wa utamaduni, namna ya kutunza vifaa hivyo na kuhifadhi utamaduni, faida za kiucumi tunazopata kutokana na utamaduni, miradi inayoweza kupangwa katika kuthamini utamaduni na hata hasara za kupuuza utamaduni.

## Kipindi cha 12: Sarufi (Wakati wa mazoea, tungo yakinishi)

**a) Malengo ya somo**

- Kutambua wakati wa mazoea katika maongezi na sentensi;
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia wakati wa mazoea;
- Kutambua matumizi ya wakati wa mazoea katika tungo yakinishi.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 30-31;
- Combo ca kunasia sauti, breli na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Katika maandalizi ya somo hili, mwalimu alenge kumsaidia mwanafunzi kubaini maana ya wakati wa mazoea. Mwalimu anaweza kuzitaja nyakati nyingine mbalimbali ambazo wanafunzi wanazifahamu kama vile: *wakati uliopo, wakati uliopita, wakati uliotimilika* na *wakati ujao*. Kutokana na msingi huu, mwalimu ataweza kufundisha wakati wa mazoea. Mwalimu ataandaa masimulizi mafupi kuhusu mambo ambayo watu huyafanya kila wakati hadi kufikia kuwa ya mazoea.

**d) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Katika utangulizi, mwalimu awaamkie wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha zoezi walilopewa katika kipindi kilicopita.

Mwalimu acukue fursa hii ya utangulizi kuwakumbusha wanafunzi kuhusu nyakati mbalimbali ambazo wamewahi kufundishwa. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kutaja nyakati hizo ambazo ni *wakati uliopo, wakati uliopita, wakati uliotimilika* na *wakati ujao*. Wanafunzi watunge sentensi sahihi kwa kutumia nyakati walizotaja.

### 4.5 Sarufi: Wakati wa mazoea, tungo yakinishi

Katika sehemu hii, wakati wa mazoea utafafanuliwa katika tungo yakinishi. Ili

kurahisisha ujifunzaji wa sarufi hii, mwalimu anaweza kutumia micoro yenye kudhihirisha watu katika shughuli zao za kila siku ambapo ratiba ya wanafunzi huweza kutumiwa. Mwalimu anaweza kuwaomba wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha wasome na kucunguza sentensi zilizo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 30. Mwalimu awaulize wanafunzi maswali yenye kudhamiria kumpa mwanafunzi ujuzi kuhusu maneno yanayodhihirisha vitendo vinavyorudiwarudiwa au vinavyofanywa mara kwa mara au kila wakati. Miongoni mwa maneno yanayoweza kuleta pica ya vitendo vya mazoea na ambayo huweza kutiliwa mkazo na mwalimu ni kama *kila siku, kila mwaka, kila asubuhi, kila jioni* na kadhalika.

Mwalimu atumie vitendo vilivyopo kwa kuonyesha kwa njia ya micoro wakati ambapo vitendo hivyo vilifanyika huku akirejelea na kulinganisha na matumizi ya wakati uliopo ambayo tayari wanafunzi wanayaelewa. Kwa hivyo, mwalimu alinganishe vitendo mbalimbali kwa kuwakumbusha wanafunzi wakati wa *leo*, *sasa* na ule wa *kila siku*. *K*wa mfano, viambishi '***na'*** na '***hu*'** vitarejelewa kama viambishi vya nyakati hizo, yaani ***na*** kwa wakati uliopo na ***hu*** kwa wakati wa mazoea.

Ili kuthibitisha kwamba wanafunzi wameelewa matumizi ya wakati wa mazoea, mwalimu awaombe wanafunzi wafanye zoezi la 4.3 kwa kutunga sentensi zao kwa kutumia neno *kila siku* na baadaye, kulinganisha sentensi zao na zile walizotolewa katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 30. Zoezi hili lisahihishwe kwa kuwashirikisha wanafunzi wote na mwalimu acukue fursa hii kuwaomba wanafunzi wacunguze maelezo muhimu yaliyoandikwa katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 31 ili waweze kuelewa kikamilifu matumizi ya wakati wa mazoea. Baadaye, zoezi la 4.4 na la 4.5 la sehemu hii nayo yafanywe na yasahihishwe kama njia ya kuhakikisha kuwa ujifunzji wa sehemu hii umefaulu na mwalimu ayatumie kwa kusahihisha makosa ya wanafunzi pale yanapojitokeza.

**Tathmini ya kipindi ca 12**

Matumizi ya wakati wa mazoea yarejelewe ambapo mwalimu atawauliza wanafunzi maswali yanayoweza kuthibitisha kwamba wanafunzi wanaweza kutoa mifano ya maneno yanayoambatana na wakati wa mazoea kama vile: *kila siku, mara kwa mara, kila asubuhi* na kadhalika huku wakirejelea kiambishi *hu* kama kiambishi ca wakati wa mazoea. Wanafunzi wahimizwe kufanya mazoezi zaidi kuhusiana na matumizi ya wakati wa mazoea katika maongezi ya kila siku na katika utunzi wa sentensi sahihi.

**Maelezo muhimu kwa mwalimu**

Katika matumizi ya wakati wa mazoea, kiambishi '***hu***' hutumiwa kuonyesha kitendo kinachofanywa mara kwa mara yaani kila wakati.

**Kwa mfano:** *Mimi huoga kila siku asubuhi.* (kitendo cha kuoga kinafanywa kila siku asubuhi)

- Kitenzi ***oga*** kimetumiwa katika ***wakati wa mazoea*** kuonyesha kuwa kitendo hicho kinafanywa kila siku asubuhi.

## 4.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Ili kuwasaidia wanafunzi wa kiwango ca cini katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe wanafunzi hawa kufanya zoezi lifuatalo:

*Andika sentensi hizi katika umoja au wingi.*

**Kwa mfano:** Mtoto huyu husoma kitabu cangu kila wiki. (umoja)

**Jibu:** Watoto hawa husoma vitabu vyetu kila wiki. (wingi)

1. Mwalimu huuliza swali zuri.
2. Nyumba kubwa hujengwa mjini Kigali.
3. Kisu kipya hununuliwa na mama yangu.
4. Vitanda vizuri hutengenezwa na mafundi hawa.
5. Wasicana wale huimba nyimbo nzuri sana.

### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

1. Walimu huuliza maswali mazuri.
2. Nyumba kubwa hujengwa mjini Kigali.
3. Visu vipya hununuliwa na mama zetu.
4. Kitanda kizuri hutengenezwa na fundi huyu.
5. Msicana yule huimba wimbo mzuri sana.

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango ca juu ca uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge sentensi kumi sahihi kwa kutumia wakati wa mazoea katika umoja na wingi:

**Kwa mfano:** Mwalimu hutufundisha somo la Kiswahili kila siku.

**Jibu:** Walimu hutufundisha masomo ya Kiswahili kila siku.

# 4.7 Majibu

**Zoezi la makundi, ukurasa 25**

Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi kwa kurejelea micoro iliyopo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 25.

**Kwa mfano:**

*Mimi ninaona vifaa vya kitamaduni vya nci yetu kama vile: ngoma za kitamaduni, nyumba ya utambulisho wa Rwanda pamoja na wacezaji wa nyimbo za kitamaduni.*

**Maswali ya ufahamu, ukurasa 26-27**

1. Watu wengi hawaelewi umuhimu wa utamaduni kwa sababu wanadhani kuwa utamaduni hauwezi kuleta faida za kiucumi. Baadhi yao wanafikiri kwamba kuhifadhi utamaduni ni ishara ya kurudi nyuma na kutocangamkia maendeleo. Watu hawa wanafananisha uhifadhi wa utamaduni na ukosefu wa elimu.
2. Utamaduni ni mazoea yetu, mila zetu na maisha yetu kwa jumla.
3. Nyumba mbalimbali za kuhifadhi vifaa na shughuli zote za kitamaduni zilijengwa na bado zinaendelea kujengwa.
4. Mjini Nyanza na mjini Huye.
5. Aina mbalimbali za mavazi yaliyotumiwa na mababu zetu, ngoma za kitamaduni, viti vya Kinyarwanda, majamvi mazuri, pica za wanawake waliovaa taji za kitamaduni, mitindo ya kitamaduni ya kukata nywele, nyumba ya zamani iliyotumiwa na mababu zetu na sehemu zake mbalimbali, vifaa vilivyotumiwa katika nyimbo na sherehe za kitamaduni pamoja na vifaa vya zamani vilivyotumiwa nyumbani.
6. Mfalme Mutara III Rudahigwa
7. Cumba kilicotumiwa kufanya vitu viwe baridi, sebule tatu zilizotumiwa kupokelea wageni na pembeni mwa uga wa nyumba hiyo unaweza kuwatazama ng'ombe wa kitamaduni '*Inyambo*' wanaosifika kwa urefu wa pembe zao.
8. Utamaduni hucangia kuleta faida za kiucumi na hivyo maendeleo ya taifa kwa jumla.

II. Mwalimu atathmini ufupisho utakaoandikwa na makundi ya wanafunzi watatu watatu. Ufupisho huo usizidi maneno sabini.

**Zoezi la msamiati, ukurasa 27**

Mwalimu atathmini msamiati ambao wanafunzi watateua na kuutolea maana kwa usahihi.

**Kwa mfano:**

1. ***utamaduni*** – *hali ya maisha ya jamii fulani. Huhusisha mila, desturi au itikadi zinazotawala jamii hiyo*
2. ***kudumisha*** – *kuendeleza au kukuza*
3. ***uga*** – *eneo lililo mbele ya nyumba*

**Zoezi la 4.1, ukurasa 27**

Mwalimu ahakikishe wanafunzi wanalinganisha maneno yaliyo katika sehemu A na maelezo yaliyo katika sehemu B kwa usahihi. Yaani:

1. - D
2. - E
3. - F
4. - A
5. - C
6. - B
7. - I
8. - J
9. - G
10. - H

**Zoezi la 4.2, ukurasa 28**

Mwalimu ahakikishe wanafunzi wanalinganisha kwa usahihi sentensi walizopewa na mcoro na pica walizopewa kwa usahihi.

Yaani:

1. - E
2. - C
3. - B
4. - A
5. - D

**Zoezi la matumizi ya lugha, ukurasa 29**

1.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| V | I | F | A | A |

2.

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | W | E | L | E | K | E | Z | A | J | I |

3.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| T | H | A | M | A | N | I |

4.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| M | N | Y | A | M | A |

5.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| M | A | V | A | Z | I |

**Zoezi la kusikiliza na kuzungumza, ukurasa 29**

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kuendeleza mjadala kuhusu utamaduni na utalii. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanajadiliana kwa kujibu maswali waliyopewa.

**Kwa mfano:**

*Utamaduni unahusu mila zetu, mazoea yetu na maisha kwa jumla. Ncini Rwanda, utamaduni wa Wanyarwanda unatambulishwa na mavazi ya mababu wa zamani, majamvi mazuri, ngoma za kitamaduni pamoja na nyumba ya utambulisho wa utamaduni wa Rwanda iliyopo mjini Nyanza. Utamaduni pia unaweza kuwavutia watalii wengi mno kisha kuleta faida kwa kuiletea nci pesa nyingi za kigeni. Ili kuhifadhi utamaduni wetu, ni vyema kuudumisha. Iwapo hatutauthamini utamaduni wetu, huenda tukawapoteza watalii pamoja na pesa zinazotokana na shughuli za kiutalii.*

**Zoezi la 4.3, ukurasa 30**

1. Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi na zihusishe kitenzi ‘pika’ na nafsi walizopewa pamoja na maneno ‘kila siku’.

**Kwa mfano:**

1. *Mimi hupika kila siku.* – *Sisi hupika kila siku.*
2. *Wewe hupika kila siku.* – *Nyinyi hupika kila siku.*
3. *Yeye hupika kila siku.* – *Wao hupika kila siku.*

2. Mwalimu atathmini ulinganisho wa sentesi za wanafunzi katika umoja na wingi.

**Zoezi la 4.4, ukurasa 31**

1. Wagonjwa hawa hupelekwa hospitalini kwa magari haya.
2. Waimbaji hawa hupata fedha nyingi kila wiki.
3. Wageni wetu hufika kwenye uwanja wa ndege kabla ya saa kumi.
4. Mimi hutembea kwa miguu hadi kanisani.
5. Mwalimu wetu huondoka saa kumi na moja.

**Zoezi la 4.5, ukurasa 31**

1. Mgonjwa huyu hupelekwa hospitalini kwa gari hili.
2. Mwimbaji huyu hupata fedha nyingi kila wiki.
3. Mgeni wangu hufika kwenye uwanja wa ndege kabla ya saa kumi.
4. Sisi hutembea kwa miguu hadi kanisani.
5. Walimu wetu huondoka saa kumi na moja.

# Somo la 5: Milima yetu

## Kipindi cha 13: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati

### a) Malengo ya somo

- Kusoma kwa usahihi kifungu ca habari kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;
- Kubaini msamiati unaotumika katika mazingira ya utalii;
- Kutumia msamiati wa mazingira ya utalii katika sentensi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Ramani yenye kuonyesha maeneo yenye milima mbalimbali;
- Micoro ya watalii wakipanda milima mbalimbali;
- Pica za milima mirefu yenye volkano kama mazingira ya kutalii;
- Pica za misitu mikubwa, ndege na wanyama wanaopatikana katika misitu hiyo;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 32-35;
- Combo ca kunasia sauti, breli na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### c) Maandalizi ya somo

Katika maandalizi ya somo hili, mwalimu atafute vifaa vitakavyohitajika kujifunzia mazingira ya milima na volkano kama vilivyobainishwa hapo juu. Mwalimu azingatie wakati unaofaa wa kuonyesha vifaa hivyo hadharani ili wanafunzi wapate ufahamu unaotarajiwa katika muda unaotakikana. Kama kuna wanafunzi wenye matatizo ya kusikia, mwalimu akumbuke kutumia micoro na pica hizo huku akiandika maelezo yake ubaoni; na wale wenye matatizo ya kuona awaombe waguse micoro hiyo kwenye breli huku wakitaja majina yake ili nao wapate ufahamu wa jambo linalozungumziwa.

Katika kipindi hiki, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi yanayotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila zoezi linalohusika.

## d) Utaratibu wa somo

### Utangulizi

Mwalimu awasalimu wanafunzi na awaulize maswali kuhusu kipindi kilicopita. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu na maswali watakayoulizwa. Mwalimu acukue fursa hii kuwaelekeza wanafunzi kuhusu usahihishaji wa zoezi lao la utafiti walilokuwa wamepewa. Mwalimu ahakikishe kuwa zoezi hilo limeeleweka na kusahihishwa.

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kuwaomba wajadiliane kuhusu pica zilizo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 32. Wanafunzi wacunguze na kujadiliana kuhusu pica hizo huku wakiandika kile kinacoendelea au wanacokiona. Mwalimu awaulize maswali mbalimbali ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wameelewa pica hizo zinahusu nini. Kwa mfano, mwalimu awaulize: *Mnaona nini katika pica hizi? Watu hawa wanafanya nini?* na kadhalika. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kudhihirisha kwamba wamefanya ucunguzi wa pica zilizopo. Kwa mfano, wanafunzi wanaweza kutoa majibu kama vile: *Mimi ninaona milima mirefu*. *Mimi ninaona msitu*. *Mimi ninaona watu*. *Watu hawa wanatazama wanyama* na kadhalika. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kupata ujuzi kuhusu tafakuri tanduizi, stadi za utafiti, ugunduzi na ubunifu, usawa wa kijinsia na elimu ya pamoja wakati wa kuuliza maswali kwa wanafunzi ambapo micoro iliyopo inajumuisha walemavu, watu wazima, wazee, wanaume na wanawake na wengine.

### 5.1 Kusoma na ufahamu: Kifungu kuhusu 'Milima yetu'

Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa kimya kifungu ca habari kinacohusika huku wakiandika msamiati mpya wanaopatana nao. Wanafunzi wasome kwa kimya na kuandika msamiati huo mpya. Hatimaye, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu kifungu hico ili kuhakikisha kuwa wamekielewa. Kwa mfano, anaweza kuuliza maswali kama vile: *Kwa nini Rwanda inasifiwa? Misitu ina umuhimu gani? Toa mfano wa msitu mmoja mkubwa uliozungumziwa katika habari hii.* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika kifungu hico. Kwa mfano: *Rwanda inasifiwa kwa milima yake mingi; milima mikubwa mikubwa na milima midogo midogo*, *misitu inaleta hewa nzuri inayopendwa sana, kuna msitu wa Nyungwe, msitu wa Gishwati, msitu wa Mukura*. Baada ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wamesoma kwa kimya kifungu kilicopo na kukielewa, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma tena kifungu hico kwa sauti na kwa usahihi. Mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa na

acunguze ikiwa wanafunzi wanazingatia matumizi ya alama za uakifishaji wakati wao wa kusoma kifungu walicopewa.

Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi wajibu maswali ya ufahamu. Baada ya kujibu, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali hayo. Mwalimu atoe maelezo yake kwa kutilia mkazo pale ambapo wanafunzi wanatatizika huku akisisitiza hoja muhimu zilizo katika kifungu ca habari. Kwa hivyo, maelezo na maelekezo ya mwalimu yalenge kucocea ujuzi wa wanafunzi kuhusu tafakuri tanduizi, usuluhishaji wa matatizo, mawasiliano katika lugha rasmi, ushirikiano, utawala binafsi na hata stadi za maisha kupitia maswali waliyopewa katika sehemu hii ya ufahamu.

### 5.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu 'Milima yetu'

Katika hatua hii, mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na awaombe wajadiliane kwa kutafuta maana za msamiati mpya waliopatana nao wakati wao wa kusoma kifungu ca habari kilicopo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kuwaomba wazingatie matumizi ya msamiati huo katika kifungu hico na watumie kamusi pale wanapoihitaji. Mwalimu ahakikishe kwamba zoezi la 5.1 linafanywa na wanafunzi wote katika makundi yao kwa kuzunguka darasani huku akiwasaidia wanafunzi wanaotatizika. Hivyo basi, wanafunzi wacunguze sentensi zilizopo kwa kutilia mkazo matumizi ya msamiati uliopigiwa mistari ili nao waweze kutunga sentensi zao na kueleza maana za msamiati huo mpya.

Mwalimu awaombe wanafunzi wacunguze pia matumizi ya msamiati huo katika kifungu ca habari walicokisoma na watumie kamusi ili kubaini maana yake na kuweza kuutumia ipasavyo katika sentensi zao. Katika zoezi hili, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kupata ujuzi kuhusu tafakuri tanduizi, usuluhishaji wa matatizo, stadi za maisha, stadi za utafiti, ubunifu na ugunduzi kupitia ucunguzi wa sentensi walizotolewa na utunzi wa sentensi zao. Hali hii iendelezwe katika zoezi la 5.2 ambapo mwalimu atawaomba wanafunzi wacunguze micoro iliyopo na sentensi walizotolewa ili kuzihusisha na micoro hiyo. Mazoezi haya mawili yafanywe kwa njia inayofaa ili kumwezesha mwanafunzi kujivunia hali ya mazingira ya Rwanda na kupata ujuzi kuhusu ushirikiano, amani na maadili, usawa wa kijinsia, elimu ya pamoja, elimu kuhusu fedha; mazingira na mabadiliko ya hali ya hewa.

Ili kufanikisha ujifunzaji wa msamiati kwa kutimiza malengo hayo hapo juu, ni vyema mwalimu awaombe wanafunzi kucunguza sentensi za wanafunzi wenzao

katika makundi yao na awaulize maswali ambata kwa micoro na sentensi zilizo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 35. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuuliza: *Ni vitu gani vinavyoweza kuharibu mazingira? Kwa nini ni lazima kutunza milima na misitu yetu?* na kadhalika. Wanafunzi wajibu maswali hayo kwa mfano kwa kudhihirisha kwamba wameelewa umuhimu wa kutunza mazingira na hasara zinazotokana na kuharibu mazingira: vitu vinavyoweza kuharibu mazingira ni kama vile: kucoma milima, kukata miti ovyo, kutupa takataka na kadhalika. Ni bora kutunza milima na misitu kwa sababu huleta hewa nzuri, hutumiwa kuhifadhi wanyama mbalimbali, hutumiwa katika shughuli za utalii na kadhalika.

**Tathmini ya kipindi ca 13**

Katika hatua hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza ili kuhakikisha kuwa wanaweza kurejelea milima mirefu na volkano zilizopo ncini, kubainisha faida za kiutalii za mazingira ya Rwanda, kutumia msamiati wa mazingira ya utalii katika mawasiliano yao.

Kwa hivyo, mwalimu awaulize maswali mbalimbali kwa kurejelea mambo hayo muhimu yaliyopitiwa katika somo hili kiasi ca kupata pica kamili ya ufahamu wa wanafunzi. Kwa mfano, anaweza kuwauliza maswali kama vile: *Milima yetu ina faida gani? Ni hasara gani tunazoweza kupata tukiharibu mazingira yetu?* na kadhalika. Wanafunzi nao wajibu maswali ya mwalimu kulingana na mambo waliyojifunza katika somo hili. Kwa mfano: *Milima yetu inavutia watalii, milima yetu inasaidia kupata hewa nzuri, milima yetu inaota misitu ambapo wanyama huishi na kufurahia*; *uharibifu wa mazingira unaweza kusababisha kukosa wanyama, uharibifu wa mazingira unaweza kuleta magonjwa mbalimbali* na kadhalika.

## Kipindi cha 14: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza

**a) Malengo ya somo**

- Kutambua msamiati maalum unaohusiana na utalii na milima mbalimbali;
- Kudhihirisha umuhimu wa volkano na milima katika shughuli za kiutalii.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Ramani yenye kuonyesha maeneo yenye milima mbalimbali;
- Pica za vivutio vya utalii vinavyohusiana na mazingira ya milima ya Rwanda;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 35-37;
- Combo ca kunasia sauti, breli na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Mwalimu atafute vifaa vitakavyohitajika kujifunzia mazingira ya milima na volkano kama vilivyobainishwa hapo juu.

**d) Utangulizi**

Mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali kuhusu kipindi kilicopita. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu na maswali watakayoulizwa. Mwalimu ahakikishe kuwa zoezi ambalo wanafunzi walipewa katika kipindi kilicopita limesahihishwa.

### 5.3 Matumizi la lugha: Zoezi la jedwali

Katika hatua hii, lengo la mwalimu ni kumsaidia mwanafunzi kupata uwezo wa kutafakari, kutafiti na kugundua maneno yaliyotolewa maelezo ili kumsaidia kupata uwezo wa kuyatumia kwa usahihi pale anapotaka kuwasiliana na wengine. Hivyo basi, mwalimu azingatie kwamba maneno yaliyoulizwa yanahusu msamiati ambao wanafunzi wanapaswa kuwa tayari wanaufahamu kiasi ca kuweza kuutambua kupitia maelezo waliyotolewa katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 36. Hata hivyo, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kuwafafanulia kile kinacotakiwa kufanywa ili kuwasaidia wanafunzi wenye uwezo mdogo katika ujifunzaji wao na ikihitajika awatolee mifano.

Ili kurahisisha shughuli hii na kuwasaidia wanafunzi kuelewa haraka, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili ili wajadiliane kuhusu zoezi hili. Wanafunzi wajadiliane kwa kujaza nafasi zilizopo katika jedwali walilopewa na mwalimu azunguke darasani ili kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote kusahihisha zoezi hili na ahakikishe pia kuwa wanafunzi wamepata ufahamu kamili kuhusu maneno yaliyotolewa maelezo ili waweze kuyatumia katika mawasiliano yao ya baadaye kwa kurejelea mifano mingine ya maneno yanayohusiana na yale waliyoyatumia kujaza nafasi zilizopo ambapo kwa mfano anaweza kurejelea tofauti kati ya mlima na volkano kama sehemu ya ardhi iliyoinuka juu sana.

### 5.4 Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano

Katika hatua hii, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu ili waweze kujadiliana kuhusu faida za utalii. Kwa hivyo, mwalimu awaombe wanafunzi wazingatie maswali yaliyo katika *Kitabu ca Mwanafunzi* ukurasa 37 na awaeleze kwamba ndiyo yataelekeza mjadala wao kuhusu ubainishaji wa faida hizo. Wanafunzi nao wajadiliane kama walivyoelezewa na mwalimu. Mwalimu ahakikishe kwamba mazungumzo yao yanawasaidia kupata ujuzi kuhusu mawasiliano katika lugha rasmi, tafakuri tanduizi, elimu kuhusu fedha, amani na maadili, usawa wa kijinsia kupitia hoja mbalimbali watakazozipata katika mjadala wao kuhusu faida za utalii ambapo watabainisha *maana ya utalii, vivutio vya utalii, watalii na malipo yao, faida za kiucumi kwa nci nzima* na kadhalika. Hivyo basi, kupitia zoezi hili, mwalimu awaelekeze wanafunzi kufahamu vivutio vya utalii ncini na faida zake, watu wanaofurahia vivutio hivyo wakiwemo wananci wa jinsia na umri tofauti, walemavu na wageni kutoka mataifa mbalimbali na kadhalika. Vilevile, mwalimu awaelekeze wanafunzi kupata ufahamu kuhusu fedha zinazolipwa katika shughuli hizo za utalii na miradi ya maendeleo inayoweza kutekelezwa kutokana na fedha hizo ili waweze kutambua mienendo mizuri ya kupokea watalii na ya kutunza vivutio vya utalii, kuthamini mambo mbalimbali yaliyo ncini na ambayo yanatumiwa katika shughuli za utalii.

### Tathmini ya kipindi ca 14

Mwalimu aulize maswali kwa kucunguza ikiwa wanafunzi wanaweza kutambua msamiati wa mazingira ya utalii uliotumiwa, vivutio vya utalii vilivyopo, kutaja baadhi ya milima inayovutia, volkano zilizopo, wanyama na faida zinazopatikana katika sekta ya utalii na kadhalika.

## Kipindi cha 15: Sarufi (Wakati wa mazoea, tungo kanushi)

### a) Malengo ya somo

- Kufahamu matumizi ya wakati wa mazoea;
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia wakati wa mazoea;
- Kutunga sentensi sahihi katika tungo kanushi.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Wanafunzi wenyewe;
- Masimulizi yaliyoandikwa kuhusu matukio ya kila siku;
- *Kitabu ca Mwanafunzi,* ukurasa 37-39;
- Combo ca kunasia sauti, breli na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Mwalimu aandae vifaa vitakavyohitajika kujifunzia somo hili kama vile kuandika masimulizi mbalimbali ya kuonyesha matukio ya kila siku. Mwalimu azingatie wakati unaofaa wa kuwasomea wanafunzi masimulizi hayo ili wanafunzi wapate ufahamu unaotarajiwa katika muda unaotakikana. Kama kuna wanafunzi wenye matatizo ya kusikia, mwalimu akumbuke kutumia micoro na pica mwafaka huku akiandika maelezo yake ubaoni; na wale wenye matatizo ya kuona mwalimu anaweza kuandaa masimulizi yake katika breli ili nao wapate ufahamu wa jambo linalozungumziwa.

**d) Utangulizi**

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake kisha awaulize maswali kuhusu kipindi kilicopita. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu wao kuhusu kipindi hico. Mwalimu acukue fursa hii ya utangulizi ili kuomba wanafunzi kusahihisha mazoezi waliyopewa kuhusiana na kipindi kilicopita. Mwalimu aendeleze somo kwa kuwaomba wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi yanayotakikana kwa kila zoezi.

## 5.5 Sarufi: Wakati wa mazoea, tungo kanushi

Katika hatua hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali ili aweze kucunguza ikiwa wanakumbuka miundo ya umoja na wingi wa vitenzi katika wakati wa mazoea, tungo yakinishi, akionyesha wanafunzi kuwa somo hili ni mwendelezo wa mambo waliyojifunza katika somo lililotangulia. Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma sentensi zilizopo na kutambua sifa za miundo iliyoandikwa kwa hati tofauti.

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu hili ili waweze kutambua tofauti iliyopo kati ya tungo yakinishi na tungo kanushi za wakati wa mazoea kwa kuwaomba wacunguze sentensi zilizo katika *Kitabu ca Mwanafunzi,* ukurasa 37 na kuwaomba watunge sentensi zao wenyewe. Aidha, mwalimu awaombe wanafunzi wacunguze maelezo muhimu yaliyotolewa katika

*Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 38 ili waweze kupata ufahamu kamili wa miundo ya wakati wa mazoea tungo yakinishi na tungo kanushi. Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi wajibu zoezi la kwanza, la pili, la tatu na la nne katika sehemu hii ya sarufi ili kucunguza ikiwa kuna wanafunzi wanaotatizika katika ufahamu wao wa wakati wa mazoea. Kila zoezi lisahihishwe kwa kuwashirikisha wanafunzi wote na mwalimu atoe maelezo yake kwa kutilia mkazo pale ambapo wanafunzi wanatatizika.

## Tathmini ya kipindi ca 15

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza katika kipindi hiki ili kuhakikisha kuwa wanaweza kutunga sentensi sahihi katika wakati wa mazoea tungo yakinishi na tungo kanushi.

### Maelezo muhimu kwa mwalimu

Kikanushi ***'ha'*** hutumiwa katika vitenzi vinavyoisha kwa irabu ***'a'*** katika tungo kanushi.

**Kwa mfano:** Mkulima ***hu***lim***a*** shamba lake. (tungo yakinishi)

**Jibu:** Mkulima ***ha***lim***i*** shamba lake. (tungo kanushi)

Viambishi vya nafsi hutumiwa baada ya kikanushi ***'ha'*** na hubadilika kulingana na nafsi au ngeli inayohusika.

**Kwa mfano:**

| **Tungo yakinishi** | **Tungo kanushi** |
|---|---|
| Sisi *hu*lim*a* shamba. | Sisi *hatu*lim*i* shamba. |
| Nyinyi *hu*lim*a* shamba. | Nyinyi *ham*lim*i* shamba. |
| Wao *hu*lim*a* shamba. | Wao *hawa*lim*i* shamba. |

**Mifano zaidi:**

**Umoja:** Chumba hiki *hu*safishw*a* kila siku. - Chumba hiki *haki*safishw*i* kila siku.

**Wingi:** Vyumba hivi *hu*safishw*a* kila siku. - Vyumba hivi *havi*safishw*i* kila siku.

**Umoja:** Nyama hii *hu*liwa na mtoto. - Nyama hii *hai*liw*i* na mtoto.

**Wingi:** Nyama hizi *hu*liw*a* na watoto. - Nyama hizi *hazi*liw*i* na watoto.

## 5.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atoe zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye kiwango ca cini katika ujifunzaji wao ili kuinua kiwango cao. Kwa mfano:

*Tunga sentensi kwa kutumia wakati wa mazoea pamoja na vitenzi hivi:*

1. Kufurahia
2. Kuharibu
3. Kucoma
4. Kutalii
5. Kupanda

### Majibu, zoezi la ziada

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe vitenzi walivyopewa katika hali ya mazoea.

**Kwa mfano:**

1. *Watalii hufurahia kuzuru milima ncini mwetu.*
2. *Ukataji wa miti huharibu misitu yetu.*
3. *Waharibifu wa mazingira hucoma misitu.*
4. *Sisi hutalii maeneo ya milima mirefu kila mwaka.*
5. *Wakulima hupanda miti mingi.*

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango ca juu ca uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge sentensi kumi sahihi katika umoja na wingi, tungo yakinishi na tungo kanushi kwa kutumia wakati wa mazoea.

**Kwa mfano:**

***Umoja:*** *Mimi hunywa maji safi.* – *Mimi sinywi maji safi.*

***Wingi:*** *Sisi hunywa maji safi.* – *Sisi hatunywi maji safi.*

## 5.7 Majibu

### Zoezi la makundi, ukurasa 32

Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi kwa kurejelea micoro iliyopo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 32.

**Kwa mfano:**

*Mimi ninaona milima mingi, miti mingi pamoja na watalii wanaopanda mlima mmoja wao.*

**i) Maswali ya ufahamu, ukurasa 34**

1. Kwa sababu Rwanda ni nci yenye milima mingi sana; milima mikubwa mikubwa na milima midogo midogo.
2. Hutuletea hewa nzuri isiyo ya joto wala ya baridi.
3. Msitu wa Nyungwe, msitu wa Gishwati na Msitu wa Mukura.
4. Milima ya Muhabura, Kalisimbi, Sabyinyo, Nyiragongo na Gahinga.
5. Sehemu za Kaskazini mwa Rwanda kuanzia mpaka wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na huendelea hadi kwenye mpaka wa Rwanda na Uganda.
6. i) Wilayani Muhanga kuna milima Ndiza, Kanyarira.
   ii) Wilayani Huye kuna Ibisi bya Huye.
   iii) Wilayani Nyanza kuna milima ya Gacu, Rwabicuma na Mpanga.
   iv) Wilayani Ngororero kuna mlima Kageyo.
7. Kuna mahali panapojulikana kama '*Mu Miko y'Abakobwa'*
8. Huu ni mwamba mrefu wenye mteremko wa maji.
9. Kutunza mazingira yao na kupambana na waharibifu wa mazingira hayo.
10. Tusikate miti ovyo ovyo na tusiharibu mazingira kwa kucoma milima na misitu. Tupande miti mingi na tujiepushe na kucafua mazingira yetu.

**ii)** Mwalimu atathmini muhtasari wa kila kikundi. Sharti wanafunzi wawe wamekifupisha kifungu ca habari walicosoma hapo awali kwa kutaja mambo muhimu pekee kwa kutumia maneno mia moja pekee.

**Kwa mfano:**

*Nci yetu ina milima mikubwa na midogo. Kuwepo kwa milima mingi ncini mwetu kumesababisha nci hii iitwe nci ya milima elfu moja. Milima katika nci yetu ina misitu ambayo hutuletea hewa nzuri na inayopendwa sana. Misitu hii huhifadhi wanyama wadogo wadogo. Kuna msitu ambao huhifadhi ndege wa aina nyingi. Huu ni msitu wa Nyungwe. Kuna milima ambayo inajulikana kama volkano. Milima hii inapatikana Kaskazini mwa nci yetu na huenda hadi kwenye mpaka wa Rwanda na Uganda. Milima hii ni kama vile: Kalisimbi na Gahinga. Kila wilaya ncini mwetu ina milima yake. Pia kuna mwamba mrefu wenye mteremko wa maji. Mwamba huu unaitwa 'Mwamba wa Ndaba'. Mwamba huu huwavutia watalii wa kigeni pamoja na Wanyarwanda. Mjini Kigali, watu hufurahi kusimama juu*

*ya mlima Kigali ambao unasemekana kuwa kilele ca Kigali. Serikali imewaomba wananci kutunza mazingira na kujiepusha na kuyacafua.*

**Zoezi la msamiati, ukurasa 34**

Mwalimu atathmini maelezo ya msamiati ambao wanafunzi wataeleza.

**Kwa mfano:**

***Hewa*** *- upepo laini ulio kwenye anga la dunia viumbe ili kuwa hai*

**Zoezi la 5.1, ukurasa 34**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi walizopewa. Kwa mfano:

1. ***Viumbe*** *wote huvuta hewa safi ili kuishi.*
2. ***Kigali*** *ni mji mkuu wa Rwanda.*

**Zoezi la 5.2, ukurasa 35**

Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanahusisha kwa usahihi mcoro na pica walizopewa pamoja na sentensi walizopewa. Yaani:

1. - C
2. - D
3. - A
4. - B

**Zoezi la matumizi ya lugha, ukurasa 35-37**

Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanajaza jedwali walilopewa kwa majibu sahihi. Yaani:

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1 M | T | 2 A | L | I | I | |
| 3 M | L | | T | | | | |
| S | I | 4 P | A | N | G | A | |
| I | N | | L | | | | |
| T | Z | | I | | | | |
| U | I | 5 S | I | 6 K | U | | |
| | | | | U | | | 9 U |
| 7 M | | | | E | | | T |
| L | | 8 K | U | L | A | L | A |
| I | | | | E | | | L |
| M | | 10 K | U | K | U | | I |
| A | | | | E | | | I |
| | 11 U | | | Z | | | |
| | 12 K | U | Z | A | A | | |
| | A | | | | | | 13 P |
| | 14 M | I | T | I | | | A |
| | E | | | 15 D | O | L | A |

**Zoezi la kusikiliza na kuzungumza, ukurasa 37**

Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi yao kisha awaelekeze katika namna ya kuendeleza majadiliano kuhusu faida za utalii. Mwalimu awaongoze ili waweze kujadili kwa kujibu maswali yaliyo kwenye vitabu vyao.

**Kwa mfano:**

1. Utalii ni shughuli ya kutembelea eneo fulani kwa ajili ya kujiburudisha na kuelimika.
2. Baadhi ya sehemu za utalii ncini mwetu ni kama vile: Mbuga ya wanyama ya Akagera, Msitu wa Nyungwe, Milima ya Virunga n.k.
3. Watu ambao huja kutalii ncini mwetu ni watalii kutoka ulimwenguni kote. Pia, Wanyarwanda wenyewe huwa watalii wanapotembea vivutio vya utalii tulivyo navyo.
4. Nci yetu hufaidika na utalii kupitia kwa pesa za kigeni ambazo watalii hao hulipia huduma mbalimbali wanazozipokea wawapo katika ziara yao ncini. Ucumi wa nci yetu huimarika sana.
5. Wananci huweza kupata ajira katika vivutio mbalimbali vya utalii kama vile kuwa waelekezaji wa watalii, wahudumu wa hoteli n.k.

**Zoezi la 5.3, ukurasa 37**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe nafsi na wakati wa mazoea katika tungo yakinishi na tungo kanushi.

**Kwa mfano:**

1. *Mimi husoma asubuhi.*
   Mimi sisomi asubuhi.
2. *Wewe husoma asubuhi.*
   Wewe husomi asubuhi.
3. *Yeye husoma asubuhi.*
   Yeye hasomi asubuhi.

**Zoezi la 5.4, ukurasa 39**

1. Wewe huandika barua ndefu.
2. Sisi husaidia walemavu katika kijiji hiki.
3. Watalii hawa hufurahia mazingira ya milima mirefu.
4. Mkulima huyu hupanda miti katika mashamba yake.
5. Mti huu huzaa matunda mengi kila mwaka.

**Zoezi la 5.5, ukurasa 39**

1. Wewe huandiki barua ndefu.
2. Sisi hatusaidii walemavu katika kijiji hiki.
3. Watalii hawa hawafurahii mazingira ya milima mirefu.
4. Mkulima huyu hapandi miti katika mashamba yake.
5. Mti huu hauzai matunda mengi kila mwaka.

**Zoezi la 5.6, ukurasa 39**

1. **Umoja:** Mwanafunzi yule hajibu vizuri maswali ya mwalimu.
   **Wingi:** Wanafunzi wale hawajibu vizuri maswali ya walimu.
2. **Umoja:** Mtalii hatembelei mbuga zetu za wanyama kila siku.
   **Wingi:** Watalii hawatembelei mbuga zetu za wanyama kila siku.
3. **Umoja:** Ukuca huu haupakwi rangi nyeupe baada ya mwezi mmoja.
   **Wingi:** Kuca hizi hazipakwi rangi nyeupe baada ya mwezi mmoja.
4. **Umoja:** Ndege yule halali kwenye mti huu.
   **Wingi:** Ndege wale hawalali kwenye miti hii.
5. **Umoja:** Kitanda cako hakitumiwi na wageni wetu.
   **Wingi:** Vitanda vyenu havitumiwi na wageni wetu.

# Somo la 6: Maji yetu

## Kipindi cha 16: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati

**a) Malengo ya somo**

- Kusoma kwa usahihi kifungu ca habari kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;
- Kubaini msamiati unaotumika katika mazingira ya utalii;
- Kutumia msamiati wa mazingira ya utalii katika sentensi.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Ramani yenye kuonyesha maziwa na mito mbalimbali ncini Rwanda;
- Micoro yenye kuonyesha umuhimu wa maji;
- Micoro ya vyombo vya kusafiria majini;
- *Kitabu ca Mwanafunzi,* ukurasa 40-43;
- Combo ca kunasia sauti, breli na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Kila mwanafunzi anafahamu maji na huyatumia katika maisha yake ya kila siku. Hata hivyo, ni wanafunzi wacace wanaoweza kutambua nafasi na faida za maji katika sekta ya utalii. Kwa hivyo, mwalimu aandae funzo hili kwa namna ya kumwezesha kuwaelekeza wanafunzi kuelewa kwa ubayana uhusiano wa utalii na maji. Vilevile, vifaa vitakavyohitajika kama vile micoro au pica za mito mbalimbali, vyombo vya kusafiria majini na maziwa madogo na makubwa, visiwa n.k viandaliwe ili ujifunzaji wa somo hili uwe rahisi. Vifaa hivyo vionyeshwe hadharani wakati unaofaa na ikiwa kuna wanafunzi wasioona au wasiosikia, mwalimu awasaidie kwa kuwaomba kugusa vifaa au micoro hiyo huku maelezo yake yakitamkwa kwa sauti na kuandikwa ubaoni.

**d) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Mwalimu atangulize somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi na kuwauliza

maswali mbalimbali kuhusu somo lililopita. Wanafunzi nao wajibu maamkizi ya mwalimu na maswali waliyoulizwa kuhusu somo lililopita. Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa kusahihisha kazi iliyotolewa kama zoezi. Wanafunzi wasahihishe zoezi hilo na mwalimu atoe maelezo yake kwa kutilia mkazo pale ambapo wanafunzi wanatatizika. Baadaye, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti kuhusu micoro na pica iliyo kwenye *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 40 ili kuwasaidia kupata ujuzi kuhusu maji, vyanzo vyake na faida zake katika maisha ya binadamu. Kwa mfano: *Mnaona nini kwenye micoro na pica hii? Maji haya yana umuhimu gani?* Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kwa kueleza kile kinacoendelea katika pica na micoro hiyo. Kwa mfano: *Mimi ninaona mto. Mimi ninaona ziwa. Maji haya yanatumiwa kuogelea. Maji haya yanahifadhi samaki* na kadhalika.

Baadaye, mwalimu awaulize maswali kuhusu pica na micoro hiyo kwa kuwaongoza wanafunzi kufahamu nafasi ya maji katika sekta ya utalii. Kwa mfano, anaweza kuuliza maswali: *Watu hawa ni nani? Watu hawa wanafanya nini?* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu wao kwa kueleza kile kinacoendelea katika pica na micoro hiyo. Kwa mfano: *Watu hawa ni watalii. Watu hawa wanatalii ziwa. Watu hawa wameabiri combo ca majini. Watu hawa wanazunguka majini* na kadhalika. Katika sehemu hii, ni vyema pia mwalimu agusie maswali yanayowaelekeza wanafunzi kupata ujuzi kuhusu tafakari tanduizi, usawa wa kijinsia, elimu kuhusu mazingira na elimu ya pamoja. Hivyo basi maswali yake yagusie aina za maji yaliyo ncini, faida zake tofauti, watu mbalimbali walioshirikishwa katika vitendo vya utalii kama vile wanawake, wanaume, wazee, watoto, walemavu na kadhalika.

### 6.1 Kusoma na ufahamu: Kifungu kuhusu 'Maji yetu'

Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa kimya kifungu ca habari kinacohusika huku wakiandika msamiati mpya wanaopatana nao. Wanafunzi nao wasome kwa kimya huku wakiandika msamiati huo mpya. Baada ya kusoma kwa kimya, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu kifungu hico ili kuhakikisha kuwa wamekisoma na kukielewa. Kwa mfano, awaulize maswali yafuatayo: *Maji yana umuhimu gani katika maisha yetu? Kwa nini wanyama huhitaji maji? Watalii hufurahia kuona nini?*

Wanafunzi nao wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma

katika kifungu hico. Kwa mfano: *Maji hutumiwa kupikia cakula. Maji hutumiwa kunawa na kuosha miili yetu na kusafisha vyombo tunavyotumia nyumbani. Wanyama wote huhitaji maji ya kunywa. Watalii hufurahia kutazama na kusafiri katika vyombo vidogo vidogo na vikubwa* na kadhalika. Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa sauti kifungu ca habari kinacohusika nao wanafunzi wasome kwa sauti mmoja baada ya mwingine. Mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wanasoma kwa usahihi na kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi huku akiwakosoa pale ambapo wanafunzi wanafanya makosa. Mwalimu acunguze pia ikiwa wanafunzi wanasoma kwa kuzingatia matumizi ya alama za uakifishaji mbalimbali katika kifungu ca habari kilicopo.

Katika hatua hii ya kusoma na kufahamu, mwalimu awaombe wajibu maswali ya ufahamu. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali hayo kwa kucunguza ikiwa wamepata ufahamu na ujuzi unaotakikana katika matumizi ya Kiswahili katika mazingira ya utalii.

### 6.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu 'Maji yetu'

Katika hatua hii, ni muhimu kwanza mwalimu awaongoze wanafunzi kutafuta maana za msamiati mpya waliopatana nao katika kifungu walicokisoma. Kwa hivyo, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili na awaombe wajadiliane kuhusu maana za msamiati huo kulingana na matumizi yake katika kifungu ca habari walicokisoma huku wakitumia kamusi pale wanapoihitaji. Mwalimu azunguke darasani kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika na kuwaelekeza ipasavyo. Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi kujadiliana kuhusu zoezi la kwanza la msamiati uliojitokeza katika kifungu hico.

Kupitia zoezi hili, mwalimu awaelekeze wanafunzi kutunga sentensi zao wenyewe kwa kucunguza sentensi zilizopo na kutumia msamiati uliopigiwa mistari. Ili kuwasaidia wanafunzi wote kuelewa kwa urahisi maana za msamiati huo, ni vyema mwalimu awafafafanulie kwamba msamiati uliopo umeshatumiwa katika kifungu ca habari walicokisoma na kuwaomba kusoma sentensi hizo na kucunguza pia matumizi yake katika kifungu ca habari kilicopo. Mwalimu aombe kila kundi lijitokeze mbele ya wenzao na kuwaonyesha sentensi walizotunga na wanafunzi wengine wazicunguze na watoe mcango wao wa kusahihisha sentensi zisizo sahihi. Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi wajibu zoezi la pili. Kupitia mazoezi haya, mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamepata ujuzi kuhusu tafakuri tanduizi, usawa wa kijinsia, elimu kuhusu fedha; mazingira,

mabadiliko ya hali ya hewa na mwendelezo na utamaduni wa kiusanifishaji. Hivyo basi, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi ipasavyo katika ucunguzi wa sentensi, pica na micoro waliyotolewa katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 40 pamoja na utunzi wa sentensi zao.

**Tathmini ya kipindi ca 16**

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza ili kuhakikisha iwapo wanaweza kutumia msamiati wa mazingira ya utalii katika sentensi zao kwa kucocea maadili na stadi za maisha. Kwa kurejelea micoro iliyo katika *Kitabu ca Mwanafunzi,* ukurasa 40, mwalimu awaulize wanafunzi kuhusu vivutio vya utalii vyenye mazingira ya maji, faida zake kwa taifa na kwa watalii wanaozuru mazingira hayo na mienendo wanayoweza kuwa nayo katika kutunza mazingira hayo.

## Kipindi cha 17: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza

**a) Malengo ya somo**

- Kutambua msamiati maalum unaohusiana na utalii na mazingira ya maji;
- Kudhihirisha umuhimu wa maji;
- Kutambua vyombo mbalimbali vya kusafiria majini;
- Kutambua mazingira mbalimbali ya maji.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Ramani yenye kuonyesha maeneo yenye mito, maziwa na cemicemi ncini Rwanda;
- Micoro au pica za vyombo vya kusafiria majini;
- Micoro au pica zenye kuonyesha umuhimu wa maji;
- *Kitabu ca Mwanafunzi,* ukurasa 43-44;
- Combo ca kunasia sauti, breli na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Mwalimu aandae vifaa vitakavyohitajika kufunzia mazingira ya maji, umuhimu wa maji na vyombo vya kusafiria majini kama vilivyobainishwa

hapo juu. Mwalimu anaweza kuandaa micoro au pica za wanyama wanaopatikana majini kama vile mamba na kiboko. Pia, mwalimu anaweza kutafuta nafasi ya kuwapeleka wanafunzi wakajionee wanyama hawa wenyewe pamoja na maziwa na mito mbalimbali.

**d) Utangulizi**

Mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali kuhusu kipindi kilicopita. Wanafunzi nao wajibu maamkizi ya mwalimu na maswali watakayoulizwa. Mwalimu ahakikishe kuwa zoezi ambalo wanafunzi walipewa katika kipindi kilicopita limesahihishwa.

### 6.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

Katika hatua hii, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wanne wanne ili wajadiliane kuhusu maeneo ya utalii ambayo wamewahi kutembea kama vile maziwa, mito, milima na hata kuabiri vyombo vyovyote majini kama vile mashua. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika makundi yao ili waweze kusimuliana kuhusu maeneo ambayo wamewahi kuyatembelea na waliyoyaona. Kila kundi litapewa dakika cace za kuwaeleza wanafunzi wengine waliyojadiliana katika makundi yao. Mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika. Ili kukamilisha maelezo ya mwalimu na yale yanayotolewa na wanafunzi darasani, ni vyema mwalimu awaombe wanafunzi wafanye zoezi la 6.4 la sehemu hii ya matumizi ya lugha.

Zoezi hili lisahihishwe kwa kuwashirikisha wanafunzi wote na maelezo ya mwalimu yatilie mkazo pale wanafunzi wanapotatizika. Baadaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kuwaomba wacunguze micoro iliyo katika *Kitabu ca Mwanafunzi,* ukurasa 44 ili waweze kuihusisha na sentensi walizotolewa. Ni vyema mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamepata ujuzi kuhusu mazingira, mabadiliko ya hali ya hewa na mwendelezo, tafakuri tanduizi, usuluhishaji wa matatizo, stadi za utafiti, ubunifu na ugunduzi, ushirikiano, utawala binafsi, stadi za maisha na mawasiliano katika lugha rasmi kupitia ucunguzi wa sentensi pamoja na micoro iliyopo kwa usahihi.

### 6.4 Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano

Hatua hii inahusu kusikiliza na kuzungumza. Mwalimu awaongoze wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi wawili wawili ili waweze kujadiliana kuhusu faida za kiutalii zinazoweza kupatikana kutokana na maji. Kwa hivyo, mwalimu awaelekeze wanafunzi ili mjadala wao udhihirishe vivutio vya utalii vilivyo katika mazingira yenye maji huku wakitaja mambo muhimu ambayo

huwavutia watalii wengi katika vivutio hivyo. Sehemu hii ipanue ujuzi wa wanafunzi kuhusu faida za kiucumi na za kiushirikiano kwa wananci na kwa wageni wanaopenda kutalii mazingira hayo. Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi yao wajitokeze mbele ya darasa ili wawaeleze wenzao kuhusu yale waliyoyapata katika mijadala yao. Wanafunzi wengine nao wasikilize matokeo ya mjadala wa kila kundi na wapewe muda wa kucangia kwa yale yaliyozungumziwa huku wakiongozwa na mwalimu.

Aidha, hatua hii ya kusikiliza na kuzungumza imehusisha pia zoezi la imla. Kwa hivyo, mwalimu awaombe wanafunzi wafunge vitabu vyao na waandike kifungu ambaco atawasomea. Wanafunzi wafunge vitabu vyao na waandike kifungu ambaco mwalimu wao atawasomea. Mwalimu ahakikishe kuwa anatamka kila neno kwa sauti ya kusikika na wanafunzi wote. Mwalimu azingatie matamshi sahihi ya maneno atakayoyasoma. Zoezi hili lisahihishwe kwa kuwashirikisha wanafunzi wote na mwalimu acunguze ikiwa wanafunzi wanaweza kuandika kwa usahihi maneno yaliyopo na kifungu kizima kwa kuzingatia matumizi ya alama za uakifishaji na matumizi ya herufi kubwa. Ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi kuepuka athari za lugha ya kwanza kwa baadhi ya wanafunzi ambapo wengi huweza kucopeka sauti 'y' au sauti 'w' kati ya irabu mbili kwa kuandika kwa mfano *wapokeyaji* badala ya *wapokeaji*, *waliwokwenda* badala ya *waliokwenda*, *vibawo* badala ya *vibao* na kadhalika. Hali hii iwacocee wanafunzi kutafiti zaidi kuhusu maneno mengine yenye sifa hizo katika lugha ya Kiswahili kama njia ya ujifunzaji wa kudumu na mawasiliano katika lugha rasmi.

## Zoezi la imla

Mwalimu awasomee wanafunzi kifungu hiki kisha wanafunzi wakiandike katika madaftari yao kwa usahihi.

*Watalii wengi walifika Uzi jioni. Walipokelewa kwenye uwanja wa ndege. Wapokeaji waliokwenda pale walikuwa wamebeba vibao vilivyoandikwa majina ya watalii hao. Watalii hao walipofika, walipokelewa vizuri na mizigo yao ilicukuliwa na kuwekwa ndani ya magari ya kiutalii ili kuelekea kwenye hoteli nzuri. Keshoye, watalii hao walianza safari yao ya kiutalii kwa kuelekea kwenye Ziwa Kivu ili kuweza kufurahia mandhari yake. Vyombo vingi vilikuwa vimetayarishwa ili kuwasaidia katika shughuli zao za kiutalii. Wengi wao walicukua mavazi yao ya kuogelea. Walizunguka visiwa vingi vinavyopatikana ziwani na kufurahia sana.*

**Tathmini ya kipindi ca 17**

Mwalimu atathmini iwapo ujifunzaji umefanywa kwa namna ya kuridhisha. Kwa hivyo, awaulize wanafunzi maswali ya kupima uwezo wao wa kurejelea umuhimu wa maji, vyanzo vya maji na faida zake katika sekta ya utalii.

Vilevile, maswali mengine yacunguze uwezo wa wanafunzi wa kutunga sentensi fupifupi kwa kutumia msamiati mpya waliojifunza katika somo hili kwa kukuza uwezo wao wa kuwasiliana katika lugha rasmi na ujuzi wao wa utamaduni wa kiusanifishaji. Mbali na hayo, mwalimu acunguze iwapo wanafunzi wamezielewa stadi za maisha kupitia maswali mbalimbali yanayohusiana na kutunza vizuri mazingira yetu yenye maji ili kuendeleza na kuimarisha utalii ncini.

## Kipindi cha 18: Sarufi (Kiulizi '-pi')

**a) Malengo ya somo**

- Kufahamu matumizi ya kiulizi ***'-pi'***;
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia kiulizi ***'-pi'***;
- Kufahamu mabadiliko ya kiulizi ***'-pi'*** katika ngeli mbalimbali.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Wanafunzi wenyewe;
- Vifaa vya wanafunzi kama vile: madaftari, kalamu, rula n.k.;
- *Kitabu ca Mwanafunzi, ukurasa* 45-46;
- Combo ca kunasia sauti, breli na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Mwalimu aandae vifaa vitakavyohitajika kujifunzia somo hili kama vile vifaa mbalimbali vinavyopatikana darasani kwa mfano, madaftari, kalamu, rula n.k. Mwalimu azingatie wakati unaofaa wa kuvitumia vifaa hivyo ili wanafunzi wapate ufahamu unaotarajiwa katika muda unaotakikana. Iwapo kuna wanafunzi wenye matatizo ya kusikia, mwalimu akumbuke kuandika ubaoni maelezo kuhusu vifaa hivyo; na wale wenye matatizo ya kuona mwalimu anaweza kuandaa kwenye breli sentensi zilizotungwa kwa kutaja vifaa husika pamoja na kiulizi '-pi'. Mwalimu anaweza pia kuandaa

micoro ya vifaa hivi kwenye breli kwa manufaa ya wanafunzi hao wasioona iwapo wapo.

**d) Utangulizi**

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake kisha awaulize maswali kuhusu kipindi kilicopita. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu wao kuhusu kipindi hico. Mwalimu acukue fursa hii ya utangulizi ili kuomba wanafunzi kusahihisha mazoezi waliyopewa kuhusiana na kipindi kilicopita. Mwalimu aendeleze somo kwa kuwaomba wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi yanayotakikana kwa kila zoezi.

### 6.5 Sarufi - Matumizi ya kiulizi '-pi'

Ujifunzaji wa sarufi katika hatua hii ucukuliwe kama mwendelezo wa yale yaliyofundishwa katika sehemu ya sarufi kuhusu viulizi katika masomo yaliyotangulia. Kwa hivyo, ni vyema mwalimu awaongoze wanafunzi kuelewa kwamba namna ya kuuliza swali hulingana na dhamira ya mzungumzaji ambapo anaweza kuuliza kuhusu jinsi jambo linavyofanywa kwa kutumia *vipi* au kuhusu kitu, mtu na mnyama ambapo mzungumzaji hutumia kiambishi ca ngeli kurejelea kitu, mtu au mnyama anayehusika katika swali hilo. Ili kurahisisha uelewa wa wanafunzi katika kipengele hiki, mwalimu awaombe wanafunzi wacunguze sentensi zilizo katika *Kitabu ca Mwanafunzi, ukurasa 45* katika umoja na wingi na awaelekeze kupata mabadiliko ya kiupatanishi yanayojitokeza kulingana na aina za nomino zinazorejelewa katika maswali kupitia sentensi za wanafunzi katika zoezi la kwanza pamoja na maelezo muhimu yaliyoandikwa katika *Kitabu ca Mwanafunzi, ukurasa 45*. Kwa mfano: *Mtu yupi? Watu wapi? Mlima upi? Milima ipi?* na kadhalika. Baadaye, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamepata ujuzi kamili katika matumizi ya kiulizi '-pi' kupitia zoezi la 6.8 la sehemu hii ya matumizi ya lugha ambapo wanafunzi wanatakiwa kutumia kipatanishi kinacofaa kulingana na ngeli inayohusika. Zoezi hili lisahihishwe kwa kuwashirikisha wanafunzi wote na maelezo ya mwalimu yatilie mkazo pale ambapo wanafunzi wanatatizika. Mwishowe, mwalimu awaombe wanafunzi wafanye zoezi la 6.9 katika sehemu hii ambapo wanahitajika kuandika sentensi za zoezi la 6.8 katika umoja au wingi. Mwalimu ahakikishe kuwa zoezi hili limesahihishwa kabla ya somo lijalo.

**Tathmini ya kipindi ca 18**

Mwalimu ahitimishe kipindi hiki kwa kuuliza maswali yanayodhamiria kucunguza iwapo wanafunzi wameelewa namna ya kuuliza maswali kadhaa

kuhusu jinsi au namna ya kufanya jambo fulani na mabadiliko ya kiupatanishi yanayoweza kuzingatiwa katika matumizi ya kiulizi ***'-pi'***. Hivyo basi, mabadiliko ya kiupatanishi yanayozingatiwa katika matumizi ya kiulizi ***'-pi'*** nayo yarejelewe kulingana na nomino mbalimbali na ngeli zake tofauti. Wanafunzi nao, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kwa kudhihirisha iwapo wameelewa mambo yote muhimu yaliyotakikana kuzingatiwa katika kipindi hiki.

## Maelezo muhimu kwa mwalimu

Kiulizi '***-pi***' hutumika kuulizia swali kwa kumtaka mtu achague kitu kimoja au vitu fulani miongoni mwa vitu vingine vilivyopo.

**Kwa mfano:**

**Swali:** Mwalimu ***yu***pi ni mgonjwa?

**Jibu:** Mwalimu mgonjwa ni **Bw. Gatete.**

*Walimu ni wengi lakini mzungumzaji anauliza swali ili ajue mwalimu mgonjwa miongoni mwa walimu wengi.*

**Swali:** Walimu ***wa***pi ni wagonjwa?

**Jibu:** Walimu wagonjwa ni **Bw. Gatete** na **Bi. Mutoni.**

*Walimu ni wengi lakini mzungumzaji anauliza swali ili ajue walimu wagonjwa tu miongoni mwa walimu wote waliopo.*

Kiulizi '-pi' hutumika kulingana na ngeli inayohusika.

**Kwa mfano:**

| **Umoja** | **Wingi** | **Ngeli** |
|---|---|---|
| Mvuvi ***yu***pi anavua? | Wavuvi ***wa***pi wanavua? | A-WA |
| Kisu ***ki***pi kinanolewa? | Visu ***vi***pi vinanolewa? | KI-VI |
| Mkeka ***u***pi umesukwa? | Mikeka ***i***pi imesukwa? | U-I |
| Nguo ***i***pi imeuzwa? | Nguo ***zi***pi zimeuzwa | I-ZI |
| Wembe ***u***pi umemkata? | Nyembe ***zi***pi zimewakata? | U-ZI |

### 6.6 Mazoezi ya ziada

#### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu aulize maswali yafuatayo katika zoezi la ziada ili kuinua kiwango ca cini ca wanafunzi dhaifu; yaani wanafunzi wasioweza kuelewa haraka kama wenzao.

*Tunga sentensi katika umoja na wingi kwa kutumia kiulizi '-pi' pamoja na majina haya:*

1. *ng'ombe*
2. *kisiwa*
3. *maji*
4. *kuimba*
5. *wimbo*
6. *dirisha*

**Kwa mfano:** Dirisha

**Jibu:** Dirisha ***lipi*** litatengenezwa? – Madirisha ***yapi*** yatatengenezwa?

#### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe maneno waliyopewa.

**Kwa mfano:**

1. *Kisiwa kipi kinapatikana Rwanda?* - *Visiwa vipi vinapatikana Rwanda?*
2. *Maji yana faida ipi kwa mtu?* - *Maji yana faida zipi kwa watu?*

#### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango ca juu ca uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge sentensi sahihi katika umoja na wingi, kwa kutumia ngeli zozote kumi za Kiswahili pamoja na kiulizi '***-pi'***.

**Kwa mfano**: Ngeli ya A-WA

**Jibu:** Mbuzi ***yupi*** atacinjwa? – Mbuzi ***wapi*** watacinjwa?

#### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe ngeli zozote kumi za Kiswahili pamoja na kiulizi ***'-pi'***.

# 6.7 Majibu

**Zoezi la makundi, ukurasa 40**

Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi kwa kurejelea micoro iliyopo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 40.

**Kwa mfano:**

*Micoro hii inaonyesha umuhimu wa maji. Mcoro A unaonyesha maji ni muhimu kwa usafiri, mcoro B unaonyesha kuwa maji ni muhimu kwa kufulia nguo na mcoro C unaonyesha kuwa maji ni muhimu kwa kuhifadhi samaki ambao huvuliwa na kuwa cakula kwa binadamu.*

**i) Maswali ya ufahamu, ukurasa 42**

1. Maji ni muhimu kwa afya zetu kwa sababu sisi hunywa maji ambayo huhitajika katika mili yetu, maji hutumiwa kupikia vyakula mbalimbali ambavyo vikiliwa huipa mili yetu virutubisho muhimu, maji hutumiwa kufulia nguo, kuoga, kusafisha vyombo na makazi yetu hivyo kuepukana na ucafu ambao ni canzo ca maradhi mbalimbali.
2. Maji hutumiwa kupikia cakula, kunawa na kuosha miili yetu, kusafisha vyombo, kufua nguo, katika ujenzi wa barabara, nyumba na hoteli, katika ukulima, ufugaji na utunzaji wa mbuga zetu za wanyama.
3. Binadamu na wanyama huweza kufariki. Mimea hunyauka hivyo cakula kukosekana. Bila maji, nguo zetu haziwezi kufuliwa na nyumba zetu haziwezi kusafishwa. Ukosefu wa maji ni canzo ca ucafu ambao huleta magonjwa ya aina mbalimbali.
4. Rwanda ina mito na maziwa mengi. Mvua hunyesha kwa kipimo kizuri.
5. *Ziwa Kivu* kwenye sehemu za Magharibi mwa nci katika wilaya za Rubavu, Rutsiro, Karongi, Nyamasheke na Rusizi, *Ziwa la Cyohoha I* na *Ziwa la Cyohoha II*, *Ziwa Rweru* wilayani Bugesera, *Ziwa Burera* na *Ziwa Ruhondo* katika sehemu za Kaskazini wilayani Burera, *Ziwa Muhazi* kuanzia sehemu za Gasabo, Rwamagana na Gicumbi, *Ziwa Mugesera* katika sehemu za wilayani Rwamagana, Bugesera na Ngoma.
6. Mto Nyabarongo, Mto Akanyaru, Mto Akagera, Mto Mukungwa, Mto Rusizi, Rukarara.
7. Kituo ca Nyabarongo, kituo ca Ntaruka na kituo ca Rusizi.
8. Ukanda wa maziwa makuu
9. Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi na Uganda

10. Visiwa vingi ambavyo hupatikana katika maziwa mbalimbali.Watalii wengi hufurahia kuzuru mazingira ya maziwa mbalimbali. Kuabiri vyombo mbalimbali vya majini huwafurahisha watalii pia.

ii) Mwalimu atathmini muhtasari wa kila kikundi. Sharti kila muhtasari uhusu mambo muhimu pekee ambayo yamejitokeza katika kifungu ca habari walicosoma hapo awali.

**Kwa mfano:**

*Maji ni muhimu kwa binadamu kwa sababu hutumiwa katika upishi na katika usafi wa mwili na vyombo. Shughuli za ujenzi wa nyumba na barabara pia hutegemea maji. Wanyama hali kadhalika huhitaji maji ili kukata kiu. Rwanda ina maji ya kutosha kwa sababu ya kuwepo kwa maziwa mengi na pia mvua hunyesha kwa kipimo kizuri. Kuna mito ambayo ndani mwake kuna vituo vya kuleta nguvu za umeme. Mito hii ni kama vile: Akanyaru, Nyabarongo, Akagera na Mukungwa. Nci ya Rwanda ni miongoni mwa nci za ukanda wa maziwa makuu kwa sababu ya maziwa yanayopatikana ndani mwake. Maziwa haya ni kama vile: Kivu, Rusizi na Nyamasheke. Pia kuna visiwa ambavyo huzungukwa na maziwa ncini Rwanda. Maziwa haya huwavutia watalii wengi. Watalii hao hufurahia kutazama na kusafiri katika vyombo vya majini maziwani humo.*

**Zoezi la 6.1, ukurasa 42**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti sentensi hizo zizingatie matumizi sahihi ya msamiati ulioteuliwa.

**Kwa mfano:**

1. *Mzazi wangu <u>anatimiza</u> ahadi yake ya kunipeleka shuleni.*
2. *Mama <u>hufua</u> sare zangu za shule.*
3. *<u>Ukosefu</u> wa mvua husababisha kiangazi.*

**Zoezi la 6.2, ukurasa 42-43**

1. ***<u>Kisiwa</u>*** ca Ijwi kinapatikana ziwani Kivu.
2. ***<u>Mtalii</u>*** huyu alilipa pesa nyingi ili aweze kuingia katika nyumba hii ya kitalii.
3. ***<u>Mbuga ya wanyama</u>*** ya Akagera inatembelewa na wageni wengi kutoka nci mbalimbali.
4. Walimu wetu wanatarajia kwenda Karongi ili kufurahia mazingira ya ***<u>ziwa</u>*** la Muhazi.
5. Watalii wawili walienda kwa gari zuri kutazama ***<u>mto</u>*** Mukungwa.

**Zoezi la 6.3, ukurasa 43**

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika majadiliano yao. Ahakikishe kuwa wanajadiliana kwa kujibu maswali waliyopewa katika vitabu vyao.

**Zoezi la 6.4, ukurasa 43**

1. ***kisiwa:*** kipande ca ardhi kilicozungukwa na maji pande zote
2. ***kuogelea:*** kwenda ndani ya maji
3. ***mbinu:*** namna ya kufanya jambo
4. ***kucangia:*** kutoa fedha au mali kwa kusaidia jambo fulani ili lifanywe
5. ***kuzunguka:*** kwenda huku na huku
6. ***ukanda:*** sehemu yenye hali fulani ya hewa, zoni
7. ***kuzalisha:*** kupata faida kwa kufanya biashara

**Zoezi la 6.5, ukurasa 44**

Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanalinganisha kwa usahihi pica walizopewa pamoja na sentensi walizopewa. Yaani:

1. - C
2. - D
3. - A
4. - B

**Zoezi la 6.6, ukurasa 44**

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kuendeleza majadiliano yao. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanajadiliana kwa kujibu maswali yaliyoorodheshwa vitabuni mwao.

**Zoezi la 6.7, ukurasa 45**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe kiulizi '***-pi'***.

**Kwa mfano:**

1. *Nitatumia kalamu ipi?* – *Tutatumia kalamu zipi?*
2. *Mti upi utakatwa?* – *Miti ipi itakatwa?*

**Zoezi la 6.8, ukurasa 45**

1. Mtoto ***yupi*** anaweza kupika uji?
2. Viatu ***vipi*** vilinunuliwa na wageni hawa?
3. Ng'ombe ***wapi*** walicinjwa sokoni jana?
4. Kikombe ***kipi*** kilijazwa cai?
5. Ubao ***upi*** ulitengenezwa wiki iliyopita?

**Zoezi la 6.9, ukurasa 45**

1. Watoto ***wapi*** wanaweza kupika uji?
2. Kiatu ***kipi*** kilinunuliwa na mgeni huyu?

3. Ng'ombe ***yupi*** alicinjwa sokoni jana?
4. Vikombe ***vipi*** vilijazwa cai?
5. Mbao ***zipi*** zilitengenezwa wiki zilizopita?

**Majibu ya tathmini ya mada ya 1**

**Zoezi la 1, ukurasa 46**

1. Mbuga za wanyama, milima, mito, misitu, vyanzo vya maji pamoja na mazingira safi ya Rwanda.
2. Pundamilia, swara, simba, ndovu, twiga n.k.
3. Sokwe watu
4. Kwa sababu utamaduni wetu hutukumbusha asili yetu na hivyo kutuunganisha pamoja kama Wanyarwanda.

**Zoezi la 2, ukurasa 46**

1. Wewe huandika ubaoni wakati wa somo letu.
2. Mimi na ndugu yangu hupika cakula baada ya somo letu.
3. Wewe na Mtalii huyu hufurahia kutazama mnyama yule.
4. Mkulima huyu na Semana hulima shamba lao katika mwezi wa Februari.
5. Wanafunzi hawa huimba nyimbo za kufurahisha.

**Zoezi la 3, ukurasa 47**

1. Naira
2. Yeni
3. Kwaca
4. Faranga
5. Dola

**Zoezi la 4, ukurasa 47**

1. Kioo **kipi** kilivunjika?
2. Mlima **upi** una wanyamapori wengi?
3. Ufagio **upi** uliharibika?
4. Ndizi **ipi** ni ya mtoto huyu?
5. Mzigo **upi** ni wa mgeni huyu?

**Zoezi la 5, ukurasa 47**

1. Nani
2. Nini
3. Nani
4. Nini
5. Nini

**Zoezi la 6, ukurasa 47**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga kwa kutumia kiulizi '***kwa nini***'.

**Kwa mfano:**

1. ***Kwa nini*** ulicelewa shuleni jana?
2. ***Kwa nini*** hujakamilisha zoezi tulilopewa na mwalimu?
3. ***Kwa nini*** mbuga ya Akagera huvutia watalii?
4. ***Kwa nini*** unalia?
5. ***Kwa nini*** unaenda sokoni leo?

Sura ya **Pili**

# Mada Kuu 2: Lugha na matukio ya kijamii na kitaifa

## Mada Ndogo: Sikukuu na sherehe nchini Rwanda

**Uwezo upatikanao katika mada hii:**

Mwanafunzi aweze kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika kwa kutumia lugha katika muktadha wa sikukuu na sherehe katika jamii anamoishi.

### Malengo ya kujifunza

| Maarifa na ufahamu | Stadi | Maadili na mwenendo mwema |
|---|---|---|
| • Kuonyesha ustadi katika kubainisha na kutaja msamiati kuhusu sikukuu na sherehe mbalimbali ncini Rwanda. | • Kutumia tarehe na majina sahihi ya sikukuu na sherehe ncini Rwanda anaposhiriki katika mawasiliano. | • Kuheshimu na kukuza mila na desturi za nci kutokana na sikukuu zinazosherehekewa. |
| • Kuonyesha ujuzi wa kusoma kalenda kwa usahihi hususani namna ya kucunguza siku kwenye kalenda (matumizi ya kalenda) na kuzitumia katika mawasiliano ya kila siku. | • Kutumia kalenda kwa urahisi katika kurejelea siku, tarehe, ratiba za kazi na matukio mengine yaliyopita na yajayo katika mawasiliano ya kila siku. | • Kujenga tabia ya kujali ratiba ya utekelezaji wa majukumu yake na ya watu wengine. |
| • Kukumbuka sikukuu zote muhimu na kueleza sababu za kila sikukuu na sherehe ncini Rwanda anapohitajika kufanya hivyo katika mawasiliano. | • Kutumia vyema alama za uakifishaji na herufi kubwa kwa kuzingatia muktadha husika. | |
| • Kueleza kwa ufasaha katika maandishi na mazungumzo juu ya sikukuu aliyohudhuria hapo zamani. | • Kulinganisha na kutofautisha matumizi ya wakati uliopita na wakati ujao katika masimulizi kuhusu matukio mbalimbali katika jamii. | |
| • Kukumbuka matumizi sahihi ya wakati uliopita kuhusu vitenzi vyenye silabi moja katika hali yakinishi na hali kanushi. | | |
| • Kuonyesha uelewa wa matumizi ya herufi kubwa pamoja na matumizi ya alama za vituo. | | |

## Maelezo kwa mwalimu

Mada hii inahusiana na somo la Sayansi ya Jamii kuhusu mada ya mwenendo bora, somo la Hesabu hasa kuhusiana na matumizi ya kalenda pamoja na somo la Historia kuhusiana na historia ya Wanyarwanda.

Mada hii inashughulikia sikukuu na sherehe mbalimbali ncini Rwanda. Shughuli za sherehe na sikukuu ncini Rwanda ni mambo muhimu na rasmi katika mila na desturi za Wanyarwanda. Kuna sherehe za kisiasa na kihistoria, sherehe za kidini, kijamii na za kienyeji. Sikukuu mbalimbali pamoja na sherehe zao huwasaidia Wanyarwanda kusherehekea matukio mbalimbali kama vile: sherehe za harusi, kupeana ng'ombe, kulima, *Umuganda* n.k. Sikukuu za kisiasa zina umuhimu wa kuhifadhi kumbukumbu za matukio ya kisiasa yaliyokuwa maarufu sana katika nci yetu siku za kale. Katika kalenda ya taifa kuna sherehe zinazoadhimishwa kama kumbukumbu za maisha ya wazee wetu wa kale. Mfano ni siku ya *Umuganura*. Miongoni mwa sikukuu za kisiasa ni: sikukuu ya mashujaa wa taifa, sikukuu ya watumishi, sikukuu ya uhuru, sikukuu ya Ukombozi na nyinginezo. Somo hili pia linahusisha matumizi ya nyakati mbalimbali kama vile: wakati uliopita na wakati ujao katika hali yakinishi, kanushi na kuuliza.

## Masuala mtambuka

Baadhi ya masuala mtambuka ambayo yatashughulikiwa katika mada hii ni usawa wa kijinsia, elimu ya pamoja, amani na maadili pamoja na mazingira, mabadiliko ya hali ya hewa na mwendelezo wake.

Amani na maadili yatashughulikiwa kupitia kwa Wanyarwanda kuwa na mazoea ya kukusanyika pamoja mara kadhaa katika mwaka kwa ajili ya sherehe na sikukuu rasmi pamoja na za kijamii. Katika harakati hizi, umoja na amani miongoni mwa Wanyarwanda huhimizwa. Wanafunzi waelekezwe kutangamana kwa amani na upendo. Usawa wa kijinsia utatiliwa mkazo kwa kuwafahamisha wanafunzi kuwa wasicana pamoja na wavulana wana uwezo sawa wa kufaulu katika maisha yao lica ya jinsia zao tofauti. Elimu ya pamoja itaendelezwa kupitia kwa wanafunzi wote kusoma pamoja kwa kuwashirikisha hata na wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali na matatizo mbalimbali. Elimu hii ya pamoja pia itahusisha wanafunzi wote kuwakubali na kushirikiana kwa pamoja na wenzao kutoka katika matabaka mbalimbali ya kijamii. Wanafunzi pia watafundishwa umuhimu wa mazingira yao na namna ya kuyahifadhi.

## Uwezo wa jumla

Katika ufundishaji wa somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanapata

uwezo wa kuwa na stadi za utafiti, tafakuri tanduizi, usuluhishaji wa matatizo, mawasiliano katika lugha rasmi, ubunifu na ugunduzi, ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha pamoja na ujifunzaji wa muda mrefu.

Mwalimu awaelekeze na awashirikishe wanafunzi wote katika kuwa na tafakuri tanduizi kwa kufikiri kwa undani zaidi kuhusiana na watakayofundishwa katika somo hili. Ujuzi huu utawawezesha kuyajibu maswali katika somo hili.

Kupitia kwa mazoezi ya kuigiza mazungumzo mbalimbali watakayokumbana nayo, wanafunzi watahimizwa kuwasiliana kwa lugha rasmi pamoja na kuwa na utawala binafsi pamoja na kuzifahamu stadi mbalimbali za maisha. Stadi za utafiti zitakuzwa kupitia kwa wanafunzi kufanya utafiti kuhusiana na sherehe na sikukuu mbalimbali zilizo rasmi, za kitaifa na kijamii. Ujifunzaji wa muda mrefu uendelezwe kupitia kwa wanafunzi kupata maarifa mbalimbali kuhusiana na siku muhimu ncini mwao watakayotumia nje ya darasa na katika maisha yao ya kila siku na kuwa wazalendo kamili.

### Msamiati maalum

Msamiati maalum na muhimu ambao wanafunzi watapatana nao katika mada hii ni kuhusu sherehe na sikukuu rasmi za kitaifa na kijamii ncini Rwanda kama vile:

| | Msamiati | Maana |
|---|---|---|
| 1. | ***sherehe*** | karamu au shamrashamra zinazofanywa ili kufurahia matukio fulani. |
| 2. | ***ukombozi*** | vita au matendo ya kuwaokoa watu kutoka kwenye hali mbaya yenye mateso. |
| 3. | ***wananci*** | watu ambao ni wenyeji wa nci fulani. |
| 4. | ***Umuganura*** | sherehe ya Wanyarwanda ya kutoa shukrani hasa kwa ajili ya mazao waliyopata na kugawana katika matabaka yote. |
| 5. | ***kalenda*** | kifaa ambaco huonyesha idadi ya siku, wiki na miezi. |
| 6. | ***sikukuu*** | siku maalum iliyo na sherehe za kuadhimisha tukio fulani. |
| 7. | ***matukio*** | jambo ambalo lilitokea au lilitendeka. |
| 8. | ***huadhimishwa*** | sherehekea tukio muhimu ambalo lilitokea au lilitendeka. |
| 9. | ***serikali*** | mfumo wa mamlaka ya kutawala nci au eneo fulani. |
| 10. | ***mashujaa*** | watu wanaoweza kukabiliana na mambo ya hatari bila woga. |

### Usuluhishaji wa tatizo

Katika sehemu hii, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi yanayotakikana kulingana na zoezi husika kisha awaombe wacunguze kwa makini kalenda ya mwaka wa 2016 iliyo katika Kitabu ca Mwanafunzi, ukurasa 49 kuhusiana na sherehe na sikukuu rasmi za kitaifa na kijamii. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika shughuli hii. Wanafunzi wacunguze kalenda hiyo na mwalimu awaulize maswali kama vile: Mnaona nini kwenye kalenda hiyo? Tarehe zilizoandikwa kwa wino mwekundu huadhimishwa kwa sababu gani? Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika makundi yao ili waweze kujibu maswali hayo na kuelewa kalenda husika. Kwa hivyo, mwalimu acocee uwezo wa wanafunzi wa kupata maarifa kuhusu ubunifu na ugunduzi na tafakuri tanduizi kwa kucunguza na kujibu maswali kuhusu kalenda husika.

### Ushirikishaji wa wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali

Mwalimu awe na vifaa maalum vya kuwasaidia wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali katika kusoma kwao. Kwa wanafunzi wasio na uwezo wa kuona, mwalimu ahusishe matumizi ya breli pamoja na vifaa vya kunasia sauti.

Kwa wanafunzi wasio na uwezo wa kusikia, mwalimu anaweza kuhusisha matumizi ya lugha ya ishara. Mwalimu anaweza kuwahusisha watafsiri wa lugha ya ishara. Haya yatawawezesha wanafunzi hawa kusoma kama wanafunzi wenzao bila vikwazo vyovyote.

Nafasi ya wanawake na walemavu katika shughuli kama vile za kuungana na Wanyarwanda wengine kuadhimisha sherehe na sikukuu rasmi mbalimbali itiliwe maanani kupitia kwa mcoro ulio katika Kitabu ca Mwanafunzi ukurasa 59 ili kukuza usawa wa kijinsia na elimu ya pamoja. Hili litadumisha ushirikiano na mienendo mizuri miongoni mwa wanafunzi na kuwafanya kuwa wazalendo kamili katika umri wao.

### Orodha ya masomo na vipindi

| Mada ya somo | Idadi ya vipindi |
|---|---|
| **Somo la 7:** Sikukuu na sherehe katika kalenda | 4 |
| **Somo la 8:** Maadhimisho mbalimbali ncini Rwanda | 4 |
| **Somo la 9:** Matumizi ya kalenda ya mwaka | 4 |
| | **JUMLA: 12** |

# Somo la 7: Sikukuu na sherehe katika kalenda

## Kipindi cha 1: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati

**a) Malengo ya somo**

- Kusoma kwa usahihi kifungu ca habari kwa utambuzi wa herufi, silabi, maneno na sentensi;
- Kutaja umuhimu wa sikukuu na sherehe katika jamii ncini Rwanda.
- Kuelewa thamani ya sikukuu na sherehe mbalimbali katika jamii.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Micoro au pica za kalenda ya miezi yote ionyeshayo sikukuu na sherehe mbalimbali ncini Rwanda.
- Micoro au pica za Wanyarwanda wakiadhimisha sherehe mbalimbali;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 49-52;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Somo hili linahusu sikukuu na sherehe mbalimbali ncini Rwanda. Kifungu kilico katika *Kitabu ca Mwanafunzi* ukurasa 50 kinasimulia aina mbalimbali za sherehe na sikukuu zinazoadhimishwa ncini Rwanda. Kalenda ya mwaka 2016 inaonyesha wazi sikukuu hizo kuanzia mwezi wa Januari mpaka mwezi wa Disemba. Kila sherehe imefafanuliwa na kuelezwa kwa kifupi pamoja na sababu ya kuadhimishwa kwake. Sherehe zote na sikukuu za kisiasa, kidini, kihistoria na kienyeji zimeshughulikiwa. Mwalimu aandae mpangilio wa sherehe na sikukuu mbalimbali ncini ili wanafunzi waelewe vizuri mfuatano wa sikukuu na sherehe hizo katika kalenda ya mwaka. Ikiwa kuna sherehe au sikukuu iliyoadhimishwa siku cace zilizopita, wanafunzi wajadili tukio hilo.

**d) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu atangulize somo hili kuhusu sherehe na sikukuu ncini Rwanda kwa kuwauliza wanafunzi maswali mepesi ya

kuwacangamsha. Maswali kama vile: *Nyinyi huadhimisha mwaka mpya vipi? Nani amewahi kuhudhuria maadhimisho ya sikukuu yoyote ncini? Taja majina ya sikukuu unazozifahamu. Taja sikukuu inayoadhimishwa tarehe ya kwanza mwezi Januari* n.k. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika majadiliano haya. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu.

Baadaye, mwalimu aendelee na somo kwa kuwaomba wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wanne wanne watazame pica zilizo kwenye *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 49. Mwalimu awaulize wanafunzi maswali kuhusu pica hizo. Kwa mfano: *Mnaona nini kwenye pica hizi?* Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kujibu maswali waliyoulizwa kwa kuwapa kitangulizi kama vile *"Mimi ninaona..."* Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu. Kwa mfano, "*Mimi ninaona kalenda ya mwaka 2016*." Katika sehemu hii, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi wake ili wapate ujuzi kuhusu tafakuri tanduizi, ubunifu na ugunduzi kwa kuwaonyesha micoro husika huku wanafunzi nao wakifikiri na kugundua kile kinacoendelea au kinacoonekana katika micoro hiyo. Mwalimu anaweza kuwaonyesha wanafunzi micoro au pica za maadhimisho ya sherehe mbalimbali ncini.

### 7.1 Kusoma na ufahamu

### Kifungu kuhusu sikukuu na sherehe ncini Rwanda

Mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wanne wanne wasome kwa kimya kifungu ca habari kuhusu sikukuu na sherehe ncini Rwanda kilico katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 50. Wanafunzi wasome kwa kimya huku wakitambua na kuandika msamiati mpya wanaopatana nao. Hatimaye, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu kifungu walicosoma ili kuhakikisha kuwa wamekisoma na kukielewa. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuwauliza: *Sikukuu inayoadhimishwa mwezi Agosti ni ipi?* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma kutoka kwenye kifungu hico. Kwa mfano, wanafunzi wanaweza kujibu: *Sikukuu inayoadhimishwa mwezi Agosti ni sherehe za Umuganura*. Baada ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wamesoma kwa kimya kifungu kilicopo na kukielewa, mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa sauti kifungu hico kwa kuhakikisha kuwa wanatamka maneno kwa namna inayofaa. Mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa. Baadaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi kujibu maswali ya ufahamu waliyopewa. Mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika.

Hatimaye, awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali hayo ya ufahamu huku akitoa maelezo pale ambapo wanatatizika. Mwalimu awasaidie wanafunzi wenye matatizo ya kuelewa msamiati uliotumika katika kifungu hico.

### 7.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu sikukuu ncini Rwanda

Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kuwaomba wajadili maana za msamiati mpya ambao walipatana nao katika usomaji wa kifungu walicopewa. Wanafunzi waeleze maana ya msamiati husika kwa kuzingatia jinsi ulivyotumiwa katika kifungu ca habari walicokisoma. Mwalimu awaombe wanafunzi watumie kamusi ya Kiswahili pale wanapoihitaji. Mwalimu azunguke darasani akiwaelekeza wanafunzi wanaopata taabu katika kuitumia kamusi au kufafanua maana ya msamiati husika. Baadaye, awaombe wanafunzi kucunguza msamiati uliopigiwa mstari katika sentensi walizopewa katika zoezi la 7.1 A. Mwisho, awaombe wanafunzi wajadili maana za msamiati huo uliopigiwa mistari. Katika sehemu B ya zoezi la 7.1, wanafunzi waelekezwe kutunga sentensi zao wenyewe kwa kutumia msamiati uliopigiwa mstari katika sentensi za sehemu A ya zoezi la 7.1. Ni vyema mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia na kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika. Baada ya wanafunzi hawa kukamilisha zoezi walilopewa, mwalimu awaombe wanafunzi kusahihisha kwa pamoja mazoezi hayo ya msamiati. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wameelewa msamiati uliokuwa mpya kwao, mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi wataje msamiati ambao hawakuelewa maana yake ili ujadiliwe tena kwa pamoja darasani kulingana na matumizi yake katika kifungu walicosoma. Ni vyema mwalimu azingatie kwamba utunzi wa sentensi za wanafunzi ndio utakaomfahamisha iwapo wanafunzi wamepata ujuzi unaotakikana katika tafakuri tanduizi, suluhisho kwa matatizo na mawasiliano kwa lugha rasmi na sahihi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kufanya zoezi la 7.2.

### Tathmini ya kipindi ca 1

Mwalimu ahitimishe funzo hili kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali hayo yaegemee haswa kwa kucunguza iwapo wanafunzi wanaweza kuzitaja na kuzieleza sherehe na sikukuu rasmi katika kalenda yao pamoja na kutumia msamiati mpya waliojifunza kuhusu sherehe na sikukuu mbalimbali ncini Rwanda, thamani ya sherehe na sikukuu hizo na umuhimu wao.

## Kipindi cha 2: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza

**a) Malengo ya somo**

- Kujadili umuhimu wa sikukuu na sherehe katika jamii ncini Rwanda;
- Kufahamu shughuli mbalimbali zinazofanyika katika sherehe na sikukuu mbalimbali;
- Kuelewa thamani ya sikukuu na sherehe mbalimbali katika jamii.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Micoro au pica za kalenda ya miezi yote ionyeshayo sikukuu na sherehe mbalimbali ncini Rwanda;
- Micoro au pica zinazoonyesha watu katika maadhimisho mbalimbali;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 52-53;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia, n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Sehemu hii itahusisha majadiliano ya wanafunzi katika makundi mbalimbali. Wanafunzi pia watapewa nafasi ya kutoa masimulizi yao wenyewe kuhusu namna wanavyoadhimisha sherehe mbalimbali. Micoro pamoja na pica zinazoonyesha watu wakiadhimisha sherehe mbalimbali itafaa hapa. Kalenda ya mwaka pia itahitajika katika kufundisha sehemu hii.

Sherehe zote na sikukuu za kisiasa, kidini, kihistoria na kienyeji zitashughulikiwa. Mwalimu aandae mpangilio wa sherehe na sikukuu mbalimbali ncini ili wanafunzi waelewe vizuri mfuatano wa sikukuu na sherehe hizo katika kalenda ya mwaka.

**d) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Mwalimu aanze kipindi kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mepesi ya kuwacangamsha kuhusu sherehe na sikukuu mbalimbali ncini Rwanda. Mifano ya maswali hayo ni kama vile: *Nyinyi huadhimisha Krismasi vipi? Nani amewahi kuhudhuria maadhimisho ya sikukuu yoyote ncini? Waislamu huadhimisha Idi-ul-Fitr vipi?*

*Taja majina ya sikukuu unazozifahamu,* n.k. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika majadiliano haya. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu.

## 7.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watano watano kisha awaombe wajadili kuhusu mambo ambayo hufanyika katika maadhimisho ya sikukuu mbalimbali. Wanafunzi waelezane:

1. *Shughuli zote zinazofanyika katika sherehe za mwaka mpya.*
2. *Nguo unazopenda kuvaa unapoenda katika sherehe za harusi.*
3. *Sikukuu unayopenda kuadhimisha katika kalenda. Toa sababu.*
4. *Umuhimu wa sikukuu na sherehe mbalimbali kwa Wanyarwanda.*
5. *Umuhimu wa kuwa na Kalenda rasmi nyumbani.*

Mbali na hayo, mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kusimulia umuhimu wa sherehe na sikukuu mbalimbali katika jamii. Katika makundi yao, wanafunzi wasimuliane kuhusu sikukuu za kidini kama vile: *Pasaka, Idi ul Fitri* n.k. Mwalimu anaweza kuwaomba wanafunzi Wakristo na Waislamu (iwapo wapo) wawasimulie wenzao kuhusu matukio ya sherehe hizi za kidini. Mwalimu awasimulie wanafunzi kuhusu sikukuu za kisiasa kama vile: *sikukuu ya Uhuru, sikukuu ya Ukombozi,* n.k. Maelezo haya yote yatawawezesha wanafunzi kuelewa tofauti kati ya sikukuu hizo mbalimbali pamoja na umuhimu wao kwa Wanyarwanda.

## 7.4 Kusikiliza na kuzungumza: Maigizo

Katika hatua hii, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha watunge na kuigiza mcezo mfupi kuhusu sherehe na sikukuu mbalimbali ncini Rwanda. Wanafunzi wadhihirishe ubunifu wao kuhusu shughuli zinazofanyika katika sikukuu na sherehe mbalimbali ncini Rwanda. Mwalimu ayafuate kwa karibu maigizo ya wanafunzi ili kuwakosoa wanapofanya makosa yoyote. Lugha ya Kiswahili sanifu na rasmi itumike, wanafunzi wawe na motisha wa kuigiza na mwalimu awahimize kuipenda nci yao pamoja na viongozi wao. Kutokana na maigizo ya wanafunzi katika makundi yao, mwalimu awaombe wanafunzi wajadiliane kuhusu sherehe na sikukuu za kijamii ncini Rwanda, kwa mfano: *Umuganura*.

## Zoezi la imla

Mwalimu awaombe wanafunzi wafunge vitabu vyao kisha wafungue madaftari yao na waandike maneno au vifungu vya maneno haya ambayo mwalimu atawasomea. Mwalimu awasomee wanafunzi maneno haya:

*1. Kuadhimisha 2. Sherehe 3. Krismasi 4. Idi-ul-Fitr 5. Umaganura*

*6. Idi ul Adha 7. Sherehekea 8. Kalenda 9. Mauaji ya kimbari 10. Sikukuu rasmi*

Mwalimu ahakikishe kuwa anayatamka maneno haya kwa matamshi sahihi na kwa sauti ili kila mwanafunzi aweze kuyasikia vizuri. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha zoezi hili.

**Tathmini ya kipindi ca 2**

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti ya kucunguza iwapo wanaweza kurejelea sherehe na sikukuu mbalimbali ncini Rwanda, shughuli mbalimbali za sherehe na sikukuu hizi katika jamii ya Wanyarwanda, tarehe za kuadhimisha sikukuu hizi n.k ili kutathmini iwapo wanafunzi wameelewa funzo hili. Kupitia kwa masimulizi ya wanafunzi pamoja na maigizo yao, wanafunzi wakuze ujasiri wao wa kuzungumza mbele ya watu na pia matumizi yao ya lugha rasmi na sahihi yaimarike zaidi.

## Kipindi cha 3: Sarufi (Wakati uliopita)

**a) Malengo ya somo**

- Kufahamu matumizi ya wakati uliopita;
- Kutunga sentensi sahihi katika wakati uliopita.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Masimulizi yaliyoandikwa katika wakati uliopita;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 53-56;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Mwalimu aandae masimulizi kadhaa yaliyoandikwa katika wakati uliopita ambayo atawasomea wanafunzi. Mwalimu anaweza pia kuwasimulia wanafunzi mambo yaliyopita. Masimulizi haya yanaweza kuhusisha sherehe na sikukuu mbalimbali ambazo huadhimishwa ncini Rwanda. Kalenda ya mwaka wa 2016 inaweza kutumika hapa ili kurejelea maadhimisho ya mwaka huo uliopita wa 2016. Ikiwa kuna sherehe au sikukuu iliyoadhimishwa siku cace zilizopita, wanafunzi wajadili tukio hilo.

### d) Utaratibu wa somo

### Utangulizi

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi ca 2. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa.

Mwalimu atumie masimulizi aliyoyaandaa kutanguliza funzo hili.

### 7.5 Sarufi: Matumizi ya wakati uliopita

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha awaombe watazame micoro iliyo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 53. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua kinacoendelea katika micoro hiyo. Katika makundi yao, wanafunzi wasome kifungu kifupi ca habari kilico kwenye *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 53 na kukijadili. Wanafunzi waelekezwe kutambua vitenzi vilivyotumika katika wakati uliopita.

Baadaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi kusimulia walivyosherehekea mwaka mpya uliopita. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kusimulia matukio yao kwa kutumia wakati uliopita. Baada ya masimulizi ya wanafunzi, mwalimu awaombe wanafunzi waeleze matumizi ya viambishi vya wakati uliopita katika sentensi.

Mwalimu awaeleze wanafunzi kuwa:

*Wakati uliopita huonyesha matukio ambayo tayari yameshatendeka.Wakati uliopita hutumia kiambishi ca wakati* ***-li-.*** *Kiambishi hiki hutumika katika nafsi zote za Kiswahili.*

***Mifano:***

a) *Ni**li**tembea pamoja na kakangu.*
b) *A**li**kuwa mzee sana.*
c) *Mimi ni**li**pika wali jana.*
d) *Kwa nini u**li**kasirika juzi?*
e) *Sisi tu**li**vuna mahindi wiki i**li**yopita.*

Baadaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi kufanya zoezi la 7.3, zoezi la 7.4 na zoezi la 7.5. Wanafunzi wote washirikishwe katika shughuli hii.

### Tathmini ya kipindi ca 3

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali ya kucunguza iwapo wanafunzi wameelewa matumizi ya wakati uliopita katika sentensi na mawasiliano yao kwa jumla. Maswali mengine yalenge kutathmini kiwango ca uelewa wa wanafunzi wa kutunga sentensi sahihi kisarufi.

## Kipindi cha 4: Sarufi (Wakati ujao)

**a) Malengo ya somo**

- Kufahamu matumizi ya wakati ujao;
- Kutambua viambishi vya wakati ujao;
- Kutunga sentensi sahihi katika wakati ujao.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Masimulizi yaliyoandikwa katika wakati ujao;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 56-58;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Mwalimu aandae masimulizi kadhaa yaliyoandikwa katika wakati ujao ambayo atawasomea wanafunzi. Mwalimu anaweza pia kuwasimulia wanafunzi kuhusu mambo anayotarajia yanaweza kufanyika. Haya ni mambo ambayo bado hayajafanyika lakini kuna uwezekano wa kufanyika hapo baadaye au usoni. Masimulizi haya yanaweza kuhusisha sherehe na sikukuu mbalimbali ambazo huadhimishwa ncini Rwanda. Kalenda ya mwaka wa 2018 inaweza kutumika hapa ili kurejelea maadhimisho ya mwaka ujao wa 2018. Ikiwa kuna sherehe au sikukuu ambazo zitaadhimishwa hivi karibuni, wanafunzi wazijadili kwa kutabiri yale ambayo huenda yakatendeka katika sherehe na sikukuu hizo.

**d) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi ca 2. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa. Wanafunzi wajikumbushe kuhusu matumizi ya wakati uliopita waliyosoma hapo awali.
Mwalimu atumie masimulizi ya wakati ujao aliyoyaandaa kutanguliza funzo hili.

### 7.6 Sarufi: Matumizi ya wakati ujao

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha awaombe watazame mcoro ulio katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 56. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua kinacoendelea katika micoro

hiyo. Katika makundi yao, wanafunzi wasome kifungu kifupi kilico kwenye *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 57 na kukijadili. Baadaye, wajaribu kusimuliana wanavyopanga kusherehekea mwaka mpya ujao. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kusimulia matukio wanayopanga kujihusisha nayo mwaka ujao kwa kutumia wakati ujao. Baada ya masimulizi ya wanafunzi, mwalimu awaombe wanafunzi waeleze matumizi ya viambishi vya wakati ujao katika sentensi.

Mwalimu awaeleze wanafunzi kuwa:

*Wakati ujao hutumiwa kuonyesha matukio ambayo bado hayajatendeka. Matukio ambayo yatatendeka wakati usio wa sasa bali unaotarajiwa kuwepo baada ya leo. Wakati huu hutumia kiambishi ca wakati* ***–ta-.*** *Kiambishi hiki hutumika katika nafsi zote za Kiswahili.*

***Mifano:***

1. *Nitaomba walinzi wa mbuga waniongoze.*
2. *Nitavaa nguo nzuri.*
3. *Mwalimu atatufundisha kesho.*
4. *Sherehe ya Idi ul Fitri itaadhimishwa mwezi ujao.*
5. *Wanafunzi watafanya mtihani wiki ijayo.*

Hatimaye, mwalimu awakumbushe wanafunzi kuhusu wakati uliopo. Mwalimu awaombe wanafunzi watunge sentensi mbalimbali katika wakati uliopo. Wanafunzi wakumbushwe kuwa wakati uliopo hutumia kiambishi **–na-** katika umoja na wingi. Huu huwa ni wakati wa matukio kutendeka sasa hivi. Kwa mfano:

a) *Mimi ni**na**andika barua.*
b) *Mama a**na**fagia nyumba yetu.*
c) *Gatete a**na**soma kitabu ca hadithi.*

Baada ya wanafunzi kuelewa aina hizi za viambishi vya wakati uliopita, ujao na uliopo, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi yanayotakikana kwa kila zoezi kisha wajibu maswali yanayohusu wakati uliopita na wakati ujao. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kutunga sentensi sahihi kwa kutumia wakati uliopita, ujao na uliopo. Mwalimu awakumbushe wanafunzi kuwa lazima kila sentensi kamili ianze kwa herufi kubwa na ikamilike kwa kikomo. Kwa mfano:

*a)* ***K****amana a**li**adhimisha sikukuu ya Krismasi.*
*b)* ***K****amana a**na**adhimisha sikukuu ya Krismasi.*
*c)* ***K****amana a**ta**adhimisha sikukuu ya Krismasi.*

## Tathmini ya kipindi ca 4

Mwalimu ahitimishe funzo hili kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza katika kipindi hiki. Maswali hayo yaegemee hasa kwa kucunguza iwapo wanafunzi wameweza kutambua matumizi ya wakati ujao pamoja na viambishi vinavyohusika. Mwalimu pia atathmini iwapo wanafunzi wameweza kutunga sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia wakati ujao. Maarifa haya yajidhihirishe katika mawasiliano ya wanafunzi hadi nje ya darasa.

### Maelezo muhimu kwa mwalimu

i) Wakati uliopita huonyesha matukio ambayo tayari yameshatendeka. Wakati uliopita hutumia kiambishi cha wakati ***-li-.*** Kiambishi hiki hutumika katika nafsi zote za Kiswahili.

Kiambishi ***-ka-*** hutumika katika sentensi iliyo na matukio yanayofuatana katika wakati uliopita.

***Mifano:***

1. *Nilikimbia pamoja na rafiki yangu.*
2. *Waliamka wakanywa kiamshakinywa.*
3. *Yeye alipika chakula, tukala na kulala.*
4. *Kamana aliwasha gari, akaliendesha haraka na kupata ajali.*
5. *Wao walivuna maharagwe mwezi uliopita.*

Katika masimulizi ya wakati uliopita, maneno kama vile: ***halafu, kisha*** na ***baadaye*** hutumika.

ii) Wakati ujao hutumiwa kuonyesha matukio ambayo yanatarajiwa kutendeka. Wakati huu hutumia kiambishi ***-ta-.*** Kiambishi hiki hutumika katika nafsi zote za Kiswahili.

***Mifano:***

1. Tu***ta***omba waelekezaji watuongoze na baadaye tu***ta***piga picha.
2. Wa**ta**vaa kanzu nzuri halafu wa***ta***enda msikitini kusali.
3. Walimu wa**ta**tufundisha kesho kisha wa***ta***tupa mitihani.
4. Sherehe ya Idi ul Adha i**ta**adhimishwa lini?
5. Watoto wa**ta**pelekwa mjini kesho.

Katika masimulizi ya matukio ya wakati ujao, maneno kama vile: ***kisha, halafu*** na ***baadaye*** hutumika.

## 7.7 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atoe zoezi la ziada ambalo linalenga kuinua kiwango ca cini ca wanafunzi wasioweza kuelewa kwa haraka kama wenzao.

***Kwa mfano:***

*Andika sentensi hizi katika wakati ujao:*

1. Mbuzi anakula nyasi.
2. Kalisa alikunywa maji.
3. Rubona alifunga mizigo.
4. Kikapu cetu kimejazwa matunda.
5. Ahishakiye ameomba msamaha.

### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

1. Mbuzi a**ta**kula nyasi.
2. Kalisa a**ta**kunywa maji.
3. Rubona a**ta**funga mizigo.
4. Kikapu cetu ki**ta**jazwa matunda.
5. Ahishakiye a**ta**omba msamaha.

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango ca juu ca uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe waandike aya moja ya masimulizi kuhusu sherehe yoyote ambayo wamewahi kuhudhuria. Pia, waandike aya moja ya masimulizi kuhusu sherehe yoyote wanayotarajia kuhudhuria hivi karibuni.

***Kwa mfano:***

*i) Mwaka uliopita, tu**li**sherehekea Krismasi kijijini. Tu**li**furahi sana kumuona nyanya na babu yetu. Kila jioni wa**li**tusimulia hadithi za kufurahisha sana. Mama na dada yangu wa**li**tupikia vyakula vitamu sana. Kwa kweli tu**li**furahia siku hiyo.*

*ii) Mwaka ujao baba yangu ametuahidi kuwa a**ta**tupeleka mjini Kigali ili kuhudhuria sherehe za Ukombozi. Sherehe hii i**ta**fanyika katika uwanja wa Cuo Kikuu ca Rwanda. Ni**ta**furahia sana kufika huku.*

# 7.8 Majibu

**Zoezi la makundi, ukurasa 49**

Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi kwa kurejelea micoro iliyopo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 49.

**Kwa mfano:**

*Kutokana na mcoro wa kalenda, wanafunzi wabaini tarehe za sikukuu maalum ncini Rwanda kama vile: tarehe moja Januari ni sikukuu ya kusherehekea mwaka mpya, tarehe moja Februari ni siku ya mashujaa, tarehe saba Aprili ni siku ya kumbukumbu za mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi, tarehe moja Julai ni siku ya Uhuru n.k.*

*Kutokana na micoro ya pili, Rais wa Rwanda anaadhimisha sikukuu ya kitaifa na Waislamu nao wanaadhimisha sikukuu yao kwa kuswali.*

**Maswali ya ufahamu, ukurasa 51**

1. Sherehe ya mwaka mpya
2. Sherehe ya Krismasi kwa Wakristo
3. Sikukuu ya kumbukumbu za mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi ncini Rwanda yaliyotokea mwaka 1994.
4. Sikukuu ya Mashujaa
5. Sikukuu ya Uhuru wa nci ya Rwanda
6. Sherehe za Pasaka na Krismasi
7. Sherehe ya *Idi ul Fitri* na sherehe ya *Idi ul Adha*
8. Kila wiki ya kwanza ya mwezi Agosti katika siku inayocaguliwa na serikali ya Rwanda
9. Dini ya Kikristo

**Zoezi la msamiati, ukurasa 51**

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika majadiliano yao kuhusu msamiati mpya. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanatoa maelezo sahihi ya msamiati waliopatana nao katika usomaji wa kifungu walicopewa.

***Kwa mfano:***

1. ***Huadhimishwa*** *– husherehekewa*
2. ***Shamrashamra*** *– shughuli za mambo ya furaha au sherehe*

**Zoezi la 7.1A, ukurasa 51**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi kuhusu msamiati wa shughuli za sikukuu na sherehe ncini Rwanda. Wanafunzi waeleze maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi walizopewa.

***Kwa mfano:***

1. **wakoloni:** watu wa taifa la kigeni wanaotawala nci nyingine kwa niaba ya nci yake
2. **wananci:** wenyeji wa nci fulani
3. **ukombozi:** matendo au vita vya kuokoa watu kutoka kwenye hali mbaya yenye mateso au hali ya unyonge
4. **serikali:** mfumo au combo cenye mamlaka ya kutawala nci au eneo fulani
5. **utawala:** namna au matendo ya kuendesha shughuli za kutawala za serikali

**Zoezi la 7.1B, ukurasa 51**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Ziwe sahihi na zihusishe msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi walizopewa. **Kwa mfano:**

1. ***Wakoloni*** *walitoweka ncini kwetu miaka mingi iliyopita.*
2. ***Wananci*** *watahudhuria sherehe ya kuadhimisha sikukuu ya Uhuru.*
3. ***Ukombozi*** *tuliopata umetufanya kuwa huru.*
4. ***Serikali*** *yetu ina viongozi wacace sana.*
5. ***Utawala*** *wa nci yetu ni mzuri.*

**Zoezi la 7.2, ukurasa 52**

1. Sherehe za mwaka mpya ***huadhimishwa*** mwanzoni mwa kila mwaka.
2. Rwanda ni ***nci*** inayopendwa na watu wengi ulimwenguni.
3. ***Sherehe*** ya Krismasi hufanyika tarehe 25 mwezi wa Disemba.
4. Siku ya ***mashujaa*** husherehekewa tarehe 1 mwezi Februari.
5. ***Umuganura*** husherehekewa wiki ya kwanza mwezi Agosti.

**Matumizi ya lugha, ukurasa 52**

Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi. Kwa mfano, kuhusu:

1. Shughuli zote zinazofanyika katika sherehe za mwaka mpya.
   *Wanafunzi waelezane namna wanavyosherehekea sherehe za mwaka mpya nyumbani kwao. Kwa mfano: kwenda kanisani, kununuliwa nguo mpya, kupewa zawadi, kukesha kanisani, kuzuru mbuga ya wanyama n.k.*
2. Nguo unazopenda kuvaa unapoenda katika sherehe za harusi.

*Wanafunzi waelezane kuhusu nguo wanazopenda kuvalia waendapo kwenye harusi. Kwa mfano: kitenge, suti, rinda zuri, viatu vizuri n.k.*

3. Sikukuu unayopenda kuadhimisha katika kalenda. Toa sababu.
   *Kila mwanafunzi aeleze sikukuu anayopenda kuadhimisha na atoe sababu za kupendelea sikukuu hiyo.*
4. Umuhimu wa sikukuu na sherehe mbalimbali kwa Wanyarwanda.
   *Wanafunzi watoe maelezo yao. Kwa mfano: Umuhimu wa sikukuu na sherehe mbalimbali kwa Wanyarwanda ni pamoja na: kuwaunganisha Wanyarwanda, kuwapa kumbukumbu za mafanikio ya Wanyarwanda, kuhifadhi mila na desturi za Wanyarwanda, kumshukuru Mola, kuhifadhi na kuendeleza dini mbalimbali, kuburudisha na kufurahisha Wanyarwanda n.k.*
5. Umuhimu wa kuwa na Kalenda rasmi nyumbani.
   W*anafunzi watoe majibu yao. Kwa mfano: kalenda hutusaidia kufahamu tarehe na siku mbalimbali za wiki, matukio muhimu katika mwaka mzima pamoja na siku za* kuadhimisha sikukuu mbalimbali.

### Zoezi la kusikiliza na kuzungumza, ukurasa 52

Mwalimu atathmini micezo ya kuigiza itakayotungwa na wanafunzi. Ahakikishe kuwa micezo hiyo inahusu sikukuu mbalimbali ncini Rwanda.

***Kwa mfano:***

**Neza:** Hujambo Kalisa?

**Kalisa:** Sijambo Neza. Je, unaenda kanisani leo?

**Neza:** Kuna nini kanisani leo?

**Kalisa:** Hukumbuki kuna mkesha wa kuukaribisha mwaka mpya?

**Neza:** Ooh! Asante kwa kunikumbusha. Nilikuwa nimesahau. Nitahudhuria.

**Kalisa:** Haya basi kwaheri. Tuonane kanisani.

**Neza:** Kwaheri rafiki. Asante.

### Zoezi la sarufi, ukurasa 53

Mwalimu atathmini masimulizi ya wanafunzi kuhusu namna walivyosherehekea mwaka mpya uliopita. Wanafunzi wazingatie matumizi ya wakati uliopita. Mifano ya vitenzi kutoka katika mazungumzo mafupi waliyopewa ni: *u**li**opita, ni**li**amka, ni**li**ondoka, ni**li**pofika, ni**li**waona, a**li**kuwa, a**li**piga, i**li**pata* n.k.

**Zoezi la 7.3, ukurasa 54**

**A.**

1. Uliopita
2. Niliamka
3. Nikaoga
4. Nikapiga mswaki
5. Nikavaa
6. Niliondoka
7. Nilipofika
8. Niliwaona
9. Alipuliza
10. Ilipata

**B.** Wakati uliotumika katika vitenzi vilivyoorodheshwa hapo juu ni ***wakati uliopita***.

**Zoezi la 7.4, ukurasa 55**

1. Kaka ***alioga***, ***akapiga*** nguo pasi na ***kwenda*** shuleni.
2. Mtoto ***alikunywa*** maziwa, ***akabembelezwa*** na ***kulala***.
3. Mwanafunzi ***alienda*** shuleni, ***akasoma*** na ***kufanya*** mtihani.
4. Ng'ombe ***alikula*** nyasi, ***akanywa*** maji na ***kurudi*** zizini.
5. Mmea ***ulipandwa***, ***ukawekewa*** mbolea na ***kunyunyiziwa*** maji.

**Zoezi la 7.5, ukurasa 55**

1. Mama a***li***pika wali.
2. Mimi ni***li***enda shule.
3. Kwa nini u***li***lia?
4. Siku ya sherehe ya Krismasi i***li***fika.
5. Wanyarwanda wa***li***adhimisha siku ya Mashujaa.

**Zoezi la 7.6, ukurasa 56**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zitangulize msamiati waliopewa katika wakati uliopita. **Kwa mfano:**

1. ***Uhuru*** *wa Wanyarwanda u**li**patikana miaka mingi i**li**yopita.*
2. ***Ukombozi*** *wa wananci u**li**kuwa muhimu.*
3. ***Ukoloni*** *wa nci yetu u**li**kuwa wa nguvu.*
4. ***Utawala*** *wa kimabavu u**li**waudhi wananci wengi.*
5. ***Siasa*** *za zamani zi**li**kuwa mbaya.*

**Sehemu ya (ii) sarufi, ukurasa 57**

Mwalimu atathmini masimulizi ya wanafunzi kuhusu namna wanavyopanga kusherehekea mwaka mpya ujao. Wanafunzi wazingatie matumizi ya wakati ujao. Mifano ya vitenzi kutoka katika mazungumzo mafupi waliyopewa ni: *ni**ta**vaa, ni**ta**kwenda, ni**ta**waona, ni**ta**furahi, ni**ta**pewa, ni**ta**mwona, ni**ta**piga* n.k.

**Zoezi la 7.7, ukurasa 57**

**A.**

1. Nitavaa
2. Nitakwenda
3. Nitawaona
4. Nitafurahi
5. Nitapewa
6. Nitamwona
7. Nitapiga

**B.** Wakati uliotumika katika vitenzi vilivyoorodheshwa hapo juu ni ***wakati ujao***.

**Zoezi la 7.8, ukurasa 57**

Katika sherehe za Pasaka za mwaka ujao, Kamana ***ataenda*** kanisani kwa ajili ya ibada. Baadaye, ***atawatembelea*** marafiki zake na kusherehekea pamoja nao. Kisha jioni ***atarudi*** nyumbani. Ndugu yake Yusuf ***atampokea*** kwenye kituo ca basi. Halafu ***wataenda*** nyumbani pamoja.

**Zoezi la 7.9, ukurasa 57**

Mwalimu atathmini aya ambayo wanafunzi watatunga. Sharti ihusishe sentensi sahihi pamoja na matukio ya wakati ujao.

***Kwa mfano:***

*Sikukuu ya Pasaka ya mwaka huu nitaamka mapema. Nitajiandaa ili niende kanisani. Nitahudhuria ibada ya siku hiyo. Mama ataninunulia kitabu ca nyimbo za injili ambaco nitabeba hadi kanisani. Nitakapofika kanisani, nitaimba nyimbo mbili za kumtukuza Mungu. Wakristo wenzangu wataimba pamoja nami.*

**Zoezi la 7.10, ukurasa 58**

1. Mwanafunzi huyu atasoma kitabu ca hadithi.
2. Mbuga hii itafunguliwa na rais wetu.
3. Darasa letu litasafishwa na wanafunzi hawa.
4. Kwa nini mtanunua vitabu vingine?
5. Wanyamapori hawa watakula nyasi.

# Somo la 8: Maadhimisho Mbalimbali nchini Rwanda

## Kipindi cha 5: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati

**a) Malengo ya somo**

- Kusoma kwa usahihi shairi kwa utambuzi wa herufi, silabi, maneno na sentensi;
- Kutaja orodha ya maadhimisho mbalimbali katika jamii ncini Rwanda.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Micoro au pica za shughuli mbalimbali za maadhimisho mbalimbali ncini Rwanda;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 59-61;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Somo hili linahusu kujenga uelewa zaidi kuhusiana na maadhimisho mbalimbali kuhusiana na sikukuu mbalimbali ncini Rwanda. Uelewa huu unahusisha utambuzi wa tarehe, siku na maadhimisho mbalimbali ambayo hutokea katika kalenda ya mwaka mzima ncini Rwanda. Kalenda ya mwaka huonyesha wazi siku hizo kuanzia mwezi wa Januari hadi mwezi wa Disemba. Kila sherehe huorodheshwa kwenye kalenda ya mwaka. Maadhimisho mbalimbali hutajwa yakiwemo ya kisiasa, kidini, kihistoria na kienyeji. Mwalimu aandae orodha ya sherehe na sikukuu mbalimbali ambazo huadhimishwa ncini ili wanafunzi waelewe vizuri mfuatano wa sikukuu na sherehe katika kalenda ya mwaka.

**d) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awacangamshe wanafunzi kwa kuwauliza maswali kuhusu somo lililopita. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kama vile: *Nyumbani mnaadhimisha mwaka mpya? Mwaka mpya unaadhimishwa tarehe gani? Taja majina ya sikukuu unazojua. Taja sikukuu inayoadhimishwa*

*tarehe ya kwanza mwezi wa Julai* n.k. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika majadiliano haya.

Baadaye, mwalimu aendelee na somo kwa kuwaomba wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu watazame pica zilizo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 59. Mwalimu awaulize wanafunzi maswali kuhusu pica hizo. Kwa mfano: *Mnaona nini kwenye pica hizi?* Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kujibu swali waliloulizwa kwa kuwapa kitangulizi kama vile *"mimi ninaona..."* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu. Kwa mfano, "*Tunaona watu wakiwa katika sherehe"*. Katika sehemu hii, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi wake ili wapate ujuzi kuhusu tafakuri tanduizi, ubunifu na ugunduzi kwa kuwaonyesha pica husika huku wanafunzi nao wakifikiri na kugundua kile kinacoendelea katika pica hizo. Mwalimu anaweza kuwaonyesha wanafunzi pica au micoro ya ziada aliyoiandaa kuhusiana na maadhimisho mbalimbali yafanyikayo ncini Rwanda. Micoro au pica zinazoonyesha wananci pamoja na viongozi mbalimbali katika maadhimisho mbalimbali pia itumike.

## 8.1 Kusoma na ufahamu

### Shairi kuhusu maadhimisho mbalimbali ncini Rwanda

Mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu wasome kwa kimya shairi kuhusu maadhimisho mbalimbali ncini Rwanda. Wanafunzi wasome kwa kimya huku wakiandika msamiati mpya wanaopatana nao. Hatimaye, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu shairi walilosoma ili kuhakikisha kuwa wamelielewa. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuuliza: *Sikukuu inayoadhimishwa mwezi Februari ni ipi?* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika shairi hilo. Kwa mfano: *Sikukuu hiyo ni siku ya Mashujaa*. Baada ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wamesoma kwa kimya shairi lililopo, mwalimu awaombe wanafunzi wakariri kwa sauti shairi hilo na pia kwa mahadhi mbalimbali. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanakariri shairi hilo kwa namna inayofaa. Mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali ya shairi hilo huku akitoa maelezo pale ambapo wanafunzi wanatatizika. Mwalimu awasaidie wanafunzi wenye matatizo ya kuelewa msamiati uliotumika katika shairi hilo.

### 8.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu maadhimisho mbalimbali

Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kuwaomba wajadili maana za msamiati mpya na jinsi ulivyotumiwa katika shairi walilosoma. Mwalimu awaombe wanafunzi watumie kamusi ya Kiswahili pale inapohitajika. Mwalimu azunguke darasani akiwaelekeza wanafunzi wanaopata taabu katika kuitumia kamusi na kueleza maana ya msamiati husika. Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi za zoezi la 8.1.

Hali kadhalika, awaombe wajadili maana ya msamiati huo. Hatimaye, wanafunzi watunge sentensi zao wenyewe kwa kutumia msamiati huo. Ni vyema mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia na kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika. Baada ya wanafunzi hawa kukamilisha zoezi walilopewa, mwalimu awaombe wanafunzi kusahihisha kwa pamoja mazoezi hayo ya msamiati. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wameelewa msamiati uliokuwa mpya kwao, mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi wataje msamiati ambao hawakuelewa maana yake ili ujadiliwe kwa pamoja darasani kulingana na matumizi yake katika shairi walilosoma. Ni vyema mwalimu azingatie kwamba utunzi wa sentensi za wanafunzi ndio utakaomfahamisha iwapo wanafunzi wamepata ujuzi unaotakikana katika tafakuri tanduizi, suluhisho kwa matatizo na mawasiliano kwa lugha sahihi.

**Tathmini ya kipindi ca 5**

Mwalimu ahitimishe kipindi hiki kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali hayo yaegemee hasa katika kucunguza ikiwa wanafunzi wanaweza kutumia msamiati mpya kuhusu maadhimisho mbalimbali ncini Rwanda, thamani ya sherehe na sikukuu ncini Rwanda na umuhimu wake.

## Kipindi cha 6: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza

### a) Malengo ya somo

- Kutaja umuhimu wa sikukuu na sherehe katika jamii ncini Rwanda.
- Kufahamu shughuli mbalimbali zinazofanyika katika sherehe na sikukuu mbalimbali.
- Kuelewa thamani ya sikukuu na sherehe mbalimbali katika jamii.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Micoro au pica za kalenda ya miezi yote ionyeshayo sikukuu na sherehe mbalimbali ncini Rwanda.
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 61-62;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.)

**c) Maandalizi ya somo**

Katika maandalizi ya funzo hili, mwalimu atafute vifaa vitakavyoweza kurahisisha uelewa wa wanafunzi kama vile micoro ya watu wakiwa katika maadhimisho mbalimbali, mavazi mbalimbali ambayo huvaliwa katika sherehe mbalimbali pamoja na nyimbo ambazo huimbwa katika maadhimisho mbalimbali. Kupitia vifaa hivyo, mwalimu aandae maswali mbalimbali yatakayowacocea wanafunzi kutambua maadhimisho mbalimbali ncini, shughuli zinazofanywa katika maadhimisho mbalimbali, watu ambao huhudhuria sherehe mbalimbali, umuhimu wa sherehe na sikukuu mbalimbali kwa Wanyarwanda na hata namna ya kukuza utamaduni wetu kupitia maadhimisho mbalimbali.

**d) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu atangulize somo hili kwa kuwauliza wanafunzi maswali kuhusu waliyojifundisha katika kipindi kilicopita. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika majadiliano haya. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu.

### 8.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

Mwalimu awaombe wanafunzi wajadili na kuelezana kuhusu mambo yanayofanyika zinapoadhimishwa sikukuu fulani. Wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watano watano ili kufanya majadiliano haya.

Mbali na hayo, mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kusimulia umuhimu wa sherehe na sikukuu mbalimbali katika jamii. Mwalimu asimulie kuhusu sherehe za kitamaduni kama vile: *harusi, kupeana ng'ombe* n.k. Awasimulie sikukuu za kisiasa kama vile: *sikukuu ya Watumishi, Mashujaa* n.k. Masimulizi haya yatawasaidia wanafunzi kuelewa tofauti kati ya sikukuu hizo. Mwalimu awaombe wanafunzi waelezane kuhusu:

1. *Shughuli zinazofanyika nyumbani kwao wakati wa sherehe za mwaka mpya.*
2. *Namna wanavyoadhimisha sikukuu iliyo katika mwezi wa Julai.*
3. *Shughuli zinazotekelezwa kwao wakati wa sherehe za Umuganura.*
4. *Shughuli zinazotekelezwa wakati wa kuadhimisha sikukuu ya Ukombozi wa Taifa.*
5. *Shughuli zinazofanyika wakati wa kuadhimisha sikukuu ya Uhuru wa Taifa.*

Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wote wanashirikishwa katika majadiliano haya katika makundi yao mbalimbali. Wanafunzi wacangie katika majadiliano haya. Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi kutoka katika makundi mbalimbali waeleze kuhusu waliyojadili mbele ya wanafunzi wenzao. Mwalimu asahihishe makosa ya matamshi na makosa mengine yanayoweza kujitokeza.

### 8.4 Kusikiliza na kuzungumza: Zoezi la mazungumzo

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha waigize mfano wa mazungumzo mafupi kuhusu maadhimisho mbalimbali ncini Rwanda waliyopewa katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 61. Wanafunzi waigize kwa ubunifu wa hali ya juu huku wakijikita katika shughuli zinazofanyika katika maadhimisho mbalimbali. Mwalimu afuatilie kwa karibu maigizo ya wanafunzi katika makundi yao. Maigizo haya yafanywe kwa lugha sanifu ya Kiswahili, wanafunzi wawe na motisha na mwalimu awahimize ili wapende lugha ya Kiswahili na waipende nci yao. Kutokana na maigizo ya wanafunzi katika makundi yao, mwalimu awaombe wanafunzi wajadiliane kuhusu maadhimisho mbalimbali ncini Rwanda. Kwa mfano: *sikukuu ya Uhuru, Mashujaa* n.k.

Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wote wanashirikishwa katika maigizo haya. Mwalimu akosoe makosa ya matamshi pamoja na makosa mengine yanayoweza kujitokeza wakati wa maigizo ya wanafunzi.

### Tathmini ya kipindi ca 6

Katika hatua hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti tofauti kwa lengo la kucunguza iwapo wanaweza kueleza kuhusu maadhimisho mbalimbali ncini Rwanda. Shughuli mbalimbali za maadhimisho mbalimbali katika jamii ya Wanyarwanda zirejelewe ili kutathmini iwapo wanafunzi wameelewa somo hili.

## Kipindi cha 7: Sarufi (Vitenzi vya silabi moja)

**a) Malengo ya somo**

- Kutambua vitenzi vya silabi moja katika lugha ya Kiswahili;
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia vitenzi vya silabi moja.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Micoro au pica zinazoonyesha vitendo vya vitenzi vya silabi moja;
- Cati yenye kuonyesha miundo ya vitenzi vya silabi moja;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 62-64;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Katika maandalizi ya somo hili, mwalimu alenge kumsaidia mwanafunzi kubaini vitenzi vya silabi katika lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, mwalimu atafute vifaa vya kutosha kufundishia somo hili kama vile: micoro au pica zinazoonyesha vitendo vya vitenzi vya silabi moja pamoja na cati yenye kuonyesha miundo ya vitenzi vya silabi moja. Ili kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wote, mwalimu afikirie wakati mwafaka wa kuonyesha vifaa hadharani na kuwatumia wanafunzi wenyewe kuelewa somo hili.

**d) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Katika utangulizi, mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali mepesi kuhusu kipindi kilicopita kuhusu sarufi ya viambishi vya wakati uliopita na wakati ujao pamoja na matumizi yao katika sentensi sahihi. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu aendelee kwa kuwashirikisha wanafunzi wote kusahihisha zoezi walilopewa katika kipindi kilicopita.

### 8.5 Sarufi: Vitenzi vya silabi moja

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha awaombe wacunguze sentensi walizopewa na kutambua vitenzi vilivyotumika katika sentensi hizo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kutambua vitenzi vilivyotumika ambavyo ni:

1. Ng'ombe wa jirani alikufa.
   *(Kitenzi ni **kufa**)*
2. Wanafunzi walikunywa maji safi.
   *(Kitenzi ni **kunywa**)*
3. Baba alipika cakula kitamu.
   *(Kitenzi ni **pika**)*
4. Watoto walikula cakula cao ca mcana.
   *(Kitenzi ni **kula**)*
5. Kaka alikuwa mgonjwa.
   *(Kitenzi ni **kuwa**)*
6. Mutoni, Uwimana na Mukamutara wana***ceza*** uwanjani.
   *(Kitenzi ni **ceza**)*
7. Imamu anawafundisha watoto Kurani.
   *(Kitenzi ni **fundisha**)*

Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika makundi yao kutambua kuwa vitenzi *kufa, kunywa, kula* na *kuwa* (katika sentensi 1,2,4 na 5) ni ***vitenzi vyenye silabi moja*** ilhali vitenzi *pika, ceza* na *fundisha* ni vitenzi vikuu. Mwalimu awaeleze wanafunzi kuwa:

*Katika lugha ya Kiswahili kuna vitenzi vyenye silabi moja. Vitenzi hivi huwa vina mizizi yenye irabu moja. Kwa mfano:*

i) kufa *(ku+f+a):* Mzizi ni ***'-f-'***

ii) kuwa *(ku+w+a):* Mzizi ni ***'-w-'***

iii) kunywa *(ku+nyw+a):* Mzizi ni ***'-nyw-'***

iv) kula *(ku+l+a):* Mzizi ni ***'-l-'***

v) kuja *(ku+j+a):* Mzizi ni ***'-j-'***

### Tathmini ya kipindi ca 7

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu vitenzi vyenye silabi moja. Mwalimu anaweza kuunganisha maswali yake na nyakati ambazo tayari wanafunzi wameshafundishwa kwa wanafunzi kutunga sentensi sahihi katika wakati uliopita na wakati ujao kwa kutumia vitenzi vyenye silabi moja.

## Kipindi cha 8: Sarufi (Tungo yakinishi na tungo kanushi)

### a) Malengo ya somo

- Kutambua maana ya tungo yakinishi na tungo kanushi;

- Kutunga sentensi sahihi katika tungo yakinishi na tungo kanushi kwa kutumia vitenzi vyenye silabi moja.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Micoro au pica zinazoonyesha vitendo katika tungo yakinishi na tungo kanushi;
- Cati yenye kuonyesha miundo ya vitenzi vya silabi moja katika tungo yakinishi na tungo kanushi;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 64-66;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Katika maandalizi ya somo hili, mwalimu alenge kumsaidia mwanafunzi kubaini tungo yakinishi na tungo kanushi za sentensi zenye vitenzi vya silabi moja katika lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, mwalimu atafute vifaa vya kutosha kufundishia somo hili kama vile: micoro au pica zinazoonyesha vitendo katika tungo yakinishi na tungo kanushi na cati yenye kuonyesha miundo ya vitenzi vya silabi moja katika tungo yakinishi na tungo kanushi.

Ili kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wote, mwalimu afikirie wakati mwafaka wa kuonyesha vifaa hadharani na kuwatumia wanafunzi wenyewe kuelewa somo hili.

**d) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Katika utangulizi, mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali mepesi kuhusu kipindi kilicopita kuhusu sarufi ya vitenzi vya silabi moja pamoja na matumizi yao katika sentensi sahihi. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu aendelee kwa kuwashirikisha wanafunzi wote kusahihisha zoezi walilopewa katika kipindi kilicopita.

### 8.6 Vitenzi vya silabi moja, tungo yakinishi na kanushi

Baada ya wanafunzi kupata uelewa wa vitenzi vyenye silabi moja, mwalimu awashirikishe katika makundi yao kutunga sentensi sahihi kwa kutumia vitenzi hivyo katika tungo yakinishi na tungo kanushi na wakati uliopita. Wanafunzi wakumbushwe kuwa ***tungo yakinishi*** ni hali ya kukubali jambo

linalozungumziwa ilhali ***tungo kanushi*** ni hali ya kupinga au kukataa jambo linalozungumziwa katika sentensi husika.

***Mifano:***

| **Tungo yakinishi** | **Tungo kanushi** |
|---|---|
| 1. Wewe *ulikunywa* maji. | Wewe *hukunywa* maji. |
| 2. Nyinyi *mlikunywa* maji. | Nyinyi *hamkunywa* maji. |
| 3. Mtoto *alikula wali.* | Mtoto *hakula* wali. |
| 4. Watoto *walikula* wali. | Watoto *hawakula* wali. |
| 5. Nilikuja jana. | Sikuja jana. |
| 6. Tulikuja jana. | Hatukuja jana. |

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kufahamu kuwa katika tungo kanushi, vitenzi vyenye silabi moja huongezewa viambishi mbalimbali kulingana na nafsi iliyotumika katika umoja na wingi.

**Kwa mfano:**

| | **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|---|
| **Nafsi ya kwanza** | si+kuja | ha+tu+kuja |
| **Nafsi ya pili** | hu+kunywa | ha+m+kunywa |
| **Nafsi ya tatu** | ha+kula | ha+wa+kula |

Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kutunga sentensi nyingine katika wakati uliopita kwa kutumia vitenzi vyenye silabi moja. Mazoezi ya aina hii yatawasaidia wanafunzi kupata uelewa na uwezo wa kutunga sentensi sahihi katika wakati uliopita kwa kutumia vitenzi vya silabi moja. Mwalimu awakumbushe wanafunzi kuwa lazima kila sentensi kamili ianze kwa herufi kubwa na ikamilike kwa alama inayofaa ya kikomo/nukta.

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kufanya zoezi la 8.4, zoezi la 8.5 na zoezi la 8.6.

### Tathmini ya kipindi ca 8

Katika hatua hii ya mwisho wa somo hili, mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali hayo yaegemee hasa katika kucunguza ikiwa wanafunzi wameelewa matumizi ya vitenzi vya silabi moja katika tungo kanushi na tungo yakinishi.

**Maelezo muhimu kwa mwalimu**

- Katika lugha ya Kiswahili kuna vitenzi vyenye silabi moja. Vitenzi hivi huambatanishwa na '***ku-***' katika matumizi.

  ***Kwa mfano:***

  kufa (ku+f+a): Mzizi ni '***-f-***'

  kuwa (ku+w+a): Mzizi ni '***-w-***'

  kunywa (ku+nyw+a): Mzizi ni '***-nyw-***'

  kula (ku+l+a): Mzizi ni '***-l-***'

  kuja (ku+j+a): Mzizi ni '***-j-***'

- Vitenzi vya silabi moja huambatanishwa na '***ku-***' katika hali yakinishi. Katika hali kanushi, vitenzi hivi huambatanishwa na kikanushi '***ha-***' na nafsi husika.

***Kwa mfano:***

1. Wagonjwa wali***kula*** chakula. - Wagonjwa ***hawakula*** chakula.
2. Walimu wali***kunywa*** chai. - Walimu ***hawakunywa*** chai.
3. Paka wa jirani wali***kufa*** jana. - Paka wa jirani ***hawakufa*** jana.

## 8.7 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atoe zoezi la ziada ambalo linalenga kuinua kiwango ca cini ca wanafunzi wasioweza kuelewa kwa haraka kama wenzao.

***Kwa mfano:***

*Andika sentensi hizi katika wakati uliopita:*

1. Mbuzi anakula nyasi.
2. Kamana amekunywa maji.
3. Rubona atafunga mizigo.
4. Kikapu cetu kimejazwa mapema.
5. Ahishakiye ameomba msamaha.

### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

1. Mbuzi alikula nyasi.
2. Kamana alikunywa maji.
3. Rubona alifunga mizigo.

4. Kikapu cetu kilijazwa mapema.
5. Ahishakiye aliomba msamaha.

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango ca juu ca uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge sentensi sahihi kwa kutumia vitenzi vifuatavyo katika tungo yakinishi na tungo kanushi.

**Kwa mfano: *kunywa***

**Tungo yakinishi:** Paka alikunywa maziwa ya mtoto.

**Tungo kanushi:** Paka hakunywa maziw aya mtoto.

1. kula
2. kuwa
3. kufa
4. kuja

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Ziwe sahihi na zihusishe vitenzi vya silabi moja walivyopewa.

## 8.8 Majibu

### Zoezi la makundi, ukurasa 59

Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi kwa kurejelea micoro iliyopo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 59.

**Kwa mfano:**

*Mcoro wa kwanza unaonyesha maadhimisho ya sikukuu maalum ya kitaifa ilhali mcoro wa pili unaonyesha wanawake wacezaji ngoma wakitumbuiza wananci katika sherehe mojawapo maalum.*

### Maswali ya tathmini, ukurasa 60

1. Sherehe ya mwaka mpya.
2. Tarehe 1 mwezi wa Februari.
3. Wakristo. Wao hukumbuka kusulubishwa, kufa na kufufuka kwa mkombozi wao Yesu Kristo.
4. *Idi ul Fitri* na *Idi ul Adha.*
5. Tarehe 1 mwezi wa Julai.
6. Tarehe 7 mwezi wa Aprili.

7. Mishororo ishirini na minne.
8. Mungu tuneemeshe, kuwa wazalendo kamili.
9. Disemba tarehe 25
10. Mwezi Agosti wiki ya kwanza.

**Zoezi la msamiati, ukurasa 60**

Mwalimu atathmini maelezo kuhusu msamiati katika shairi husika ambayo wanafunzi wataeleza. **Kwa mfano:**

1. ***tele*** – *nyingi.*
2. ***tulijikomboa*** – *tulijitoa katika hali ya kunyanyaswa.*

**Zoezi la 8.1, ukurasa 61**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi na zihusishe maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi walizopewa. **Kwa mfano:**

1. ***Sikukuu*** *ya Uhuru wa Taifa itaadhimishwa kesho.*
2. *Huu ni* ***mwaka*** *wenye mafanikio mengi.*
3. ***Januari*** *ndio mwezi wa kwanza katika kalenda ya mwaka.*
4. ***Wakristo*** *wanaamini kuwa Yesu Kristo ni mkombozi wao.*
5. ***Waislamu*** *hutoa zaka zao.*
6. *Sherehe ya* ***Idi ul Fitri*** *husherehekewa na Waislamu.*
7. *Sikukuu ya* ***Krismasi*** *imekaribia.*
8. ***Wanyarwanda*** *wanapenda amani na upendo.*
9. *Tutafanya mtihani wetu mwezi wa* ***Disemba****.*
10. *Sherehe za* ***Umuganura*** *zinaadhimishwa sasa hivi.*

**Zoezi, matumizi ya lugha, ukurasa 61**

Mwalimu atathmini masimulizi ya wanafunzi kuhusu:

1. *Shughuli zinazofanyika nyumbani kwenu wakati wa sherehe za mwaka mpya.*
2. *Namna mnavyoadhimisha sikukuu iliyo katika mwezi Julai.*
3. *Shughuli zinazotekelezwa kwenu wakati wa sherehe za Umuganura.*
4. *Shughuli zinazotekelezwa wakati wa kuadhimisha sikukuu ya Ukombozi wa Taifa.*
5. *Shughuli zinazofanyika wakati wa kuadhimisha sikukuu ya Uhuru wa Taifa.*

**Zoezi, kusikiliza na kuzungumza, ukurasa 61**

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kusoma mazungumzo yaliyo katika

kitabu cao katika makundi yao. Ahakikishe kuwa wanasoma kwa kuzingatia silabi, maneno na alama za uandishi kwa usahihi.

**Zoezi la sarufi, ukurasa 62-63**

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua vitenzi katika sentensi walizopewa kwa kuvihusisha na sentensi walizopewa. Maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi hizi ndiyo vitenzi:

1. Ng'ombe wa jirani ali***kufa***.
2. Wanafunzi wali***kunywa*** maji safi.
3. Kaka ali***pika*** cakula kitamu.
4. Watoto wali***kula*** cakula cao ca mcana.
5. Daktari alim***pima*** kaka aliye***kuwa*** mgonjwa.
6. Wanafunzi wali***ceza*** uwanjani.
7. Shehe aliwa***fundisha*** watoto kuhusu Kurani.

**Zoezi la 8.2, ukurasa 63**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi na zihusishe vitenzi vya silabi moja walivyopewa.

***Kwa mfano:***

1. *Mbwa wake ali**kufa** jana usiku.*
2. *Mtoto ata**kunywa** maziwa jioni.*
3. *Wageni wali**kula** cakula cote.*
4. *Mwalimu ali**kuwa** mnyonge jana.*
5. *Rais ali**kuja** ukumbini kutusalimia.*

**Zoezi la 8.3A, ukurasa 64**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

1. Mwalimu alikuja darasani.
2. Mbuzi wetu alikufa jana.
3. Kalisa alikunywa maji.
4. Dada alikula wali.
5. Mama alikuwa mgonjwa.

**Zoezi la 8.3B, ukurasa 64**

Mwalimu atathmini ukanushi wa wanafunzi.

1. Mwalimu ***ha***kuja darasani.
2. Mbuzi wetu ***ha***kufa jana.
3. Kalisa ***ha***kunywa maji.

4. Dada ***ha***kula wali.
5. Mama ***ha***kuwa mgonjwa.

**Zoezi la 8.4, ukurasa 65**

Mwalimu atathmini sentensi zote ambazo zitatungwa na wanafunzi katika makundi yao. Ahakikishe kuwa wametunga sentensi sahihi kwa kutumia vitenzi vya silabi moja walivyopewa na katika hali yakinishi kwa kuzingatia wakati uliopita katika umoja na wingi.

***Kwa mfano:***

1. *Mimi nilikuwa jikoni jioni. – Sisi tulikuwa jikoni jioni.*
2. *Wewe ulikuja juzi. – Nyinyi mlikuja juzi.*
3. *Kuku alikufa asubuhi. – Kuku walikufa asubuhi.*
4. *Yeye alikula mkate. – Wao walikula mikate.*

**Zoezi la 8.5, ukurasa 66**

Mwalimu atathmini sentensi zote ambazo zitatungwa na wanafunzi katika makundi yao. Ahakikishe kuwa wametunga sentensi sahihi kwa kutumia vitenzi vya silabi moja walivyopewa na katika hali kanushi kwa kuzingatia wakati uliopita katika umoja na wingi.

***Kwa mfano:***

1. *Mimi sikuwa jikoni jioni. – Sisi hatukuwa jikoni jioni.*
2. *Wewe hukuja juzi. – Nyinyi hamkuja juzi.*
3. *Kuku hakufa asubuhi. – Kuku hawakufa asubuhi.*
4. *Yeye hakula mkate. – Wao hawakula mikate.*

**Zoezi la 8.6, ukurasa 66**

1. Watu hawa walikuja jana jioni.
2. Mwanafunzi huyu anakunywa maziwa.
3. Watoto wanakula mikate.
4. Panya walikufa mitegoni.
5. Kiongozi alikuwa mjini Kigali.

# Somo la 9 - Matumizi ya kalenda ya mwaka

## Kipindi cha 9: Kusoma ufahamu

**a) Malengo ya somo**

- Kusoma kwa usahihi kifungu ca mazungumzo kwa utambuzi wa herufi, silabi, maneno na sentensi;
- Kucunguza kwa usahihi kalenda ya mwaka kwa kutambua vizuri tarehe, siku na miezi ya sikukuu na sherehe mbalimbali ncini Rwanda.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Micoro au pica za kalenda ya mwaka ionyeshayo siku za wiki, miezi pamoja na sikukuu na sherehe mbalimbali ncini Rwanda;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 67-69;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Somo hili linahusu kifungu ca mazungumzo kuhusu matumizi ya kalenda ya mwaka. Kalenda ya mwaka inaonyesha wazi siku za wiki pamoja na miezi mbalimbali kuanzia mwezi wa Januari hadi mwezi wa Disemba. Katika kalenda, sherehe zote na sikukuu zimetajwa zikiwa za kisiasa, kidini, kihistoria na kienyeji. Vilevile, ni vyema mwalimu awe tayari kushughulikia sarufi katika somo hili. Mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kufahamu matumizi ya herufi kubwa na sheria zote za kuandika. Mbali na sheria za kuandika, mwalimu awashirikishe wanafunzi kutumia vitenzi katika wakati ujao, hali yakinishi na hali kanushi katika kutunga sentensi mbalimbali sahihi. Katika kufanikisha somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelezo yaliyotolewa kwa kila zoezi husika.

**d) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi wake maswali mepesi kuhusiana na somo lililopita. Wanafunzi kwa upande

wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofunzwa katika somo lililotangulia. Baada ya haya, mwalimu atangulize somo hili kuhusu matumizi ya kalenda ya mwaka ionyeshayo siku za wiki, miezi mbalimbali pamoja na sherehe na sikukuu mbalimbali ncini Rwanda. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi ya kuwacangamsha kuhusiana na mcoro ulio katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 67. Maswali kama vile: *Katika kalenda hii unaona nini? Mwaka una miezi mingapi? Taja majina ya miezi ya mwaka* n.k. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kujibu maswali waliyoulizwa kwa kuwapa kitangulizi kama vile *"Mimi ninaona…."* Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika majadiliano haya. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kulingana na wanayoyaona katika micoro waliyopewa. Kwa mfano: *Mimi ninaona siku za wiki, miezi na sikukuu mbalimbali. Mwaka una miezi kumi na miwili. Miezi ya mwaka ni kama vile: Januari, Februari, Maci, Aprili…Disemba".*

Katika sehemu hii, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi wake ili wapate ujuzi kuhusu tafakuri tanduizi, ubunifu na ugunduzi kwa kuwaonyesha micoro husika huku wanafunzi nao wakifikiri na kugundua kile kinacoendelea au wanacokiona katika micoro hiyo.

### 9.1 Kusoma na ufahamu: Mazungumzo kuhusu kalenda ya mwaka

Mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili wasome kwa kimya mazungumzo kati ya Birasa na Kalisa kuhusu matumizi ya kalenda ya mwaka. Wanafunzi wasome mazungumzo hayo kwa kimya huku wakiandika msamiati mpya wanaopatana nao. Hatimaye, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu mazungumzo hayo waliyosoma ili kuhakikisha kuwa wameyaelewa. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuuliza: *Siku ya tatu katika wiki ni ipi? Mwezi wa Julai una Jumapili ngapi?* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika mazungumzo hayo. Kwa mfano: *Siku ya tatu katika wiki ni Jumatano. Mwezi wa Julai una Jumapili tano.*

Mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa sauti mazungumzo hayo ili kuhakikisha kuwa wanasoma kwa namna inayofaa. Mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali ya ufahamu huku akitoa maelezo pale ambapo wanafunzi wanatatizika. Mwalimu awasaidie wanafunzi wenye matatizo ya kuelewa msamiati uliotumika katika kifungu hico.

**Tathmini ya kipindi ca 9**

Katika hatua hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti kwa kucunguza iwapo wanaweza kurejelea matumizi ya kalenda ya mwaka. Shughuli mbalimbali za sherehe na sikukuu zilizotajwa katika kalenda ya mwaka husika zijadiliwe pamoja na umuhimu wao katika jamii ya Wanyarwanda ili kutathmini ikiwa wanafunzi wameelewa somo hili.

## Kipindi cha 10: Kujifunza msamiati

**a) Malengo ya somo**

- Kutambua msamiati unaohusiana na kalenda ya mwaka, tarehe, siku na miezi ya sikukuu na sherehe mbalimbali ncini Rwanda.
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia msamiati wa kalenda ya mwaka, siku za wiki na miezi ya mwaka mzima.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Micoro au pica za kalenda ya mwaka ionyeshayo siku za wiki, miezi pamoja na sikukuu na sherehe mbalimbali ncini Rwanda.
- Micoro au pica za wananci wakiadhimisha sikukuu mbalimbalii ncini Rwanda.
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 69;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.)

**c) Maandalizi ya somo**

Somo hili linahusu ujifunzaji wa msamiati unaohusiana na kalenda ya mwaka, siku za wiki, miezi pamoja na sikukuu mbalimbali ncini Rwanda. Mwalimu aandae kalenda ya mwaka 2017 ili kuweza kuwaonyesha wanafunzi siku za wiki pamoja na miezi mbalimbali kuanzia mwezi Januari hadi mwezi Disemba pamoja na sherehe zote na sikukuu za kisiasa, kidini, kihistoria na kienyeji.

**d) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu

maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kuhusiana na kipindi kilicopita. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofunzwa katika kipindi kilicotangulia.

### 9.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu kalenda ya mwaka

Baada ya haya, mwalimu atangulize somo hili kuhusu msamiati unaohusiana na kalenda ya mwaka kwa kuwaonyesha wanafunzi kalenda ya mwaka ionyeshayo siku za wiki, miezi mbalimbali pamoja na sherehe na sikukuu mbalimbali ncini Rwanda.

Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kuwaomba wajadili maana za msamiati mpya waliopatana nao katika usomaji wao na jinsi msamiati huo ulivyotumiwa katika mazungumzo waliyosoma. Mwalimu awaombe wanafunzi watumie kamusi ya Kiswahili pale inapohitajika. Mwalimu azunguke darasani akiwaelekeza wanafunzi wanaopata taabu katika kuitumia kamusi au kufafanua msamiati husika.

Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi wasome msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi walizopewa katika zoezi la 9.1. Hali kadhalika, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kujadili maana za msamiati huo kisha wanafunzi watunge sentensi zao wenyewe kwa kutumia msamiati huo. Ni vyema mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia na kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika. Baada ya wanafunzi hawa kukamilisha zoezi walilopewa, mwalimu awaombe wanafunzi kusahihisha kwa pamoja mazoezi hayo ya msamiati. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wameelewa msamiati uliokuwa mpya kwao, mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi wataje msamiati ambao hawakuelewa maana yake ili ujadiliwe kwa pamoja darasani kulingana na matumizi yake katika mazungumzo waliyosoma. Ni vyema mwalimu azingatie kwamba utunzi wa sentensi za wanafunzi ndio utakaomfahamisha iwapo wanafunzi wamepata ujuzi unaotakikana katika tafakuri tanduizi, suluhisho kwa matatizo na mawasiliano kwa lugha sahihi.

### Tathmini ya kipindi ca 10

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali hayo yaegemee hasa kwa kucunguza iwapo wanafunzi wanaweza kutumia msamiati mpya kuhusu matumizi ya kalenda ya mwaka, sherehe na sikukuu ncini Rwanda, thamani ya sherehe na sikukuu ncini Rwanda.

## Kipindi cha 11: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza

**a) Malengo ya somo**

- Kucunguza kwa usahihi kalenda ya mwaka kwa kutambua vizuri tarehe, siku na miezi ya sikukuu na sherehe mbalimbali ncini Rwanda;
- Kutaja orodha ya siku za wiki na miezi ya mwaka mzima;
- Kuelewa kalenda yote ya mwaka na mfuatano wa sherehe na sikukuu ncini Rwanda;

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Micoro au pica za kalenda ya mwaka ionyeshayo siku za wiki, miezi pamoja na sikukuu na sherehe mbalimbali ncini Rwanda;
- Micoro au pica za wananci wakiadhimisha sikukuu mbalimbalii ncini Rwanda;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 69-71;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.)

**c) Maandalizi ya somo**

Somo hili linahusu matumizi ya lugha pamoja na kusikiliza na kuzungumza kuhusiana na kalenda ya mwaka wa 2017. Mwalimu aandae micoro au pica za kalenda ya 2017 au kalenda halisi za mwaka 2017 kwa ajili ya kufundishia somo hili. Kalenda ya mwaka ionyeshe wazi siku za wiki pamoja na miezi mbalimbali kuanzia mwezi Januari hadi mwezi Disemba. Katika kalenda hizi, sherehe zote na sikukuu zitajwe zikiwa za kisiasa, kidini, kihistoria na kienyeji.

**d) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Mwalimu aanze kipindi hiki kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kuhusiana na somo lililopita. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofunzwa katika kipindi kilicotangulia.

### 9.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

Baada ya haya, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha wajadili kuhusu:

1. *Miezi yote katika kalenda iliyo na siku thelathini.*
2. *Miezi yote katika kalenda iliyo na siku thelathini na moja.*
3. *Mwezi katika kalenda ulio na siku cace kuliko thelathini.*
4. *Miezi katika kalenda iliyo na Jumapili nyingi kuliko mingine.*
5. *Miezi katika kalenda iliyo na sikukuu rasmi za kusherehekewa*

Mbali na hayo, mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kusimulia umuhimu wa siku za wiki, miezi mbalimbali pamoja na sherehe na sikukuu mbalimbali katika jamii ya Wanyarwanda. Mwalimu asimulie kuhusu umuhimu wa kuwa na kalenda ya mwaka, umuhimu wa kuwa na sherehe na sikukuu mbalimbali, umuhimu wa kujua miezi ya mwaka, wiki za mwaka na siku za wiki ili wanafunzi waelewe umuhimu wa kalenda. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuelewa kalenda ya mwaka kwa kuwashirikisha kujadili kuhusu:

- ✓ *Mwaka una wiki hamsini na mbili (52).*
- ✓ *Mwaka una miezi kumi na miwili (12).*
- ✓ *Mwezi una wiki nne (4).*
- ✓ *Wiki ina siku saba (7).*

## 9.4 Kusikiliza na kuzungumza: Maigizo

Katika hatua hii, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha waigize mazungumzo kati ya Birasa na Kalisa kuhusu matumizi ya kalenda ya mwaka. Mwalimu afuatilie kwa karibu maigizo ya wanafunzi. Awahimize wanafunzi kutumia lugha ya Kiswahili sanifu iliyo rasmi pamoja na kuwa na ujasiri wa kuzungumza mbele ya watu. Wanafunzi wawe na motisha na mwalimu awahimize kupenda nci yao kwa kuwa wazalendo. Kutokana na maigizo ya wanafunzi, mwalimu asahihishe makosa ya kimatamshi yanayoweza kujitokeza pindi tu yanapotokea.

## Tathmini ya kipindi ca 11

Mwalimu ahitimishe kipindi hiki kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali hayo yaegemee hasa kwa kucunguza iwapo wanafunzi wanaweza kutumia kalenda kwa usahihi bila matatizo yoyote. Pia, mwalimu acunguze iwapo wanafunzi wamepata ujasiri wa kuzungumza mbele ya wanafunzi wenzao kwa lugha rasmi na sahihi kupitia maigizo watakayoyafanya.

## Kipindi cha 12: Sarufi (Herufi kubwa na alama za uandishi)

**a) Malengo ya somo**

- Kufahamu  matumizi ya herufi kubwa;
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia herufi kubwa kwa usahihi;
- Kutumia herufi kubwa kwa usahihi katika masimulizi na mazungumzo kwa jumla;

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Masimulizi yaliyoandikw akwa kutumia herufi kubwa kwa usahihi;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 71;
- Wanafunzi wenyewe;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Somo hili linahusu sarufi ya matumizi ya herufi kubwa katika sentensi na aya. Mwalimu anaweza kuandaa na kuandika kwenye cati masimulizi yaliyotumia herufi kubwa kwa usahihi.

Mwalimu ajiandae kuwashirikisha wanafunzi katika kufahamu matumizi ya herufi kubwa kwa kutunga sentensi mbalimbali sahihi.

**d) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi wake maswali mepesi kuhusiana na somo la sarufi lililopita kuhusu matumizi ya wakati ujao na wakati uliopita katika tungo yakinishi na tungo kanushi. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofunzwa katika somo lililotangulia.

**9.5 Matumizi ya herufi kubwa na alama za uandishi**

Baada ya haya, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha awaombe wasome kifungu kifupi walicopewa katika *Kitabu*

*ca Mwanafunzi*, ukurasa 71 kuhusu Mwalimu Biruta. Baadaye, wanafunzi watambue matumizi ya herufi kubwa katika sentensi za kifungu hico.

Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi waeleze matumizi mbalimbali ya herufi kubwa katika sentensi. Baada ya majadiliano, mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua  matumizi mbalimbali ya herufi kubwa.

Mwalimu awakumbushe wanafunzi kuwa lazima kila sentensi kamili ianze kwa herufi kubwa na ikamilike kwa alama ya uandishi inayofaa. Kwa mfano: *Sikukuu itaadhimishwa kesho. Utaadhimisha sikukuu gani kesho? n.k.*

Pia, mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kubaini alama mbalimbali za uandishi pamoja na matumizi yao katika sentensi, maongezi na vifungu.

### Tathmini ya kipindi ca 12

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali hayo yaegemee haswa kwa kucunguza iwapo wanafunzi wanaweza kutambua matumizi mbalimbali ya herufi kubwa kwa kutunga  sentensi sahihi.

**Maelezo muhimu kwa mwalimu**

- ***Kalenda*** ni kifaa kinachoonyesha siku, tarehe na miezi katika mwaka.
- Mwaka una miezi kumi na miwili ambayo ni: ***Januari, Februari, Machi, Aprili, Mei, Juni, Julai, Agosti, Septemba, Oktoba, Novemba*** na ***Disemba***.
- Siku katika kila mwezi huanza kwa Jumapili hadi Jumamosi.
- Mwaka mmoja una wiki hamsini na  mbili.
- Wiki moja ina siku saba ambazo ni: ***Jumapili, Jumatatu, Jumanne, Jumatano, Alhamisi, Ijumaa*** na ***Jumamosi*.**
- Katika kalenda, siku za Jumapili na Jumamosi huandikwa kwa kutumia wino wa rangi tofauti.
- Siku za matukio makuu ya sherehe za kitaifa na kijamii huandikwa pia kwa kutumia wino wa rangi tofauti.

### 9.6  Mazoezi ya ziada

### i)  Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atoe zoezi la ziada ambalo linalenga kuinua kiwango ca cini kwa wanafunzi wasioweza kuelewa kwa haraka kama wenzao.

***Kwa mfano:***

*Andika sentensi hizi kwa usahihi.*

1. siku ya uhuru itaadhimishwa na wananci mjini kigali.
2. idi ul fitri itaadhimishwa ijumaa.
3. rubona alifunga mlango.
4. kikapu ca gasimba kimejazwa matunda.
5. ahishakiye aliadhimisha *umuganura*.

**Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu**

1. Siku ya Uhuru itaadhimishwa na wananci mjini Kigali.
2. Idi ul Fitri itaadhimishwa Ijumaa.
3. Rubona alifunga mlango.
4. Kikapu ca Gasimba kimejazwa matunda.
5. Ahishakiye aliadhimisha *Umuganura*.

**ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka**

Kwa wanafunzi wenye kiwango ca juu ca uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge sentensi tano zenye kuonyesha matumizi matano ya herufi kubwa.

***Kwa mfano:***

1. ***C**akula hiki kitaliwa na mtoto wake.*
   **Matumizi:** Herufi kubwa imetumika mwanzoni mwa sentensi.
2. ***N**gabo anasomea udaktari cuoni.*
   **Matumizi:** Herufi kubwa imetumika mwanzoni mwa jina la mtu.
3. *Somo la **K**iswahili hufundishwa kila **I**jumaa.*
   **Matumizi:** Herufi kubwa imetumika mwanzoni mwa somo pamoja na jina la siku ya wiki.

# 9.7 Majibu

**Zoezi la makundi, ukurasa 67**

Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi kwa kurejelea mcoro uliopo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 67.

**Kwa mfano:**

*Mcoro unaonyesha wanafunzi wawili wanaojadiliana kuhusu kalenda ya 2017 iliyo ukutani.*

**Maswali ya ufahamu, ukurasa 69**

1. Jumapili tano (5)
2. Ijumaa
3. Siku 365
4. Jumatano nne (4)
5. Tarehe moja mwezi Februari
6. Jumatatu
7. Jumapili tarehe moja mwezi wa Januari
8. Thelathini na moja
9. Alhamisi nne (4)
10. Miezi minne: Juni, Septemba, Oktoba, Novemba

**Zoezi la 9.1(i), ukurasa 69**

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi. Wanafunzi wafafanue maana ya maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi walizopewa.

***Mifano:***

1. **Jumamosi:** siku inayofuata siku ya Ijumaa katika wiki; siku inayotangulia Jumapili.
2. **mwezi:** kipindi mojawapo kati ya kumi na viwili katika mwaka ambaco huwa na siku kati ya 28-31.
3. **siku:** muda wa saa ishirini na nne.
4. **kalenda:** kifaa kinacotumiwa kuonyesha idadi ya siku, wiki na miezi ya mwaka.
5. **mwaka:** kipindi ca kuanzia Januari hadi kufikia Disemba.
6. **Disemba:** Mwezi wa kumi na mbili katika kalenda ya mwaka.
7. **tarehe:** siku ya mwezi ambayo hutajwa kwa idadi.
8. **Mei:** mwezi wa tano katika kalenda ya mwaka.

**Zoezi la 9.1(ii), ukurasa 69**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi na zihusishe maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi walizopewa.

***Kwa mfano:***

1. *Sisi huenda sokoni kila **Jumamosi**.*
2. *Huu ni **mwezi** wa Ramadhani.*
3. *Hii ndiyo **siku** ya harusi yao.*
4. ***Kalenda** yetu imeraruka.*
5. *Nitamaliza elimu ya kiwango ca sekondari **mwaka** ujao.*

6. *Tutaenda kumtembelea nyanya yetu mwezi wa **Disemba**.*
7. *Hatukuelezwa **tarehe** ya kufungua shule.*
8. *Nitasafiri kuelekea Marekani mwezi **wa Mei**.*

**Zoezi la matumizi ya lugha, ukurasa 69-70**

Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi katika makundi yao. Majibu yao yawe sahihi. Yaani:

1. Aprili, Juni, Septemba, Novemba
2. Januari, Maci, Mei, Julai, Agosti, Oktoba, Disemba
3. Februari
4. Januari, Aprili, Julai, Oktoba, Disemba (Miezi hii ina Jumapili 5)
5. Januari, Februari, Maci, Aprili, Mei, Julai, Agosti, Disemba
6. Mwezi wa Disemba una Jumapili tano.
7. Tarehe ya kwanza katika mwezi wa Septemba ni siku ya Ijumaa.
8. Tarehe kumi mwezi wa Agosti ni siku ya Alhamisi.

**Zoezi la kusikiliza na kuzungumza, ukurasa 71**

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili na ahakikishe kuwa wanaigiza mazungumzo kati ya Birasa na Kalisa. Wanafunzi wazingatie matamshi sahihi katika maigizo yao.

**Zoezi la maswali ya tathmini, ukurasa 72**

1. Herufi kubwa zimetumika**:**
    a) Kutajia majina ya watu.
    **Kwa mfano:** Biruta
    b) Kutajia majina ya mahali maalumu.
    **Kwa mfano:** Gikondo, Kigali na Kamashashi
    c) Kutajia majina ya siku na sherehe.
    **Kwa mfano:** Jumamosi, Krismasi
    d) Kutajia majina ya lugha na masomo.
    **Kwa mfano:** Kiswahili, Kiingereza, Historia na Hisabati
2. Alama nyingine za uandishi zilizotumika ni:
    a) Alama ya kiulizi (?)
    Alama hii imetumika kuulizia swali.
    **Mfano wa sentensi:** *"Kwa nini mmecelewa leo**?**"*
    b) Alama za usemi ("")
    Alama hizi zimetumika kuonyesha maneno yaliyotamkwa na mtu moja kwa moja katika unenaji wake.

ch) Alama ya hisi (!)
Alama hii imetumika kuonyesha hisia ya mshangao. Pia huitwa alama ya mshangao.

**Mfano wa sentensi:** *"Ooh! Kumbe wewe unapenda kusoma hivi?"*

**Zoezi la 9.2, ukurasa 72**

1. Kwa nini ulichelewa shuleni?
2. Lo! Umebeba mzigo huo peke yako!
3. Mama alienda sokoni kununua: ndizi, machungwa, viazi na nanasi.
4. Paka amekunywa maziwa.
5. Ngabo atakuja lini?

**Zoezi la 9.3, ukurasa 72**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi. Yaani:

*Siku moja nilienda sokoni kununua: ndizi, sukari, samaki, mboga na machungwa. Njiani nilipatana na rafiki yangu Birasa. Alishangaa kuniona na kusema, "Ah! Kumbe wewe pia huja sokoni?" Nikamjibu kuwa mimi hupenda kumsaidia mama kununua bidhaa mbalimbali. Nilimuuliza, "Umekuja kununua nini?" Akanijibu kuwa alikuja kununua mboga na samaki.*

**Majibu ya tathmini ya mada ya 2**

**Zoezi la 1, ukurasa 73**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi katika makundi yao. Kwa mfano:

1. *Wakristo husherehekea sikukuu ya Pasaka mwezi Aprili kila mwaka. Sherehe hizi huwa kwa ajili ya kukumbuka na kuheshimu kusulubiwa na kufa kwa Yesu Kristo. Yesu Kristo anaaminiwa kuwa mwana wake Mungu Muumba wa mbingu na ardhi. Sikukuu hii huwahusisha Wakristo kukusanyika makanisani na kutubu dhambi zao na kuomba pamoja wakikumbuka jinsi Yesu Kristo alivyowafia msalabani ili kuziondoa dhambi zao. Kufufuka kwake Yesu huwa ndio kilele cha sherehe hizi. Yesu Kristo anaaminiwa kuwa hai na Mkombozi wa Wakristo na anaishi mbinguni pamoja na Mungu.*
2. *Waislamu husherehekea sikukuu ya Idil ul Fitri mwezi wa Julai kila mwaka. Ili kuwa na sherehe hizi, Waislamu hufunga kwa mwezi mzima kuadhimisha mwezi wa Ramadhani tukufu. Katika kipindi hiki, Waislamu hula tu alfajiri na magharibi kisha hushinda kwenye maombi mchana wote. Pia, katika kipindi hikii wao hutoa misaada mbalimbali kwa wasiojiweza katika jamii zao. Kilele cha mwezi huu kukamilika huwa sherehe hizi za Idi ul Fitri.*
3. *Sherehe za harusi huhusisha familia mbili, moja ya bwana harusi na nyingine*

*ya bibi harusi pamoja na wageni, marafiki na waalikwa mbalimbali. Watu hujumuika pamoja kushuhudia kuunganishwa pamoja kwa mume na mke na kuwapa baraka za wao wawili kuanza familia yao pamoja. Watu hula vyakula mbalimbali, hucheza densi, ngoma na nyimbo mbalimbali. Sherehe hizi huwa zenye furaha tele, vifijo na nderemo. Watu huvalia nadhifu sana. Magari mazuri pia hutumika kulingana na uwezo wa kifedha wa wanaohusika. Sherehe hizi hufanywa wakati wowote katika kalenda ya mwaka mzima.*

4. *Waislamu husherehekea sikukuu ya Idi ul Adha kila mwaka. Sherehe hii hufanyika tarehe ambayo hutangazwa na Jumuiya ya Waislamu Rwanda. Katika sherehe hizi Waislamu hukumbuka na kuheshimu utiifu wa Ibrahim katika Kurani Tukufu kukubali kumtoa kafara mwana wake wa kipekee aliyeitwa Isaka.*
5. *Sherehe ya Krismasi huadhimishwa na Wakristo Disemba tarehe 25 kila mwaka. Katika sherehe hii, wakristo hukumbuka na kuheshimu kuzaliwa kwa Mkombozi wao Yesu Kristo kama inavyoelezwa kwenye Biblia Takatifu. Wakristo hufurahia siku hii kwa kuhudhuria ibada makanisani, kupika na kula vyakula mbalimbali, burudani na kupeana zawadi mbalimbali.*

**Zoezi la 2, ukurasa 73**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi katika makundi yao.

***Kwa mfano:***

1. Baadhi ya sherehe katika kalenda yetu ni: Pasaka, Krismasi na *Umuganura*.
2. Siku ya kwanza ya wiki ni Jumapili katika kalenda ya mwaka.
3. Kamana anaishi wapi?
4. Lo! Simu yangu imeanguka majini!
5. Kilo moja ya chumvi huuzwa faranga mia mbili (200).

**Zoezi la 3, ukurasa 73**

1. Mwalimu atatufundisha Hisabati.
2. Ng'ombe atakunywa maji mengi.
3. Babu atatusimulia hadithi nzuri.
4. Sikukuu ya Krismasi itaadhimishwa kwa sherehe kubwa.
5. Manzi atanunua vitabu na kalamu.

**Zoezi la 4, ukurasa 74**

Mwalimu atathmini usahihi wa sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti watunge sentensi zenye vitenzi vya silabi moja katika wakati uliopita hali kanushi.

**Kwa mfano:**

1. *Mimi sikunywa maziwa ya mtoto.*
2. *Wageni hawakula viazi vitamu.*
3. *Mwalimu hakuwa mcangamfu leo.*
4. *Mgeni hakuja jana.*
5. *Ndege hakufa alipogongwa na jiwe.*

**Zoezi la 5, ukurasa 74**

1. Alama ya kiulizi (**?**)
   **Matumizi katika sentensi:** *Nani amecukua kalamu yangu**?***
2. Alama ya hisi/ mshangao (**!**)
   **Matumizi katika sentensi:** *Ala! Paka yuko juu ya mti!*
3. Koma/kipumuo (**,**)
   **Matumizi katika sentensi:** *Ninataka mkate**,** muwa**,** viazi na maharagwe.*
4. Koloni/ nukta mbili (**:**)
   **Matumizi katika sentensi:** *Miezi miwili ya kwanza katika kalenda ni**:** Januari na Februari.*
5. Mabano **( )**
   **Matumizi katika sentensi:** *Kikombe kimoja ca maziwa ni faranga tano **(**5**)** pekee.*
6. Ritifaa (**'**)
   **Matumizi katika sentensi:** *Ng**'**ombe wetu hula nyasi na kunywa maji mengi.*

**Zoezi la 6, ukurasa 74**

Mwalimu atathmini masimulizi ya wanafunzi. Sharti yatumie sentensi sahihi kisarufi katika wakati uliopita.

***Kwa mfano:***

*Mwaka uliopita tuliadhimisha sikukuu ya Krismasi. Ilikuwa tarehe 25 mwezi wa Disemba. Mimi na kaka yangu tulienda kanisani. Tulihudhuria ibada ambayo ilikuwa ya kufurahisha sana. Huko kanisani kulikuwa na waimbaji wengi. Waliimba nyimbo za kumsifu Yesu Kristo. Baada ya ibada tulienda hotelini na tukala nyama iliyocomwa. Mwisho, tulikunywa soda na kuelekea nyumbani.*

**Zoezi la 7, ukurasa 75**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti sentensi ziwe sahihi kisarufi na zihusishe maneno waliyopewa katika wakati ujao, tungo yakinishi na tungo kanushi.

***Kwa mfano:***

1. *Mimi nita**sherehekea** sikukuu ya Pasaka mjini Kigali.*

   *Mimi sita**sherehekea** sikukuu ya Pasaka mjini Kigali.*

2. *Mama ata**kula** muhogo jioni.*

   *Mama hata**kula** muhogo jioni.*

3. *Tuta**adhimisha** sikukuu ya Uhuru mwaka huu.*

   *Hatuta**adhimisha** sikukuu ya Uhuru mwaka huu.*

4. *Neza ata**kunywa** uji.*

   *Neza hata**kunywa** uji.*

5. *Mutoni ata**soma** hadithi.*

   *Mutoni hata**soma** hadithi.*

**Zoezi la 8, ukurasa 75**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi kama ifuatavyo:

*Sikukuu ya mwaka mpya huadhimishwa tarehe moja Januari. Siku ya Mashujaa huadhimishwa tarehe moja mwezi Februari. Je, wewe uliadhimisha sikukuu ya mwaka mpya kwa njia gani? Waislamu wana sherehe mbili kuu ambazo ni: Idi ul Fitri pamoja na Idi ul Adha. Wakristo vilevile wana sherehe mbili kuu ambazo ni: Krismasi pamoja na Pasaka. Je, wewe husherehekea sikukuu gani ya kidini?*

**Zoezi la 9, ukurasa 75**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi kama ifuatavyo:

1. *Rais aliongoza sherehe ya siku ya Uhuru katika uwanja wa Gikondo.*
2. *Je, wewe ulihudhuria sherehe ya Umuganura mwaka jana?*
3. *Lo! Sikujua unaweza kuimba vizuri hivyo kwenye sherehe hiyo.*

Sura ya
# Tatu

# Mada Kuu 3: Ukuzaji wa matumizi ya lugha kimazungumzo

## Mada Ndogo: Midahalo na mijadala kuhusu shughuli za maendeleo na uzalishajimali dhidi ya umaskini nchini

### Uwezo upatikanao katika mada hii

Mwanafunzi aweze kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika kwa kutumia lugha katika muktadha wa midahalo na mijadala darasani.

### Malengo ya kujifunza

| Maarifa na ufahamu | Stadi | Maadili na mwenendo mwema |
|---|---|---|
| • Kubaini mambo ya kuzingatia katika namna bora ya kujielezea na kujadili katika makundi.<br>• Kuelezea mwenendo unaofaa wakati wa kutoa hoja katika midahalo.<br>• Kuonyesha sifa ya kuzungumza hadharani bila woga wala wasiwasi kwa kutumia Kiswahili sanifu.<br>• Kubainisha maoni yake na msamiati unaofaa, matumizi sahihi ya nyakati kwa ujumla.<br>• Kukumbuka na kuainisha mabadiliko yanayojitokeza kwenye vitenzi vinapotumiwa katika wakati timilifu hali yakinishi na hali kanushi.<br>• Kuelezea mabadiliko yanayojitokeza wakati wa kunukuu maneno yaliyotamkwa na mtu mwingine. | • Kujadili na kujitetea hadharani kulingana na mada ya midahalo na mijadala inayotolewa kwa kujenga hoja inayothibitisha dai.<br>• Kutoa maoni binafsi, kuzingatia na kutetea au kupinga hoja za wenzake kwa njia ya mazungumzo.<br>• Kucambua na kupangilia hoja kabla ya kushiriki katika mdahalo au majadiliano.<br>• Kuzingatia sifa au mwenendo wa mjadala katika kufanya maandalizi na hatimaye kucangia majadiliano kwa maandishi au mazungumzo.<br>• Kuongoza au kuongozwa katika mdahalo wa watu wanaotoa maoni juu ya mada fulani kwa kuzingatia mwenendo na maadili mema yanayojitokeza katika mdahalo.<br>• Kutambua viambishi wakati vya vitenzi katika hali yakinishi na hali kanushi.<br>• Kutoa ripoti ya habari fulani kwa njia ya kunukuu. | • Kujali na kuthamini kazi yoyote katika maisha yake ya kila siku.<br>• Kucukia tabia zote zinazokwamisha ufanisi wa kazi kama vile: *uvivu, ulevi, ubaguzi, ukabila* n.k.<br>• Kujiamini na kuwaamini wengine.<br>• Kuunga umoja kwa minajili ya ushirikiano.<br>• Kujenga utamaduni wa kusikiliza wengine na kuheshimu maoni yao.<br>• Kujenga utamaduni wa kushindana kwa hoja. |

## Maelezo muhimu kwa mwalimu

Mwalimu afahamu na awafahamishe wanafunzi kuwa mada hii inahusiana na masomo mengine kama vile: ***somo la karatasi ya maarifa*** kuhusu mada inayohusu usafiri, kazi, ukosefu wa kazi na athari zake kiucumi pamoja na ***somo la Ujasiriamali*** kuhusu mada ya maendeleo binafsi.

Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanaelewa kuwa mazungumzo ni njia nzuri ya kukuza uwezo wa mwanafunzi wa kutumia lugha. Kwa hivyo, mada hii inacukuliwa kama fursa muhimu ya kumsaidia mwanafunzi kukuza uwezo wake wa kuwasiliana na wengine na kujenga hoja kamili za kujitetea mbele ya wengine. Hivyo basi, mwanafunzi apewe nafasi kubwa na mazoezi ya kutosha ambayo huweza kumfaa katika kuongeza umahiri wa kujadiliana na kutoa maoni mbalimbali kwa kupinga au kutetea hoja za wengine na hata kufafanua jambo fulani linalohitaji ufumbuzi na uamuzi fulani. Mwalimu atafute namna ya kuwahimiza wanafunzi kushiriki katika midahalo na mijadala ya darasani na ile ya nje ya darasa ambapo wanafunzi wanaweza kuanzisha vilabu mbalimbali vinavyodhamiria kukuza uwezo wao kimaongezi kwa kutumia lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi.

Katika mada hii, dhana za kisarufi pia zimejitokeza: *wakati uliotimilika, tungo, hali yakinishi, hali kanushi, umoja, wingi, usemi wa asili, usemi wa taarifa, kiunganishi, alama za vituo* na kadhalika.

## Masuala mtambuka

Baadhi ya masuala mtambuka ambayo yatashughulikiwa katika mada hii ni elimu ya pamoja, amani na maadili, usawa wa kijinsia, elimu kuhusu fedha, mazingira pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa na mwendelezo wake.

Elimu ya pamoja itaendelezwa kupitia kwa wanafunzi wote kusoma pamoja kwa kuwashirikisha hata na wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali na matatizo mbalimbali. Elimu hii ya pamoja pia itahusisha wanafunzi wote kuwakubali na kushirikiana kwa pamoja na wenzao kutoka katika matabaka mbalimbali ya kijamii.

Usawa wa kijinsia utatiliwa mkazo kwa kuwafahamisha wanafunzi kuwa wasicana pamoja na wavulana wana uwezo sawa wa kufaulu katika maisha yao lica ya jinsia zao tofauti. Mwalimu awahusishe wanafunzi wa kike pamoja na wale wa kiume katika midahalo na mijadala mbalimbali watakayopewa. Wanafunzi pia watafundishwa umuhimu wa mazingira yao na namna ya kuyahifadhi.

Elimu kuhusu pesa itafundishwa kwa kuwashirika wanafunzi katika midahalo na mijadala mbalimbali kuhusiana na shughuli za kuboresha ucumi wa taifa lao.

Amani na maadili yatafundishwa kupitia kwa wanafunzi kushirikiana katika kazi mbalimbali za makundi darasani hasa midahalo na mijadala mbalimbali watakayopewa.

### Uwezo wa jumla

Mwalimu ahakikishe kuwa katika ufundishaji wake, wanafunzi wanapata uwezo wa kuwa na tafakuri tanduizi, usuluhishaji wa matatizo, mawasiliano katika lugha rasmi, stadi za utafiti, ubunifu na ugunduzi, ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha pamoja na ujifunzaji wa muda mrefu.

Wanafunzi wataweza kuwa na tafakuri tanduizi kwa kufikiri kwa undani (kutafakari zaidi) ili kuweza kushiriki katika midahalo na mijadala mbalimbali pamoja na kuyajibu maswali katika mada hii. Kupitia kwa mazoezi ya kuigiza pamoja na kushiriki katika midalo na mijadala mbalimbali, wanafunzi watahimizwa kuwasiliana kwa lugha rasmi na sahihi pamoja na kuwa na utawala binafsi pamoja na kuzifahamu stadi mbalimbali za maisha. Stadi za utafiti zitahitajika hapa ambapo wanafunzi watafanya utafiti mbalimbali kuhusiana na midahalo na mijadala mbalimbali watakayoshiriki. Ujifunzaji wa muda mrefu uendelezwe kupitia kwa wanafunzi kupata maarifa mbalimbali kuhusiana na shughuli zinazoweza kuboresha ucumi wa nci yao pamoja na maarifa watakayotumia nje ya darasa na katika maisha yao ya kila siku.

### Msamiati maalum

Msamiati maalum na muhimu ambao wanafunzi watapatana nao katika mada hii ni kuhusu ukuzaji wa matumizi ya lugha kimazungumzo ncini Rwanda kama vile:

| | **Msamiati** | **Maana** |
|---|---|---|
| 1. | ***mwenyekiti*** | mtu aliyecaguliwa kuongoza mkutano, cama au shirika kwa kipindi fulani. |
| 2. | ***mdahalo*** | mazungumzo maalum ambayo hufanywa na watu wenye mitazamo inayokinzana. |
| 3. | ***mjadala*** | mazungumzo yanayohusu mada fulani ambayo hufanywa kwa kujenga hoja. |
| 4. | ***katibu*** | mtu anayeandika na kuhifadhi hoja katika mdahalo au mjadala. |

| | | |
|---|---|---|
| 5. | ***mpinzani*** | mtu aliye na mtazamo tofauti na watu wengine anaoshindana nao. |
| 6. | ***mtetezi*** | mtu anayeunga mkono hoja Fulani katika majadiliano. |
| 7. | ***hoja*** | maelezo ambayo huunga mkono au kupinga jambo linalojadiliwa. |
| 8. | ***mshiriki*** | mtu anayehusika katika shughuli fulani. |
| 9. | ***mazungumzo*** | maongezi kati ya watu wawili au zaidi. |
| 10. | ***kujadili*** | kuzungumza kwa kutoa hoja aidha ya kuunga mkono au ya kupinga. |

### Usuluhishaji wa tatizo

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi yanayotakikana kisha awaombe wacunguze kwa makini mcoro ulio katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 77 kuhusiana na midahalo na mijadala mbalimbali watakayopewa. Wanafunzi pia wacunguze mada za midahalo na mijadala waliyopewa. Wanafunzi wote washirikishwe katika shughuli hii. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika makundi yao ili waweze kujibu maswali watakayoulizwa na mwalimu ili kuelewa kinacohitajika kujadiliwa katika mada mbalimbali husika. Kwa hivyo, mwalimu acocee uwezo wa wanafunzi wa kupata maarifa kuhusu ubunifu na ugunduzi na tafakuri tunduizi kwa kucunguza mada mbalimbali za midahalo na mijadala iliyo katika vitabu vya wanafunzi.

### Ushirikishaji wa wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali

Ili kuwashirikisha kwa pamoja wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali, ni vyema mwalimu awe na vifaa maalum vya kuwasaidia wanafunzi wa aina hii katika kusoma na kujifundisha kwao. Kwa wanafunzi wasio na uwezo wa kuona, mwalimu ahusishe matumizi ya breli pamoja na vifa vya kunasia sauti. Kwa wanafunzi wasio na uwezo wa kusikia, mwalimu ahusishe matumizi ya lugha ya ishara. Mwalimu anaweza kuwahusisha watafsiri wa lugha ya ishara. Haya yatawawezesha wanafunzi hawa kusoma kama wenzao bila vikwazo vyovyote. Nafasi ya wanawake katika shughuli kama vile za kushiriki katika midahalo na mijadala mbalimbali itiliwe maanani kupitia mcoro ulio katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 77 ili kukuza usawa wa kijinsia na elimu ya pamoja kwa kudumisha ushirikiano na mienendo mizuri miongoni mwa wanafunzi.

**Orodha ya masomo na vipindi**

| Mada ya somo | Idadi ya vipindi |
|---|---|
| **Somo la 10:** Mdahalo | 5 |
| **Somo la 11:** Mjadala | 5 |
| **Somo la 12:** Mjadala | 4 |
| | **JUMLA: 14** |

# Somo la 10: Mdahalo

## Kipindi cha 1: Kusoma ufahamu

**a) Malengo ya somo**

- Kusoma kwa usahihi mfano wa mdahalo kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;
- Kutaja majina ya watu wanaoshiriki katika mdahalo.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Mdahalo uliorekodiwa;
- Micoro ya wasemaji na wasikilizaji katika mdahalo;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 77-80;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia, n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Mdahalo ulioandaliwa utumiwe kuongoza wanafunzi na kuwapa mwelekeo kamili wa kuendesha mdahalo wowote. Mwalimu aandae somo kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu utaratibu wa mdahalo kupitia wahusika wote wanaojitokeza katika mfano huu ili mwanafunzi apate pica kamili ya mdahalo mzuri na jinsi unavyofanywa. Kwa kuwa mdahalo huu unahusu shughuli za maendeleo na uzalishaji mali dhidi ya umaskini, ni vyema mwalimu alete vifaa vingine vinavyoweza kurahisisha uelewa wa mada hii kwa kurejelea shughuli za elimu na biashara. Katika hali hii, mwalimu anaweza kucora kwa mfano pica za mwalimu na wanafunzi, pica zinazoonyesha mafanikio ya mtu mwenye elimu na shughuli ambazo anaweza kuzifanya ili azalishe mali, shughuli za mfanyabiashara na biashara zake mbalimbali na kadhalika.

Hivyo basi, mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kufundishia somo hili ili kuwaelekeza ipasavyo wanafunzi wakati wa kusoma na kuigiza mazungumzo yao. Ikiwa kuna wanafunzi wasioweza kuona au kusikia, ni lazima mwalimu atafute namna ya kuwaelekeza kuelewa somo hili kwa kuhusisha vifaa alivyovileta na kueleza micoro iliyopo kwa kutamka huku maelezo mengine yakiandikwa ubaoni. Ni vyema pia mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli ya wanafunzi iliyopendekezwa katika kitabu ca mwanafunzi.

**d) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake, kisha awaulize maswali kuhusu somo lililopita. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu na hatimaye wasahihishe kazi waliyopewa kama kazi ya ziada. Mwalimu atangulize somo kwa kuwagawa wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha awacangamshe kwa kuwauliza maswali kuhusu mcoro ulio katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 77. Mwalimu awaelekeze kuelewa maana ya mdahalo na lengo lake la jumla. Mwalimu awaulize maswali kama vile: *Mnaona nini kwenye mcoro huu? Watu hawa wanafanya nini?* Wanafunzi wajibu maswali waliyoulizwa na mwalimu. Kwa mfano: *Mimi ninaona watu. Watu hawa wanazungumza* na kadhalika.

Mwalimu atumie pica au micoro aliyoileta ili aweze kufafanua mielekeo tofauti ya wasemaji wanaoshiriki katika mdahalo ambapo upande wa utetezi unadhihirisha umuhimu wa elimu dhidi ya biashara katika njia tofauti za kuzalisha mali dhidi ya umaskini. Kupitia pica na micoro hiyo, ni vyema mwalimu awaongoze wanafunzi kuelewa umuhimu wa kupanga na kutoa hoja kamili zenye kueleweka kwa wanaoshiriki katika mazungumzo. Aidha, mwalimu aulize maswali kwa kuwataka wanafunzi waweze kugundua kile kinacoendelea katika pica na micoro iliyopo ili wakuze uwezo wao wa kuwasiliana katika lugha rasmi na kuwasaidia kupata ujuzi katika ubunifu na ugunduzi, tafakuri tunduizi, usawa wa kijinsia kupitia wahusika wanaoshiriki katika mazungumzo na zile za wasikilizaji waliopo. Ili kufikia lengo lake, mwalimu awe ameleta pica au micoro yenye wahusika wa jinsia tofauti, rika tofauti na wenye ulemavu tofauti ili afanikiwe kuyagusia masuala ya elimu ya pamoja ambayo ni muhimu katika kukuza na kuendeleza mienendo mizuri na stadi za maisha miongoni mwa wanafunzi. Hivyo basi, ni lazima mwalimu awaelekeze wanafunzi ili waweze

kuelewa kile kinacofanywa katika mazungumzo ya aina ya mdahalo kabla ya kusoma mfano uliopendekezwa katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 77.

### 10.1 Kusoma na ufahamu: Mdahalo kuhusu 'Elimu ni muhimu kwa maendeleo ya wananci kuliko biashara'

Mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa kimya mazungumzo yaliyo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 77-79. Wanafunzi wasome kama wanavyoelekezwa na mwalimu. Baada ya kusoma huku, mwalimu awateue wanafunzi tofautitofauti ili wasome kwa sauti mazungumzo hayo. Katika shughuli hii, mwalimu acunguze iwapo wanafunzi wanajaribu kuiga mazungumzo huku wakizingatia kanuni zifaazo za kisarufi, utamkaji sahihi na kiimbo kinacotakiwa. Baadaye, mwalimu acunguze iwapo wanafunzi wote wameyaelewa mazungumzo waliyosoma kwa kuwauliza maswali kama vile: *Ni watu gani wanaozungumza katika kifungu hiki? Watu hao wanazungumzia nini? Watu hao wana mitazamo gani? Ni wahusika gani waliotoa maoni mazuri?* na kadhalika. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu na watoe hoja zao kuhusu mhusika aliyetoa hoja nzuri kuliko wengine.

Mwalimu aendelee kwa kuwauliza wanafunzi sababu za ucaguzi wao na awaongoze wajitetee kwa kutoa maoni yao kikamilifu. Shughuli hii itawezesha kuwepo kwa pande tofauti zenye mawazo na misimamo tofauti. Mwalimu acukue fursa hii kuwafafanulia wanafunzi utaratibu wa mdahalo ambapo watu wa pande mbili hujadiliana na kutoa hoja zinazotetea au kupinga wazo lililo katika mada inayozungumziwa huku akiuliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusiana na yale waliyosoma. Mwalimu asahihishe makosa ya kimatamshi pindi yanapojitokeza.

Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali ya mazungumzo waliyosoma huku akitoa maelezo pale ambapo wanafunzi wanatatizika. Mwalimu awasaidie wanafunzi wenye matatizo ya kuelewa msamiati uliotumika katika mazungumzo hayo.

#### Tathmini ya kipindi ca 1

Katika hatua hii, mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali tofauti kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali haya yatilie mkazo uwezo wa wanafunzi wa kubainisha watu muhimu wanaohitajika katika mazungumzo ya mdahalo na kudhihirisha majukumu yao katika kuendeleza mazungumzo hayo: *mwenyekiti, katibu, watetezi, wapinzani* na *wasikilizaji washiriki*. Vilevile, mwalimu acunguze iwapo wanafunzi wanaweza kueleza utaratibu wa mdahalo na mambo muhimu yanayozingatiwa ili mdahalo uweze kufanyika kwa njia inayofaa kama vile: *nidhamu, kutunza muda uliopangwa* na kadhalika.

## Kipindi cha 2: Kujifunza msamiati

### a) Malengo ya somo

- Kubaini msamiati unaotumika katika mdahalo;
- Kutaja majina ya watu wanaoshiriki katika mdahalo;
- Kutumia msamiati wa mdahalo katika sentensi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Mdahalo uliorekodiwa;
- Micoro au pica za wasemaji na wasikilizaji katika mdahalo;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 80-81;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### c) Maandalizi ya somo

Mwalimu aandae somo hili kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu utaratibu wa midahalo na mijadala kupitia wahusika wote wanaojitokeza katika mfano watakaousoma kutoka katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 80 ili mwanafunzi apate pica kamili ya midahalo na mijadala mizuri na jinsi inavyofanywa. Kwa kuwa mdahalo huu unahusu shughuli za maendeleo na uzalishajimali dhidi ya umaskini, ni vyema mwalimu alete vifaa vingine vinavyoweza kurahisisha uelewa wa mada hii kwa kurejelea shughuli za elimu na biashara.

Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kujifunzia somo hili. Ikiwa kuna wanafunzi wasioweza kuona au kusikia, ni lazima mwalimu atafute namna ya kuwaelekeza kuelewa somo hili kwa kuwaomba wao wenyewe kuvigusa vifaa alivyovileta na kueleza micoro iliyopo kwa kutamka huku maelezo mengine yakiandikwa ubaoni. Ni vyema pia mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli ya wanafunzi iliyopendekezwa katika kitabu ca mwanafunzi.

### 10.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu mdahalo

Katika hatua hii, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu ili wajadiliane kuhusu maana za msamiati mpya waliopatana nao huku wakitumia kamusi pale inapohitajika. Ili kuwaelekeza kupata uelewa wa msamiati huo, mwalimu awaongoze wanafunzi katika kucunguza matumizi ya msamiati huo katika kifungu ca mazungumzo walicokisoma. Wanafunzi wajadiliane na mwalimu azunguke darasani akitoa maelekezo kwa wanafunzi wanaotatizika. Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi wajadiliane kuhusu zoezi la 10.1 la msamiati na ahakikishe kuwa wanafunzi wote wamejibu maswali yaliyopo. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanatunga sentensi zao wenyewe kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi walizopewa. Mwalimu awaongoze wanafunzi kutunga sentensi zenye kuimarisha tabia za kujali na kuthamini kazi yoyote katika maisha ya kila siku, kucukia tabia zote zinazozuia ufanisi wa kazi, kujiamini, kuwaamini wengine na kuunga mkono umoja kwa minajili ya ushirikiano. Baadaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi kufanya zoezi la 10.2 na zoezi la 10.3.

### Tathmini ya kipindi ca 2

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti kwa kurejelea msamiati mahususi uliopatikana katika kifungu ca mdahalo kuhusu ‘Elimu ni muhimu kwa maendeleo ya wananci kuliko biashara’ kama vile: *mwenyekiti, mtetezi, mpinzani, hoja, mdahalo* na kadhalika. Kwa hivyo, vifaa na pica zilizotumiwa kujifunzia somo hili zinaweza kutumiwa kucunguza ikiwa wanafunzi wanaweza kurejelea midahalo mbalimbali kuhusiana na namna ya kushiriki katika mdahalo katika kiwango ca utetezi na upinzani.

## Kipindi cha 3: Matumizi ya lugha

### a) Malengo ya somo

- Kutaja majina ya watu wanaoshiriki katika mdahalo;
- Kutumia msamiati wa mdahalo katika sentensi;
- Kuongoza mdahalo;
- Kuandaa mdahalo wenye mada yoyote ile.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Wanafunzi wenyewe;

- Mdahalo uliorekodiwa;
- Micoro ya wasemaji na wasikilizaji katika mdahalo;
- Pica za mwenyekiti na katibu wa mdahalo,
- Micoro ya watu katika shughuli za kimaendeleo zenye kuzalisha mali;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 81-83;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Mwalimu ahakikishe amewagawa wanafunzi wake katika makundi ya wanafunzi yanayotakikana. Mdahalo ulioandaliwa utumiwe kuongoza wanafunzi na kuwapa mwelekeo kamili wa kuendesha mdahalo. Mwalimu aandae somo kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu utaratibu wa mdahalo kupitia wahusika wote wanaojitokeza katika mfano huu ili mwanafunzi apate pica kamili ya mdahalo mzuri na jinsi unavyofanywa.

Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kujifunzia somo hili ili kuwaelekeza ipasavyo wanafunzi wakati wa kushiriki katika mdahalo watakaopewa katika makundi yao.

**d) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi ca 2. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa.

Mwalimu atumie mdahalo alioandaa kutanguliza funzo hili.

### 10.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu wajadiliane kuhusu:

1. *Mdahalo ni nini?*
2. *Toa mifano ya mada mbili zinazoweza kuzungumziwa katika mdahalo.*
3. *Ni watu gani ambao hushirikishwa katika mdahalo?*
4. *Watu hao huwa na mawazo au misimamo tofauti. Eleza misimamo hiyo.*
5. *Taja tabia za kujiepusha nazo katika mdahalo.*

Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kujadili maswali yaliyo hapo juu. Kwa swali la 5, wanafunzi wanaweza kutoa majibu kama vile:

a) *Kutozingatia muda uliopangwa kwa kila mshiriki.*
b) *Kutumia lugha ya matusi.*
c) *Kutumia lugha ya kuwadhalilisha watu wa jinsia fulani au walemavu.*
d) *Kutoa hoja zisizo za kweli.*
e) *Kuibua vita.*
f) *Kutoheshimu kazi ya mwenyekiti n.k.*

Wanafunzi wanaweza kurejelea mdahalo waliosoma na kujibu maswali waliyopewa katika sehemu hii. Baadaye, mwalimu aombe kila kundi la wanafunzi wajitokeze mbele ya darasa na kuwaeleza wenzao matokeo ya majadiliano yao. Katika hatua hii, mwalimu arekebishe makosa ya kimatamshi pindi yanapotokea.

Katika zoezi la 10.4, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha wacunguze vijisanduku vya maneno walivyopewa na kujaza mapengo yaliyopo ili kuunda maneno kamili. Ni vyema mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanaweza kujibu swali hili kwa kiwango ca kuridhisha na kuonyesha kwamba wanaweza kukumbuka msamiati muhimu katika mazingira ya midahalo na kuutumia katika mawasiliano yao. Mwalimu azunguke darasani na kutoa maelezo pale yanapotakiwa ili kuelekeza makundi yanayotatizika.

**Tathmini ya kipindi ca 3**

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti kwa kurejelea msamiati mahususi waliojifunza kuhusu mdahalo huku wakirejelea wahusika wanaopatika katika mdahalo na majukumu yao katika kuendeleza mazungumzo yao. Kwa hivyo, vifaa na pica zilizotumiwa kujifunzia somo hili zaweza kutumiwa kucunguza iwapo wanafunzi wanaweza kurejelea nafasi ya *mwenyekiti, katibu, watetezi, wapinzani* na *wasikilizaji* katika kuendeleza mdahalo na hata kubainisha mienendo mizuri inayotakikana katika mazingira ya mazungumzo ya mdahalo: *kuwa na adabu, kutoa maoni kwa kuheshimiana, kuzingatia maelekezo ya mwenyekiti wakati wa kuzungumza* na kadhalika.

## Kipindi cha 4: Kusikiliza na kuzungumza

**a) Malengo ya somo**

- Kuandaa mdahalo wenye mada yoyote ile;
- Kuongoza mdahalo;
- Kushiriki katika mazungumzo na kutoa hoja mbalimbali katika mdahalo;

- Kuandika hoja muhimu zilizotolewa katika mdahalo;
- Kueleza majukumu ya wahusika wa mdahalo.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Mdahalo uliorekodiwa;
- Micoro na pica za wasemaji, mwenyekiti, katibu na wasikilizaji katika mdahalo;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 83;
- Combo ca kunasia sauti na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji ujifunzaji na uangalifu maalum.

**c) Maandalizi ya somo**

Mwalimu ahakikishe amewagawa wanafunzi wake katika makundi ya wanafunzi yanayotakikana. Mdahalo ulioandaliwa utumiwe kuongoza wanafunzi na kuwapa mwelekeo kamili wa kuendesha mada za midahalo mbalimbali walizopewa kwenye *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 83. Mwalimu aandae somo kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu utaratibu wa kushiriki katika midahalo kuhusu mada mbalimbali kupitia kwa wahusika wote wanaohusika ili mwanafunzi apate pica kamili ya mdahalo mzuri na jinsi unavyofanywa.

Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kujifunzia somo hili ili kuwaelekeza ipasavyo wanafunzi wakati wa kushiriki katika mdahalo watakaopewa katika makundi yao.

**d) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi ca 3. Wanafunzi wajibu maswali waliyoulizwa. Mwalimu atumie midahalo aliyoandaa kutanguliza funzo hili.

### 10.4 Kusikiliza na kuzungumza: Kuandaa mdahalo

Sehemu hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kutoa maoni yake kuhusu mada mbalimbali na kujadiliana na wengine kwa kutumia lugha fasaha. Kwa hivyo, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wanane wanane ili waweze kuandaa mdahalo na kujadiliana kuhusu mojawapo ya mada hizi:

1. *Elimu ndio msingi wa maisha mazuri.*
2. *Wazazi wana nafasi kubwa katika malezi ya watoto wao kuliko walimu.*

3. *Ni lazima viongozi wa kidini washirikiane na wanasiasa katika mipango ya maendeleo ya wananci.*
4. *Vitabu ndivyo vifaa muhimu katika elimu.*

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika makundi yao ambapo kila kundi litateua mada moja. Pia kila kundi litateua mwenyekiti, katibu wa mdahalo, wasemaji wakuu: watetezi wawili na wapinzani wawili na wasikilizaji washiriki wawili. Ili kufanikisha mazungumzo ya wanafunzi katika makundi yao, mwalimu awaongoze waelewe utaratibu unaozingatiwa katika maandalizi na utekelezaji wa mdahalo. Wanafunzi waandae mdahalo wao katika makundi yao. Baadaye, mwalimu awaombe wajitokeze mbele ya darasa, wapange viti kwa njia inayorahisisha mazungumzo yao halafu mwenyekiti afungue mdahalo na aongoze mazungumzo kwa kuzingatia muda uliopendekezwa kwa kila kundi. Wanafunzi wengine wafuate mazungumzo ya wenzao kwa kuandika kasoro na mafanikio yanayojitokeza katika mazungumzo yao. Hivyo basi, kila kundi la wanafunzi lizungumze na mwishoni wenzao wapewe muda wa kutoa mcango wao kuhusu jinsi ambavyo mdahalo huo ulivyoendelea. Mwalimu naye acukue muda wake kwa kusahihisha makosa ya wanafunzi pindi yanapotokea na awapongeze pale wanapofanikiwa huku akiomba makundi mengine kuwaiga wenzao na kusahihisha makosa waliyofanya ili wafanye mdahalo mzuri zaidi kuliko kundi lililotangulia.

Vilevile, mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi na acunguze iwapo wanafunzi wanatunga sentensi kamili zisizo na makosa ya kisarufi ili wapate uwezo wa kuwasiliana katika lugha fasaha. Aidha, ni vyema pia mwalimu awasaidie wanafunzi kupata ujuzi katika tafakuri tunduizi, usuluhishaji wa matatizo, stadi za utafiti, ubunifu na ugunduzi, ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha, elimu kuhusu fedha na kadhalika kupitia maoni wanayoyatoa katika mazungumzo kwa lengo la kudumisha ujifunzaji wao wa muda mrefu kupitia mazungumzo yao.

## Tathmini ya kipindi ca 4

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali kuhusu mambo muhimu waliyojifunza katika kusikiliza na kuzungumza. Maswali yake yacunguze uwezo wa wanafunzi wa kuongoza midahalo, kushiriki katika midahalo pamoja na kutoa hoja za aidha kupinga au kuunga mkono mada mbalimbali.

# Kipindi cha 5: Sarufi (Wakati uliotimilika)

**a) Malengo ya somo**

- Kutambua matumizi ya wakati uliotimilika;
- Kutumia wakati uliotimilika katika hali yakinishi na kanushi;
- Kutunga sentensi sahihi katika wakati uliotimilika, hali yakinishi na kanushi.

**b) Vifaa vya kujifunza**

- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 84-87;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Mwalimu aandae masimulizi kadhaa yaliyoandikwa katika wakati uliotimilika ambayo atawasomea wanafunzi. Mwalimu anaweza pia kuwasimulia wanafunzi kuhusu mambo ambayo tayari yameshatendeka. Haya ni mambo ambayo yametendeka muda mfupi uliopita. Masimulizi haya yanaweza kuhusisha mdahalo ambao mwalimu atauteua yeye mwenyewe. Ikiwa kuna mdahalo ambao umekamilika muda mfupi uliopita, wanafunzi waujadili kwa kueleza hoja muhimu zilizotolewa na wapinzani, watetezi pamoja na uamuzi wa mwenyekiti.

**d) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu nyakati mbalimbali ambazo wamewahi kujifundisha hapo awali, kwa mfano: wakati uliopita, wakati ujao na wakati uliopo. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa. Wanafunzi wajikumbushe kuhusu matumizi ya nyakati mbalimbali walizotaja.

Mwalimu atumie masimulizi ya wakati uliotimilika aliyoyaandaa kutanguliza funzo hili.

**10.5 Sarufi: Wakati uliotimilika, tungo yakinishi**

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha wacunguze sentensi walizopewa katika jedwali.

Wanafunzi wacunguze sentensi walizopewa zilizotumia kitenzi ***toa*** katika tungo yakinishi, umoja na wingi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua matumizi ya kiambishi ***me*** ca wakati uliotimilika. Mwalimu awaelezee wanafunzi kuwa wakati uliotimilika ni wakati unaoonyesha vitendo ambavyo tayari vimeishatendeka aidha muda mcace tu uliopita au kitambo kidogo. Mwalimu awaongoze wanafunzi kufanya zoezi la tano kwa kutunga sentensi kwa kutumia kitenzi ***zungumza*** pamoja na kiambishi ***me*** ca wakati uliotimilika katika nafsi zote katika Kiswahili. Wanafunzi wajibu zoezi hilo na mwalimu awaombe wacunguze maelezo muhimu yaliyotolewa katika kitabu ca mwanafunzi ili wapate kuelewa matumizi ya wakati uliotimilika. Maswali katika zoezi la 10.6 yatumiwe na mwalimu kama njia ya kucunguza iwapo wanafunzi wameishafahamu muundo wa vitenzi vya Kiswahili katika wakati uliotimilika. Kwa hivyo, mwalimu awaongoze wanafunzi katika kujibu maswali hayo na awaombe wayasahihishe kwa pamoja huku akiwashirikisha wanafunzi wote kutambua makosa ya wenzao na kuyasahihisha.

### 10.5.1 Wakati uliotimilika, tungo kanushi

Katika sehemu ya hii ya ujifunzaji wa sarufi, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wawili wawili ili wacunguze sentensi walizopewa katika wakati uliotimilika, hali yakinishi na kanushi. Wanafunzi wacunguze sentensi hizo na mwalimu awaelekeze kuelewa tofauti za kimuundo kati ya tungo yakinishi na tungo kanushi. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wameelewa, mwalimu awaombe wanafunzi wajibu maswali katika zoezi la saba. Maelezo muhimu yaliyoandikwa katika kitabu ca mwanafunzi yatumiwe kuwaelekeza wanafunzi kutambua muundo wa wakati uliotimilika katika nafsi mbalimbali.

### Tathmini ya kipindi ca 5

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali tofauti kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali haya yatilie mkazo uwezo wa wanafunzi wa kubainisha iwapo wanafunzi wamepata uelewa wa kutosha katika matumizi ya wakati uliotimilika na miundo yake katika hali yakinishi na kanushi.

## Maelezo muhimu kwa mwalimu

a) Mdahalo ni mazungumzo au majadiliano kati ya watu wengi ambao huzungumzia jambo moja maalumu na huwa na mitazamo tofauti:

- Mtazamo wa kwanza hutoa hoja zinazotetea au kuunga mkono wazo kuu.
- Mtazamo wa pili hutoa hoja za kupinga au kukataa wazo kuu.
- Washiriki wa mdahalo ni:

✓ **Mwenyekiti:**

❖ Kazi yake ni:

- Kuongoza mazungumzo au majadiliano.
- Kuhakikisha kuwa kuna nidhamu wakati wa majadiliano.
- Kupanga muda utakaotumiwa na kila msemaji kutoa hoja.
- Kuchagua wasemaji katika mdahalo.
- Kupigisha kura baada ya mazungumzo ili kutaka kujua upande ulioshinda katika ya upande wa watetezi na ule wa wapinzani.

✓ **Katibu:**

❖ Kazi yake ni:

- Kuandika hoja za wasemaji wote.
- Kusoma hoja zote zilizotolewa.
- Kutangaza matokeo ya kura zilizopigwa baada ya mazungumzo.

✓ **Watetezi:**

- Hawa ni wasemaji wanaotetea mada au wazo kuu linalozungumziwa.

✓ **Wapinzani:**

- Hawa ni wasemaji wanaopinga mawazo yanayotetea wazo kuu la mada.

✓ **Wasikilizaji washiriki:**

- Hawa wanashiriki kwa kusikiliza hoja za pande mbili: upande wa utetezi na upande wa upinzani.

Baadhi ya tabia za kuepuka katika mdahalo ni: *matumizi ya lugha yenye matusi na uchochezi, kutohifadhi wakati uliotengewa, kupandwa na hasira upande wako unaposhindwa* n.k.

b) Kiambishi ***'me'*** kinarudiwarudiwa katika vitenzi vyote baada ya viambishi nafsi ***ni, u, a, tu, m*** na ***wa***. Kiambishi ***<u>'me'</u>*** ni kiambishi cha **<u>wakati uliotimilika, tungo yakinishi</u>**.

- Wakati uliotimilika huonyesha kuwa tendo tayari limefanyika na kumalizika.

***Kwa mfano:***

- Mimi *nimefanya* kazi yangu. (kazi tayari imeshafanywa)
- Kageruka *amesafiri* leo asubuhi. (tendo la kusafiri tayari limeshamalizika)

## 10.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Kwa wanafunzi wenye kiwango ca cini katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe kusoma tena kifungu ca mazungumzo kuhusu mada '***Elimu ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananci kuliko biashara***' kisha waandike sentensi tano zenye vitenzi katika wakati uliotimilika.

### Majibu ya zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi wataandika. Sharti zihusishe vitenzi vilivyotumika katika wakati uliotimilika katika kifungu ca mdahalo walicosoma hapo awali. Kwa mfano:

1. *Wasemaji na wasikilizaji ambao m**me**kuja hapa leo, hamjambo!*
2. *Watu wa**me**elimishwa ili waweze kuwa na uelewa wa mahitaji ya jamii zao.*
3. *Kupitia elimu tu**me**weza kupata teknolojia ya kuboresha maisha yetu.*
4. *Rwanda i**me**wekeza katika elimu.*
5. *Mpango wa elimu ya msingi ya miaka kumi na miwili u**me**anza kuzaa matunda mema.*

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango ca juu ca uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge sentensi kumi sahihi katika wakati uliotimilika tungo kanushi na tungo yakinishi.

***Kwa mfano:***

1. *Cakula kimeiva.* – *Cakula hakijaiva.*
2. *Mtoto amelala sana.* - *Mtoto hajalala sana.*
3. *Mwalimu ameandika ubaoni.* – *Mwalimu hajaandika ubaoni.*

# 10.7 Majibu

**Zoezi la makundi, ukurasa 77**

Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi kwa kurejelea mcoro uliopo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 77.

**Kwa mfano:**

*Mcoro huu unaonyesha wanafunzi wanaoshiriki katika mdahalo. Kuna mwanafunzi mmoja aliyesimama akizungumza (huenda huyu ndiye mwenyekiti), kisha kuna wanafunzi walioketi pande mbili (watetezi na wapinzani) pamoja na wanafunzi wengine wawili walioketi mbele kabisa (katibu na mtunza wakati na nidhamu).*

**Maswali ya ufahamu, ukurasa 80**

1. Mada ya mdahalo ilikuwa: ***Elimu ni muhimu kwa maendeleo ya wananci kuliko biashara***
2. Watetezi ni watu ambao huunga mkono jambo fulani. Wapinzani ni watu ambao hupinga na kukataa jambo fulani.
3. Bigirimana alikuwa mtetezi aliyesema kuwa elimu huwezesha watu kubuni mikakati ya kuanzisha miradi ya kuboresha na kuendeleza maisha yao. Kupitia elimu tumeweza kupata teknolojia ya kuboresha maisha yetu.
4. Mukamwiza alikuwa mpinzani aliyesema kuwa biashara ni bora kuliko elimu kwa sababu biashara ndiyo inayotuletea pesa na pesa hizo ndizo zinazotumiwa katika miradi mingi ya kimaendeleo ncini.
5. Mukandayisenga alitoa hoja za kudhihirisha nafasi ya elimu katika kuinua ucumi wa nci yetu. Alieleza kuwa elimu ni muhimu kuliko biashara kwani bila elimu biashara haiwezi kufanyika vyema.
6. Msikilizaji mshiriki 1 alieleza kuwa elimu na biashara yote ni mambo muhimu ya kuboresha ucumi wa nci yetu.
7. Msikilizaji mshiriki 2 alieleza kuwa elimu ndiyo ya kwanza na baadaye mambo mengine hufuata. Kulingana na msemaji huyu, bila elimu, mtu hawezi kujua namna ya kutunza biashara yake, kupiga hesabu na kuiendeleza.
8. Mjadala, majadiliano
9. Mwenyekiti hucaguliwa na kazi zake huwa:
   - Kuongoza mazungumzo.
   - Kuhakikisha kuwa kuna nidhamu wakati wa majadiliano.
   - Kuanzisha mdahalo na kuendesha mazungumzo.
   - Kupanga muda utakaotumiwa na kila msemaji kutoa haoja zake.

- Kupanga muda utakaotumiwa na kila msikilizaji mshiriki iwapo atakuwa na hoja ya kuzungumzia.
- Kucagua wasemaji katika mdahalo.
- Kucunguza iwapo wasemaji wanazingatia muda uliopangwa.
- Kupigisha kura baada ya mazungumzo ili kutaka kujua upande ulioshinda kati ya upande wa watetezi na ule wa wapinzani.

**Zoezi la msamiati, ukurasa 80**

Mwalimu atathmini maelezo yatakayotolewa na wanafunzi katika makundi yao. Sharti wazingatie msamiati uliotumika katika mjadala waliosoma.

***Kwa mfano:***

1. ***wasemaji*** – *watu wanaozungumza katika mjadala.*
2. ***muda*** – *kipindi fulani ca dakika, saa au sekunde.*

**Zoezi la 10.1, ukurasa 80**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi kuhusu kutoa maelezo ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi walizopewa.

***Kwa mfano:***

1. ***fursa:*** nafasi ya kufanya jambo
2. ***hoja:*** wazo au fikra ya mtu kuhusu jambo fulani
3. ***tulitetea:*** tulipigia debe, tulishikilia msimamo kuhusu jambo fulani
4. ***ninapinga:*** ninakataa, nina maoni au mawazo tofauti
5. ***mwenyekiti:*** mtu anayesimamia au anayeongoza kikundi, mdahalo n.k.
6. ***kuwekeza:*** weka rasilimali katika biashara ili kupata faida
7. ***gharama:*** pesa zinazohitajika kutekeleza jambo fulani
8. ***matokeo:*** zao la kazi au tendo lililotendeka
9. ***kikwazo:*** kizuizi; kitu cocote kinacozuia maendeleo ya jambo fulani
10. ***pato:*** kitu ambaco mtu huwa naco baada ya kufanya biashara au kazi.

Baadaye, mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga wakitumia msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi walizopewa.

***Kwa mfano:***

1. *Nilipewa fursa ya kuzungumza.*
2. *Hoja zangu katika mjadala huu ni za kupinga mada ya leo.*

**Zoezi la 10.2, ukurasa 81**

1. Watu hawa wana ***maarifa*** mbalimbali ya kutekeleza miradi.
2. Washiriki wote wa mkutano ***walipiga makofi*** baada ya kusikia hoja nzuri za Kayisabe na wenzake.
3. Mwenyekiti wa mkutano wetu anasema kuwa kila ***mshiriki*** anapaswa kutoa hoja zake.
4. Mtu huyu ***anafananisha*** elimu na utajiri.
5. Kazi hii ***itatunufaisha*** wote kwa kutuwezesha kupata pesa za kujisaidia.

**Zoezi la 10.3, ukurasa 81**

1 - C
2 - A
3 - B
4 - E
5 - D

**Zoezi la matumizi ya lugha, ukurasa 81**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi. Wanafunzi wajadiliane katika makundi yao. Kwa mfano:

1. Mdahalo ni mazungumzo yanayofanywa kwa kutetea au kupinga mada fulani.
2. a) Ni bora kuwa mvulana kuliko kuwa msicana.
   b) Masomo ya Sayansi ni bora kuliko masomo ya Sanaa.
   c) Afadhali kuwa daktari kuliko kuwa mwalimu.
3. Mdahalo hushirikisha watu kadhaa kama vile: *mwenyekiti, watetezi, wapinzani, katibu pamoja* na *wasikilizaji.*
4. Watetezi hukubaliana na mada teule ilhali wapinzani hupinga wazo kuu la mada teule.
5. Baadhi ya tabia za kujiepusha nazo katika mdahalo ni:
   *a) Kuibua ugomvi wakati wa majadiliano.*
   *b) Kutozingatia wakati uliotengwa kwa ajili ya majadiliano.*
   *c) Kutumia lugha isiyo ya heshima kama vile: matusi.*

**Zoezi la 10.4, ukurasa 82**

1.

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | **P** | I | N | **Z** | A | N | **I** |

2.

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | **S** | **H** | I | R | I | **K** | I |

3.

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | **S** | I | K | I | **L** | I | Z | A | **J** | I |

4.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M | **D** | A | H | **A** | L | **O** |

**Zoezi la kusikiliza na kuzungumza, ukurasa 83**

Mwalimu awapange wanafunzi katika namna ya mjadala na awaelekeze katika kujadili mojawapo ya mada walizopewa katika vitabu vyao. Ahakikishe kuwa kila mwanafunzi anashiriki katika mjadala huo.

**Sarufi**

**Zoezi la makundi, ukurasa 84**

Mwalimu atathmimi majibu ya wanafunzi. Wanafunzi waelezane kuwa sentensi walizopewa wacunguze zimetumia kiambishi '***-me-'*** ca wakati uliotimilika.

**Zoezi la 10.5, ukurasa 84**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti zihusishe kiambishi ***me*** ca wakati uliotimilika, kitenzi ***zungumza*** pamoja na nafsi katika Kiswahili. Kwa mfano:

1. ***Mimi*** *ni**mezungumza** na mwalimu mkuu.*
2. **Sisi** *tu**mezungumza** na walimu wakuu.*
3. ***Wewe*** *u**mezungumza** na mwalimu mkuu.*
4. ***Nyinyi*** *m**mezungumza** na walimu wakuu.*
5. ***Yeye*** *a**mezungumza** na mwalimu mkuu.*
6. ***Wao*** *wa**mezungumza** na walimu wakuu.*

**Zoezi la 10.6, ukurasa 86**

1. Sisi na viongozi wetu ***tumejadiliana*** kuhusu umuhimu wa Kiswahili.
2. Wewe ***umetazama*** mcezo wa kandanda kwenye runinga.

3. Mama yangu ***ameagiza*** bidhaa nyingi kutoka Ucina.
4. Mtetezi huyu na wasikilizaji washiriki wote ***wamezungumzia*** mambo muhimu.
5. Mlango wa nyumba hii ***umefunguliwa*** ili wageni wote waingie.
6. Kisu cangu ***kimepotea***.
7. Nyumba zile ***zimepakwa*** rangi na mafundi wawili.
8. Vitabu vingi vya Kiswahili ***vimecapishwa***.
9. Midahalo miwili ***imeshirikisha*** wasemaji wenye hoja nzuri.
10. Mimi ***nimeimba*** wimbo wa kumsifu Mungu katika ibada yetu.

**Zoezi la 10.7, ukurasa 87**

a) Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti zihusishe kitenzi ***imba*** katika wakati uliotimilika hali yakinishi pamoja na nafsi zote katika Kiswahili. Kwa mfano:
   1. ***Mimi nimeimba*** wimbo mzuri.
   2. ***Sisi tumeimba*** nyimbo nzuri.
   3. ***Wewe umeimba*** wimbo mzuri.
   4. ***Nyinyi mmeimba*** nyimbo nzuri.
   5. ***Yeye ameimba*** wimbo mzuri.
   6. ***Wao wameimba*** nyimbo nzuri.

b) Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti zihusishe kitenzi ***imba*** katika wakati uliotimilika hali kanushi pamoja na nafsi zote katika Kiswahili. Kwa mfano:
   ***1. Mimi sijaimba*** wimbo mzuri.
   ***2. Sisi hatujaimba*** nyimbo nzuri.
   ***3. Wewe hujaimba*** wimbo mzuri.
   ***4. Nyinyi hamjaimba*** nyimbo nzuri.
   ***5. Yeye hajaimba*** wimbo mzuri.
   ***6. Wao hawajaimba*** nyimbo nzuri.

**Zoezi la 10.8, ukurasa 87**

1. Yeye hajaagiza bidhaa nyingi kutoka Kigali.
2. Mimi sijazunguka mji kwa gari.
3. Mtoto wangu hajafaulu katika mtihani wake.
4. Nyumba yangu haijasafishwa.
5. Mgomba haujacomwa.

**Zoezi la 10.9, ukurasa 87**

1. Wao hawajaagiza bidhaa nyingi kutoka Kigali.

2. Sisi hatujazunguka miji kwa magari.
3. Watoto wetu hawajafaulu katika mitihani yao.
4. Nyumba zetu hazijasafishwa.
5. Migomba haijacomwa.

## Somo la 11: Mjadala

### Kipindi cha 6: Kusoma ufahamu

**a) Malengo ya somo**

- Kusoma kwa usahihi mfano wa mjadala kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;
- Kushiriki katika mazungumzo na kutoa hoja mbalimbali katika mjadala;
- Kuandika hoja muhimu zilizotolewa katika mjadala.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Mjadala uliorekodiwa,
- Micoro ya mwenyekiti na wasemaji wengine katika mjadala;
- Micoro ya watu katika shughuli za kilimo zenye kuzalisha mali;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 88-89;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Somo hili linalenga kumpa mwanafunzi ujuzi zaidi kuhusu nafasi ya kilimo katika kupunguza umaskini na kuendeleza maisha mazuri ya wanajamii. Mbali na kumwezesha mwanafunzi kutoa maoni muhimu katika uwanja huu, somo hili litasaidia pia kufikiria kuhusu cangamoto zinazojitokeza katika sekta ya kilimo na namna ya kuziepuka. Ni vyema mwalimu alenge kumsaidia mwanafunzi kupata maarifa ya kuongoza mjadala na kushiriki katika mijadala mbalimbali kwa kutumia lugha fasaha. Katika maandalizi ya somo lake, mwalimu ahakikishe kwamba ameleta pica au micoro ya mwenyekiti na wasemaji wengine katika mjadala pamoja na shughuli mbalimbali zinazohusika na kilimo ili kuwasaidia wanafunzi waelewe kwa urahisi hasa wanafunzi wenye ulemavu wa aina tofauti.

Hivyo basi, micoro na pica zilizoletwa zitumiwe au zionyeshwe hadharani wakati maalumu na mwalimu awaombe wanafunzi watoe maelezo kwa kuzigusa au kwa kuandika maelezo yake ubaoni ili kuwasaidia wanafunzi wasioona au wasioweza kusikia vizuri.

### d) Utaratibu wa somo

### Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi na awaulize maswali kuhusu somo lililopita kuhusiana na mdahalo walioshiriki. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu awashirikishe wanafunzi kusahihisha zoezi walilopewa katika somo lililopita na awaelekeze wanafunzi kupata ufahamu wa mambo yaliyoonekana kuwatatiza. Baadaye, mwalimu awacangamshe wanafunzi kwa kuwauliza maswali kadhaa kuhusiana na micoro iliyo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 88. Kwa mfano: *Mnaona nini kwenye micoro hii?* Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kwa kueleza kile wanacokiona katika micoro hiyo. Kwa mfano: *"Mimi ninaona watu. Mimi ninaona wazungumzaji* na kadhalika. Katika sehemu hii, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanapata ujuzi kuhusu tafakuri tunduizi, ubunifu na ugunduzi kwa kuwaonyesha pica hizo huku akiwataka kufikiria na kugundua kile kinacoendelea katika pica hizo. Vilevile, nafasi ya wasicana, wanawake na walemavu katika mazungumzo nazo zigusiwe katika maelezo yanayotolewa pale ambapo mwenyekiti na wasemaji wengine ni watu wa jinsia zote na wenye hali tofauti n.k.

### 11. 1 Kusoma na ufahamu: Mjadala kuhusu 'Nafasi ya ukulima katika uzalishajimali dhidi ya umaskini'

Mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa kimya kifungu ca mazungumzo kilicopo huku wakiandika msamiati mpya wanaopatana nao. Wanafunzi nao wasome kwa kimya huku wakiandika msamiati huo mpya. Hatimaye, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu kifungu ca mazungumzo walicokisoma ili kuhakikisha kuwa wamekisoma na kukielewa. Kwa mfano, anaweza kuuliza swali lifuatalo: *Taja majina ya wasemaji walio katika mazungumzo haya*. Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika kifungu hico. Kwa mfano: *Wasemaji wanaopatikana katika mazungumzo haya ni Kawera, Mukandayisenga na Bagirishya*. Baada ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wamesoma kwa kimya kifungu kilicopo, mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa sauti na kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi zilizopo. Kwa hivyo, mwalimu awacague wanafunzi ili wacukue

nafasi za wasemaji na waweze kusoma kwa kuigiza mazungumzo yaliyopo. Mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wanasoma kwa kuzingatia alama za vituo na asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa huku akiwaelekeza kutumia sehemu za mwili kwa kuigiza mazungumzo hayo katika kutetea hoja wanazozisoma.

**Tathmini ya kipindi ca 6**

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu mambo muhimu waliyojifunza kama vile: maana ya mjadala, uzingatifu wa nidhamu, watu muhimu wanaohitajika katika mazungumzo ya mjadala na kudhihirisha majukumu yao katika kuendeleza mazungumzo yao.

## Kipindi cha 7: Kujifunza msamiati

**a) Malengo ya somo**

- Kubaini msamiati unaotumika katika mjadala;
- Kutaja majina ya watu wapatikanao katika mjadala;
- Kutumia msamiati wa mjadala katika sentensi sahihi.

**b) Vifaa vya kujifunza**

- Mjadala uliorekodiwa;
- Micoro ya mwenyekiti, katibu na wasemaji wengine katika mjadala;
- Micoro ya watu katika shughuli za kilimo zenye kuzalisha mali;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 90;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Somo hili linalenga kumpa mwanafunzi ujuzi zaidi kuhusu msamiati unaohusiana na nafasi ya kilimo katika kupunguza umaskini na kuendeleza maisha mazuri ya wanajamii. Mbali na kumwezesha mwanafunzi kutoa maoni muhimu katika uwanja huu, somo hili litasaidia pia kuelewa maana ya msamiati unaohusiana na sekta ya kilimo. Ni vyema mwalimu alenge kumsaidia mwanafunzi kupata maarifa ya kuongoza mjadala na kushiriki katika mijadala mbalimbali kwa kutumia lugha fasaha. Katika maandalizi ya somo lake, mwalimu ahakikishe

kwamba ameleta pica au micoro ya mwenyekiti, katibu na wasemaji wengine katika mjadala pamoja na shughuli mbalimbali zinazohusika na kilimo ili kuwasaidia wanafunzi waelewe kwa urahisi haswa wanafunzi wenye ulemavu wa aina tofauti.

### (d) Utaratibu wa somo

#### Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi na awaulize maswali kuhusu somo lililopita kuhusiana na mjadala kuhusu nafasi ya kilimo katika kupunguza umaskini na kuendeleza masiha mazuri ya wanajamii mbalimbali. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu awashirikishe wanafunzi kusahihisha zoezi walilolipewa katika somo lililopita na awaelekeze wanafunzi wapate ufahamu wa mambo yaliyoonekana kuwatatiza.

### 11.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu ukulima

Baadaye, mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na awaombe watafute maana za msamiati mpya waliopatana nao katika kifungu ca mazungumzo walicokisoma. Ni vyema mwalimu awakumbushe wanafunzi wacunguze matumizi ya msamiati huo katika mazungumzo waliyosoma na kutumia kamusi pale inapohitajika. Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi wacunguze sentensi walizopewa katika zoezi la 11.1 ili watunge sentensi zao wenyewe kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mstari. Ni vyema mwalimu awakumbushe wanafunzi wacunguze matumizi ya maneno hayo katika kifungu walicosoma na watumie kamusi pale inapohitajika ili kukamilisha zoezi hilo. Aidha, mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia na kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika. Katika kufanikisha uelewa wa wanafunzi katika zoezi hili, mwalimu awaombe walisahihishe kwa pamoja huku akihakikisha kwamba utunzi wa sentensi zao umezingatia amani na maadili, usawa wa kijinsia, elimu ya pamoja, elimu kuhusu fedha; mazingira, mabadiliko ya hali ya hewa na mwendelezo wa utamaduni wa kiusanifishaji. Hivyo basi, maelekezo ya mwalimu katika zoezi hili yatilie mkazo mtazamo ambapo masuala hayo muhimu yatagusiwa na wanafunzi katika utunzi wao wa sentensi na mifano watakayoitoa.

Baada ya kusahihisha zoezi hili, mwalimu awaombe wanafunzi wajadiliane kuhusu zoezi la 11.2 la sehemu hii ya msamiati. Wanafunzi nao katika makundi yao wajadiliane kuhusu maana za maneno na vifungu vya maneno walivyopewa katika sehemu A huku wakicunguza maelezo yake katika sehemu B kwa ajili

ya kuyahusisha na maneno hayo au vifungu vya maneno hivyo kwa kutumia mshale. Kupitia mazoezi ya sehemu hii ya msamiati, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kutoa mcango wao kwa kutambua pale ambapo wenzao wanafanya makosa ili aweze kucocea ujuzi wao wa usuluhishaji wa matatizo na kujenga utawala binafsi, stadi za maisha pamoja na kujenga mienendo mizuri katika mazingira ya kuzalisha mali kupitia shughuli za kilimo.

**Tathmini ya kipindi ca 7**

Katika hatua hii ya tathmini, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kwa kurejelea msamiati mahususi waliojifunza kuhusu mjadala huku wakirejelea wahusika wanaopatikana katika mazungumzo ya aina ya mjadala na majukumu yao katika kuendeleza mazungumzo hayo. Hivyo basi, vifaa na pica zilizotumiwa kujifunzia somo hili zitumiwe kucunguza iwapo wanafunzi wanaweza kurejelea nafasi ya mwenyekiti na wazungumzaji wengine wakati wa kuendeleza mjadala na hata wabainishe mienendo mizuri inayotakikana katika mazingira ya mazungumzo ya mjadala: *kuwa na adabu, kutoa maoni kwa kuheshimiana, kutoa maoni au hoja zenye mashiko ambazo huwacocea wasemaji wengine kuungwa mkono, kuzingatia maelekezo ya mwenyekiti wakati wa kuzungumza* na kadhalika.

## Kipindi cha 8: Matumizi ya lugha

**a) Malengo ya somo**

- Kutaja majina ya watu wapatikanao katika mjadala;
- Kutambua msamiati unaohusiana na mjadala.

**b) Vifaa vya kujifunza**

- Wanafunzi wenyewe;
- Micoro ya mwenyekiti, katibu na wasemaji wengine katika mdahalo;
- Micoro ya watu katika shughuli za kilimo zenye kuzalisha mali;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 91-92;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Mwalimu alenge kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi zaidi kuhusu matumizi ya msamiati unaohusiana na mjadala kuhusu nafasi ya kilimo katika kupunguza

umaskini na kuendeleza maisha mazuri ya wanajamii. Mbali na kumwezesha mwanafunzi kutoa maoni muhimu katika uwanja huu, somo hili litasaidia pia kumwezesha mwanafunzi kujaza jedwali walilopewa katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 91.

### d) Utaratibu wa somo

### Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi na awaulize maswali kuhusu somo lililopita kuhusiana na msamiati wa mjadala. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu awashirikishe wanafunzi kusahihisha zoezi walilopewa katika somo lililopita na awaelekeze wanafunzi wapate ufahamu wa mambo yaliyowatatiza.

### 11.3 Matumizi ya lugha: Zoezi la jedwali

Mwalimu azingatie kwamba katika hatua hii ya matumizi ya lugha ndipo anatakiwa kuwaelekeza wanafunzi kupata ujuzi unaotakikana kuhusu mawasiliano katika lugha rasmi, stadi za utafiti, ubunifu na ugunduzi na hata utawala binafsi na stadi za maisha kupitia mazoezi yaliyotolewa. Hivyo basi, mwalimu awaelekeze wanafunzi kucunguza maelekezo yaliyotolewa katika sehemu hii ili waweze kugundua maneno yenye maelezo yaliyo katika jedwali lililo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 91, kwenda kulia na kwenda cini. Wanafunzi wajadiliane kati yao na wagundue maneno yanayofaa kukamilisha nafasi za mcezo wa cemshabongo waliopewa katika sentensi. Baadaye, mwalimu awaongoze wanafunzi wasahihishe zoezi hili kwa kuwashirikisha wanafunzi wote na kuwasaidia kutambua maana za msamiati waliokutana nao katika somo hili.

Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi wasome na wacunguze maelezo waliyopewa katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 92 kwa pamoja ili wapate uelewa unaohitajika katika kipengele hiki ca matumizi ya lugha.

### Tathmini ya kipindi ca 8

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kwa kurejelea msamiati mahususi waliojifunza kuhusu mjadala huku wakirejelea wahusika wanaopatikana katika mjadala na majukumu yao katika kuendeleza mjadala. Hivyo basi, vifaa na pica zilizotumiwa kujifunzia somo hili zitumiwe kucunguza iwapo wanafunzi wanaweza kurejelea msamiati maalum unaohusiana na mjadala kwa ujumla pamoja na mazungumzo ya kawaida. Wanafunzi

waelekezwe kubaini nafasi ya mwenyekiti na wazungumzaji wengine wakati wa kuendeleza mjadala na hata wabainishe mienendo mizuri inayotakikana katika mazingira ya mazungumzo ya mjadala.

## Kipindi cha 9: Kusikiliza na kuzungumza

**a) Malengo ya somo**

- Kuandaa mjadala wenye mada yoyote ile;
- Kushiriki katika mazungumzo na kutoa hoja mbalimbali katika mjadala;
- Kuandika hoja muhimu zilizotolewa katika mjadala;
- Kueleza majukumu ya wahusika wa mjadala.

**b) Vifaa vya kujifunza**

- Mjadala uliorekodiwa;
- Micoro ya mwenyekiti, katibu na wasemaji wengine katika mdahalo;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 92;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Mwalimu ahakikishe amewagawa wanafunzi wake katika makundi ya wanafunzi yanayotakiwa. Mjadala ulioandaliwa au uliorekodiwa utumiwe kuongoza wanafunzi na kuwapa mwelekeo kamili wa kuendesha mada za mijadala mbalimbali walizopewa kwenye *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 92. Mwalimu aandae somo kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu utaratibu wa kushiriki katika mijadala kuhusu mada mbalimbali kupitia kwa wahusika wote wanaohusika ili mwanafunzi apate pica kamili ya mjadala mzuri na jinsi unavyofanywa.

Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kujifunzia somo hili ili kuwaelekeza wanafunzi ipasavyo wakati wa kushiriki katika mjadala watakaopewa katika makundi yao.

**a) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu

waliyosoma katika kipindi ca 8. Wanafunzi wajibu maswali waliyoulizwa. Mwalimu atumie mijadala aliyoandaa kutanguliza funzo hili.

## 11.4 Kusikiliza na kuzungumza: Kuandaa mjadala

Katika hatua hii, ni muhimu mwalimu alenge kumwezesha mwanafunzi kutoa maoni yake kuhusu mada mbalimbali na kuzungumza na wengine kwa kutetea hoja zake ili aweze kuungwa mkono. Kwa hivyo, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watano watano ili waweze kuandaa mjadala na kujadiliana kuhusu mojawapo ya mada walizopewa katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 92.

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika makundi yao ambapo kila kundi linapewa mada moja kisha wateue mwenyekiti na wasemaji wengine. Ili kufanikisha mazungumzo ya wanafunzi katika makundi yao, ni vyema mwalimu awaongoze ili waelewe utaratibu wa mjadala. Wanafunzi wajadiliane kuhusu maana za mada zilizopo na waandae mjadala wao kwa kutilia mkazo maoni yanayocangia kufafanua zaidi mada hizo kwa lengo la kufikia uamuzi wao wa pamoja. Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi wajitokeze mbele ya darasa, wapange viti kwa njia inayorahisisha mazungumzo yao halafu mwenyekiti afungue mjadala na aongoze mazungumzo kwa kuzingatia muda uliopangwa. Wanafunzi wengine wafuate mazungumzo ya wenzao kwa kuandika kasoro na mafanikio yanayojitokeza katika mazungumzo yao ili, baadaye, waweze kutoa mcango wao kwa kuboresha mazungumzo yao katika mijadala mingine.

Mwalimu acunguze jinsi wanafunzi wanavyojadiliana na awaelekeze kutambua kasoro zilizopo huku akisahihisha matamshi ya wanafunzi na kuwasaidia kutunga sentensi kamili kwa kucocea uwezo wao wa ubunifu na ugunduzi, tafakuri tunduizi na kudumisha uwezo wao wa kuwasiliana katika lugha rasmi. Aidha, ni vyema pia mwalimu awasaidie wanafunzi kupata ujuzi kuhusu usuluhishaji wa matatizo, ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha, elimu kuhusu fedha na kadhalika kupitia maoni watakayoyatoa katika mazungumzo yao kwa lengo la kudumisha ujifunzaji wao wa muda mrefu kupitia mada walizopewa.

### Tathmini ya kipindi ca 9

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali kuhusu mambo muhimu waliyojifunza katika sehemu hii ya kusikiliza na kuzungumza. Maswali yake yacunguze uwezo wa wanafunzi wa kuongoza mijadala, kushiriki katika mijadala pamoja na kutoa hoja za kujenga mada mbalimbali.

## Kipindi cha 10: Sarufi (Kauli asili na kauli taarifa)

### a) Malengo ya somo

- Kutambua matumizi ya kauli asili na kauli taarifa;
- Kutunga sentensi katika kauli asili na kauli taarifa;
- Kugeuza sentensi za kauli asili na kuziandika katika kauli taarifa;
- Kudhihirisha mambo muhimu yanayobadilika wakati wa kugeuza kauli asili hadi kuwa kauli taarifa.

### b) Vifaa vya kujifunza

- Wanafunzi wenyewe;
- Mazungumzo yaliyorekodiwa;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 92-94;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### c) Maandalizi ya somo

Mwalimu aandae mazungumzo kadhaa yaliyoandikwa katika kauli asili na kauli taarifa ambayo atawasomea wanafunzi. Mwalimu anaweza pia kuwasimulia wanafunzi kuhusu mambo ambayo tayari yameishatendeka hivyo kutumia kauli taarifa. Kauli asili inaweza kujitokeza katika mafundisho ya mwalimu ya wakati huo akiwa darasani. Mazungumzo haya yanaweza kuhusisha mjadala ambao mwalimu atauteua yeye mwenyewe.

### d) Utaratibu wa somo

### Utangulizi

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu mazungumzo yao ya kila siku ambapo wakati mwingine wanazungumza kwa kauli asili na kauli taarifa. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa.

Mwalimu atumie mazungumzo aliyoyaandika katika kauli asili na kauli taarifa aliyoyaandaa kutanguliza somo hili.

## 11.5 Sarufi: Kauli asili na kauli taarifa

Katika hatua hii, mwalimu alenge kuwawezesha wanafunzi kuelewa na kutofautisha kauli asili na kauli taarifa. Mwalimu ahakikishe kwamba ametumia mifano isiyohitaji mabadiliko makubwa katika kubadilisha kauli asili na kauli taarifa ili wanafunzi waelewe kwa urahisi. Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wawili wawili ili wacunguze sentensi walizopewa. Aidha, ujifunzaji wa sehemu hii unaweza kufanywa kwa njia ya uigizaji ambapo mwalimu anaweza kucagua mwanafunzi A kurudia maneno yaliyotamkwa na mtu mwingine katika hali yake ya kwanza huku mwanafunzi B akiyarudia kimaelezo au katika hali ya kutoa taarifa bila kuyarudia maneno hayo yalivyokuwa katika hali yake ya kwanza.

Hivyo basi, kupitia ishara za sehemu ya mwili, mwalimu awasaidie wanafunzi kuigiza matamshi katika hali yake ya kwanza ili wapate tofauti iliyopo kati ya kauli asili na kauli tarifa. Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi wajibu maswali katika zoezi la makundi na mwalimu azunguke darasani kuwasaidia na kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika. Wanafunzi wafanye zoezi hilo na mwalimu awaombe walisahihishe kwa kuwashirikisha wanafunzi wote kutoa mcango wao kuhusu majibu yanayotolewa na wenzao. Mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wanaweza kulinganisha kauli asili na kauli taarifa na watoe mifano ya sentensi sahihi katika kauli asili na wazibadilishe katika kauli taarifa. Ili kurahisisha uelewa wa wanafunzi katika kipengele hiki, mwalimu awaombe wanafunzi wasome na wacunguze maelezo waliyopewa katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 93. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kufanya mazoezi katika sehemu hii.

### Tathmini ya kipindi ca 10

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Vilevile, mwalimu awaulize wanafunzi maswali ya kuhakikisha iwapo wanafunzi wameweza kuelewa kauli asili na kauli taarifa pamoja na kutoa mifano ya sentensi katika kauli asili na kuibadilisha katika kauli taarifa.

Ili kuwasaidia wanafunzi kuendeleza ujifunzaji wao hata nje ya darasa lao, mwalimu awaelekeze wanafunzi namna ya kujibu zoezi katika sehemu ya sarufi. Zoezi hili litasahihishwa kabla ya kuanza somo lijalo.

**Maelezo muhimu kwa mwalimu**

- Sentensi za kauli asili zinatumia maneno yaliyotamkwa na mtu bila kubadilisha chochote katika usemi wake.
- Kauli asili huandikwa kwa kutumia alama za usemi (“ ”) na huanza kwa herufi kubwa.
  - ✓ **Kwa mfano:** Mwanafunzi alisema, “Mimi nitasoma somo la Kiswahili. ”
- Sentensi katika kauli taarifa zinalenga kutuambia maneno ambayo yalizungumzwa na mtu mwingine bila kuyarudia kama yalivyokuwa katika usemi wake wa kwanza. ✓

**Kwa mfano:** Mwanafunzi alisema kwamba yeye angesoma somo la Kiswahili.

- Katika kauli taarifa mambo haya huzingatiwa:
  - ✓ **Nafsi hubadilika**
- **Mimi** hubadilika na kuwa **yeye**
- **Sisi** hubadilika na kuwa **wao**
  - ✓ Katika kauli asili, maneno katika hali yake ya kwanza huwekwa katika alama za usemi (“ ”).
  - ✓ Katika kauli taarifa alama za usemi hazitumiwi. Sentensi inaishia kwa nukta (.). Viunganishi **kuwa** au **kwamba** hutumiwa.
- **Kwa mfano:**
  - A. Mkuu wa shule alisema, “Wanafunzi wote wataleta madaftari yao.”
  - B. Mkuu wa shule alisema **kwamba/kuwa** wanafunzi wote wangeleta madaftari yao.

## 11.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Kwa wanafunzi wenye kiwango ca cini katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge sentensi tano katika kauli asili na wazibadilishe sentensi hizo katika kauli taarifa. ***Kwa mfano:***

***Kauli asili:*** *“Mtalii huyu anataka mtu wa **kumwelekeza** mbugani,” mlinda lango alisema.*

***Kauli taarifa**:* *Mlinda lango alisema kuwa mtalii huyo alitaka mtu wa **kumwelekeza** mbugani.*

**Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga.

Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe usemi asili na usemi taarifa.

***Kwa mfano:***

***Usemi asili:*** *"Mimi ninaenda sokoni," mama alisema.*

***Usemi taarifa:*** *Mama alisema kuwa yeye alikuwa akienda sokoni.*

**ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka**

Kwa wanafunzi wenye kiwango ca juu ca uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe waziandike sentensi zifuatazo katika usemi taarifa.

1. "Birasa, twende shuleni." Kalisa alisema.
2. "Nitakuadhibu usiposoma kwa bidii." Mama alimwambia mwanawe.
3. "Sijapata kitabu cangu dawatini." Mutoni alisema.
4. Baba alisema, "Ninunulie gazeti moja."
5. "Cakula hiki ni kitamu." Mgeni alisema.

**Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

1. Kalisa alimwambia Birasa kuwa waende shuleni.
2. Mama alimwambia mwanawe kuwa angemwadhibu ikiwa hangesoma kwa bidii.
3. Mutoni alisema kuwa hakuwa amepata kitabu cake dawatini.
4. Baba alisema kuwa anunuliwe gazeti moja.
5. Mgeni alisema kuwa cakula hico kilikuwa kitamu.

## 11.7 Majibu

**Zoezi la makundi, ukurasa 88**

Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi kwa kurejelea micoro iliyopo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 88.

**Kwa mfano:**

*Mcoro A unaonyesha wanafunzi wanaoshiriki katika mjadala. Mjadala unahusu nafasi ya kilimo katika uzalishajimali dhidi ya umaskini. Mcoro B unaonyesha wakulima wakiwa shambani.*

**Majibu, maswali ya ufahamu, ukurasa 89**

1. Mada ya mjadala ilikuwa: ***Nafasi ya kilimo na ufugaji katika uzalishaji mali.***
2. Ukulima unahusisha upanzi wa mimea shambani na kupata mavuno ilhali ufugaji unahusisha kufuga wanyama na ndege nyumbani ambao hutupatia mazao mbalimbali.
3. Kulingana na Kawera, tatizo lililopo ni kwamba kila mkulima anataka kupanda mimea yake mwenyewe katika shamba lake dogo.
4. Serikali yetu inapaswa kuwaelekeza wakulima kwa namna ya kuweka mashamba yao pamoja na kupanda mmea mmoja katika mashamba hayo yote ili kupata soko kubwa na mauzo mengi.
5. Bagirisha alitoa hoja kuwa wakulima wanahitaji kutumia mbegu zilizofanyiwa majaribio na taasisi ya kilimo. Taasisi hii pia ihakikishe kwamba imewapa wakulima mbolea nzuri kwa bei nafuu.
6. Mukandayisenga alitoa hoja kuwa umaskini unatokana na uvivu wa baadhi ya watu.
7. Mwenyekiti alihitimisha kwa kusema kuwa kila mtu akitimiza wajibu wake nci yetu itaweza kuwa tajiri, kupata cakula ca kutosha kwa wananci na hata kubakiza cakula ca kuuza nje ya nci yetu kiasi ca kukuza ucumi wetu.

**Zoezi la msamiati, ukurasa 90**

Mwalimu atathmini maelezo ya msamiati ambayo wanafunzi watatoa. Ahakikishe kuwa maneno watakayoeleza maana yake ni msamiati uliotumika kwenye mjadala waliousoma hapo awali.

***Kwa mfano:***

1. ***wataalamu*** - watu wenye ujuzi maalumu kuhusu jambo fulani
2. ***tatizo*** - cangamoto au shida
3. ***mawazo*** - maoni au fikra

**Zoezi la 11.1, ukurasa 90**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi. Wanafunzi waeleze maana ya maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi walizopewa kisha wayatungie maneno hayo sentensi sahihi.

***Kwa mfano:***

1. **mbegu:** punje au kokwa inayopandwa ardhini ili kuwa mmea
2. **bei nafuu:** bei iliyo rahisi; isiyokuwa ghali
3. **uvivu:** hali ya kutotaka kufanya kazi
4. **mtaalamu:** mtu mwenye elimu au ujuzi wa jambo fulani
5. **bidii:** juhudi ya kufanya jambo fulani
6. **wajibu:** jambo ambalo lazima mtu alitekeleze; jukumu
7. **wadau:** mtu mwenye masilahi katikajambo fulani
8. **sekta:** sehemu ya eneo lenye shughuli maalumu

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi na zihusishe maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi walizopewa.

***Kwa mfano:***

1. ***Mbegu*** *zote zitapandwa.*
2. *Mazao yaliuzwa kwa* ***bei nafuu****.*
3. ***Uvivu*** *umeathiri shughuli za kilimo ncini mwetu.*
4. ***Mtaalamu*** *wa kilimo amewasili shambani.*
5. ***Bidii*** *ya wakulima huzalisha mazao mengi.*

## Zoezi la 11.2, ukurasa 90

1 - C
2 - B
3 - E
4 - D
5 - A

## Zoezi la matumizi ya lugha, ukurasa 91

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M 1/2 | J | A 3 | D | A | L 4 | A | | | | K 5 |
| A | | N | | | U | | K 6/7 | U | R | A |
| D 8 | U | A | | | G | | U | | | T |
| A | | T 9 | U | | H 10 | O | J | A | | I |
| | | E | | | A | | A | | | B |
| K 11 | I | T | I | | | Z 12 | A | O | | U |
| | | E | | | | | | | P 13 | |
| A 14 | N | A | P | I 15 | N | G | A | | E | |
| | | | | L | | | | | S | |
| M 16 | D | A | H | A | L | O | | | A | |

## Zoezi la kusikiliza na kuzungumza, ukurasa 92

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watano watano kisha awape fursa ya kucagua mada watakayojadili. Ahakikishe kuwa wanafunzi wanajadiliana kuhusu mada hiyo kwa kuzingatia kanuni za mjadala mwema.

**Zoezi la sarufi (makundi), ukurasa 92 - 93**

1. Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi. Kwa mfano: *Sentensi za sehemu A zimetumia kauli asilia ilhali sentensi za sehemu B zimetumia kauli taarifa.*
2. Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi na zihusishe kauli asili pamoja na kauli taarifa. Kwa mfano:
   a) "*Nenda sokoni ukanunue ndizi.*" *Mama alimwambia kaka yangu.*
   *Mama alimwambia kaka yangu aende sokoni akanunue ndizi.*
   b) "*Mimi siwezi kutembea.*" *Mutoni alisema.*
   Mutoni alisema kuwa yeye hawezi kutembea.

**Zoezi la 11.3, ukurasa 94**

1. Wazungumzaji wale walisema kuwa wao wanapenda kutoa maoni yao.
2. Mwanafunzi mmoja alisema kuwa Kabera angejijengea nyumba nzuri.
3. Ndayisaba alisema kuwa yeye angeingia darasani saa nane kamili.
4. Wakulima walisema kuwa mvua ingenyesha na mimea yao ingestawi.
5. Baba yangu alisema kuwa ni lazima watoto wote wasome kwa bidii.
6. Mkuu wa wilaya alisema kuwa wao wangewasaidia wakulima wao kupata mbegu nzuri.
7. Mkuu wa kiwanda hiki alisema kuwa yeye alihitaji dereva mwenye ujuzi.
8. Mama yangu alisema kuwa kisu cake kilipotea.
9. Mgeni mmoja alisema kuwa kitanda cake ni kizuri.
10. Mpinzani yule alisema kuwa yeye hakukubaliana na mawazo ya mtetezi wa pili.

**Zoezi la 11.4, ukurasa 94**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

1. "Ukifika Kigali ununue sare mpya." Baba aliniambia.
2. "Sitaki kwenda shambani. " Kaka alisema.
3. "Njoo hapa! "Mwalimu alisema.
4. Kalisa alisema, "Mimi nimeandika barua hii."
5. "Wewe huwezi kubeba mzigo huu!" Birasa alishangaa.
6. "Kwa nini unalia?" Mwalimu mkuu aliuliza.

# Somo la 12: Mjadala

## Kipindi cha 11: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati

**a) Malengo ya somo**

- Kusoma kwa usahihi mfano wa mjadala kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;
- Kubaini msamiati unaotumika katika mjadala;
- Kutaja majina ya watu wapatikanao katika mjadala;
- Kutumia msamiati wa mjadala katika sentensi.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Mjadala uliorekodiwa;
- Micoro ya mwenyekiti na wasemaji wengine katika mdahalo;
- Micoro ya watu katika shughuli za kilimo zenye kuzalisha mali;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 95-97;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Somo hili ni mwendelezo wa masomo mawili yaliyotangulia ambapo lengo kuu la mwalimu ni kusaidia na kuelekeza wanafunzi katika kujadali, kutetea hadharani na kupanga hoja kwa kushawishi kuungwa mkono katika mada zinazohusiana na uzalishajimali dhidi ya umaskini. Kwa hivyo, mwalimu aandae vifaa mbalimbali vinavyohitajika katika shughuli za ufugaji ambazo ndizo zinazosisitizwa katika somo hili. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuandaa micoro au pica za mifugo mbalimbali wanaopatikana kijijini pamoja na pica za watu mbalimbali walioweza kupata maisha mazuri kutokana na shughuli za ufugaji.

**d) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Mwalimu aamkie wanafunzi wake na awaulize maswali kuhusu somo lililopita. Wanafunzi wajibu maamkizi pamoja na maswali mengine wanayoulizwa na mwalimu wao. Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi wasahihishe zoezi walilopewa kama zoezi la utafiti ili aweze kuendelea na somo jipya. Wanafunzi wasahihishe zoezi hilo na mwalimu aendelee kwa kuwagawa wanafunzi

katika makundi ya wanafunzi watatu watatu ili wajadiliane kuhusu kile kinacoendelea katika micoro iliyo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 95. Wanafunzi wacunguze micoro na pica hizo kwa kuandika sentensi mbalimbali zinazoonyesha kuwa wameweza kuelewa kile kinacoendelea katika pica hizo. Mwalimu azunguke darasani kuhakikisha kuwa wanafunzi wanajadiliana na kuandika sentensi zao kama inavyotakikana. Mwalimu awaongoze wanafunzi wajitokeza mbele ya darasa ili waelezee wenzao matokeo ya mjadala wao. Kutokana na zoezi hili, mwalimu aelekeze wanafunzi kupata ujuzi katika tafakuri tanduizi na acocee uwezo wao katika kupata stadi za utafiti na ugunduzi huku akihakikisha kuwa wanapata ujuzi ainasafu kuhusu usawa wa kijinsia, elimu ya pamoja na elimu kuhusu fedha kupitia ucunguzi wa micoro iliyopo ambapo walemavu, wasicana na wanawake wanajitokeza katika shughuli za ufugaji na hata biashara zinazotokana na ufugaji.

## 12.1 Kusoma na ufahamu: Mjadala kuhusu 'Ufugaji kama njia ya kupigana na umaskini ncini'

Katika hatua hii ya somo, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa kimya kifungu ca mazungumzo kinacohusika huku wakiandika msamiati mpya wanaokutana nao. Wanafunzi wasome kwa kimya pamoja na kuandika msamiati huo mpya. Baadaye, mwalimu acunguze ikiwa wanafunzi wote wamesoma kama walivyoambiwa. Kwa hivyo, mwalimu aulize maswali mbalimbali kuhusu kifungu ca mazungumzo walicokisoma. Kwa mfano, anaweza kuuliza maswali yafuatayo: *Ni faida gani tunazopata kutokana na ufugaji?* Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kuonyesha kuwa wamesoma kwa kimya. Kwa mfano: *Mifugo huweza kuleta pesa, maziwa, nyama* na kadhalika. Baada ya kupata pica ya uelewa wa jumla wa wanafunzi kuhusu kifungu ca mazungumzo walicokisoma, mwalimu awaombe wasome kwa sauti na kwa usahihi. Mwalimu acague wanafunzi kulingana na idadi ya wahusika waliopo katika mazungumzo na awaambie wasome kwa njia ya maigizo na kwa kuzingatia matumizi ya alama za vituo vinavyopatikana katika kifungu hico. Ni vyema mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa kwa lengo la kutambua herufi, silabi na sentensi zilizopo.

## 12.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu ufugaji

Katika hatua hii ya tatu, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu ili waweze kujadiliana kuhusu msamiati mpya waliokutana nao. Mwalimu awaombe wazingatie matumizi yake katika kifungu ca mazungumzo walicokisoma na watumie kamusi pale wanapoihitaji.

Wanafunzi wajadiliane kama walivyoelekezwa naye mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi pale wanapotatizika. Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi wajibu maswali katika zoezi la 12.1 la msamiati ambapo watajigawa katika makundi ya wanafunzi wawili wawili na kucunguza sentensi zilizopo ili waweze kutunga sentensi zao kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mstari.

Wanafunzi watunge sentensi zao kwa kuzingatia jinsi maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi walizopewa yalivyotumika katika kifungu ca mazungumzo walicokisoma. Mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika na awashirikishe wanafunzi wote kusahihisha zoezi hilo mara moja wanapomaliza kujadiliana katika makundi yao. Hivyo basi, mwalimu aombe kila kundi liandike sentensi zao ubaoni na wanafunzi wengine wazicunguze na watoe mcango wao kuzikubali au kuzikataa na kuzisahihisha.

Baadaye, mwalimu awaambie wanafunzi wafanye zoezi la 12.2 ambapo anawaomba kukamilisha tungo zilizopo kwa kutumia maneno waliyopewa. Kupitia kwa mazoezi yaliyotolewa kwa wanafunzi katika sehemu hii ya msamiati, mwalimu ahakikishe kwamba wamepata ujuzi ainasafu wa elimu kuhusu fedha; mazingira, mabadiliko ya hali ya hewa na mwendelezo na hata utamaduni wa kiusanifishaji kwa kucunguza na kutunga sentensi zao wenyewe.

### Tathmini ya kipindi ca 11

Katika hatua hii, mwalimu ahitimishe kwa kuuliza maswali mbalimbali kuhusu mambo muhimu waliyojifunza kama vile shughuli muhimu katika kuboresha ufugaji, umuhimu wa ufugaji na mambo ya kufanya katika njia ya kupambana na umaskini katika jamii zetu. Wanafunzi pia waulizwe maswali kuhusu msamiati unaohusiana na mijadala pamoja na shughuli za ufugaji za kuboresha maisha ya wanajamii mbalimbali.

## Kipindi cha 12: Matumizi ya lugha

**a) Malengo ya somo**

- Kutambua msamiati maalum unaohusiana na mjadala;
- Kueleza majukumu ya wahusika wa mjadala.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Micoro ya mwenyekiti, katibu na wasemaji wengine katika mdahalo;

- Micoro ya watu katika shughuli za ufugaji zenye kuzalisha mali;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 98;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### c) Maandalizi ya somo

Katika somo hili, ni vyema mwalimu aandae maswali ya kuelekeza mijadala ya wanafunzi darasani kuhusiana na shughuli zinazofanywa katika sekta ya ufugaji ili kubainisha umuhimu wa ufugaji miongoni mwa shughuli nyingine za uzalishajimali dhidi ya umaskini. Mwalimu ahakikishe pia kwamba wanafunzi wanapata pica nzuri ya shughuli ya ufugaji ili kuwasaidia kuwa na mitazamo mizuri kuhusu ufugaji kiasi ca kucocea uwezo wao wa kuimarisha utamaduni wa kiusanifishaji, utawala binafsi na stadi za maisha hata na nje ya masomo yao ya shuleni kama njia ya kudumisha ujifunzaji wao wa muda mrefu.

### d) Utaratibu wa somo

#### Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake na kuwauliza maswali kuhusu somo lililopita. Wanafunzi wajibu maamkizi pamoja na maswali mengine wanayoulizwa na mwalimu wao. Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi wasahihishe zoezi walilolipewa katika somo lililopita ili aweze kuendelea na somo hili jipya. Wanafunzi wasahihishe zoezi hilo.

#### 12.3 Matumizi ya lugha: Kuunda maneno kamili

Mazoezi yaliyotolewa katika sehemu hii ya matumizi ya lugha yanalenga kumwezesha mwanafunzi kufikiria miundo ya maneno na sentensi za lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, ni mazoezi yanayokuza uwezo wa mwanafunzi wa kupanga sehemu za maneno ili kuzalisha maneno kamili au pengine kutambua nafasi za aina mbalimbali za maneno katika sentensi. Kwa hivyo, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili na awaombe wacunguze sehemu za maneno walizopewa ili waweze kuzipanga kwa ajili ya kuunda maneno kamili. Maneno yaliyopo ni yale waliyokutana nayo na ambayo wanahitaji kuyaelewa na kuyatumia katika mijadala yao kuhusu shughuli za uzalishajimali dhidi ya umasikini. Wanafunzi wafanye zoezi hilo na mwalimu awaongoze walisahihishe baada ya kukamilisha mjadala wao.

Ni vyema mwalimu akiwasaidia wanafunzi kupata baadhi ya kanuni zinazoweza kuwasaidia kujua herufi na silabi zinazotangulia maneno ya Kiswahili kama:

vile *u* kwa kuunda maneno yenye kuelezea hali kama *ufugaji, upinzani* na kadhalika na *m/mw* kuhusiana na maneno yenye kuzungumzia vitu na watu kama *mdahalo, mtetezi, mzunguzaji* na kadhalika. Ili kufanikisha malengo ya mwalimu katika sehemu hii, mwalimu awaombe wanafunzi wafanye zoezi la 12.3 ambapo wanatakiwa kupanga upya maneno yaliyopo kwa kuunda sentensi kamili. Wanafunzi wajibu swali hili na mwalimu acunguze uwezo wa wanafunzi wa kufikia sentensi zenye maana na acukue fursa hii kuwaelekeza wapate muundo kamili wa sentensi za Kiswahili. Ni vyema mwalimu awaombe wanafunzi wengine wabainishe makosa yanayofanywa na wenzao ili kukuza uwezo wao wa usuluhishaji wa matatizo na utawala binafsi kwa kulenga kuboresha mawasiliano kati yao katika lugha rasmi.

**Tathmini ya kipindi ca 12**

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kwa kurejelea msamiati mahususi waliojifunza kuhusu mjadala huku wakirejelea wahusika wanaopatikana katika mjadala na majukumu yao katika kuendeleza mjadala. Hivyo basi, vifaa na pica zilizotumiwa kujifunzia somo hili zitumiwe kucunguza iwapo wanafunzi wanaweza kurejelea msamiati maalum unaohusiana na mjadala kwa ujumla pamoja na mazungumzo ya kawaida.

## Kipindi cha 13: Kusikiliza na kuzungumza

**a) Malengo ya somo**

- Kuongoza mjadala;
- Kuandaa mjadala wenye mada yoyote ile;
- Kushiriki katika mazungumzo na kutoa hoja mbalimbali katika mjadala;
- Kuandika hoja muhimu zilizotolewa katika mjadala;
- Kueleza mwongozo kamili wa mjadala;
- Kueleza majukumu ya wahusika wa mjadala.

**b) Vifaa vya kujifunza**

- Mjadala uliorekodiwa;
- Micoro ya mwenyekiti, katibu na wasemaji wengine katika mjadala;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 99;
- Combo ca kunasia sauti na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum.

### c) Maandalizi ya somo

Mwalimu ahakikishe kuwa amewagawa wanafunzi wake katika makundi ya wanafunzi yanayotakikana. Mwalimu anaweza kutumia mjadala alioandaa au aliorekodi kabla ya somo hili ili autumie kufundishia wanafunzi na kuwaongoza kwa kuwapa mwelekeo kamili wa kuendesha mada za mijadala mbalimbali walizopewa kwenye *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 99. Mwalimu aandae somo kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu utaratibu wa kushiriki katika mijadala kuhusu mada mbalimbali kupitia kwa wahusika wote wanaohusika ili mwanafunzi apate pica kamili ya mjadala mzuri na jinsi unavyofanywa.

Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kufundishia somo hili ili kuwaelekeza ipasavyo wanafunzi wakati wa kushiriki katika mjadala watakaopewa katika makundi yao.

### d) Utaratibu wa somo

#### Utangulizi

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi ca 12. Wanafunzi wajibu maswali waliyoulizwa. Mwalimu atumie mijadala aliyoandaa kutanguliza funzo hili.

#### 12.4 Kusikiliza na kuzungumza: Kuandaa mjadala

Baada ya haya, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watano watano ambapo kila kundi litapewa mada ya kujadili. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika shughuli ya kuteua wahusika wa mijadala yao. Kwanza, kila kundi liteue mwenyekiti wa mjadala na wasemaji wengine. Baadaye, wanafunzi waanze kuandaa mjadala wao na mwalimu awaelekeze wazingatie mambo muhimu yaliyoandikwa katika kitabu ca mwanafunzi ili kufanikisha mjadala wao. Wanafunzi wajadiliane kuhusu maana za mada zilizopo na waandae mjadala wao kwa pamoja. Baada ya kumaliza kuandaa mjadala wao, mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi yao wajitokeze mbele ya darasa, wapange viti kwa njia inayorahisisha mazungumzo yao ili waanze kuzungumza kuhusu mada waliyopewa. Wanafunzi wengine wafuate mazungumzo ya wenzao kwa kuandika kasoro na mafanikio yanayojitokeza katika mazungumzo yao ili, baadaye, waweze kutoa mcango wao kwa kuboresha mazungumzo yao katika mijadala mingine.

Mwalimu acunguze jinsi wanafunzi wanavyojadiliana na awaelekeze katika

kusahihisha matamshi yao na kutunga sentensi kamili zenye uzito wa mawazo yanayoweza kucocea kuungwa mkono na wengine. Ni vyema mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamepata uwezo wa kiubunifu na kiugunduzi pamoja na tafakuri tunduizi kwa kudumisha pia uwezo wao wa kuwasiliana katika lugha rasmi. Vilevile, mazoezi ya mijadala darasani yatumiwe kama msingi wa kuwezesha wanafunzi kupata mienendo mizuri na stadi za maisha zinazoweza kuwasaidia kusuluhisha matatizo yanayojitokeza katika jamii zetu kuhusiana na uzalishaji mali. Pengine, mawazo yanayotolewa na wanafunzi yatilie mkazo uwezo wao wa kujenga ushirikiano na kufanya shughuli za pamoja, kujitwala na kujithamini kupitia miradi ya kuzalisha mali kupitia maoni wanayoyatoa katika mazungumzo yao.

**Tathmini ya kipindi ca 13**

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mepesi yenye kucunguza uwezo wa wanafunzi wa kudhihirisha uwezo wao wa kushiriki katika mijadala inayohusu mada mbalimbali kwa kutilia mkazo mambo muhimu yanayozingatiwa kama vile: kuwa na adabu, kutoa maoni kwa kuheshimiana, kutoa hoja zenye uzito na ambazo huwacocea wasemaji wengine kuunga mkono, kuzingatia maelekezo ya mwenyekiti wakati wa kuzungumza na kadhalika.

Vilevile, tofauti kati ya mjadala na mdahalo nayo irejelewe katika sehemu hii ya tathmini ambapo mwalimu atawaongoza wanafunzi kutofautisha utaratibu wa mdahalo na ule wa mjadala.

## Kipindi cha 14: Sarufi (Kauli asili na kauli taarifa)

**a) Malengo ya somo**

- Kutambua matumizi ya kauli asili na kauli taarifa;
- Kugeuza sentensi za kauli asili na kuziandika katika kauli taarifa;
- Kudhihirisha mambo muhimu yanayobadilika wakati wa kugeuza kauli asili ili kuwa katika kauli taarifa.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 99-101;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### c) Maandalizi ya somo

Somo hili ni mwendelezo wa somo la sarufi lililotangulia kuhusu kauli asili na kauli taarifa. Mwalimu aandae mazungumzo kadhaa yaliyoandikwa katika kauli asili na kauli taarifa ambayo atawasomea wanafunzi. Mwalimu anaweza pia kuwasimulia wanafunzi kuhusu mambo ambayo tayari yameishatendeka hivyo kutumia kauli taarifa. Kauli asili inaweza kujitokeza katika mafundisho ya mwalimu ya wakati huo akiwa darasani. Mazungumzo haya yanaweza kuhusisha mjadala ambao mwalimu atauteua yeye mwenyewe.

### d) Utaratibu wa somo

**Utangulizi**

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu mazungumzo yao ya kila siku ambapo wakati mwingine wanazungumza kwa kauli asili na kauli taarifa. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa.

Mwalimu atumie mazungumzo aliyoyaandika katika kauli asili na kauli taarifa aliyoyaandaa kutanguliza funzo hili.

Katika somo hili, mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila zoezi linalohusika.

### 12.5 Sarufi: Mabadiliko ya kauli asili na kauli taarifa

Ujifunzaji wa sarufi katika sehemu hii ni mwendelezo wa yale yaliyofundishwa katika somo lililotangulia. Kwa hivyo, mwalimu awaulize kwanza wanafunzi maswali mbalimbali kwa kuwataka waeleze na watoe mifano yao katika kauli asili na kauli taarifa. Mwalimu asahihishe makosa ya wanafunzi na awaelekeze wapate kuelewa tofauti kati ya kauli asili na kauli taarifa kabla ya kuwagawa katika makundi ya wanafunzi wawili wawili ili wacunguze sentensi katika sehemu A na zile zilizoandikwa katika sehemu B. Baadaye, mwalimu awaongoze wacunguze mifano ya sentensi katika kauli asili na kauli taarifa kama ilivyotolewa katika kitabu ca mwanafunzi. Wanafunzi wajigawe kama walivyoelekezwa na mwalimu na wajadiliane kuhusu mifano hiyo huku wakizingatia mabadiliko yaliyojitokeza katika kauli taarifa. Mwalimu acunguze uwezo wa wanafunzi wa kutafiti na kugundua mabadiliko hayo kwa kuwaomba wafanye zoezi la kwanza. Mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi kutambua sifa za kauli asili na kauli taarifa katika mjadala wao kwa kuwaomba walinganishe sentensi za

kauli asili na za kauli taarifa. Hatimaye, mwalimu awaongoze wanafunzi katika kucunguza maelezo muhimu waliyotolewa katika kitabu ca mwanafunzi kama njia ya kukamilisha mjadala walioufanya kuhusiana na sifa za kauli asili na kauli taarifa.

**Tathmini ya kipindi ca 14**

Katika hatua hii ya mwisho wa somo, mwalimu ahitimishe kwa kuuliza maswali mbalimbali kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha. Mwalimu pia awaulize wanafunzi maswali ya kumhakikishia kuwa wameelewa tofauti kati ya kauli asili na kauli taarifa, kutoa mifano ya sentensi katika kauli asili na kuzigeuza katika kauli taarifa kwa kubainisha mambo muhimu yanayobadilika wakati wa kugeuza sentensi za kauli asili na kuziandika katika kauli taarifa.

Ili kuwasaidia wanafunzi kuendeleza ujifunzaji wao hata na nje ya darasa lao, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika namna ya kujibu zoezi walilopewa katika sehemu ya sarufi na kuwaomba walifanye kama zoezi la utafiti; yaani kazi ya nje ya darasa. Zoezi hili litasahihishwa kabla ya kuanza somo lijalo.

**Maelezo muhimu kwa mwalimu**

- Sentensi za kauli asili hutanguliwa na kitenzi 'alisema' au 'aliuliza' (kitenzi ***sema*** au ***uliza*** katika wakati uliopita).
  - ✓ **Kwa mfano:**
  - *Wafanyakazi walisema, "Leo tunafurahia matunda ya kazi yetu."*
  - *Dereva aliuliza, "Nani anataka kufika mjini Kigali?"*
  - *Mwanafunzi mmoja aliuliza, "Mdahalo utafanyiwa wapi?"*
- Alama ya kuuliza (?) na alama za kufunga na kufungua (" ") hazitumiwi katika kauli taarifa
  - ✓ **Kwa mfano:** *Dereva aliuliza mtu ambaye alitaka kufika mjini Kigali.*
- Mambo yafuatayo hubadilika wakati wa kugeuza sentensi za kauli asili na kuziandika katika kauli taarifa:

**Nyakati**

Wakati uliopo ***(-na-)*** hugeuka wakati uliopita ***(-li-)***

Wakati ujao ***(-ta-)*** hutumia ***(-nge-)***

| **Vivumishi vionyeshi** | **Vielezi vya wakati** |
|---|---|
| *Hapa* hugeuka *hapo* | *Leo* hugeuka *siku hiyo* |
| *Watu hawa* hugeuka *watu hao* | *Sasa* hugeuka *wakati huo* |
| *Kitu hiki* hugeuka *kitu hicho* | *Kesho* hugeuka siku *iliyofuata* |

| **Vivumishi vimilikishi** | **Maneno ya kuuliza maswali** |
|---|---|
| *Changu* hugeuka *chake* | *Nini* hugeuka *kitu ambacho* |
| *Wetu* hugeuka *wao* | *Nani* hugeuka *mtu ambaye* |
| *Zetu* hugeuka *zao* | *Nyumba gani* hugeuka *nyumba ambayo* |
| *Wangu* hugeuka *wao* | *Kitu gani* hugeuka *kitu ambacho* |
| | *Wapi* hugeuka *mahali ambapo* |

## 12.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu awasaidie wanafunzi wenye kiwango ca cini katika ujifunzaji wao kwa kuwaomba wageuze sentensi hizi kutoka kauli asili hadi katika kauli taarifa.

***Kwa mfano:***

***Kauli asili:*** *"Huku ni kwetu," Gatete alisema.*

***Kauli taarifa:*** *Gatete alisema kuwa huko ni kwao.*

1. Mugabo alisema, "Mimi ninapenda kufuga ng'ombe."
2. Mukamunana alisema, "Baba yangu analima shamba kubwa."
3. Kabera alisema, "Ninataka kuenda mjini Kigali leo."
4. Izere alisema, "Kesho nitaenda nitanunua mbuzi watatu."
5. Ineza alisema, "Wimbo huu ni mzuri sana."

**Majibu ya zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga, ahakikishe kuwa sentensi hizo ni sahihi na kuwa zimehusisha kauli asili pamoja na kauli taarifa. Mabadiliko ya kauli taarifa hadi kauli taarifa yazingatiwe kwa usahihi.

1. Mugabo alisema kuwa yeye anapenda kufuga ng'ombe.
2. Mukamunana alisema kuwa baba yake alilima shamba kubwa.
3. Kabera alisema kuwa alitaka kwenda mjini Kigali siku hiyo.
4. Izere alisema kuwa angeenda kununua mbuzi watatu siku ambayo ingefuata.
5. Ineza alisema kuwa wimbo huo ulikuwa mzuri sana.

**ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka**

Kwa wanafunzi wenye kiwango ca juu ca uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe waandike aya moja ya masimulizi katika kauli asili kisha waibadilishe aya hiyo katika kauli taarifa.

# 12.7 Majibu

**Zoezi la makundi, ukurasa 95**

Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi kwa kurejelea micoro iliyopo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 95.

**Kwa mfano:**

*Mcoro A unaonyesha wanafunzi wanaoshiriki katika mjadala. Mjadala unahusu ufugaji kama njia ya kupigana na umaskini ncini. Mcoro B unaonyesha aina mbalimbali ya mifugo pamoja na mfugaji anayemkama ng'ombe.*

**Maswali ya ufahamu, ukurasa 96**

1. Mjadala unahusu nafasi na umuhimu wa ufugaji katika shughuli za uzalishaji mali ncini mwetu.
2. Niyibizi alisema kuwa ufugaji ni muhimu katika kuboresha maisha yetu. Afya ya miili yetu itaboreka kutokana na maziwa, nyama na mafuta kutoka kwa mifugo. Pia, alisema mifugo humsaidia mfugaji kupata pesa za kutimiza mahitaji mengine.
3. Nyiraneza alicangia kwa kusema kuwa ufugaji una nafasi kubwa katika maisha yetu kwani mtu anapopatwa na uhaba wa pesa anaweza kumuuza mnyama mmoja na akatatua shida yake. Mambo mengine huweza kutekelezwa kutokana na mapato ya ufugaji.
4. Muhirwa alisema kuwa nci yetu haina maeneo makubwa ya kutengea shughuli za ufugaji pekee bali pia shughuli nyingine za viwanda, kilimo na hata biashara. Mifugo micace iliyopo haiwezi kutatua shida za wafugaji.
5. Hoja alizotoa Bwana Rwambibi ni kuwa ufugaji ni muhimu sana kwa kuwa ndio unaofanya kilimo kuwa bora. Ufugaji huleta rutuba inayotumiwa katika mashamba yetu kustawisha mimea. Katika ufugaji wa leo, watu wanafuga ng’ombe wa kisasa wenye kuleta maziwa mengi ambayo huwa na mapato mengi yakiuzwa. Viwanda navyo vinahitaji malighafi ya kutengeneza vyakula, vinywaji, mafuta na nguo. Ufugaji ni muhimu katika kupigana na umaskini na kuboresha maisha yetu.
6. Mwenyekiti alihitimisha mjadala kwa kuwashukuru washiriki wote wa mjadala. Aliwashukuru kwa maoni waliyotoa na akasema kuwa kila mtu ameweza kuelewa umuhimu wa ufugaji na jinsi ambavyo unaweza kucangia katika kupigana na umaskini ili kutuwezesha kuwa na maisha mazuri.

**Zoezi la msamiati, ukurasa 97**

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watau kisha awaelekeze katika kutafuta msamiati mpya uliotumika katika mjadala na kueleza maana yake. Awasisitizie kuwa ni sharti msamiati huo uwe umetumika katika mjadala waliosoma.

***Kwa mfano:***

*1. **ufugaji**: kazi ya kutunza wanyama au ndege; ukulima wa mifugo kama vile: ng’ombe na mbuzi*

*2. **mfugaji**: mtu anayefanya kazi ya kutunza ndege na mifugo kwa ajili ya faida fulani*

*3. **fursa**: nafasi*

### Zoezi la 12.1, ukurasa 97

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi na zitumie maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi walizopewa.

***Kwa mfano:***

1. ***Maziwa*** *ya ng'ombe yatauzwa leo jioni.*
2. *Rais alitusihi* ***tupambane*** *na umaskini kwa kushiriki katika ufugaji.*
3. *Wazazi wangu hupeleka mazao shuleni ili kunilipia* ***karo****.*
4. *Mama* ***ametenga*** *faranga hamsini za kununulia mifugo dawa.*
5. *Ngozi za wanyama waliocinjwa zitapelekwa katika* ***kiwanda*** *ca kutengeneza viatu.*
6. *Mfugaji alipoteza mifugo wake kwa* ***kupuuza*** *mawaidha ya mshauri wake.*
7. *Mwenyekiti* ***amegusia*** *mada ya mjadala wetu.*
8. *Shamba letu lina* ***rutuba*** *nyingi.*
9. ***Malighafi*** *nyingi huhitajika katika shughuli za viwandani.*
10. *Ufugaji hautafikia* ***kikomo*** *ncini mwetu.*

### Zoezi la 12.2, ukurasa 97

1. Wizi wa ***mifugo*** unaweza kuleta hasara kubwa kwa wafugaji na kuwarudisha katika hali ya ***umaskini***.
2. Watu wengi wanapenda kunywa ***maziwa*** ili kupambana na magonjwa mbalimbali.
3. Wafugaji hawa wamejiunga katika shirika kubwa kwa sababu wanajua kwamba ***umoja*** ni nguvu.
4. ***Mjadala*** wetu umetufurahisha sana kwa sababu washiriki wote walitoa ***hoja*** nzuri.

### Zoezi la matumizi ya lugha, ukurasa 98

1. Mdahalo
2. Mwenyekiti
3. Mzungumzaji
4. Upinzani
5. Mjadala
6. Uzalishajimali
7. Ufugaji
8. Mkulima
9. Maoni
10. Kilimo

**Zoezi la 12.3, ukurasa 98**

1. Ni lazima kujiepusha na tabia mbaya za ulevi na uvivu kwa sababu zinakwamisha kazi.
2. Kazi za ufugaji na kilimo zinaweza kuwasaidia raia wengi kupigana dhidi ya umaskini.
3. Ni lazima watu wote wafanye kazi kwa bidii ili waweze kuwa na maisha mazuri.
4. Watu wengi hushiriki katika mjadala na mdahalo kwa kutoa hoja zao.
5. Sisi tunajadiliana kuhusu namna ya kuanzisha miradi ya maendeleo na umuhimu wa kazi.

**Zoezi la kusikiliza na kuzungumza, ukurasa 99**

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kujigawa katika makundi ya wanafunzi watano watano kisha awape fursa ya kucagua mada moja kati ya zile walizopewa na kuijadili katika makundi yao.

**Zoezi la 12.4, ukurasa 99**

1.
   i) Sentensi za A ziko katika kauli asili na sentensi za B ni za kauli taarifa.
   ii) Mifano ya sentensi katika ***kauli asili*** ni:
      a. *"Njoo uwasilishe hoja zako." Mwenyekiti alisema.*
      b. *Kalisa alisema, "Kiwanda ca maziwa kitajengwa hapa."*
      c. *"Sijafuga mifugo wengi." Mkulima alituambia.*
      d. *"Nani ameona umuhimu wa ufugaji?" Mkulima aliuliza.*
      e. *" Mwenyekiti hajanicagua leo." Neza alisema*
      f. *Mama alimaka,"Ng'ombe wangu amepotea!"*

***Sentensi za kauli taarifa:***

a. *Mwenyekiti alisema niende niwasilishe hoja zangu.*
b. *Kalisa alisema kuwa kiwanda ca maziwa kingejengwa hapo.*
c. *Mkulima alituambia kuwa hajafuga mifugo wengi.*
d. *Mkulima aliuliza kuwa ni nani aliyekuwa ameona umuhimu wa ufugaji.*
e. *Neza alisema kuwa mwenyekiti hakuwa amemcagua siku hiyo.*
f. *Mama alishangaa kuwa ng'ombe wake alikuwa amepotea.*

**Zoezi la 12.5, ukurasa 101**

1. Seremala mmoja alisema kuwa yeye aliunda vitanda vikubwa.
2. Mfugaji alisema kwamba wanyama wao walikosa maji.
3. Mwalimu alisema kuwa wanafunzi hao walienda kuceza.

4. Mtoto wake alisema kuwa yeye angeenda kucota maji na ndugu yake.
5. Bwana yule aliuliza nilicotaka hapo.

**Majibu ya tathmini ya mada ya 3**

**Zoezi la 1, ukurasa 101**

1. Mwalimu atathmini midahalo ambayo wanafunzi wataandaa na kuwasilisha mbele ya wanafunzi wenzao kuhusu '*Shule za umma ni bora kuliko shule za kibinafsi*'. Wanafunzi watetezi waeleze uzuri wa shule za umma huku wanafunzi wapinzani wakieleza ubora wa shule za kibinafsi.

**Kwa mfano:**

*Shule za umma ni nafuu kwa karo zikilinganishwa na shule za kibinafsi ambazo huwa ghali sana.*

2. Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

**Kwa mfano:**

a) ***Mwenyekiti*** huongoza majadiliano, hupanga muda wa majadiliano na hucagua wasemaji katika majadiliano.

b) ***Katibu*** huandika na kusoma hoja za wasemaji.

c) ***Wapinzani*** hupinga mawazo yanayotetea wazo kuu la mada.

d) ***Watetezi*** hutetea mada au wazo kuu linalozungumziwa.

**Zoezi la 2, ukurasa 101**

Mwalimu atathmini mjadala ambao wanafunzi wataandaa na kuwasilisha mbele ya wanafunzi wenzao kuhusu' *Athari za mavazi ya kisasa kwa wanajamii*'.

**Kwa mfano:**

*Mavazi ya kisasa huathiri maadili ya wanajamii kwa kuiga mitindo ya kigeni.*

**Zoezi la 3, ukurasa 101 - 102**

1. Yeye hajaagiza bidhaa nyingi kutoka Kigali.
2. Mimi sijazunguka mjini kwa gari.
3. Mtoto wangu hajafaulu mtihani wake.
4. Nyumba yangu haijasafishwa.
5. Mgomba haujacomwa.
6. Kazi hii haijafanywa vizuri.
7. Kitabu cako hakijaharibika.
8. Utambi haujakauka.
9. Udevu mrefu haujanyolewa.
10. Barua haijatumwa.

**Zoezi la 4, ukurasa 102**

1. Wao hawajaagiza bidhaa nyingi kutoka Kigali.
2. Sisi hatujazunguka mijini kwa magari.
3. Watoto wetu hawajafaulu mitihani yao.
4. Nyumba zetu hazijasafishwa.
5. Migomba haijacomwa.
6. Kazi hizi hazijafanywa vizuri.
7. Vitabu vyenu havijaharibika.
8. Tambi hazijakauka.
9. Ndevu ndefu hazijanyolewa.
10. Barua hazijatumwa.

**Zoezi la 5, ukurasa 102**

1. Viti vimevunjika.
2. Watu hawa wametuimbia vizuri.
3. Wazee hawa wamelewa.
4. Wanafunzi hawa wameelewa somo la Kiswahili.
5. Ng'ombe wetu wamezaa leo.
6. Mito hii imefurika.
7. Viongozi wamewasili mapema.
8. Mbwa wamekula vyakula.
9. Nyuso zao zimeharibika.
10. Miguu yetu imetibiwa vizuri.

**Zoezi la 6, ukurasa 103**

1. Viti havijavunjika.
2. Watu hawa hawajatuimbia vizuri.
3. Wazee hawa hawajalewa.
4. Wanafunzi hawa hawajaelewa somo la Kiswahili.
5. Ng'ombe wetu hawajazaa leo.
6. Mito hii haijafurika.
7. Viongozi hawajawasili mapema.
8. Mbwa hawajakula vyakula.
9. Nyuso zao hazijaharibika.
10. Miguu yetu haijatibiwa vizuri.

**Zoezi la 7, ukurasa 103**

1. Kila mwananci anapaswa kufanya kazi kwa bidii ili ***kuinua*** kiwango ca maisha yake.
2. ***Ucumi*** wa nci yetu utastawi baada ya kuanzisha miradi mingi mizuri.
3. Viongozi hawa ***wanatushawishi*** kutumia mbinu za kisasa katika shughuli zetu za kilimo na ufugaji.
4. Ni ***dhahiri*** kwamba raia wa Rwanda walipata maisha mazuri baada ya kuanzishwa kwa shughuli za '*Gira inka Munyarwanda'*.
5. Juzi wanafunzi wote ***walipiga kura*** kwa sababu Mkuu wa shule alitaka orodha ya viongozi wa madarasa yote.

**Zoezi la 8, ukurasa 103**

1. Kiwanda hiki ca kutengeneza mafuta kinaagiza ***maziwa*** kutoka kwa wafugaji wengi wilayani Nyagatare.
2. ***Uzalishaji*** mali unategemea sana shughuli za ***kilimo*** na ***ufugaji*** kwa sababu shughuli hizo zinafanywa na watu wengi ncini.
3. Watu hawa ***wanaunga mkono*** miradi ya maendeleo ya nci yetu kwa sababu wanashirikiana sana na viongozi wao.
4. Mkuu wa wilaya yetu ***alihimiza*** wakulima kupanda miti mingi katika mashamba yao.

**Zoezi la 9, ukurasa 104**

1. Rais alisema kuwa kila mwananci angeweza kujitajirisha kwa kufanya kazi kwa bidii.
2. Mkuu wa shule alisema kuwa wanafunzi wawili hawakujua kusoma vizuri.
3. Wafanyakazi walisema kwamba hawakutaka kufanya kazi na watu wavivu.
4. Wazazi waliuliza ni nani ambaye angeenda kununua mavazi ya watoto wao.
5. Mkulima alisema kuwa mvua haikunyesha sana siku hizo.

**Zoezi la 10, ukurasa 104**

1. "Nitaenda Kigali kesho," Kalisa anamwambia shangazi yake.
2. "Cumbani mwangu mna nyoka!" Bagirishya anasema akitetemeka.
3. "Mkitaka kuendelea vyema maishani, lazima muwe na heshima," kasisi anatuambia.
4. "Ukimwi ni ugonjwa hatari sana," daktari anatuambia.
5. "Mlifungwa mabao mangapi mcezoni?" Baba anauliza.

Sura ya
Nne

# Mada Kuu 4: Uimarishaji wa stadi ya uandishi na masimulizi kupitia lugha ya Kiswahili

## Mada Ndogo: Utungaji wa insha

**Uwezo upatikanao katika mada hii:**

Mwanafunzi aweze kusikiliza, kusema, kusoma na kuandika mada juu ya shughuli za ujenzi wa taifa kupitia kwa utungaji wa insha.

**Malengo ya kujifunza**

| Maarifa na ufahamu | Stadi | Maadili na mwenendo mwema |
|---|---|---|
| • Kutaja sehemu kuu za insha.<br>• Kuainisha sehemu kuu zinazounda insha yoyote.<br>• Kueleza aina mbalimbali za insha.<br>• Kukusanya msamiati wa kutosha wa kutumia katika utungaji wa insha.<br>• Kukumbuka uundaji wa aya iliyokamilika kwa kuzingatia kanuni za uandishi wa aya.<br>• Kutoa mfano wa jinsi ya kupangilia fikra katika uandishi wa insha.<br>• Kubaini matumizi ya utokeaji wa majina ya ngeli ya U-ZI katika tungo na jinsi yanavyobadilika kufuatana na vivumishi husika. | • Kutumia maarifa kuhusu uundaji wa aya na sehemu zinazounda insha.<br>• Kucambua mada iliyotolewa kwa ajili ya kutafuta hoja au maoni yatakayoijenga insha yake.<br>• Kutunga insha fulani kulingana na kicwa au mada iliyotolewa.<br>• Kufanya ucambuzi wa insha iliyotungwa kwa kubainisha mambo makuu yanayojitokeza katika insha hiyo kisha kutoa maoni yake kuhusu mada au suala linalojadiliwa katika insha.<br>• Kutoa au kuelezea muhtasari wa insha aliyoitunga au aliyoisoma kwa njia ya masimulizi akizingatia mambo muhimu katika insha hiyo.<br>• Kuhakiki insha mbalimbali kutokana na maudhui yake.<br>• Kutumia kwa ufasaha majina ya ngeli ya U-ZI katika tungo fupi. | • Kucukua msimamo binafsi juu ya swali au wazo fulani.<br>• Kujali na kutathmini tabia nzuri katika maendelezo ya jamii.<br>• Kujiamini na kuwaamini wenzake.<br>• Kutoa ushauri katika ujenzi wa nci ya amani na maendeleo.<br>• Kujenga utamaduni wa kujenga hoja na kuzitetea. |

## Maelezo muhimu kwa mwalimu

Mada hii inahusiana na ***somo la karatasi ya maarifa*** katika mada inayohusu kazi za ujenzi wa taifa na kujitegemea.

Mada hii inashughulikia utungaji wa insha. Huu ni uandishi wa aina mbalimbali za insha kama vile: insha za methali, insha za maelezo, insha za mazungumzo, insha za barua na hata insha za wasifu. Kwa hivyo, mifano ya aina mbalimbali za insha, sehemu kuu za kila aina ya insha hizo, kanuni au mbinu za kuzingatiwa katika utungaji wa insha hizo, hayo yote yamezungumziwa katika mada hii. Mbali na hayo, mada hii imegusia majina ya ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vyake husika.

Dhana muhimu zinazojitokeza katika mada hii ni pamoja na sehemu kuu za insha, mambo ya kuzingatia katika utungaji wa insha, aina mbalimbali za insha, majina ya ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vyake husika.

## Masuala mtambuka

Baadhi ya masuala mtambuka ambayo yatashughulikiwa katika mada hii ni amani na maadili, usawa wa kijinsia, elimu ya pamoja, elimu kuhusu fedha pamoja na mazingira, mabadiliko ya hali ya hewa na mwendelezo wake.

Elimu ya pamoja itaendelezwa kupitia kwa wanafunzi wote kusoma pamoja kwa kuwashirikisha hata na wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali na matatizo mbalimbali iwapo wapo. Elimu hii ya pamoja pia itahusisha wanafunzi wote kuwakubali na kushirikiana kwa pamoja na wenzao kutoka katika matabaka mbalimbali ya kijamii. Wanafunzi pia watafundishwa umuhimu wa mazingira yao na namna ya kuyahifadhi.

Amani na maadili yatashughulikiwa kupitia kwa utungaji wa insha zenye kuendeleza maadili mema, uzalendo pamoja na ushirikiano miongoni mwa Wanyarwanda. Wanafunzi waelekezwe kutangamana kwa amani na upendo. Usawa wa kijinsia utatiliwa mkazo kwa kuwafahamisha wanafunzi kuwa wasicana pamoja na wavulana wana uwezo sawa wa kufaulu katika maisha yao lica ya jinsia zao tofauti.

## Uwezo wa jumla

Mwalimu ahakikishe kuwa katika ufundishaji wa somo hili wanafunzi wanapata uwezo wa kuwa na stadi za utafiti, usuluhishaji wa matatizo, mawasiliano katika lugha rasmi, ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha, ubunifu na ugunduzi, tafakuri tunduizi pamoja na ujifunzaji wa muda mrefu.

Mwalimu awaelekeze na awashirikishe wanafunzi wote katika kuwa na tafakuri tanduizi kwa kufikiri kwa undani zaidi kuhusiana na utungaji wa insha mbalimbali. Katika ufundishaji wa somo hili, utunzi mwingi na utoaji wa maelezo mengi utahusishwa. Ujuzi huu utawawezesha wanafunzi kuyajibu maswali yaliyo katika somo hili.

Kupitia kwa mazoezi ya kuandika insha mbalimbali watakayokumbana nayo, wanafunzi watahimizwa kuwasiliana kwa lugha rasmi pamoja na kuwa na utawala binafsi pamoja na kuzifahamu stadi mbalimbali za maisha. Stadi za utafiti zitakuzwa kupitia kwa wanafunzi kufanya utafiti kuhusiana na namna ya kuandika insha mbalimbali, maumbo ya insha mbalimbali pamoja na taratibu za kuzingatiwa katika uandishi wa insha hizo. Ujifunzaji wa muda mrefu uendelezwe kupitia kwa wanafunzi kupata maarifa mbalimbali kuhusiana na utungaji wa insha mbalimbali watakayotumia nje ya darasa na katika maisha yao ya kila siku na kuwa wazalendo kamili.

## Msamiati maalum

Msamiati maalum na muhimu ambao wanafunzi watapatana nao katika mada hii ni kuhusu utungaji wa insha mbalimbali kama vile:

| | Msamiati | Maana |
|---|---|---|
| 1. | ***insha*** | mtungo ulioandikwa kwa lugha ya mfululizo kuhusu kitu, mtu au jambo fulani |
| 2. | ***utangulizi*** | maelezo ambayo huandikwa mwanzoni mwa insha ili kueleza kwa ufupi mambo yatakayozungumziwa katika insha nzima |
| 3. | ***mada*** | kicwa ca insha kinacoeleza insha inahusu nini |
| 4. | ***hitimisho*** | maelezo yanayoandikwa mwishoni mwa insha |
| 5. | ***mwendelezo*** | namna ya kuandika neno kwa usahihi kwa kuzingatia silabi zote husika |
| 6. | ***hati*** | mwandiko wa mtu; namna mtu anavyoandika |
| 7. | ***uandishi*** | uandikaji; kazi ya kuandika |
| 8. | ***utungaji*** | namna au tendo la kubuni (kutunga) kisa au hadithi |
| 9. | ***masimulizi*** | maelezo ya jambo fulani |
| 10. | ***mwandishi*** | mtu anayeandika au anayetunga maelezo fulani |

### Usuluhishaji wa tatizo

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi yanayotakikana kulingana na kila zoezi husika kisha awaombe wacunguze kwa makini mifano ya insha iliyo katika *Kitabu ca Mwanafunzi* kuhusiana na umuhimu wa adabu, ubaya wa uvivu, malezi mema pamoja na umuhimu wa maadili mema katika jamii. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika shughuli hii. Wanafunzi wacunguze insha hizo na mwalimu awaulize maswali kama vile: *Mmejifundisha nini kutokana na insha hizo?* Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika makundi yao ili waweze kujibu swali hilo. Kwa hivyo, mwalimu acocee uwezo wa wanafunzi wa kupata maarifa kuhusu ubunifu na ugunduzi na tafakuri tunduizi kwa kucunguza na kujibu maswali kuhusu insha husika.

### Ushirikishaji wa wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali

Katika sehemu hii, ni vyema mwalimu awe na vifaa maalum vya kuwasaidia wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali katika ujifundishaji wao. Kwa wanafunzi wasio na uwezo wa kuona, mwalimu anaweza kuhusisha matumizi ya breli pamoja na vifaa vya kunasia sauti.

Kwa wanafunzi wasio na uwezo wa kusikia, mwalimu anaweza kuhusisha matumizi ya lugha ya ishara. Mwalimu anaweza kuwahusisha watafsiri wanaotumia lugha ya ishara. Vifaa hivi vitawawezesha wanafunzi hawa kusoma kama wanafunzi wenzao bila vikwazo vyovyote.

Nafasi ya wanawake na walemavu katika shughuli kama vile za kuungana na Wanyarwanda wengine itiliwe maanani kupitia kwa micoro iliyo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa wa 106 ili kukuza usawa wa kijinsia na elimu ya pamoja. Hili litadumisha ushirikiano na mienendo mizuri miongoni mwa wanafunzi na kuwafanya kuwa wazalendo kamili katika umri wao.

### Orodha ya masomo na vipindi:

| | Mada ya somo | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|
| **Somo la 13:** | Sehemu kuu za insha | 4 |
| **Somo la 14:** | Mambo ya kuzingatia katika kuandika insha | 3 |
| **Somo la 15:** | Aina mbalimbali za insha | 4 |
| **Somo la 16:** | Madhara ya uvivu | 3 |
| | | **JUMLA: 14** |

# Somo la 13: Sehemu kuu za insha

## Kipindi cha 1: Kusoma ufahamu

### a) Malengo ya somo

- Kusoma kwa usahihi kifungu kuhusu sehemu kuu za insha kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;
- Kutambua sehemu kuu za insha.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Cati yenye mcoro wa umbo la insha kwa ujumla kuonyesha sehemu zake kuu;
- Insha zilizorekodiwa;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 106-107;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### c) Maandalizi ya somo

Mwalimu anaweza kuanza somo hili kwa kuwaomba wanafunzi wasimuliane hadithi fupi katika makundi ya wanafunzi wanne wanne. Hili litawawezesha wanafunzi kufahamu utangulizi, mwili na vilevile mwisho wa hadithi watakazosimuliana. Mwanafunzi mmoja anaweza kusimama mbele ya darasa na kuwasimulia wanafunzi wengine hadithi moja fupi. Baada ya hapa, wanafunzi wajadiliane kuhusiana na utangulizi, mwili na mwisho wa hadithi hiyo. Hapa mwalimu ataweza kupata nafasi ya kuwatangulizia wanafunzi somo hili la sehemu kuu za insha.

Mwalimu ahakikishe pia kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kujifunzia somo hili ili kuwaelekeza wanafunzi ipasavyo hasa wale wa kiwango ca cini katika ujifunzaji. Vifaa kama vile cati yenye umbo la insha linaloonyesha sehemu kuu za insha na insha mbalimbali zilizoandikwa zitamsaidia mwalimu katika somo hili. Vilevile, ni vyema mwalimu azingatie wakati unaofaa wa kuonyesha vifaa hivyo hadharani ili wanafunzi wapate ufahamu unaotarajiwa katika muda unaotakikana. Ikiwa kuna wanafunzi wasioweza kuona, ni lazima mwalimu atumie vifaa maalum kuwafundishia. Katika somo hili, mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli inayohusika darasani.

## d) Utaratibu wa somo

### Utangulizi

Mwalimu atangulize somo hili kwa kuwaamkia wanafunzi wake. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Baada ya mwalimu kuwajulia hali wanafunzi wake, anaweza kuwaomba watazame micoro iliyo kwenye *Kitabu ca Mwanafunzi,* ukurasa 106. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wote wanashirikishwa katika shughuli hii. Mwalimu awacangamshe wanafunzi wake kwa kuwauliza maswali kuhusu micoro ambayo wanafunzi watakuwa wameitazama.

***Kwa mfano:***

✓ Je, mnaona nini katika micoro hii?

Mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kuhusu namna ya kujibu maswali waliyoulizwa kwa kuwapa kitangulizi kama: "*Mimi ninaona...*" Kwa mfano: *Mimi ninaona mwanafunzi akisoma*. Ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kupata ujuzi kuhusu ubunifu na ugunduzi, tafakuri tunduizi kwa kusisitiza ucunguzi wa micoro husika ili kuelewa mtiririko wa ufahamu mzima. Mwalimu awahusishe wanafunzi katika kueleza shughuli ambazo zinaendelea katika micoro husika. Vilevile, masuala ya elimu ya pamoja nayo yasisitiziwe pale ambapo miongoni mwa wanafunzi pale darasani huenda kukawa na wanafunzi wenye ulemavu na ambao wanajifunza pamoja na wengine. Wanafunzi wenye ulemavu wahusishwe pia. Kwa hivyo, wanafunzi watazame au waguse pica walizoonyeshwa na mwalimu wao na kujibu maswali waliyoulizwa. Kwa mfano: *Mimi ninaona mwanafunzi akisoma*. *Mimi ninaona mwalimu akifundisha* na kadhalika.

### 13.1 Kusoma na ufahamu: Kifungu kuhusu somo la Kiswahili

Katika hatua hii, mwalimu awaelekeze wanafunzi kusoma kwa makini na kwa kimya kifungu ca habari kumhusu Bwana Gasimba kisha baadaye wajibu maswali ya ufahamu yaliyotolewa. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali hayo huku akitoa maelezo yake kwa kutilia mkazo pale ambapo wanafunzi wanatatizika. Katika kiwango hiki mwalimu anaweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa maana ya msamiati wowote ambao utakuwa unawatatiza.

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kusoma tena kwa kimya kifungu ca habari kuhusu Bwana Gasimba huku wakiandika katika madaftari yao msamiati mpya

wanaokutana nao. Baada ya dakika cace za kusoma kwa kimya, mwalimu atathmini usomaji wa wanafunzi wake. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wamesoma kwa kimya kama inavyotakikana, mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu kifungu ca habari walicokisoma. Kwa mfano, anaweza kuwauliza swali lifuatalo: *Ni mwalimu yupi aliyependwa na wanafunzi wote?* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika kifungu hico. Kwa mfano: *Wanafunzi wote wanampenda Bwana Gasimba*. Baada ya kupata pica ya uelewa wa jumla wa wanafunzi kuhusu kifungu kinacohusika, mwalimu awaulize wanafunzi wasome kwa sauti kifungu hico ca habari kuhusu Bwana Gasimba mmoja baada ya mwingine. Katika hatua hii, ni lazima mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa.

### Tathmini ya kipindi ca 1

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha ili kutambua ikiwa wanaweza kueleza maana ya insha na sehemu kuu za insha. Mwalimu anaweza kuuliza maswali mengine ambayo yanalenga kutathmini malengo ya ujifunzaji wa mada hii.

## Kipindi cha 2: Kujifunza msamiati

### a) Malengo ya somo

- Kutambua msamiati unaohusiana na sehemu kuu za insha;
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia msamiati unaohusiana na sehemu kuu za insha.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Cati yenye mcoro wa umbo la insha kwa ujumla kuonyesha sehemu zake kuu;
- Insha zilizorekodiwa;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 108;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### c) Maandalizi ya somo

Somo hili linalenga kumpa mwanafunzi ujuzi zaidi kuhusu msamiati unaohusiana na sehemu kuu za insha mbalimbali. Mbali na kumwezesha mwanafunzi kutoa maoni muhimu katika uandishi wa insha, somo hili litasaidia pia kuelewa maana ya msamiati unaohusiana na utungaji wa insha. Ni vyema mwalimu alenge kumsaidia mwanafunzi kupata maarifa ya kuandika insha nzuri kwa kutumia lugha fasaha. Katika maandalizi ya somo lake, mwalimu ahakikishe kwamba ameleta cati yenye mcoro wa umbo la insha kwa ujumla ili kuonyesha sehemu kuu za insha ili kuwasaidia wanafunzi kuelewa kwa urahisi hasa wanafunzi wenye ulemavu wa aina tofauti.

### d) Utaratibu wa somo

### Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi na awaulize maswali mepesi kuhusu uandishi wa insha ambao walijifundisha katika kidato ca pili au hapo awali. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kusahihisha zoezi walilopewa katika somo lililopita na awaelekeze wanafunzi katika kupata ufahamu wa mambo yaliyoonekana kuwatatiza.

### 13.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu sehemu za insha

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kujadiliana kwanza kuhusu maana za msamiati mpya waliokutana nao katika kifungu walicosoma. Wanafunzi wajadiliane kuhusu maana za msamiati huo kwa kuzingatia matumizi yake katika kifungu ca habari kinacohusika. Wanafunzi wanaweza kutumia kamusi pale panapohitajika. Kwa hivyo, mwalimu azunguke darasani akitoa maelekezo pale yanapohitajika. Hatimaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kufanya zoezi la 13.1A la msamiati lililo katika *Kitabu ca Mwanafunzi* ukurasa 108. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wote wameelewa maana ya misamiati yote iliyopigiwa mistari katika sentensi walizopewa. Hivyo basi, wanafunzi, katika makundi yao ya wanafunzi watatu watatu, wajadiliane kuhusu zoezi hilo la msamiati huku mwalimu akizunguka darasani kuwaelekeza wale wanaotatizika. Baada ya kujibu maswali yaliyotolewa kuhusu zoezi hili, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kujibu zoezi hilo.

Kuhusu zoezi la 13.1B, mwalimu awaelekeze wanafunzi kujipanga katika makundi ya wanafunzi watatu watatu ili waweze kujadiliana kuhusu maana za msamiati unaotakiwa kutumiwa kutunga sentensi sahihi. Ni vyema mwalimu

awaambie wanafunzi warejelee matumizi ya msamiati husika katika kifungu ca habari walicokisoma hapo awali. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kujibu maswali ya zoezi hilo. Wakati wa kujibu zoezi hili, mwalimu arejelee pia mifano mingine inayoweza kuwasaidia wanafunzi kupata stadi za utafiti, utawala binafsi na stadi za maisha. Kwa mfano, anaweza kuwacocea wanafunzi kucunguza na kufikiria kuhusu umuhimu wa kufuata umbo linalotakikana katika kuandika insha, mienendo mizuri inayomtambulisha mwanafunzi mwenye adabu kwa kuzingatia lugha anayotumia katika kuandika insha.

**Tathmini ya kipindi ca 2**

Katika hatua hii ya tathmini, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kwa kurejelea msamiati mahususi waliojifunza kuhusu sehemu kuu za insha wakirejelea mambo muhimu ya kuzingatia katika kuandika insha. Hivyo basi, vifaa na pica zilizotumiwa kujifunzia somo hili zitumiwe kucunguza iwapo wanafunzi wanaweza kurejelea sehemu kuu za insha mbalimbali na hata wabainishe mienendo mizuri inayotakikana katika uandishi wa insha.

## Kipindi cha 3: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza

**a) Malengo ya somo**

- Kutaja sehemu kuu za insha;
- Kutoa maelezo kuhusu sehemu kuu za insha;
- Kuandika insha yenye sehemu kuu za insha;
- Kuandika imla.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Wanafunzi wenyewe;
- Cati yenye mcoro wa umbo la insha kwa ujumla kuonyesha sehemu zake kuu;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 109-110;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### c) Maandalizi ya somo

Mwalimu alenge kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi zaidi kuhusu sehemu kuu za insha. Mbali na kumwezesha mwanafunzi kutoa maoni muhimu katika uwanja huu, somo hili litasaidia pia kumwezesha mwanafunzi kujadili na wenzake katika makundi kuhusiana na sehemu kuu za insha ambazo wamefundishwa.

### d) Utaratibu wa somo

### Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi na awaulize maswali kuhusu somo lililopita kuhusiana na msamiati wa sehemu kuu za insha. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu awashirikishe wanafunzi kusahihisha zoezi walilopewa katika somo lililopita na awaelekeze wanafunzi katika kupata ufahamu wa mambo yaliyoonekana kuwatatiza.

### 13.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

Katika sehemu hii, mwalimu awaombe wanafunzi wajipange katika makundi ya wanafunzi wanne wanne ili kujadiliana kuhusu sehemu kuu za insha ambazo wanazifahamu. Wanafunzi katika makundi yao waelezane mada ya insha huhusu nini, utangulizi wa insha huandikwa kwa namna gani, mwili wa insha huhusu nini, hitimisho la insha huandikwa kwa namna gani na lugha inayotumika kuandika insha hustahili kuwa ya aina gani? Baadaye, kila kundi lieleze waliyoyazungumzia. Mwalimu arekebishe makosa ya kimatamshi katika maelezo ya wanafunzi.

Baadaye, mwalimu acukue fursa hii kuwaeleza wanafunzi kuhusu muundo wa insha yoyote ile. Awaeleze kuwa umbo la insha yoyote ile ni insha kuwa na: mada inayofaa, utangulizi wa kuvutia, mwili wenye ujumbe unaofaa, hitimisho la kuvutia pamoja na lugha sahihi na iliyopambwa. Wanafunzi washirikishwe katika kuzitaja sehemu kuu za kuzingatia katika kuandika insha.

Mambo ya kuzingatiwa ni kama vile: mada au kicwa ca insha, utangulizi au mwanzo wa insha, mwili wa insha pamoja na hitimisho au mwisho wa insha.

### 13.4 Kusikiliza na kuzungumza: Somo la imla

Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kusoma kifungu ca habari kwa usahihi na kwa utambuzi wa herufi, silabi, neno na sentensi. Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi wafunge vitabu vyao na wafungue madaftari yao. Mwalimu awasomee wanafunzi sentensi tano zinazofuata kwa sauti na kwa matamshi sahihi kisha wanafunzi wazinakili sentensi hizo katika madaftari yao:

1. *Utangulizi ndio kioo ca insha.*
2. *Lugha ya Kiswahili ina wazungumzaji wengi.*
3. *Mwili wa insha ni sehemu muhimu sana katika uandishi wa insha.*
4. *Mwisho wa insha unafaa kuvutia sana.*
5. *Insha iliyopambwa humvutia msomaji.*

Katika sehemu hii, ni vyema mwalimu awe na uwezo wa kutamka maneno kwa usahihi na kwa sauti ya kusikika na wanafunzi wote darasani. Baada ya hapa, mwalimu ayacukue madaftari ya wanafunzi asahihishe makosa ya maendelezo ili kuwazoesha wanafunzi wake kuandika kwa usahihi herufi, silabi, maneno na hata sentensi za Kiswahili.

### Tathmini ya kipindi ca 3

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti kwa kurejelea waliyosoma kuhusu sehemu kuu za insha ili kutathmini ikiwa wanafunzi wameelewa. Vilevile, mwalimu awaulize maswali mbalimbali kwa kucunguza ikiwa wanafunzi wametambua jinsi ya kutoa maelezo kwa kila sehemu kuu ya insha. Wanafunzi wanaweza pia kueleza umuhimu wa kuandika insha kwa kuzingatia sehemu zake kuu. Mwalimu awazoeshe wanafunzi wake kunyosha mkono kila wakati mwanafunzi anapotaka kuuliza au kujibu swali kwa kuonyesha mienendo ya kuwa na adabu shuleni na kadhalika.

## Kipindi cha 4: Sarufi (Ngeli ya U-ZI na vivumishi vya sifa)

### a) Malengo ya somo

- Kutambua majina katika ngeli ya U-ZI;
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia majina katika ngeli ya U-ZI;
- Kutambua maana ya vivumishi vya sifa;
- Kutunga sentensi sahihi zenye majina katika ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vya sifa.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Wanafunzi wenyewe;
- Micoro ya vitu vinavyopatikana katika ngeli ya U-ZI kama vile: *nyuzi, funguo, nyembe, kuta* n.k.;

- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 110-114;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Mwalimu aandae micoro kadhaa ya vitu ambavyo vinapatikana katika ngeli ya U-ZI kama vile: *nyuzi, funguo, nyembe, kuta, fito, kuca, nyuso, panga n.k* ambavyo atawaonyesha wanafunzi. Mwalimu anaweza pia kuwaomba wanafunzi walete vifaa hivi iwapo wanavyo. Kwa mfano: *nyuzi, nyembe, funguo* na *nyaraka*. Ujifundishaji wa somo hili unaweza pia kuhusisha wanafunzi wenyewe kwa kutumia *nyuso* zao, *nyimbo* ambazo wanaweza kuimba na hata *kuca* zao. *Kuta* za darasa lao pia zinaweza kutumika kama mfano wa jina katika ngeli ya U-ZI.

**d) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu ngeli mbalimbali za Kiswahili ambazo wamewahi kufundishwa na ambazo wanazifahamu. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa.

Mwalimu atumie micoro ya vifaa vinavyopatikana katika ngeli ya U-ZI pamoja na vifaa halisi walivyoleta wanafunzi katika kufundishia somo hili.

### 13.5 Sarufi: Ngeli ya U-ZI

Katika hatua hii, wanafunzi watapata fursa ya kusoma masimulizi mafupi waliyopewa yanayohusisha majina yanayopatikana katika ngeli ya U-ZI. Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha awaombe kusoma masimulizi hayo yaliyo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa, 110. Wanafunzi waelekezwe kutambua majina yaliyotumika katika masimulizi hayo ambayo yanapatikana katika ngeli ya U-ZI. Baada ya utambuzi wa majina haya, wanafunzi washirikishwe katika kutunga sentensi sahihi katika umoja na wingi kwa kutumia majina waliyoorodhesha kutoka kwenye masimulizi waliyosoma. Sharti majina watakayotumia yawe katika ngeli ya U-ZI. Mwalimu ahakikishe kuwa sentensi zao zinatumia majina waliyoorodhesha. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kutambua kuwa majina ambayo wanafunzi waliorodhesha yanapatikana katika ngeli ya U-ZI.

***Kwa mfano:***

| ***Umoja*** | ***Wingi*** |
|---|---|
| *Ukuta* | *Kuta* |
| *Ufagio* | *Fagio* |
| *Uso* | *Nyuso* |
| *Wimbo* | *Nyimbo* |
| *Ufunguo* | *Funguo* |

Mifano ya sentensi ambazo wanafunzi wanaweza kutunga katika umoja na wingi ni:

1. *Uso wake umeumia.*
   *Nyuso zao zimeumia.*
2. *Ufunguo wa gari lake ulipotea.*
   *Funguo za magari yao zilipotea.*

Mwalimu awaombe wanafunzi wataje mifano zaidi ya majina katika ngeli ya U-ZI kama vile: *uzi, wembe, udevu, ufito, ubeti, ukoo, ukuni, unywele, wakati, wavu* n.k. Wanafunzi waelekezwe katika kutambua wingi wa majina haya yote ambao ni: *nyuzi, nyembe, ndevu, fito, beti, koo, nywele, nyakati, nyavu* n.k. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kufanya zoezi la 13.2 na zoezi la 13.3 ambapo wanafunzi wanafaa kutunga sentensi sahihi katika umoja na wingi, tungo yakinishi na tungo kanushi kwa kutumia majina waliyopewa yaliyo katika ngeli ya U-ZI. Katika hatua hii, mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wote wanashirikishwa katika kusahihisha mazoezi yaliyopo kwa kuwacocea kupata ujuzi ainasafu kama vile tafakuri tunduizi ambapo anaweza kuomba wanafunzi wengine kucunguza majibu yanayotolewa na wenzao.

### 13.5.1 Ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vya sifa

Mwalimu awaombe wanafunzi watatu wasimame mbele ya wanafunzi wenzao kisha wanafunzi wengine waeleze wanayoyaona kwa wanafunzi waliosimama mbele yao. Wanafunzi wanaweza kutoa majibu kama vile: *Uwase ni mrefu. Gatete ni mweusi. Birasa ni mnene. Uwase ana nguo safi. Gatete ni mfupi. Uwase ana meno meupe. Birasa ana nywele nyeusi. Gatete ana viatu vipya* n.k. Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kutambua maneno yaliyopigiwa mistari ni ya aina gani.

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha awaombe wacunguze pica na micoro waliyopewa pamoja na sentensi walizopewa katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 113. Wanafunzi waelezane

maneno yaliyopigiwa mistari ni ya aina gani. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika majadiliano haya kisha mwanafunzi mmoja kutoka kwa kila kundi awasilishe majibu ya wenzao.

Baada ya hapa, mwalimu awaeleze wanafunzi kuwa:
*Maneno ambayo hutumiwa kutoa maelezo zaidi kuhusu nomino huitwa* ***vivumishi.***
*Maneno yanayoeleza mwonekano na tabia ya nomino huitwa* ***vivumishi vya sifa.***

## Tathmini ya kipindi ca 4

Mwalimu atathmini iwapo malengo yake ya kufundisha kuhusu ngeli ya U-ZI na vivumishi vya sifa yametimizwa.

### Maelezo muhimu kwa mwalimu

Mwalimu afafanue zaidi kuhusiana na sehemu kuu za insha kwa kuwaeleza wanafunzi:

- ***Mada au kichwa cha insha***

*Mada ya insha hutambulisha jambo linalozungumziwa katika insha. Mada ya insha haifai kuzidi maneno manane. Mara nyingi mada ya insha huandikwa kwa herufi kubwa na kupigiwa mstari. Lazima mada iwe na mvuto kwa msomaji.*

- ***Utangulizi au mwanzo wa insha***

*Utangulizi wa insha mara nyingi huwa ni aya moja tu. Unafaa kuvutia kwa kiwango cha juu ili kumpa msomaji hamu ya kutaka kusoma insha nzima.*

- ***Mwili wa insha***

*Hii ndiyo sehemu muhimu sana kwa sababu inabeba ujumbe kamili wa insha nzima. Aya nyingi huandikwa hapa na ni bora aya hizi ziandikwe kwa namna ya kutiririsha matukio kuanzia mwanzo hadi mwisho wa insha.*

- ***Hitimisho au mwisho wa insha***

*Sehemu hii huwa na sentensi chache tu katika aya moja. Hitimisho hufupisha yaliyoandikwa katika mwili wa insha kwa namna ya kuvutia msomaji.*

Vilevile, mwalimu awaeleze wanafunzi kuwa: *majina ya ngeli ya U-ZI katika upatanisho wa kisarufi katika sentensi hutumia kiambishi '**u-**'katika umoja na kiambishi '**zi-**'katika wingi.*

### 13.6 Mazoezi ya ziada

#### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Ili kuwasaidia wanafunzi wa kiwango ca cini katika ujifunzaji wao, mwalimu awaelekeze wanafunzi hao dhaifu katika kutunga sentensi sahihi kwa kutumia majina yaliyo katika ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vya sifa.

#### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi pamoja na sentensi ambazo watatunga. Sharti ziwe sahihi na zihusishe majina ya ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vya sifa.

***Kwa mfano:***

1. *Wimbo mrefu uliandikwa na mwalimu wetu.*
   *Nyimbo ndefu ziliandikwa na walimu wetu.*
2. *Ufagio mpya utanunuliwa.*
   *Fagio mpya zitanunuliwa.*

#### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango ca juu ca uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge kisa kifupi sana cenye kuonyesha mwanzo, mwili na mwisho wake. Kwa kufanya hivi, wanafunzi hawa wataelewa kuwa insha yoyote ile sharti iwe na utangulizi, mwili na hitimisho.

## 13.7 Majibu

#### Zoezi la makundi, ukurasa 106

Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi kwa kurejelea micoro iliyopo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 106.

**Kwa mfano:**

*Mcoro A unaonyesha wanafunzi watatu wanaoenda shuleni. Mcoro B unaonyesha wanafunzi hao pamoja na wengine wakiwa darasani na mwalimu wao (Bwana Gasimba) anawafundisha. Mcoro C unaonyesha mwanafunzi mmoja kati ya waliokuwa shuleni akiwa nyumbani kwao akisoma.*

#### Maswali ya ufahamu, ukurasa 107

1. Bwana Gasimba, mwalimu wao wa somo la Kiswahili.
2. Bwana Gasimba ni mpole, mwenye bidii, mceshi na anayependa kuwasaidia watu walio na matatizo.

3. Mtu anayecekesha watu. Pia, ni mtu mwenye furaha anayependa kutabasamu au kuceka.
4. Kwa sababu somo hili lilijaa masimulizi mengi mazuri.
5. Mada na utangulizi hueleza kwa ufupi kitakacozungumziwa katika insha nzima.
6. Mwili wa insha huhusu maelezo mapana ya kinacozungumziwa katika insha nzima.
7. Mwanafunzi anahitajika kaundika aya moja inayotoa muhtasari wa insha nzima. Funzo linalotokana na insha husika huandikwa hapa.
8. Nimejifundisha kuhusu sehemu kuu za insha pamoja na umuhimu wa kuwa na bidii maishani.

### Zoezi la msamiati, ukurasa 108

Mwalimu atathmini maelezo yatakayotolewa na wanafunzi. Sharti maelezo hayo yawe sahihi kisarufi. **Kwa mfano:**

*1.* ***mpole*** *– mtulivu*
*2.* ***uandishi*** *– shughuli ya kuandika*

### Zoezi la 13.1A, ukurasa 108

Mwalimu atathmini maelezo ambayo wanafunzi watatoa kwa msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi walizopewa. Sharti maelezo hayo yawe sahihi kisarufi na yalingane na muktadha wa matumizi yake.

***Kwa mfano:***

1. ***somo*** **-** maarifa maalumu ambayo hufundishwa shuleni
2. ***insha*** **-** mtungo ulioandikwa kwa lugha ya mjazo kuhusu tukio au kitu fulani
3. ***utangulizi*** **-** mwanzo
4. ***mwili wa insha*** **-** sehemu ya mtungo (insha) inayobeba ujumbe kamili wa mtungo huo
5. ***hitimisho*** **-** mwisho
6. ***masimullizi*** **-** maelezo (usimuliaji) wa jambo au tukio

### Zoezi la 13.1B, ukurasa 108

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti sentensi hizo ziwe sahihi kisarufi na zihusishe msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi za zoezi la 1A.

***Kwa mfano:***

1. **Somo** letu la Kiswahili limeanza.
2. Kesho nitaandika **insha** juu ya umuhimu wa elimu.
3. **Utangulizi** wa hadithi kuhusu sungura na fisi ni wa kusisimua.
4. Mwalimu alitueleza kuwa **mwili wa insha** hubeba ujumbe wote kuhusu mada ya insha.
5. Mwanafunzi bora alitumia methali katika **hitimisho** la insha yake.
6. Ninayapenda **masimulizi** ya babu.

### Zoezi la matumizi ya lugha, ukurasa 109

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi. Wanafunzi wajadili kuhusu maswali waliyopewa kwa kutoa majibu kama vile:

1. Mada ya insha huhusu kutambulisha jambo litakalozungumziwa katika insha nzima.
2. Utangulizi wa insha huhusisha kueleza tu kwa mdokezo ujumbe wa insha nzima.
3. Mwili wa insha huhusu ujumbe wa insha.
4. Hitimisho huandikwa kwa aya moja tu kwa kufupisha ujumbe wa insha.
5. Lugha rasmi, inayovutia na iliyo sahihi kisarufi hutumiwa.

### Zoezi la imla, ukurasa 110

Mwalimu awasomee wanafunzi sentensi hizi kwa sauti na matamshi sahihi:

1. *Utangulizi ndio kioo ca insha.*
2. *Lugha ya Kiswahili ina wazungumzaji wengi.*
3. *Mwili wa insha ni sehemu muhimu sana katika uandishi wa insha.*
4. *Mwisho wa insha unafaa kuvutia sana.*
5. *Insha iliyopambwa humvutia msomaji.*

### Zoezi la sarufi, ukurasa 110

Mwalimu atathmini maneno ambayo wanafunzi wataorodhesha. Sharti yawe katika ngeli ya U-ZI na yawe yametumika katika kifungu walicosoma hapo awali.

***Kwa mfano:***

1. Kuta
2. Uso
3. Fagio
4. Ufunguo
5. Nyimbo

Baadaye, mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe maneno ya ngeli ya U-ZI yaliyoorodheshwa hapo juu kutoka kwenye kifungu walicosoma hapo awali.

**Mifano ya sentensi katika umoja na wingi:**

1. *Ukuta wa darasa umebomoka.*
   *Kuta za madarasa zimebomoka.*
2. *Uso wangu unang'aa.*
   *Nyuso zetu zinang'aa.*
3. *Ufagio umepotea.*
   *Fagio zimepotea.*
4. *Ufunguo wa mlango ulivunjika.*
   *Funguo za milango zilivunjika.*
5. *Mwanafunzi aliimba wimbo mzuri.*
   *Wanafunzi waliimba nyimbo nzuri.*

**A. Zoezi la kukanusha, ukurasa 112**

1. Ulimi wake haujapona.
2. Upanga huu hautatumiwa kukatia muwa.
3. Uzi wangu haujakatika.
4. Ukuca wako haujaumia.
5. Wimbo mrefu hautaimbwa na wanafunzi.

**B. Sentensi za A katika wingi, ukurasa 112**

1. Ndimi zao hazijapona.
2. Panga hizi hazitatumiwa kukatia miwa.
3. Nyuzi zetu hazijakatika.
4. Kuca zenu hazijaumia.
5. Nyimbo ndefu hazitaimbwa na wanafunzi.

**Zoezi la 13.2, ukurasa 112**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga kwa kutumia majina waliyopewa katika umoja na wingi, hali yakinishi. Sharti sentensi hizo ziwe sahihi kisarufi.

***Kwa mfano:***

1. ***Umoja:*** Ukurasa wa kitabu cangu umelowa maji.

   ***Wingi:*** Kurasa za vitabu vyetu zimelowa maji.
2. ***Umoja:*** Udevu wa baba umekuwa mrefu.

   ***Wingi:*** Ndevu za baba zimekuwa ndefu.
3. ***Umoja:*** Wakati wa jua kali umeanza.

***Wingi:*** Nyakati za jua kali zimeanza.

4. ***Umoja:*** Wembe alionunua umepotea.

   ***Wingi:*** Nyembe walizonunua zimepotea.

5. ***Umoja:*** Upanga wa kukatia muwa umenolewa.

   ***Wingi:*** Panga za kukatia miwa zimenolewa.

6. ***Umoja:*** Ulimi wa mtoto una kidonda.

   ***Wingi:*** Ndimi za watoto zina vidonda.

**Zoezi la 13.3, ukurasa 112**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watakanusha kwa kutumia sentensi watakazotunga katika zoezi la 2 hapo juu. Sharti sentensi hizo ziwe sahihi kisarufi.

***Kwa mfano:***

1. ***Umoja:*** Ukurasa wa kitabu cangu haujalowa maji.

   ***Wingi:*** Kurasa za vitabu vyetu hazijalowa maji

2. ***Umoja:*** Udevu wa baba haujakuwa mrefu.

   ***Wingi:*** Ndevu za baba hazijakuwa ndefu.

3. ***Umoja:*** Wakati wa jua kali haujaanza.

   ***Wingi:*** Nyakati za jua kali hazijaanza.

4. ***Umoja:*** Wembe alionunua haujapotea.

   ***Wingi:*** Nyembe walizonunua hazijapotea.

5. ***Umoja:*** Upanga wa kukatia muwa haujanolewa.

   ***Wingi:*** Panga za kukatia miwa hazijanolewa.

6. ***Umoja:*** Ulimi wa mtoto hauna kidonda.

   ***Wingi:*** Ndimi za watoto hazina vidonda.

**Zoezi la 13.4, ukurasa 114**

a) mzuri
b) mweupe
c) mpya
d) mweusi
e) ndefu

**Zoezi la 13.5, ukurasa 114**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi na zitumie vivumishi vya sifa vilivyoorodheshwa pamoja na majina katika ngeli ya U-ZI.

***Kwa mfano:***

1. Uso mcafu ulisafishwa.
2. Uteo safi utaweka nafaka.
3. Nyuzi nyeusi zimekatwa.
4. Ufagio mkubwa ulinunuliwa.
5. Uwanja mdogo hautacezewa kandanda.

## Somo la 14: Mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha

### Kipindi cha 5: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati

**a) Malengo ya somo**

- Kusoma kwa usahihi kifungu ca habari kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;
- Kutambua maendelezo sahihi ya msamiati husika;
- Kutaja mambo muhimu ya kuzingatia katika kuandika insha kwa ujumla.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 115-118;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Somo hili linahusu kifungu ca habari kuhusu malezi bora kwa Mutesi. Mwalimu aandae vifaa vitakavyohitajika kufunzia somo hili kama vilivyobainishwa hapo juu. Katika kufanikisha somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila zoezi linalohusika.

## d) Utaratibu wa somo

### Utangulizi

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi wake na kuwauliza maswali kuhusu somo lililopita. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kusahihisha mazoezi waliyopewa. Baadaye, mwalimu aendelee na somo kwa kuwaomba wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili watazame micoro iliyo kwenye *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 115. Mwalimu awacangamshe wanafunzi wake kwa kuwauliza maswali kuhusu micoro hiyo.

Kwa mfano: *Mnaona nini kwenye micoro hiyo?* Mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kuhusu namna ya kujibu swali waliloulizwa kwa kuwapa kitangulizi kama vile *"mimi ninaona…."* Baadaye, mwalimu aendelee na somo kwa kuwauliza wanafunzi waeleze kinacoendelea katika micoro husika. Kwa mfano, anaweza kuuliza: *"Mutesi anafanya nini?"* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu wao. Kwa mfano, *Mutesi anafagia*. Katika sehemu hii, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi wake ili wapate ujuzi kuhusu tafakuri tunduizi, ubunifu na ugunduzi kwa kuwaonyesha mcoro husika huku wanafunzi nao wakifikiri na kugundua kile kinacoendelea katika mcoro huo.

### 14.1 Kusoma na ufahamu: Kifungu kuhusu malezi bora

Mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa kimya kifungu ca habari kuhusu malezi bora huku wakiandika msamiati mpya wanaopatana nao. Wanafunzi wasome kwa kimya huku wakiandika msamiati huo mpya. Hatimaye, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu kifungu walicosoma ili kuhakikisha kuwa wamekielewa. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuuliza: *Kwa nini ni jukumu la kila mzazi kumlea mtoto wake?* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika kifungu ca habari husika. Kwa mfano: *Kila mtoto hukua kwa kuziiga na kuzifuata tabia za watu wanaomlea*. Baada ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wamesoma kwa kimya kifungu kilicopo, mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa sauti kifungu hico kwa kuhakikisha kuwa wanasoma kwa namna na matamshi yanayofaa. Mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali hayo ya msamiati huku akitoa maelezo pale ambapo wanafunzi wanatatizika. Mwalimu awasaidie wanafunzi wenye matatizo ya kuelewa msamiati uliotumika katika kifungu hico.

Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kujibu maswali ya ufahamu pamoja na maswali ya uhakiki yaliyo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 116.

### 14.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu uandishi wa insha

Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kuwaomba watafute maana za msamiati mpya kwa jinsi ulivyotumiwa katika kifungu ca habari walicosoma. Mwalimu awaombe wanafunzi watumie kamusi ya Kiswahili pale wanapohitaji. Mwalimu azunguke darasani akiwaelekeza wanafunzi wanaopata taabu katika kuitumia kamusi hiyo. Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma sentensi walizopewa na kujadiliana kuhusu maana za msamiati uliopigiwa mistari. Kisha wanafunzi watunge sentensi zao wenyewe kwa kutumia msamiati huo. Ni vyema mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia na kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika. Baada ya wanafunzi hawa kukamilisha zoezi walilopewa, mwalimu awaombe wanafunzi kusahihisha kwa pamoja mazoezi hayo ya msamiati. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wameelewa msamiati uliokuwa mpya kwao, mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi wataje msamiati ambao hawakuelewa maana yake ili ujadiliwe kwa pamoja darasani kulingana na matumizi yake katika kifungu walicosoma. Ni vyema mwalimu azingatie kwamba utunzi wa sentensi za wanafunzi ndio utakaomfahamisha iwapo wanafunzi wamepata ujuzi unaotakikana katika tafakuri tunduizi, suluhisho kwa matatizo na mawasiliano kwa lugha rasmi.

### Tathmini ya kipindi ca 5

Mwalimu atathmini iwapo malengo ya kufundisha kuhusu uandishi wa insha yametimizwa.

## Kipindi cha 6: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza

**a) Malengo ya somo**

- Kutaja mambo ya kuzingatia katika kuandika insha kwa ujumla;
- Kujadili kuhusu vipengelee muhimu katika uandishi wa insha;
- Kuandika insha kwa kuzingatia sehemu zake kuu.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Insha mbalimbali zilizoandikwa kwa kuzingatia sehemu zake kuu;
- Wanafunzi wenyewe;

- Cati yenye umbo la sehemu za insha;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 118;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### c) Maandalizi ya somo

Katika maandalizi ya funzo hili, mwalimu atafute vifaa vitakavyoweza kurahisisha uelewa wa wanafunzi kama vile insha mbalimbali zilizoandikwa kwa kuzingatia sehemu zake kuu pamoja na mambo muhimu ambayo hufaa kuzingatiwa katika uandishi wa insha nzuri. Kupitia vifaa hivyo, mwalimu aandae maswali mbalimbali yatakayowacocea wanafunzi kutambua mambo muhimu ya kuzingatia katika kuandika insha nzuri ya kuvutia inayoweza kutuzwa alama nyingi.

### d) Utaratibu wa somo

**Utangulizi**

Mwalimu atangulize somo hili kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mepesi kuhusu waliyojifundisha katika kipindi kilicopita kuhusu sehemu kuu za insha. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika majadiliano haya. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu.

### 14.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha wajadiliane kuhusu mambo ambayo yanafaa kuzingatiwa katika uandishi wa insha. Wanafunzi waelezane kuhusu: *mwandiko safi wa insha, maendelezo sahihi ya maneno, urefu wa insha unaofaa, mapambo mbalimbali ya insha na mada mbalimbali za insha*. Mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao. Baada ya muda mfupi wa majadiliano, mwalimu awaombe wanafunzi wasome mambo waliyojadiliana. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kuelewa mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa insha. Majadiliano katika makundi yatasaidia kuelewa jambo hili.

Mwalimu awashirikishe wanafunzi kutambua mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa insha zao kama vile: *mwandiko safi, urefu unaofaa, maendelezo sahihi ya maneno, mapambo yanayofaa* n.k. Mwalimu awahimize wanafunzi kufanya mazoezi zaidi kuhusu namna ya kuandika kwa hati nzuri inayoweza kusomeka kwa urahisi.

### 14.4 Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha wajadili kuhusu namna ya kuandika insha bora. Baada ya wanafunzi kuandika insha hii, mwalimu ateue mwanafunzi mmoja mmoja kutoka kwa kila kundi asimame mbele ya wanafunzi wenzake na awasomee insha waliyoandika katika kundi lao. Mwalimu asahihishe makosa ya kimatamshi ya wanafunzi. Wanafunzi wapewe fursa ya kujadili insha watakazosomewa kwa kucunguza iwapo zimedhibiti mada waliyopewa pamoja na kuzingatia sehemu kuu za insha na mambo mengine muhimu ya kuzingatia katika kuandika insha nzuri.

### Tathmini ya kipindi ca 6

Mwalimu atathmini iwapo malengo ya kufundisha kuhusu uandishi wa insha yametimizwa.

## Kipindi cha 7: Sarufi – Ngeli ya U-ZI na vivumishi viashiria

**a) Malengo ya somo**

- Kutambua majina katika ngeli ya U-ZI;
- Kufahamu maana na mifano ya vivumishi viashiria;
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia majina katika ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi viashiria.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Micoro au pica zinazoonyesha vifaa vyenye majina katika ngeli ya U-ZI;
- Vifaa halisi vyenye majina katika ngeli ya U-ZI;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 118-120;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Katika maandalizi ya somo hili, mwalimu alenge kumsaidia mwanafunzi kubaini vivumishi viashiria katika lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, mwalimu atafute vifaa vya kutosha kufundishia somo hili kama vile: micoro au pica zinazoonyesha vifaa vyenye majina katika ngeli ya U-ZI pamoja na vifaa halisi vyenye majina

katika ngeli ya U-ZI. Ili kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wote, mwalimu afikirie wakati mwafaka wa kuonyesha vifaa hadharani na kuwatumia wanafunzi wenyewe kuelewa somo hili.

## d) Utaratibu wa somo

### Utangulizi

Katika utangulizi, mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali mepesi kuhusu kipindi kilicopita kuhusu sarufi ya vivumishi vya sifa, majina katika ngeli ya U-ZI pamoja na matumizi yake katika sentensi sahihi. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu aendelee kwa kuwashirikisha wanafunzi wote kusahihisha zoezi walilopewa katika kipindi kilicopita.

### 14.5 Sarufi: Ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi viashiria

Katika hatua hii, wanafunzi watapata fursa ya kufahamu majina yanayopatikana katika ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi viashiria. Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wanne wanne kisha awaelekeze kuitazama micoro iliyo katika *Kitabu ca Mwanafunzi* ukurasa 119 na kuiambatanisha na sentensi zilizo cini yao. Wanafunzi wasome sentensi hizo wakiziambatanisha na micoro inayozifaa. Wanafunzi wahakikishe kuwa kila sentensi inaambatana kwa usahihi na mcoro unaofaa. Katika micoro hii pamoja na sentensi husika, mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua kuwa kuna matumizi ya vivumishi viashiria vya mahali karibu na mzungumzaji, mahali mbali kidogo na mzungumzaji na mahali mbali sana na mzungumzaji.

Hatimaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kufanya zoezi la 14.5 ambapo wanafunzi wanafaa watumie majina ya ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi viashiria panapostahili. Katika hatua hii, mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wote wanashirikishwa kusahihisha mazoezi yaliyopo kwa kuwacocea kupata ujuzi ainasafu kama vile tafakuri tunduizi ambapo anaweza kuomba wanafunzi wengine kucunguza majibu yanayotolewa na wenzao.

Baada ya wanafunzi kuelewa matumizi ya vivumishi viashiria pamoja na majina katika ngeli ya U-ZI, mwalimu awaelekeze kuandika wingi wa sentensi za zoezi la 14.2 na kuzisahihisha. Baada ya haya, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kutunga sentensi zenye kutumia majina ya ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi viashiria. Mwalimu awasisitizie wanafunzi kuwa lazima kila sentensi kamili ianze kwa herufi kubwa na ikamilike kwa nukta. Kwa mfano: *Ukuta huu umekamilika kujengwa.; Kuta hizi zimekamilika kujengwa, n.k.*

## Tathmini ya kipindi ca 7

Mwalimu atathmini iwapo malengo ya kufundisha kuhusu uandishi wa insha yametimizwa.

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali hayo yaegemee hasa kwa kucunguza ikiwa wanafunzi wanaweza kutaja majina ambayo yanapatikana katika ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi viashiria vinavyoambatana na majina hayo.

**Maelezo muhimu kwa mwalimu**

Mwalimu awaeleze wanafunzi kuwa:

*Maneno ambayo hutumiwa kuonyesha umbali wa nomino huitwa **vivumishi viashiria**. Yaani, ni maneno yanayoashiria iliko nomino. Kuna umbali wa aina tatu:*

*a) Karibu na mzungumzaji. Kwa mfano: ukuta huu, uso huu, uzi huu n.k.*
*b) Mbali kidogo na mzungumzaji. Kwa mfano: Ukuta huo, uso huo, uzi huo n.k.*
*ch Mbali sana na mzungumzaji. Kwa mfano: Ukuta ule, uso ule, uzi ule n.k.*

*Vivumishi viashiria katika wingi hutegemea umbali wa nomino inayorejelewa:*

*a) Nomino ikiwa karibu na mzungumzaji katika umoja, kivumishi kiashiria kitakuwa 'huu' na katika wingi kitakuwa 'hizi'.*
*b) Nomino ikiwa mbali kidogo na mzungumzaji, katika umoja kivumishi kiashiria kitakuwa 'huo' na katika wingi kitakuwa 'hizo'.*
*ch) Nomino ikiwa mbali sana na mzungumzaji, katika umoja kivumishi kiashiria kitakuwa 'ule' na katika wingi kitakuwa 'zile'.*

## 14.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atoe zoezi la ziada lifuatalo ambalo linalenga kuinua kiwango ca cini kwa wanafunzi wasioweza kuelewa kwa haraka kama wenzao.

*Tunga sentensi sahihi katika umoja na wingi kwa kutumia majina katika ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi viashiria vifuatavyo.*

1. huu
2. huo
3. ule
4. hizi

5. hizo
6. zile

***Kwa mfano:***

***Umoja:*** *Waraka huu umeandikwa na mwanafunzi.*

***Wingi:*** *Nyaraka hizi zimeandikwa na wanafunzi.*

**Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe majina katika ngeli ya U-ZI.

**ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka**

Kwa wanafunzi wenye kiwango ca juu ca uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge kisa kifupi kitakacohusisha majina katika ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi viashiria.

***Kwa mfano:***

*Darasa letu lina **kuta** zilizopakwa rangi ya manjano. **Kuta hizi** husafishwa kila Ijumaa. Sisi hulifagia darasa letu kila siku asubuhi kwa kutumia **fagio hizi** ndefu. Baada ya kulifagia, sisi hukusanyika kwenye eneo la gwaride na kuimba **wimbo** wa taifa. **Wimbo huu** hutuhimiza kuzidi kuwa wazalendo wa nci yetu.*

**Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka**

Mwalimu atathmini visa ambavyo wanafunzi watatunga. Sharti visa hivyo vihusishe sentensi sahihi zilizotumia majina katika ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi viashiria.

## 14.7 Majibu

**Zoezi la makundi, ukurasa 115**

Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi kwa kurejelea micoro iliyopo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 115.

**Kwa mfano:**

*Micoro inaonyesha mama akiosha vyombo, baba akikama ng'ombe na mvulana mmoja (mtoto wao) akifagia. Haya yanaonyesha malezi mema ambapo watu wa familia moja wanasaidiana kutekeleza majukumu ya nyumbani.*

**Maswali ya ufahamu, ukurasa 116**

1. Wazazi wa Mutesi ni wenye bidii.

2. Mutesi ameiga tabia ya kutia bidii katika masomo yake, kuamka mapema na kuwasaidia wazazi wake kazi.
3. Kuielewa mada, kubuni kisa cocote akilini kuhusiana na mada hiyo na kutiririsha kisa kutoka mwanzo hadi mwisho kwa kutumia aya, kuandika kwa mwandiko bora, kuepuka makosa ya maendelezo na kuzingatia urefu unaofaa.
4. Malezi bora ni kumlea mtoto kwa njia zinazokubalika na zinazofaa katika jamii.
5. Nimejifunza kuwa watoto huiga tabia za wazazi wao. Pia, kuna mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kuandika insha. Mambo haya ni pamoja na: kuandika kwa hati bora, kutumia aya wakati wa kuandika kisa, kuelewa mada inayostahili kuandikiwa insha na kuepuka makosa ya maendelezo na kisarufi.

**Maswali ya uhakiki, ukurasa 116**

1. Kifungu kina aya nne (4).
2. Watu waliozungumziwa ni: Mutesi, Byiringiro, Uwera na Ngabo.
3. Watu katika kifungu nilicosoma ni wenye bidii katika kazi zao.
4. Katika ***aya ya kwanza***, tunaelezwa kuwa malezi bora huanza mtoto anapozaliwa na kila mtoto huiga tabia za wazazi wake anapokua. ***Aya ya pili*** ina ujumbe kuwa wazazi wa Mutesi ni wenye bidii sana. Mama yake huamka mapema ili kuitayarishia familia yake kiamshakinywa. Baba yake naye huwakama ng'ombe. Mutesi halikadhalika huamka mapema na kuwasaidia wazazi wake kufagia, kupika na kuwafungulia ng'ombe zizini. Katika ***aya ya tatu***, Mutesi anaelezwa kama mwanafunzi ambaye huongoza katika masomo yote. Yeye pia hufanya marudio na Ngabo kuhusu jinsi ya kuandika insha bora. Pia, tunaelezwa kuhusu mambo ya kuzingatia katika kuandika insha. Katika ***aya ya mwisho***, wazazi wa Mutesi huhakikisha kuwa ameenda kanisani kwa kuwa wanafahamu umuhimu wa kumca Mungu. Pia, tunaelezwa kuhusu maadili kwa Mutesi kushauriwa kusema asante, kuwakaribisha wageni na kutumia lugha yenye adabu.
5. Aya ya kwanza ni ya utangulizi, aya za pili na tatu ni za mwili wa insha na aya ya nne ni hitimisho la insha.

**Zoezi la msamiati, ukurasa 117**

Mwalimu atathmini maelezo ya msamiati ambayo wanafunzi watatoa. Ahakikishe kuwa ni sahihi kisarufi na yamezingatia maneno yaliyotumika katika kifungu walicokisoma.

***Kwa mfano:***

1. ***Malezi*** - *namna ya kumlea mtoto kwa taratibu zinazokubalika katika jamii*
2. ***Zizini*** - *mahali wanapolala ng'ombe*

### Zoezi la 14.1A, ukurasa 117

Mwalimu atathmini maelezo ambayo wanafunzi watatoa kwa msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi walizopewa. Sharti maelezo hayo yawe sahihi kisarufi na yalingane na muktadha wa matumizi yake.

**Kwa mfano:**

1. ***aya*** - fungu la maneno lenye maana au ujumbe kamili
2. ***mada*** - anwani au kicwa ca insha
3. ***ubuni*** - utunge
4. ***kutiririka*** - kufuatana kwa mtiririko au mfuatano fulani
5. ***mwandiko*** - namna ya uandikaji wa mtu; hati
6. ***maendelezo*** - namna ya utaratibu wa kuandika maneno
7. ***malezi*** - namna ya kumlea mtoto kwa taratibu zinazokubalika katika jamii
8. ***aliziiga*** - alizifuata

### Zoezi la 14.1B, ukurasa 117

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zizingatie matumizi ya maneno waliyotolea maana katika zoezi la 1A hapo juu.

***Kwa mfano:***

*1. Insha yangu ina **aya** sita pekee.*

*2. Mwalimu alituambia tujicagulie **mada** ya kuandikia insha.*

### Zoezi la matumizi ya lugha, ukurasa 118

Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha awape fursa ya kujadiliana kuhusu mambo ambayo yameorodheshwa vitabuni mwao. Ahakikishe kuwa wanazingatia mambo hayo na wanatumia lugha sanifu katika majadiliano yao.

### Zoezi la kusikiliza na kuzungumza, ukurasa 118

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika majadiliano yao kuhusu namna ya kuandika insha bora. Sharti wanafunzi waweze kurejelea hoja muhimu kuhusu

mambo ya kuzingatia wakati wa kuandika insha. Hoja hizi zinapatikana katika kifungu walicosoma.

**Zoezi la sarufi, ukurasa 118 - 119**

Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kutazama micoro waliyopewa na kuilinganisha kwa usahihi na sentensi walizopewa. Wanafunzi wataweza kuelewa matumizi ya vivumishi viashiria mbalimbali.

**Zoezi la 14.2, ukurasa 120**

1. Kuta hizi zimekamilika kujengwa.
2. Nyuso hizo zina vidonda.
3. Fagio zile zimetumika kwa muda mrefu.
4. Nyuzi hizi zinahitajika na kina mama.
5. Nyimbo hizo zinavutia.
6. Nyembe zile ziliwakata watoto.

**Zoezi la 14.3, ukurasa 121**

1. Ukurasa huu umelowa maji.
2. Ukuca huu utakatwa.
3. Ufunguo huo ni wa nyumba ya mwalimu wangu.
4. Upanga huu utatumika shambani.
5. Wimbo huo unaimbwa vizuri sana.

**Zoezi la 14.4, ukurasa 121**

1. ule
2. hizo
3. zile
4. huu
5. zile

**Zoezi la 14.5, ukurasa 121**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga.

**Kwa mfano:**

1. *Wimbo ulioimbwa ni mzuri.*
2. *Waraka alioniandikia ulinifika jana.*
3. *Ukuta wa nyumba yao umepakwa rangi.*
4. *Udevu wa baba umekatwa.*
5. *Unywele wa mtoto umekatwa kwa makasi.*

# Somo la 15: Aina mbalimbali za insha

## Kipindi cha 8: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati

**a) Malengo ya somo**

- Kusoma kwa usahihi kifungu ca habari kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;
- Kutambua umuhimu wa adabu katika maisha ya binadamu.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Masimulizi yaliyorekodiwa kuhusu umuhimu wa adabu;
- Micoro iliyo kwenye kitabu ca mwanafunzi;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 122-124;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.)

**b) Maandalizi ya somo**

Somo hili linahusisha kifungu ca habari kuhusu umuhimu wa adabu katika maisha ya Mutoni. Mwalimu aandae vifaa vitakavyohitajika kufunzia somo hili kama vilivyobainishwa hapo juu. Mwalimu anaweza kuandaa masimulizi kuhusu umuhimu wa adabu ambayo atawasomea wanafunzi darasani. Masimulizi haya yatamsaidia sana mwalimu katika kuwapa wanafunzi uzoefu wa kuwa na adabu. Katika kufanikisha somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakiwa kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila zoezi linalohusika.

**c) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake na kuwauliza maswali kuhusu somo lililopita. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu wao. Pia wanafunzi wajibu maswali waliyoulizwa na mwalimu wao. Baadaye, mwalimu acukue fursa hii kuomba wanafunzi wasahihishe zoezi walilopewa wakati wa somo lililopita ili waweze kuendelea na somo jipya. Baada ya haya, mwalimu awacangamshe wanafunzi wake kwa kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu micoro iliyo katika

*Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 122. Kwa mfano mwalimu anaweza kuuliza: *Mnaona nini kwenye micoro hii?* Mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kuhusu namna ya kujibu maswali waliyoulizwa kwa kuwapa kitangulizi kama vile *“mimi ninaona...”* Kwa mfano: *Mimi ninaona baba*. Katika hatua hii, ni lazima mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kupata ujuzi kuhusu tafakuri tunduizi huku akiwasaidia kuwasiliana kwa lugha rasmi na sahihi.

### 15.1 Kusoma na ufahamu: Kifungu kuhusu umuhimu wa adabu

Mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa kimya kifungu ca habari kuhusu umuhimu wa adabu huku wakiandika msamiati mpya wanaokutana nao. Hivyo basi, wanafunzi wasome kwa kimya pamoja na kuandika msamiati huo mpya. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wamesoma kwa kimya kama walivyoambiwa, mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu kifungu ca habari kilicopo. Kwa mfano, anaweza kuuliza swali lifuatalo: *Baba anafanya nini? Kwa nini mama amelala?* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika kifungu hico. Kwa mfano: *Mama amelala kwa sababu yeye ni mgonjwa*. Baada ya kupata pica ya uelewa wa jumla wa wanafunzi kuhusu kifungu ca habari kinacohusika, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa sauti kifungu hico. Wanafunzi wasome kwa sauti kama walivyoambiwa na mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa kwa lengo la kutambua herufi, silabi na sentensi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kujibu maswali ya kifungu ca habari walicosoma.Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali hayo huku akitoa maelezo yake kwa kutilia mkazo pale ambapo wanafunzi wanatatizika. Wanafunzi pia waelekezwe kujibu maswali ya uhakiki waliyopewa vitabuni mwao.

### 15.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusiana na umuhimu wa adabu

Mwalimu atoe maelekezo kuhusu namna ya kutafuta maana za msamiati mpya ulioorodheshwa na wanafunzi wakati wao wa kusoma kifungu ca habari kilicopo. Mwalimu awaombe wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi wawili wawili na kujadiliana kuhusu msamiati huo. Wanafunzi wazingatie matumizi ya msamiati huo katika kifungu kilicopo. Wanafunzi wanaweza kujadili msamiati huo huku wakitumia kamusi pale panapohitajika. Mwalimu azunguke darasani huku akiwasaidia wanafunzi na kuwaelekeza pale wanapotatizika. Hatimaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi kufanya zoezi la 15.1A la msamiati kwa kuwafafanulia kile kinacotakiwa kutimizwa katika zoezi hilo. Mwalimu awaombe wanafunzi kucunguza maana ya maneno yaliyopigiwa mistari na kuihusisha

na sentensi zilizopo huku akiwatolea mfano. Wanafunzi wajibu zoezi hilo kama walivyoelekezwa na mwalimu na kulisahihisha mara moja wanapolimaliza. Katika zoezi la 15.1B, mwalimu awaombe wanafunzi watunge sentensi sahihi kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mistari katika zoezi la 15.1A.

Isitoshe, ni lazima mwalimu azingatie kwamba wanafunzi wanatakiwa kurejelea matumizi ya msamiati husika katika kifungu ca mazungumzo walicokisoma ili kuelewa zaidi.

**Tathmini ya kipindi ca 8**

Mwalimu alenge kutambua ikiwa ujifundishaji umefanywa kwa namna ya kuridhisha. Kwa hivyo, apime uwezo wa wanafunzi kupitia maswali mbalimbali kuhusiana na utambuzi wa umuhimu wa adabu, matumizi ya msamiati waliojifunza katika sentensi fupifupi na hata matumizi ya msamiati huo katika maongezi yao nje ya darasa. Mwalimu awazoeshe wanafunzi wake kunyosha mkono kila wakati mwanafunzi anapotaka kuuliza au kujibu swali kwa kuonyesha mienendo ya kuwa na adabu shuleni.

## Kipindi cha 9: Matumizi ya lugha

### a) Malengo ya somo

- Kusoma kwa usahihi aina mbalimbali za insha zilizopo kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;
- Kutaja aina mbalimbali za insha;
- Kuandika aina mbalimbali za insha kwa utaratibu unaofaa.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Cati zenye mifano ya insha mbalimbali;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 124-127;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.)

### c) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu matumizi ya lugha kuhusiana na aina mbalimbali za insha. Mwalimu aandae cati zenye mifano ya insha mbalimbali pamoja na kuonyesha miundo yao kwa ajili ya kufundishia somo hili. Mwalimu anaweza kuandaa insha kadhaa au hata akazirekodi ili kuwasomea wanafunzi darasani au kuwawekea wakazisikiliza. Ili kufanikisha somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa amewagawa wanafunzi katika makundi yanayotakikana kwa kila zoezi husika.

### d) Utaratibu wa somo

### Utangulizi

Mwalimu aanze kipindi hiki kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kuhusiana na somo lililopita kuhusu mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa insha zinazokubalika na zilizo nzuri. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofunzwa katika kipindi kilicotangulia.

### 15.3 Matumizi ya lugha: Mifano ya insha

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wanne wanne kisha wasome na kujadiliana kuhusu mfano wa *insha ya wasifu* wa baba na mfano wa *insha ya mazungumzo* kati ya daktari na mgonjwa waliyopewa. Mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao. Baada ya muda mfupi wa majadiliano mwalimu anaweza kuwacagua wanafunzi kadhaa kutoka katika makundi mbalimbali wasome mifano hiyo ya aina mbalimbali za insha mbele ya wanafunzi wengine na kuwaomba wanafunzi waelezane ugunduzi wao. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kuelewa namna ya kuandika aina mbalimbali za insha kama vile: *insha ya wasifu* na *insha ya mazungumzo.* Majadiliano katika makundi yatasaidia kuelewa jambo hili. Wanafunzi waelekezwe kuelewa sehemu kuu za aina mbalimbali za insha walizosoma.

Mwalimu awahimize wanafunzi wafanye mazoezi zaidi kuhusu namna ya kuandika insha ya wasifu pamoja na insha ya mazungumzo katika makundi yao. Baada ya kupata uzoefu, mwanafunzi anaweza kuandika insha nyingine anazozifahamu kwa kujitegemea.

**Tathmini ya kipindi ca 9**

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali haya yatamsaidia mwalimu kudhibitisha iwapo wanafunzi wanaweza kutaja aina mbalimbali za insha na namna ya kuziandika kwa kuzingatia sehemu kuu za insha na mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wao.

## Kipindi cha 10: Kusikiliza na kuzungumza

**a) Malengo ya somo**

- Kujadili aina mbalimbali za insha;
- Kueleza utaratibu wa kuandika aina mbalimbali za insha.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Wanafunzi wenyewe;
- Aina mbalimbali za insha zilizoandikwa awali au kurekodiwa;
- Cati zenye mifano ya insha mbalimbali;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 127;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.)

**c) Maandalizi ya somo**

Mwalimu ahakikishe kuwa amewagawa wanafunzi wake katika makundi ya wanafunzi yanayotakikana. Mwalimu anaweza kutumia aina mbalimbali za insha alizoandika awali au alizorekodi kabla ya somo hili ili azitumie kuwafundishia wanafunzi na kuwaongoza kwa kuwapa mwelekeo kamili wa kuandika aina za insha walizopewa kwenye *Kitabu ca Mwanafunzi*. Mwalimu aandae somo kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu utaratibu wa kuzingatia katika uandishi wa insha husika ili mwanafunzi apate pica kamili ya insha nzuri na jinsi inavyofaa kuandikwa.

Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kufundishia somo hili ili kuwaelekeza wanafunzi ipasavyo katika uandishi wa insha watakazopewa katika makundi yao.

### d) Utaratibu wa somo

**Utangulizi**

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi ca 9. Wanafunzi wajibu maswali waliyoulizwa. Mwalimu atumie aina za insha alizoandaa kutanguliza funzo hili.

### 15.4 Kusikiliza na kuzungumza: Somo la imla

Katika sehemu hii, mwalimu awape wanafunzi zoezi la imla. Mwalimu awaombe wanafunzi wafungue madaftari yao na waandike sentensi zifuatazo ambazo mwalimu atawasomea.

1. *Insha ya wasifu huhusisha kueleza sifa za mtu au kitu.*
2. *Insha ya methali huhitaji makini kuiandika.*
3. *Insha ya maelezo hufafanua kitu, mtu au hali fulani.*
4. *Insha ya barua rasmi hutumia lugha rasmi.*
5. *Insha ya mazungumzo huhusisha wazungumzaji wawili au zaidi.*

Katika hatua hii, mwalimu ahakikishe kuwa anatamka maneno ya kila sentensi kwa ufasaha na kwa sauti ili kila mwanafunzi aweze kusikia na kuandika vizuri.

**Tathmini ya kipindi ca 10**

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mepesi yenye kucunguza uwezo wa wanafunzi wa kudhihirisha uwezo wao wa kuandika insha mbalimbali kwa kutilia mkazo mambo muhimu yanayozingatiwa kama vile: *sehemu kuu za insha, mwandiko unaosomeka, urefu unaokubalik*a na kadhalika.

## Kipindi cha 11: Sarufi (Ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vimilikishi)

### a) Malengo ya somo

- Kutambua majina katika ngeli ya U-ZI;
- Kufahamu maana na mifano ya vivumishi vimilikishi;
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia majina katika ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vimilikishi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Micoro au pica zinazoonyesha vifaa vyenye majina katika ngeli ya U-ZI;
- Vifaa halisi vyenye majina katika ngeli ya U-ZI;
- Wanafunzi wenyewe;

- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 128-130;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.)

### c) Maandalizi ya somo

Katika maandalizi ya somo hili, mwalimu alenge kumsaidia mwanafunzi kubaini maana na mifano ya vivumishi vimilikishi katika lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, mwalimu atafute vifaa vya kutosha kufundishia somo hili kama vile: micoro au pica zinazoonyesha vifaa vyenye majina katika ngeli ya U-ZI pamoja na vifaa halisi vyenye majina katika ngeli ya U-ZI. Ili kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wote, mwalimu afikirie wakati mwafaka wa kuonyesha vifaa vyake hadharani na kuwatumia wanafunzi wenyewe ili kuelewa somo hili.

## d) Utaratibu wa somo

### Utangulizi

Katika utangulizi, mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali mepesi kuhusu kipindi kilicopita kuhusu sarufi ya vivumishi viashiria, majina katika ngeli ya U-ZI pamoja na matumizi yake katika sentensi sahihi. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu aendelee kwa kuwashirikisha wanafunzi wote kusahihisha zoezi walilopewa katika kipindi kilicopita.

### 15.5 Sarufi: Ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vimilikishi

Katika hatua hii, wanafunzi watapata fursa ya kujikumbusha majina yanayopatikana katika ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vimilikishi. Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha awaelekeze kuitazama pica na micoro iliyo katika *Kitabu ca Mwanafunzi* ukurasa 128 na kuiambatanisha na sentensi zilizo cini ya pica na micoro hiyo. Wanafunzi wasome sentensi hizo wakiziambatanisha na pica na micoro inayozifaa. Wanafunzi wahakikishe kuwa kila sentensi inaambatana kwa usahihi na pica au mcoro unaofaa. Katika pica na micoro hii pamoja na sentensi husika, mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua kuwa kuna matumizi ya vivumishi vimilikishi katika umoja na wingi na katika nafsi tatu.

Mwalimu awaombe wanafunzi wataje mifano ya majina katika ngeli ya U-ZI kama vile: *ukuta, uso, uzi, wimbo, wembe, udevu, ufagio, ufunguo, ufito* n.k. Wanafunzi waelekezwe katika kutambua wingi wa majina haya yote ambayo ni: *kuta, nyuso, nyuzi, nyimbo, nyembe, ndevu, fagio, funguo, fito* n.k. Baada ya haya,

mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kutunga sentensi zenye majina katika ngeli ya U-ZI katika umoja na wingi kwa usahihi.

Hatimaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kufanya zoezi la 15.2 na zoezi la 15.3 ambapo wanafunzi wanafaa watumie majina ya ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vimilikishi panapostahili. Katika hatua hii, mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wote wanashirikishwa kusahihisha mazoezi yaliyopo kwa kuwacocea kupata ujuzi ainasafu kama vile tafakuri tunduizi ambapo anaweza kuomba wanafunzi wengine kucunguza majibu yanayotolewa na wenzao.

Baada ya wanafunzi kuelewa matumizi ya vivumishi vimilikishi pamoja na majina katika ngeli ya U-ZI, mwalimu awaelekeze katika kutunga sentensi zenye kutumia majina ya ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vimilikishi. Mwalimu awasisitizie wanafunzi kuwa lazima kila sentensi kamili ianze kwa herufi kubwa na ikamilike kwa nukta. Kwa mfano: *<u>Uso wangu</u> umeumia.; <u>Nyuso zetu</u> zimeumia. n.k.*

## Tathmini ya kipindi ca 11

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali hayo yaegemee hasa katika kucunguza ikiwa wanafunzi wanaweza kutaja majina ambayo yanapatikana katika ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vimilikishi vinavyoambatana na majina hayo. Wanafunzi pia waweze kutunga sentensi sahihi kwa kutumia majina katika ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vimilikishi kwa usahihi.

## Maelezo muhimu kwa mwalimu

Mwalimu awaeleze wanafunzi kuwa:

*Maneno ambayo hutumiwa kuonyesha mtu, kitu au hali fulani inamilikiwa na nani huitwa vivumishi vimilikishi. Vivumishi vimilikishi hutegemea nafsi tatu katika lugha ya Kiswahili ambazo ni:*

| | |
|---|---|
| *1. Nafsi ya kwanza (Mimi – Sisi):* | *Uso wangu umeumia. (umoja)* |
| | *Nyuso zetu zimeumia. (wingi)* |
| *2. Nafsi ya pili (Wewe – Nyinyi):* | *Uso wako umeumia. (umoja)* |
| | *Nyuso zenu zimeumia. (wingi)* |
| *3. Nafsi ya tatu (Yeye – Wao);* | *Uso wake umeumia. (umoja)* |
| | *Nyuso zao zimeumia. (wingi)* |

*Vivumishi vimilikishi ni:* ***-angu, -etu, -ako, -enu, -ake na -ao.***

*Vivumishi hivi vinatumia '**w**' katika umoja na '**z**' katika wingi (wangu, wako, wake, zetu, zenu, zao).*

### 15.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Ili kuwasadia wanafunzi wa kiwango ca cini katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe wanafunzi hawa kutunga na kuandika sentensi tano zinazoonyesha matumizi sahihi ya vivumishi vimilikishi pamoja na majina katika ngeli ya U-ZI. Mwalimu awape mfano wa sentensi na awaelekeze kwa kile wanacotakiwa kufanya.

***Kwa mfano:***

*1. <u>Ufunguo wake</u> umepotea. – <u>Funguo zao</u> zimepotea.*

*2. <u>Ukuca wako</u> utakatika. – <u>Kuca zenu</u> zitakatika.*

### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi na zihusishe majina katika ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vimilikishi.

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango ca juu ca uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge aya moja ya masimulizi yatakayohusisha majina katika ngeli uya U-ZI pamoja na vivumishi vimilikishi.

**Kwa mfano:** ***Uso wangu*** *ulikuwa umeumia sana. Nilikuwa nimeanguka cini na kugongwa na* ***ufagio wao*** *uliokuwa karibu na* ***ukuta wetu****. Nilihisi maumivu sana. Hata* ***kuca zangu*** *ziliumia sana.*

# 15.7 Majibu

**Zoezi la makundi, ukurasa 122**

Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi kwa kurejelea micoro iliyopo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 122.

**Kwa mfano:**

*Micoro hii inaonyesha msicana anayetoka katika familia maskini. Babake ana ulemavu mguuni na mama yake ni mgonjwa. Lica ya yote haya, msicana huyu anapata elimu.*

**Maswali ya ufahamu, ukurasa 123**

1. Mutoni ni mtiifu, mpole na mwenye bidii katika masomo yake.
2. Familia ya Mutoni inapitia hali ngumu kimaisha kwa sababu wazazi wake wana uwezo mdogo wa kukidhi mahitaji yake ya karo, cakula pamoja na kutimiza mahitaji mengine ya nyumbani.
3. Mwalimu aliamua kumfadhili Mutoni kwa sababu Mutoni hakuwa na uwezo wa kununua vitabu na sare ya shule.
4. Wanafunzi walimpenda Mutoni kwa sababu yeye alipenda kuwasaidia wanafunzi wenzake katika masomo yao.
5. Kozi ambayo Mutoni alifanya cuoni ilimpa uwezo wa kuwatibu na kuwatunza wazazi wake. Pia aliweza kuwajengea nyumba nzuri na kuajiri wafanyakazi wa kuwasaidia wazazi wake.

**Maswali ya uhakiki, ukurasa 123**

1. Mada ya insha inahusiana na insha nzima kupitia kwa mafanikio ya Mutoni katika masomo yake na hatimaye kupata kazi yaliyotokana na adabu aliyokuwa nayo. Adabu aliyokuwa nayo kwa walimu wake inamsaidia kupata ufadhili katika masomo hadi anapopata kazi nzuri baada ya cuo kikuu. (*Mwalimu atathmini namna wanafunzi wataeleza hoja zao*).

2. Kwanza, kuna maelezo kuhusu hali ya kimaisha ya Mutoni na familia yake. Tunaambiwa kuwa waliishi katika hali ngumu ya kutoweza kujikimu kutokana na ulemavu wa babake na ugonjwa wa mamake. Pili, tunaelezwa kuhusu sifa za Mutoni. Yeye ni mwenye bidii, mtiifu na mpole. Tabia yake inapelekea wanafunzi wenzake kumpenda sana. Mbali na kuwa Mutoni ana sifa hizo, yeye hawezi kujinunulia vitabu na sare ya shule. Mwalimu wake anamnunulia na kuahidi kumfadhili iwapo atapita mtihani wake. Mutoni anaupita mtihani wake na kufadhiliwa masomoni hadi cuo kikuu na baadaye anapata kazi katika hospitali mojawapo.
3. Mawazo ya swali hili ni hayo yaliyoelezwa katika nambari 2. Mwalimu atathmini namna wanafunzi wataandika mawazo hayo kimuhtasari.

### Zoezi la msamiati, ukurasa 123

Mwalimu atathmini maelezo ya msamiati ambayo yatatolewa na wanafunzi katika makundi yao. Sharti yahusishe maneno waliyosoma katika kifungu husika.

***Kwa mfano:***

1. ***mwanafunzi*** - mtu ambaye anajifundisha elimu au maarifa fulani
2. ***kisukari*** - ugonjwa unaotokana na mwili kushindwa kudhibiti kiwango ca sukari kwenye damu

### Zoezi la 15.1A, ukurasa 124

Mwalimu atathmini maelezo watakayotoa wanafunzi. Sharti yawe sahihi kisarufi.

***Kwa mfano:***

1. ***kidato ca tatu*** - darasa la tatu katika kiwango ca sekondari
2. ***karo*** - malipo yanayotolewa ili kupata mafunzo au maarifa fulani
3. ***mahitaji*** - jumla ya vitu muhimu kwa ajili ya kutimiza haja ya mtu
4. ***kijiji duni*** - sehemu yenye hali mbaya ya kimaisha kwa watu wanaoishi hapo
5. ***mpole*** - mwenye utulivu
6. ***kiranja mkuu*** - mwanafunzi anayetwikwa jukumu la kuwa kiongozi miongoni mwa wanafunzi na mwenye majukumu ya juu zaidi ya viongozi wengine shuleni
7. ***sare*** - mavazi yanayofanana na ambayo huvaliwa na wanafunzi
8. ***ufadhili*** - usaidizi wa kifedha
9. ***udaktari*** - kozi ya kuwafundisha watu kuwa madaktari

**Zoezi la 15.1B, ukurasa 124**

Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi. Sharti sentensi hizo zitumie maneno yaliyoelezewa katika zoezi la 1A hapo juu.

***Kwa mfano:***

1. *Gasore yuko katika **kidato ca tatu**.*
2. *Kalisa alilipiwa **karo** yake Ijumaa.*
3. ***Mahitaji** ya mwanafunzi yametimizwa.*
4. *Wananci walisafisha **kijiji duni** cao.*
5. *Mwalimu wetu wa Kiswahili ni **mpole**.*
6. ***Kiranja mkuu** katika shule yetu ametuzwa.*
7. *Wanafunzi wamevaa **sare** nzuri sana.*
8. *Neza alipata **ufadhili** wa masomo yake.*
9. *Kozi ya **udaktari** cuoni ina wanafunzi wengi.*

**Maswali ya uhakiki, ukurasa 125**

1. Ni insha ya wasifu kwa sababu inatoa ufafanuzi wa tabia na mienendo ya baba (John Mugabo).
2. Mambo ya kuzingatia katika kuandika insha za aina hii ni: maelezo ya tabia, hali na maumbile ya mtu anayefafanuliwa.
3. Baba yangu
4. Ni mrefu, mwenye rangi ya ngozi ya maji ya kunde, ana maco mazuri na nywele nyingi nyeusi kicwani.
5. Yeye ni mkarimu, hupenda kuwasaidia watu walio na matatizo mbalimbali, ni mpole, ni mceshi na mwenye heshima kwa wengine.
6. Kwa sababu ya sifa zake nzuri.
7. Yeye huamka asubuhi na mapema kwenda kazini.

**Maswali ya uhakiki, ukurasa 127**

1. Insha ya mazungumzo
2. Katika kuandika insha ya mazungumzo, sharti pawepo na watu wanaozungumza kuhusu jambo fulani mahususi.
3. Mazungumzo kati ya Mgonjwa na Daktari.
4. Wazungumzaji ni Daktari na Mgonjwa.
5. Daktari huwatibu wagonjwa mbalimbali.
6. Daktari anampa Kayitesi mikebe miwili ili amletee coo cake na mkojo ili apime na kutambua kinacomdhuru.
7. Kayitesi anaumwa na tumbo, anaendesha na kutapika sana.

**Zoezi la maigizo, ukurasa 127**

Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi yao na awape fursa ya kuigiza mazungumzo waliyosoma awali. Ahakikishe kuwa wanaigiza kwa kuzingatia matamshi bora ya maneno.

**Zoezi la kuandika, ukurasa 127**

Mwalimu atathmini maigizo ya wanafunzi baada ya kubuni mazungumzo kati ya mwalimu na mwanafunzi.

**Zoezi la imla, ukurasa 127**

Mwalimu awasomee wanafunzi sentensi zilizo kwenye ukurasa 222 kwa sauti na matamshi sahihi. Mwalimu akosoe makosa ya tahajia.

**Zoezi la 15.2, ukurasa 129**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti sentensi hizo ziwe sahihi kisarufi na zitumie maneno pamoja na vivumishi vimilikishi walivyopewa.

***Kwa mfano:***

1. *Mtoto alirarua **kurasa zetu** za vitabu.*
2. *Mwashi ataziba **ufa wako**.*
3. *Neza amecukua **nyuzi zenu**.*
4. ***Ufito wangu** utanifaa.*
5. *Mimi niliokota **nyembe zao**.*

**Zoezi la 15.3, ukurasa 130**

1. Mbao zao zimepakwa rangi nyekundu.
2. Kuta zenu zimeangukia nyumba zetu.
3. Kuca zetu zimeumia vibaya.
4. Nyakati zenu zimekwisha.
5. Nyimbo zao zilirekodiwa jana mjini Kigali.

**Zoezi la 15.4, ukurasa 130**

1. Udevu wa mvulana yule umekuwa mrefu sana.
2. Unywele wa binti huyu ni mweusi tititi.
3. Wayo wa mtoto huyo una tope.
4. Wakati wa mwanafunzi kusoma umekwisha.
5. Uso wa mzee yule umepakwa mafuta.

**Zoezi la 15.5, ukurasa 130**

1. Nyayo
2. Nyakati
3. Nyimbo
4. Fito
5. Pinde

## Somo la 16: Aina za insha

### Kipindi cha 12: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati

**a) Malengo ya somo**

- Kusoma kwa usahihi kifungu ca habari kwa utambuzi wa herufi, silabi, maneno na sentensi;
- Kutaja ubaya wa uvivu katika maisha ya binadamu;
- Kutambua maana ya msamiati mpya kutokana na kifungu husika.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Micoro au pica zinazoonyesha madhara ya uvivu;
- Masimulizi yaliyoandikwa au yaliyorekodiwa;
- Micoro au pica za Wanyarwanda wakifanya kazi pamoja;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 131-133;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Somo hili linahusu madhara ya uvivu katika maisha ya binadamu na hasa mwanafunzi. Kifungu kilico katika *Kitabu ca Mwanafunzi* ukurasa 131-132 kinasimulia kuhusu ubaya wa uvivu na namna uvivu unavyoweza kumletea mtu balaa na shida tupu. Uvivu ni adui wa maendeleo, hivyo palipo na uvivu maendeleo hukosekana. Kila binadamu anahimizwa kutia bidii katika shughuli zake zote ili kuweza kufanikiwa maishani na kujiepusha na hatia. Mwalimu aandae mapema vifaa vitakavyomsaidia katika ufundishaji wa somo hili.

## d) Utaratibu wa somo

### Utangulizi

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu atangulize somo hili kuhusu madhara ya uvivu kwa kuwauliza wanafunzi maswali mepesi ya kuwacangamsha. Maswali kama vile: *Wewe huamka saa ngapi? Wewe hufanya kazi zako za ziada saa ngapi? Wewe huwasaida wazazi wako kufanya kazi za nyumbani?* n.k. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika majadiliano haya. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu.

Baadaye, mwalimu aendelee na somo kwa kuwaomba wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu watazame mcoro ulio kwenye *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 131. Mwalimu awaulize wanafunzi maswali kuhusu mcoro huo. Kwa mfano: *Mnaona nini kwenye mcoro huo?* Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kujibu maswali waliyoulizwa kwa kuwapa kitangulizi kama vile *"Mimi ninaona…."*. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu. Kwa mfano, "*Mimi ninaona wanafunzi wakijadiliana*." Katika sehemu hii, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi wake ili wapate ujuzi kuhusu tafakuri tunduizi, ubunifu na ugunduzi kwa kuwaonyesha micoro husika huku wanafunzi nao wakifikiri na kugundua kile kinacoendelea au kinacoonekana katika micoro hiyo.

### 16.1 Kusoma na ufahamu: Kifungu kuhusu madhara ya uvivu

Mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu wasome kwa kimya kifungu ca habari kuhusu madhara ya uvivu kilico katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 131-132. Wanafunzi wasome kwa kimya kifungu hico huku wakitambua na kuandika msamiati mpya wanaopatana nao. Hatimaye, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu kifungu walicosoma ili kuhakikisha kuwa wamekisoma na kukielewa. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuwauliza: *Madhara ya uvivu ni yapi*? Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma kutoka kwenye kifungu hico. Kwa mfano wanafunzi wanaweza kujibu: *Uvivu huweza kumsababisha mtu kujiingiza katika uhalifu kama vile wizi ili kutimiza mahitaji yake ya kila siku. Kosa la wizi linaweza kumpeleka mtu gerezani na hivyo kupata adhabu kali sana. Pia, mwizi akishikwa na umati wa watu anaweza kujeruhiwa vibaya sana au hata kuuawa*. Baada ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wamesoma kwa kimya kifungu kilicopo na kukielewa, mwalimu awaombe wanafunzi wasome tena

kwa sauti kifungu hico kwa kuhakikisha kuwa wanatamka maneno kwa namna inayofaa. Mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa.

Baadaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi kujibu maswali ya ufahamu waliyopewa. Mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika.

Hatimaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali hayo ya ufahamu huku akitoa maelezo pale ambapo wanafunzi wanatatizika. Mwalimu awasaidie wanafunzi wenye matatizo ya kuelewa msamiati uliotumika katika kifungu hico.

### 16.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu madhara ya uvivu

Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kuwaomba wajadili maana za msamiati mpya ambao walipatana nao katika usomaji wa kifungu walicopewa. Wanafunzi waeleze maana ya msamiati husika kwa kuzingatia jinsi ulivyotumiwa katika kifungu ca habari walicokisoma. Mwalimu awaombe wanafunzi watumie kamusi ya Kiswahili pale wanapoihitaji. Mwalimu azunguke darasani akiwaelekeza wanafunzi wanaopata taabu katika kuitumia kamusi au kufafanua maana ya msamiati husika.

Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi kucunguza msamiati uliopigiwa mstari katika sentensi walizopewa katika zoezi la 16.1 na kuutolea maana kisha watunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo. Ni vyema mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia na kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika. Baada ya wanafunzi hawa kukamilisha zoezi walilopewa, mwalimu awaombe wanafunzi kusahihisha kwa pamoja mazoezi hayo ya msamiati.

Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wameelewa msamiati uliokuwa mpya kwao, mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi wataje msamiati ambao hawakuelewa maana yake ili ujadiliwe tena kwa pamoja darasani kulingana na matumizi yake katika kifungu walicosoma. Ni vyema mwalimu azingatie kwamba utunzi wa sentensi za wanafunzi ndio utakaomfahamisha iwapo wanafunzi wamepata ujuzi unaotakikana katika tafakuri tunduizi, suluhisho kwa matatizo na mawasiliano kwa lugha rasmi na sahihi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kufanya zoezi la 16.2.

### Tathmini ya kipindi ca 12

Mwalimu ahitimishe funzo hili kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali hayo yaegemee hasa katika kucunguza iwapo wanafunzi wanaweza kutaja madhara ya uvivu, umuhimu

wa kufanya bidii katika shughuli zao mbalimbali pamoja na kutumia msamiati mpya waliojifunza katika maongezi yao hata nje ya darasa.

## Kipindi cha 13: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza

### a) Malengo ya somo

- Kujadili kuhusu uandishi wa insha za maelezo;
- Kujadili kuhusu uandishi wa insha za barua rasmi;
- Kutambua taratibu za kufuata katika uandishi wa insha husika.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Micoro au pica za kalenda ya miezi yote ionyeshayo sikukuu na sherehe mbalimbali ncini Rwanda.
- Micoro au pica zinazoonyesha watu katika maadhimisho mbalimbali;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 133-136;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.)

### c) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza kwa kurejelea aina mbalimbali za insha hasa insha za maelezo pamoja na insha za barua rasmi. Mwalimu aandae cati zenye mifano ya insha za maelezo na insha za barua rasmi pamoja na kuonyesha miundo yao kwa ajili ya kufundishia somo hili. Mwalimu anaweza kuandaa insha kadhaa au hata akazirekodi nyingine ili kuwasomea wanafunzi darasani au kuwawekea wakazisikiliza. Ili kufanikisha somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa amewagawa wanafunzi katika makundi yanayotakikana kwa kila zoezi husika.

### d) Utaratibu wa somo

#### Utangulizi

Mwalimu aanze kipindi hiki kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kuhusiana na somo lililopita kuhusu mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa insha za wasifu pamoja na insha za mazungumzo. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofunzwa katika kipindi ca hapo awali.

### 16.3 Matumizi ya lugha: Mifano ya insha

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha wasome na kujadiliana kuhusu mfano wa *insha ya maelezo* na mfano wa *insha ya barua rasmi* waliyopewa. Mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao. Baada ya muda mfupi wa majadiliano, mwalimu anaweza kuwacagua wanafunzi kadhaa kutoka katika makundi mbalimbali wasome mifano hiyo ya aina hizo za insha mbele ya wanafunzi wengine na kuwaomba wanafunzi waelezane ugunduzi wao. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kuelewa namna ya kuandika aina hizi za insha.

Majadiliano katika makundi yatasaidia kuelewa funzo hili. Wanafunzi waelekezwe kuelewa utaratibu wa kuandika insha ya maelezo pamoja na insha ya barua rasmi.

Mwalimu awahimize wanafunzi wafanye mazoezi zaidi kuhusu namna ya kuandika insha ya maelezo pamoja na insha ya barua rasmi katika makundi yao. Baada ya kupata uzoefu, mwanafunzi anaweza kuandika insha nyingine anazozifahamu kwa kujitegemea.

### 16.4 Kusikiliza na kuzungumza: Somo la imla

Katika sehemu ya kusikiliza na kuzungumza, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kufanya zoezi la imla. Mwalimu awasomee wanafunzi insha aliyobuni. Wanafunzi waandike kwa usahihi insha fupi watakayosomewa. Wazingatie mwendelezo sahihi na hati ya kusomeka. Baadaye, wanafunzi wafanye zoezi la kubuni insha yao wenyewe.

### Zoezi la imla

Mwalimu awasomee wanafunzi mwaliko ufuatao nao wauandike katika madaftari yao kwa usahihi.

*Kwa Bi Mukamutara,*

*Shule ya sekondari ya Uzaze ina furaha kukualika katika sherehe ya kuadhimisha miaka ishirini ya elimu bora. Sherehe hii itafanyika katika uwanja wa shule hiyo mnamo Jumatatu tarehe 27/ 03/ 2017 kuanzia saa mbili asubuhi. Karibu tusherehekee ufanisi wetu pamoja nawe.*

### Tathmini ya kipindi ca 13

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali haya yatamsaidia mwalimu kuthibitisha

iwapo wanafunzi wanaweza kutaja aina mbalimbali za insha na namna ya kuziandika kwa kuzingatia sehemu kuu za insha na mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wao.

Maswali yabainishe iwapo wanafunzi wanaweza kuandika insha ya maelezo pamoja na insha ya barua rasmi kwa kuzingatia utaratibu unaofaa.

## Kipindi cha 14: Sarufi (Ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vya idadi)

**a) Malengo ya somo**

- Kufahamu majina katika ngeli ya U-ZI, umoja na wingi;
- Kutambua vivumishi vya idadi katika ngeli ya U-ZI;
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia majina katika ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vya idadi.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Masimulizi yaliyoandikwa kwa kutumia majina katika ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vya idadi;
- Wanafunzi wenyewe;
- Vifaa halisi vyenye majina katika ngeli ya U-ZI;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 136-139;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.)

**c) Maandalizi ya somo**

Mwalimu aandae masimulizi kadhaa yaliyoandikwa kwa kutumia majina yanayopatikana katika ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vya idadi ambayo atawasomea wanafunzi. Mwalimu anaweza pia kuwapa wanafunzi fursa ya kuwasimulia wenzao kisa cocote ca kubuni ambaco kitahusisha majina katika ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vya idadi.

### d) Utaratibu wa somo

**Utangulizi**

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi ca sarufi kilicotangulia kuhusu

ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vimilikishi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa.

Mwalimu atumie masimulizi aliyoyaandaa kutanguliza funzo hili.

### 16.5 Sarufi: Ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vya idadi

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanne wanne kisha awaombe watazame pica na micoro iliyo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 137. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua vifaa vilivyopo pamoja na idadi yao katika pica na micoro hiyo. Katika makundi yao, wanafunzi wajadili kuhusu pica na micoro hiyo na kuelezana ugunduzi wao. Wanafunzi waelekezwe kutambua majina ya ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vya idadi vilivyotumika.

Baadaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi kusimulia visa vyovyote vya kubuni kwa kutumia aya moja tu kwa kushirikisha matumizi ya majina katika ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vya idadi. Baada ya masimulizi ya wanafunzi, mwalimu awaombe wanafunzi waeleze mabadiliko ya vivumishi vya idadi jumla na vivumishi vya idadi halisi katika sentensi wakirejelea majina katika ngeli ya U-ZI.

Baadaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kufanya zoezi la 16.3. Wanafunzi wote washirikishwe katika shughuli hii.

### Tathmini ya kipindi ca 14

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali ya kucunguza iwapo wanafunzi wameelewa matumizi na mabadiliko ya vivumishi vya idadi katika sentensi kwa kurejelea majina katika ngeli ya U-ZI. Maswali mengine yalenge kutathmini kiwango ca uelewa wa wanafunzi wa kutunga sentensi sahihi kisarufi zenye kuhusisha majina ya ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vya idadi.

**Maelezo muhimu kwa mwalimu**

Maneno ambayo hutumiwa kutaja hesabu, idadi au kiasi cha vitu au viumbe fulani huitwa ***vivumishi vya idadi***.

Vivumishi vya idadi hugawika katika aina mbili:

***i) Vivumishi vya idadi kamili***. Kwa mfano: *ukuta* ***mmoja***, *kuta* ***nne***, *uso* ***mmoja***, *nyuso* ***tano***, *upanga* ***mmoja***, *panga* ***nane*** n.k.

***Mifano katika sentensi:***

*a) Uzi* ***mmoja*** *umepotea.*
*b) Nyuzi* ***tano*** *zimepotea.*
*ch) Ukuta* ***mmoja*** *umejengwa.*
*d) Kuta* ***nne*** *zimejengwa.*

***ii) Vivumishi vya idadi isiyo kamili***. Kwa mfano: *kuta* ***chache***, *kurasa* ***nyingi***, *nyimbo* ***kadhaa***, *nyaraka* ***tele*** n.k.

***Mifano katika sentensi:***

*a) Nyimbo* ***nyingi*** *ziliimbwa jana.*
*b) Nyaraka* ***kadhaa*** *zimepotea.*

## 16.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atoe zoezi la ziada ambalo linalenga kuinua kiwango ca cini ca wanafunzi wasioweza kuelewa kwa haraka kama wenzao.

***Kwa mfano:***

*Kamilisha sentensi hizi kwa jibu sahihi kutoka kwenye mabano.*

1. Ufunguo _________ utatumika kufungua mlango ule. (mmoja, moja)
2. Nyuso ___________ zimepakwa mafuta yanayonukia. (mbili, wawili)
3. Rubona aliimba nyimbo ___________. (mbili, mawili)
4. Kikapu cetu kimebeba nyaraka ___________. (tano, matano)
5. Ahishakiye amejenga kuta __________. (nane, manane)

**Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu**

1. Ufunguo ***mmoja*** utatumika kufungua mlango ule.
2. Nyuso ***mbili*** zimepakwa mafuta yanayonukia.
3. Rubona aliimba nyimbo ***mbili***.

4. Kikapu cetu kimebeba nyaraka ***tano***.
5. Ahishakiye amejenga kuta ***nane***.

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango ca juu ca uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe waandike aya moja ya masimulizi ya kubuni yatakayohusisha majina katika ngeli ya U-ZI pamoja na vivumishi vya idadi.

***Kwa mfano:***

*Mama alipokea **nyaraka tatu** kutoka kwa dada yetu anayeishi ng'ambo. Nyuso zetu zilijaa furaha. Dada yangu mdogo alituimbia **wimbo mmoja** wa furaha nasi tukamsaidia kwa kupiga makofi.*

## 16.7 Majibu

### Zoezi la makundi, ukurasa 131

Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi kwa kurejelea mcoro uliopo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 131.

**Kwa mfano:**

*Mcoro unaonyesha mvulana ambaye ni mwanafunzi akiwahutubia wanafunzi wenzake pamoja na walimu/wazazi.*

### Maswali ya ufahamu, ukurasa 132

1. Uvivu ni hali ya kutopenda au kutofanya kazi.
2. Madhara ya uvivu ni mtu kukosa pesa za kukidhi mahitaji yake ya kila siku hali ambayo huweza kumsababisha kujiingiza katika matendo ya uhalifu kama wizi na uuaji. Kwa namna hii, mtu huyo anaweza kufungwa jela, kujeruhiwa au kuuawa na umma.
3. Mwanafunzi mvivu hawezi kufaulu katika masomo yake.
4. Nci huathirika kwa kutoendelea kiucumi kutokana na uvivu.
5. Afya za watu wavivu huathirika kwa kutumia dawa za kulevya ili kujisahaulisha matatizo yao.
6. Kutokana na kifungu hiki, nimejifunza kuwa uvivu hulemaza maendeleo ya mtu binafsi, jamii na pia nci kwa ujumla.
7. Kuepukana na uvivu ni kufanya mambo ambayo hayaendelezi uvivu kwa namna yoyote. Yaani, kuwa mwenye bidii katika kila jambo alifanyalo mtu. (*Mwalimu atathmini hoja za wanafunzi wake.*)

**Zoezi la msamiati, ukurasa 132**

Mwalimu atathmini maelezo ambayo wanafunzi watatoa. Ahakikishe kuwa wameeleza msamiati kama ulivyotumika katika kifungu walicokisoma.

***Kwa mfano:***

1. ***mvivu -*** mtu asiyependa kufanya kazi
2. ***madhara -*** matokeo mabaya ya jambo

**Zoezi la 16.1, ukurasa wa 133**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti sentensi hizo ziwe sahihi na zihusishe maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi walizopewa.

***Kwa mfano:***

1. *Mwalimu wetu wa Kiswahili hapendi **uvivu**.*
2. *Watumiaji wa **dawa za kulevya** huathirika kiafya.*
3. *Watu wengi wanaoishi katika hali ya **umaskini** huteseka.*
4. *Mwanafunzi wa kwanza katika darasa letu ni mwenye **bidii** masomoni.*
5. *Mjini hakupatikani **ombaomba** wengi.*
6. *Mara nyingi **uhalifu** husababisha vifo na uharibifu wa mali.*
7. *Mwalimu **alijitahidi** katika kuwafundisha wanafunzi wenye matatizo ya kusikia.*

**Zoezi la 16.2, ukurasa 133**

1. Ombaomba
2. maendeleo
3. masomo
4. dawa za kulevya
5. bidii

**Majibu ya maswali ya uhakiki, ukurasa 135**

1. Insha ya maelezo.
2. Katika kuandika insha za maelezo, sharti mambo ya ukweli yajadiliwe wala sio mambo ya kubuni.
3. Binadamu hutumia maji: kupikia, kunywa, kuogea, kufulia nguo, kuoshea vyombo na kusafishia nyumba.
4. Maji hunyunyiziwa mimea ili kukua. Dawa za kunyunyizia mimea hucanganywa kwa kutumia maji.
5. Wanyama hunywa maji ili kuishi na kukua. Wanyama hupigwa dawa ambazo huwa zimecanganywa kwa maji.
6. Miti huleta mvua.

**Zoezi la kuandika, ukurasa 135**

Mwalimu atathmini insha ambazo wanafunzi wataandika. Sharti insha hizo zihusishe vivutio vya utalii ncini Rwanda. Ahakikishe kuwa wanafunzi wamezingatia namna ya kuandika insha kwa kufuata muundo wa insha. Yaani, insha iwe na mwanzo, mwili na hitimisho.

**Majibu ya maswali ya uhakiki, ukurasa 136**

1. Barua rasmi
2. Katika kuandika barua rasmi, lazima kuwe na: anwani mbili (anwani ya mwandishi na ya mwandikiwa), mtajo (anayeandikiwa barua), kuhusu (sababu ya kuandika barua), utangulizi, mwili, hitimisho pamoja na sahihi ya anayeandika barua mwishoni mwa barua.
3. Barua kwa mwalimu mkuu
4. Anwani mbili: Anwani ya mwandishi na ya mwandikiwa.
5. Kuomba ruhusa ya kupumzika kutoka kwa mwalimu mkuu.

**Zoezi la kuandika/utafiti, ukurasa 136**

1. Mfano wa barua ya kirafiki:

*Maria Neza,*

*Shule ya sekondari ya Gitarama,*

*S.L.P 574,*

*GITARAMA.*

*12/03/2017*

*Kwa mwalimu mpendwa,*

*Hujambo mwalimu? Natumai hali yako ni shwari. Mimi ni mzima na wazazi wangu pia ni wazima. Ninaandika barua hii ili kuomba ruhusa ya kulikariri shairi langu siku ya wazazi shuleni mwetu. Shairi langu ni la kuwasifu wanafunzi wa shule yetu ambao wana nidhamu ya hali ya juu na bidii katika masomo yao. Mbali na kuwasifu wanafunzi, nimewasifu na kuwapongeza walimu wetu kwa juhudi zao za kuhakikisha wanafunzi wanaelewa wanacofundishwa.*

*Naomba uniruhusu kukariri shairi hili pia ili niwahimize wazazi wetu kulipa karo yetu kwa wakati ili kutuwezesha kuwa shuleni kwa muda wote wa muhula. Ninaahidi kuwa shairi langu litawaburudisha na kuwaelimisha wote watakaohudhuria. Niliwahi kukariri shairi jingine kanisani na liliwafurahisha washiriki wote. Natumai ombi langu litakubaliwa. Asante*

*Wako mkweli,*

*Maria Neza*

2. Barua ya mwaliko huandikwa ili kumwomba mtu au kundi la watu kuhudhuria hafla fulani. Barua hizi huandikwa kwa kutaja shughuli husika, mahali ambapo shughuli hiyo itafanyika, saa, siku, tarehe na wakati wa kufanyika kwa shughuli hiyo. Barua hizi huandikwa na kutumwa mapema kabla ya siku ya shughuli. Mfano wa barua ya mwaliko:

*Kwa Kalisa John*

*Familia ya Bwana na Bi. Kayitesi ina furaha kukualika kwenye sherehe ya maombi ya mtoto wao ambaye atajiunga na shule ya sekondari ya Gisenyi. Sherehe hii itafanyika siku ya Jumomosi tarehe 25/05/2017 nyumbani kwao Kamonyi kuanzia saa nne asubuhi. Unakaribishwa.*

3. Mambo ya kuzingatia wakati wa kuandika:

**a) Barua rasmi**

i) Anwani mbili (ya mwandishi na mwandikiwa)
ii) Mtajo
iii) Sababu ya kuandika barua hiyo (mintarafu)
iv) Barua yenyewe
v) Sahihi ya mwandishi

**b) Barua ya kirafiki**

i) Anwani moja (ya mwandishi)
ii) Mtajo
iii) Barua yenyewe
iv) Jina la mwandishi mwishoni (sahihi haiwekwi)

**c) Barua ya mwaliko**

i) Jina la anayeandikiwa
ii) Jina la anayeandika
iii) Mwaliko wenyewe
iv) Tarehe, siku, saa na wakati wa kufanyika hafla yenyewe

**Zoezi la 16.3, ukurasa 138**

Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi. Sharti sentensi hizo zihusishe majina na vivumishi vya idadi walivyopewa katika vitabu vyao.

***Kwa mfano:***

1. *Kuta mbili zitabomolewa.*
2. *Mama amenunua fagio tatu.*

3. *Teo nne zitatumika kupepetea nafaka.*
4. *Uzi mmoja umekatika.*
5. *Nyuso tano hazijapakwa mafuta.*
6. *Nyaraka kumi zilisomwa asubuhi.*

**Zoezi la 16.4, ukurasa 138**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga.

**Kwa mfano:**

1. ***Wimbo mmoja*** hautoshi.
2. Mtoto amerarua ***kurasa nyingi***.
3. ***Nyufa mbili*** zitazibwa.
4. ***Uzi mmoja*** umenunuliwa.
5. ***Fito kadhaa*** zimekatwa.
6. ***Nyembe cace*** zitatumika.

**Zoezi la 16.5, ukurasa 139**

1. mmoja
2. nyingi
3. cace
4. tano
5. mmoja

**Majibu ya tathmini ya mada ya 4**

**Zoezi la 1, ukurasa 139**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga.

**Kwa mfano:**

1. Wimbo wao utatumbuiza wageni.
2. Mtoto amerarua kurasa zake.
3. Kuna mende kwenye nyufa zetu.
4. Ninataka uzi wangu.
5. Pelekeni fito zenu kwa seremala.
6. Ninaomba nyembe zako.

**Zoezi la 2, ukurasa 140**

1. Utepe wangu haukupotea.
2. Kucha zenu hazipendezi.
3. Upanga wake haukuvunjika.
4. Wimbo wa taifa hauimbwi sasa.
5. Wakati wa mapumziko haujawadia.

**Zoezi la 3, ukurasa 140**

Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi.

**Kwa mfano:**

1. Tepe zetu zimepotea.
2. Ukucha wako unapendeza.
3. Panga zao zilivunjika.
4. Nyimbo za mataifa zinaimbwa sasa.
5. Nyakati za mapumziko zimewadia.

**Zoezi la 4, ukurasa 140**

1. mfupi
2. mpana
3. nyepesi
4. mzee
5. mweusi

**Zoezi la 5, ukurasa 140**

Mwalimu atathmini insha ambazo wanafunzi watabuni.

**Zoezi la 6, ukurasa 140**

Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi kuhusu madhara ya uvivu katika jamii hasa kwa mwanafunzi.

**Kwa mfano:** *Uvivu humfanya mwanafunzi asifaulu katika masomo yake.*

Sura ya
Tano

# Mada Kuu 5: Lugha na teknolojia

## Mada Ndogo: Kiswahili katika teknolojia ya habari na mawasiliano

**Uwezo upatikanao katika mada hii:**

Mwanafunzi aweze kutumia lugha ya Kiswahili katika muktadha wa teknolojia ya habari na mawasiliano.

**Malengo ya kujifunza**

Mwalimu ahakikishe kwamba katika ufundishaji wake, wanafunzi wanapata maarifa, ufahamu, stadi, maadili na mwenendo mwema ufuatao:

| Maarifa ya ufahamu | Stadi | Maadili na mwenendo mwema |
|---|---|---|
| • Kuonyesha uelewa wa matumizi na kujitosheleza kwa Kiswahili katika uwanja wa teknolojia ya habari na mawasiliano. | • Kutumia kwa utoshelevu msamiati wa Kiswahili unaohusiana na teknolojia ya habari na mawasiliano katika mawasiliano mbalimbali na kupitia kwa njia tofauti za mawasiliano. | • Kusikia hali ya uhuru na ya kujitoa gizani kwa kutumia mbinu mbalimbali za kupata na kupashana habari kwa urahisi. |
| • Kukumbuka msamiati mbalimbali wa kiteknolojia unaotumiwa katika mawasiliano na shughuli mbalimbali za teknolojia ya habari na mawasiliano. | • Kucunguza kwenye mitandao ya intaneti na vyanzo vingine kuhusu istilahi zinazofaa katika teknolojia ya mawasiliano. | • Kufurahia nguvu za nci na raia wake katika harakati za maendeleo ya teknolojia ya mawasiliano. |
| • Kuonyesha ustadi juu ya namna mbalimbali ya kuwasiliana na watu mbalimbali kwa kutumia njia moja au nyingine za teknolojia ya habari na mawasiliano ya kisasa. | • Kulinganisha na kutofautisha muundo wa mawasiliano katika aina mbalimbali za teknolojia ya habari na mawasiliano. | • Kujivunia ukuzaji wa ujuzi au akili katika mambo ya teknolojia ya habari na mawasiliano. |

| | | |
|---|---|---|
| • Kubainisha matumizi sahihi ya hali ya kuamrisha katika mawasiliano kwa kutumia neno 'tafadhali'. | • Kutumia njia au aina mbalimbali za teknolojia ya habari na mawasiliano kwa ufasaha katika mawasiliano ya kila siku. | |
| | • Kutafsiri na kuelezea maandishi tofauti kwa kuzingatia msamiati unaotumika katika teknolojia ya mawasiliano kutoka lugha moja kwenda katika nyingine (Kiingereza - Kiswahili). | |
| | • Kutumia kwa usahihi hali ya kutoa amri kwa watu katika mawasiliano kwa kuanzisha neno la heshima au lenye adabu. | |

### Maelezo muhimu kwa mwalimu

Mwalimu afahamu na awafahamishe wanafunzi kuwa mada hii inahusiana na masomo mengine kama vile: ***somo la Teknohama*** katika mada inayohusu msingi wa teknohama na msingi wa intaneti.

Mwalimu awashirikishe wanafunzi kufahamu kuwa mada hii inashughulikia lugha na teknolojia na hasa lugha ya Kiswahili na teknolojia ya habari. Hii ni mada muhimu sana kwani inalenga kumulika jinsi lugha ya Kiswahili inavyocangia na kuwezesha mawasiliano kwa kutumia teknolojia. Nyingi ya hizi teknolojia ni mpya na kwa hivyo kuna haja ya kubuni msamiati mpya unaoelezea masuala mbalimbali, vyombo na vifaa husika pamoja na teknolojia yenyewe.

Mlaca, (1995) alisema kwamba vyombo vya habari vina jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba ujumbe unaifikia hadhira kubwa na pana iwezekanavyo. Aidha, kuhakikisha kuwa ujumbe kutoka katika nyanja mbalimbali unawafikia watu popote walipo. Wazo hili ni muhimu kwa sababu vyombo vya habari vina uwezo wa kuwafikia watu walio kwenye sehemu ambazo hazina muundo msingi

wowote. Ujumbe kupitia kwa redio na runinga huwafikia watu wengi mno hata walio vijijini.

Combo kingine ambaco kimekuwa maarufu sana siku hizi ni simu ya mkononi. Mbali na matumizi yake ya kimsingi ya kupiga na kupokea simu, simu nyingi zina redio, runinga, *Google, WhatsApp, Facebook*, *YouTube* na huduma nyingine ambazo ni muhimu katika upitishaji wa habari. Isitoshe, simu hizi zina kamera na rekoda. Ni muhimu kucunguza lugha inavyotumika katika teknolojia hii mpya na hapa ndipo Kiswahili kinajibainisha kwa kubuni msamiati mwafaka ambao unaweza kutegemewa katika habari katika mazingira ya teknolojia.

F. Mpiranya, (1995) akizungumza kuhusu lugha ya Kiswahili katika vyombo vya habari ncini Rwanda alisema kuwa: magazeti yalianza kuingia ncini Rwanda mwanzoni mwa enzi za ukoloni. Magazeti hayo yalikuwa yameanza kuletwa ncini Rwanda kutoka pwani ya Afrika Mashariki. Msomi huyu anatoa mfano wa *Deutc Ost Afrika* ambayo ilisimamia Tanganyika, Rwanda na Burundi. Magazeti hayo yalikuwa *Kiongozi, Rafiki yangu* na *Pwani na Bara*. Kufikia mwezi wa Septemba 1977, gazeti la *Umunyurango* lilianza kutoa ukurasa ulioandikwa kwa lugha ya Kiswahili.

Ni muhimu mwalimu arejelee historia ya teknolojia ncini Rwanda ili aweze kubaini maendeleo ambayo yamefanyika kufikia sasa. Mwalimu apanue mawanda yake hadi kwenye vyombo vingine vya habari zaidi ya magazeti kama vile: redio, runinga, tarakilishi, kipakatalishi n.k.

Kipengele ca kisarufi kinacohusiana na matumizi ya hali ya kuomba na hali ya kuamrisha katika tungo yakinishi na tungo kanushi kimeandaliwa katika mada hii. Kwa hivyo, mwalimu awasaidie wanafunzi kufahamu matumizi ya msamiati wa hali ya kuomba pamoja na msamiati wa hali ya kuamrisha.

### Masuala mtambuka

Baadhi ya masuala mtambuka ambayo yatashughulikiwa katika mada hii ni elimu ya pamoja, amani na maadili, usawa wa kijinsia, elimu kuhusu fedha pamoja na mazingira, mabadiliko ya hali ya hewa na mwendelezo wake.

Elimu ya pamoja itaendelezwa kupitia kwa wanafunzi wote kusoma pamoja kwa kuwashirikisha hata na wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali na matatizo mbalimbali. Elimu hii ya pamoja pia itahusisha wanafunzi wote kuwakubali na kushirikiana kwa pamoja na wenzao kutoka katika matabaka mbalimbali ya kijamii. Usawa wa kijinsia utatiliwa mkazo kwa kuwafahamisha wanafunzi kuwa wasicana pamoja na wavulana wana uwezo sawa wa kufaulu katika maisha yao lica

ya jinsia zao tofauti. Wanafunzi wote wahimizwe kuheshimiana lica ya jinsia zao tofauti. Wanafunzi pia watafundishwa umuhimu wa mazingira yao na namna ya kuyahifadhi. Elimu kuhusu pesa itafundishwa kwa kuwaeleza wanafunzi kuhusu umuhimu wa pesa na namna ya kutotumia pesa vibaya. Teknolojia inahusisha matumizi ya pesa. Kwa hivyo, wanafunzi watapata ufahamu wa namna ya kutumia pesa zozote wapatazo. Wanafunzi wanaweza kufundishwa namna ya kujiwekea akiba kutokana na pesa wanazopata kwa matumizi ya baadaye.

Amani na maadili yatafundishwa kupitia kwa wanafunzi kushirikiana katika kazi mbalimbali za makundi darasani.

### Uwezo wa jumla

Mwalimu ahakikishe kuwa katika ufundishaji wake, wanafunzi wanapata uwezo wa kuwa na tafakuri tunduizi, usuluhishaji wa matatizo, mawasiliano katika lugha rasmi, stadi za utafiti, ubunifu na ugunduzi, ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha pamoja na ujifunzaji wa muda mrefu.

Ujifunzaji wa muda mrefu uendelezwe kupitia kwa wanafunzi kupata maarifa mbalimbali kuhusiana na teknolojia ya habari na mawasiliano ncini mwao watakayotumia hata nje ya darasa na katika maisha yao ya kila siku.

Wanafunzi washirikishwe katika kuwa na tafakuri tunduizi kwa kufikiri kwa undani (kutafakari zaidi) ili kuweza kuyajibu maswali katika mada hii kuhusiana na micoro waliyopewa pamoja na fahamu watakazosoma. Kupitia kwa mazoezi ya kuigiza, mazoezi ya makundi mbalimbali pamoja na mazoezi ya imla, wanafunzi watahimizwa kuwasiliana kwa lugha rasmi pamoja na kuwa na utawala binafsi pamoja na kuzifahamu stadi mbalimbali za maisha. Stadi za utafiti zitahitajika hapa ambapo wanafunzi watafanya utafiti mbalimbali kuhusiana na vyombo vya teknolojia ya habari na mawasiliano ncini Rwanda.

### Msamiati maalum

Msamiati maalum na muhimu ambao wanafunzi watapatana nao katika mada hii ni kuhusu teknolojia ya habari na mawasiliano ncini Rwanda kama vile:

| | **Msamiati** | **Maana** |
|---|---|---|
| 1. | ***simu*** | combo cenye namba za kubofya ambaco hutumiwa kupeleka au kupokea ujumbe |
| 2. | ***redio*** | combo kinacopokea mawimbi ya sauti kutoka hewani ili mtu asikie habari, ujumbe au muziki unaocezwa |

| | | |
|---|---|---|
| 3. | ***runinga*** | combo ambaco hunasa pica, sauti na maandishi kutoka kituo kimoja ca mawasiliano na kuziwasilisha kwa mtazamaji |
| 4. | ***tarakilishi*** | kifaa ca kielektroniki ca kuhifadhi na kucanganua taarifa zilizoingizwa humo ndani |
| 5. | ***intaneti*** | mtandao mkuu unaounganisha mitandao mingine mikubwa kadhaa ya duniani kote |
| 6. | ***teknolojia*** | maarifa ya Sayansi na matumizi yake katika mitambo, vyombo vya habari au njia za mawasiliano |
| 7. | ***mawasiliano*** | upashanaji wa habari kwa kutumia barua, simu au vyombo vingine vya habari |
| 8. | ***mtandao*** | mfumo wa mawasiliano ya kielektroniki unaopitia katika kompyuta ambao watu huutumia kupata taarifa au kuwasiliana |
| 9. | ***arafa*** | ujumbe unaotumwa na kupokelewa kupitia kwa simu ya mkononi |
| 10. | ***baruapepe*** | waraka au ujumbe unaotumwa kwa njia ya mtandao kupitia kwa vyombo vya kielektroniki kama vile: tarakilishi na simu |

## Usuluhishaji wa tatizo

Katika sehemu hii, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi yanayotakiwa katika zoezi husika kisha awaombe wacunguze kwa makini micoro iliyo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 142 kuhusiana na teknolojia ya habari na mawasiliano. Wanafunzi wote washirikishwe katika shughuli hii. Wanafunzi wacunguze micoro hiyo na mwalimu awaulize maswali kama vile: *Mnaona nini kwenye micoro hii? Vifaa hivi hutumika vipi?* Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika makundi yao ili waweze kujibu maswali hayo na kuelewa kinacoendelea katika micoro iliyopo. Kwa hivyo, mwalimu acocee uwezo wa wanafunzi wa kupata maarifa kuhusu ubunifu na ugunduzi na tafakuri tunduizi kwa kucunguza na kujibu maswali kuhusu micoro waliyopewa.

## Ushirikishaji wa wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali

Ili kuwashirikisha kwa pamoja wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali, ni vyema mwalimu awe na vifaa maalum vya kuwasaidia wanafunzi wa aina hii katika ujifundishaji wao.

Kwa wanafunzi ambao hawana uwezo wa kuona, mwalimu ahusishe matumizi

ya breli pamoja na vifaa vya kunasia sauti. Kwa wanafunzi ambao hawana uwezo wa kusikia, mwalimu ahusishe matumizi ya lugha ya ishara. Mwalimu anaweza kuwahusisha watafsiri walio na ujuzi wa kutumia lugha ya ishara. Vifaa hivi vitawawezesha wanafunzi hawa kusoma kama wenzao bila vizuizi vyovyote.

Nafasi ya wanawake na walemavu katika shughuli za kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano itiliwe maanani kupitia mcoro ulio katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 145 na 147 ili kukuza usawa wa kijinsia na elimu ya pamoja kwa kudumisha ushirikiano na mienendo mizuri miongoni mwa wanafunzi wote.

**Orodha ya masomo na vipindi**

| | Mada ya somo | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|
| **Somo la 17:** | Simu ya mkononi | 3 |
| **Somo la 18:** | Matumizi ya tarakilishi | 4 |
| **Somo la 19:** | Redio na runinga | 4 |
| **Somo la 20:** | Barua kwa mhariri | 3 |
| | | **JUMLA: 14** |

## Somo la 17: Simu ya mkononi

### Kipindi cha 1: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati

**a) Malengo ya somo**

- Kusoma kwa usahihi kifungu ca mazungumzo kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;
- Kubaini msamiati unaotumika katika teknolojia ya habari na mawasiliano;
- Kutaja visawe vya msamiati wa teknolojia ya habari katika lugha ya Kiswahili;
- Kueleza manufaa ya teknolojia ya habari na mawasiliano.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Micoro au pica za aina mbalimbali za simu za mkononi;
- Simu za mkononi halisi za aina mbalimbali;
- *Kitabu ca Mwanafunzi,* ukurasa 142-145;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.)

### c) Maandalizi ya somo

Hili ni somo la kwanza katika masomo mengine yanayohusu teknolojia ya habari na mawasiliano ncini Rwanda. Kwa hivyo, mwalimu atafute kwanza vifaa vinavyoweza kurahisisha uelewa wa wanafunzi katika somo hili kama vile: micoro au pica za aina mbalimbali za simu za mkononi au hata simu za mkononi halisi za aina mbalimbali na kadhalika. Kupitia vifaa hivyo, mwalimu aandae maswali mbalimbali yatakayowacocea wanafunzi kutambua maana ya teknolojia, matumizi ya simu ya mkononi, madhara ya kutumia simu ya mkononi, umuhimu wa kutumia simu ya mkononi pamoja na aina mbalimbali za simu za mkononi.

Wakati wa kuendesha somo, mwalimu atambue wakati mwafaka wa kuweka hadharani vifaa alivyovileta kwa kukumbuka kuwa matumizi ya micoro na pica au vifaa halisi ni mbinu nzuri sana ya kuwafundisha wanafunzi; hasa wale ambao wana matatizo mbalimbali katika kuelewa na kufahamu haraka yale wanayofundishwa darasani au wale walio na kiwango ca cini katika ujifundishaji wao. Ikiwa kuna wanafunzi wasio na uwezo wa kuona, ni lazima mwalimu awaombe wao wenyewe kuvigusa vifaa vilivyopo wakivitolea maelezo na wale wasio na uwezo wa kusikia wavionyeshe kwa kuvigusa huku wakiandika maelezo yake ubaoni.

Ili kutimiza malengo yake katika somo hili, ni vyema mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli ya wanafunzi iliyopendekezwa katika Kitabu ca Mwanafunzi.

### d) Utaratibu wa somo

#### Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu simu za mkononi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu kisha waendelee kujibu maswali mbalimbali kuhusu simu za mkononi ambazo wamekumbana nazo na hata labda kuzitumia. Mwalimu awacangamshe wanafunzi kwa kuwauliza maswali kuhusu pica na micoro ya simu za mkononi aliyoileta pamoja na simu halisi alizozileta darasani ili kucocea ufahamu wao kuhusu matumizi ya simu ya mkononi. Wanafunzi wajibu maswali kama walivyoulizwa naye mwalimu aendelee kwa kuwaomba wacunguze pica na micoro iliyo katika *Kitabu ca Mwanafunzi, ukurasa* 142. Wanafunzi wacunguze pica na micoro hiyo na mwalimu awaulize maswali kama vile: *Mnaona nini kwenye pica na micoro hii?*

Mwalimu awaelekeze wanafunzi ili waweze kujibu maswali hayo na kuelewa vyombo vinavyoonekana katika pica na micoro iliyopo.

Kwa hivyo, mwalimu acocee uwezo wa wanafunzi wa kupata maarifa kuhusu ubunifu na ugunduzi, tafakuri tunduizi kwa kucunguza na kujibu maswali kuhusu micoro hiyo. Mkazo utiliwe kuhusiana na ushirikiano unaojitokeza kati ya wavulana na wasicana ili waweze kufanikisha utambuzi wao wa matumizi ya simu za mkononi mbalimbali. Vilevile, masuala ya elimu ya pamoja nayo yasisitizwe pale ambapo hata watu wenye ulemavu wa aina tofauti wanaweza kutumia simu hizi za mkononi kufanikisha mawasiliano yao.

### 17.1 Kusoma na ufahamu: Kifungu kuhusu matumizi ya simu ya mkononi

Mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa kimya kifungu ca mazungumzo walicopewa katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 142-143 na kuandika msamiati mpya wanaopatana nao. Baadaye, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wote wamesoma na kuelewa kama alivyowaomba kwa kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu kifungu ca mazungumzo walicosoma. Kwa mfano, anaweza kuwauliza: *Ni watu gani wanaozungumza katika kifungu hiki? Watu hao wanazungumzia nini?* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu wao kulingana na yale waliyoyasoma katika kifungu hico ca mazungumzo. Kwa mfano: *Watu wanaozungumza ni Mama na Baba; Wao wanazungumzia matumizi ya simu ya mkononi aliyonunuliwa Mama*.

Baada ya haya, mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa sauti na kwa usahihi baada ya kutambua kwamba wanafunzi wamepata uelewa wa kile kinacozungumziwa katika kifungu ca mazungumzo kilicopo. Mwalimu akumbuke kusahihisha matamshi ya wanafunzi pale wanapokosea.

Mwalimu awaombe wanafunzi wajibu maswali ya ufahamu. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali hayo huku akitoa maelezo yake kwa kutilia mkazo pale ambapo wanafunzi wanatatizika.

### 17.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu simu ya mkononi

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu ili wajadiliane kuhusu maana za msamiati mpya waliopatana nao wakati wao wa kusoma kifungu ca mazungumzo kinacohusika. Ili kuimarisha stadi za utafiti na kudumisha uwezo wao wa kupata suluhisho kwa matatizo wanayokutana nayo, mwalimu awaombe wanafunzi wacunguze matumizi ya msamiati huo katika kifungu walicokisoma huku wakitumia kamusi pale wanapoihitaji. Mwalimu azunguke darasani akiwaelekeza wanafunzi

wanaotatizika. Wanafunzi wajadiliane kwa kuzingatia maelekezo ya mwalimu wao.

Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi kujadiliana pia kuhusu sentensi zilizo katika zoezi la 17.1 la msamiati ili waweze kutunga sentensi zao kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mistari. Wanafunzi nao, katika makundi yao ya wanafunzi watatu watatu, wajadiliane kuhusu zoezi hilo. Ili kurahisisha uelewa wa wanafunzi wa zoezi hilo, mwalimu awaombe walinganishe msamiati uliopigiwa mistari na matumizi ya msamiati huo katika kifungu ca mazungumzo walicosoma. Katika kutunga sentensi zao, mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wanapata ujuzi wa mawasiliano katika lugha rasmi, ubunifu na ugunduzi, ushirikiano na hata utawala binafsi na stadi za maisha kupitia sentensi za wanafunzi na zile zilizopendekezwa katika *Kitabu ca Mwanafunzi, ukurasa 144.* Hivyo basi, mwalimu azunguke darasani ili kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika katika utunzi wao wa sentensi na baadaye awashirikishe wote kutoa mcango wao katika kusahihisha zoezi hilo.

Hatimaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kufanya zoezi la 2 ambalo litasahihishwa kabla ya kipindi kitakacofuata.

**Tathmini ya kipindi ca 1**

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti kwa kurejelea msamiati mahususi uliopatikana katika kifungu ca mazungumzo walicokisoma kama vile: *simu ya mkononi, teknolojia, kubofya vidude, arafa, kiwambo, kugusa, kamera, intaneti* na kadhalika. Kwa hivyo, vifaa na pica zilizotumiwa kujifunzia somo hili zinaweza kutumiwa kucunguza ikiwa wanafunzi wanaweza kurejelea matumizi ya simu ya mkononi katika kufanikisha mawasiliano.

## Kipindi cha 2: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza

### a) Malengo ya somo

- Kufahamu matumizi ya simu ya mkononi;
- Kubaini madhara ya kutumia simu ya mkononi;
- Kujadili umuhimu wa kutumia simu ya mkononi.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Micoro au pica za aina mbalimbali za simu za mkononi;
- Simu za mkononi halisi za aina mbalimbali;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu ca Mwanafunzi,* ukurasa 145-146*;*
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.)

**c) Maandalizi ya somo**

Mwalimu atafute vifaa vitakavyoweza kurahisisha uelewa wa wanafunzi katika somo hili kama vile: micoro au pica za aina mbalimbali za simu za mkononi, simu za mkononi halisi za aina mbalimbali pamoja na combo ca kunasia sauti au breli na kadhalika. Kupitia vifaa hivyo, mwalimu aandae maswali mbalimbali yatakayowacocea wanafunzi kutambua matumizi ya simu ya mkononi, madhara yake pamoja na umuhimu wake katika mawasiliano ya kila siku ya Wanyarwanda.

Wakati wa kuendeleza somo, mwalimu atambue wakati mwafaka wa kuweka hadharani vifaa alivyovileta kwa kukumbuka kuwa matumizi ya micoro, pica na vifaa halisi ni mbinu nzuri sana ya kuwafundisha wanafunzi; hasa wale ambao wana matatizo mbalimbali katika kuelewa na kufahamu kwa haraka yale wanayofundishwa darasani au wale walio na kiwango ca cini katika ujifunzaji wao.

Ili kuyatimiza malengo yake katika somo hili, ni vyema mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli ya wanafunzi iliyopendekezwa katika *Kitabu ca Mwanafunzi*.

**d) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi ca 1. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa. Wanafunzi waeleze kuhusu matumizi mbalimbali ya simu za mkononi.

### 17.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

Katika hatua hii, mwalimu alenge kuwaelekeza wanafunzi kupata ujuzi kuhusu

stadi za utafiti kwa kuwaomba wanafunzi wabaini madhara ya kutumia simu za mkononi pamoja na umuhimu wa simu hizi. Mwalimu awaonyeshe wanafunzi aina mbalimbali za simu zinazotumika ncini Rwanda. Mwalimu anaweza pia kuwaonyesha wanafunzi pica au micoro ya aina mbalimbali za simu za mkononi iwapo hakupata simu halisi.

Ni vyema mwalimu acukue fursa hii kuwaelekeza wanafunzi ili wapate ujuzi kuhusu madhara yanayoweza kumpata mtu katika matumizi ya simu ya mkononi pamoja na umuhimu wa kutumia simu hizi katika kufanikisha mawasiliano. Ikiwezekana, mtandao utumiwe ili kuwasaidia wanafunzi kupata habari kamili kuhusu matumizi ya simu za mkononi pamoja na aina zake mbalimbali.

### 17.4 Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano

Katika hatua hii, mwalimu awaombe wanafunzi waigize mazungumzo kati ya Mama na Baba katika makundi ya wanafunzi wanne wanne. Mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wanatamka maneno kwa usahihi na kwa utambuzi wa herufi, silabi, neno na sentensi. Ili kuigiza mazungumzo kwa namna inayotakikana, mwalimu awaombe wanafunzi hawa wajitokeze mbele ya wanafunzi wengine na acunguze pia ikiwa uigizaji wa ishara unaambatana na maana kusudiwa au inayozungumziwa na mhusika. Wanafunzi waigize namna watu wanavyotumia simu za mkononi wakati wa mazungumzo. Mwalimu asahihishe makosa ya kimatamshi kila mara yanapojitokeza ili kuwazoesha wanafunzi kutamka maneno kwa usahihi na kudumisha uwezo wao wa kuwasiliana kwa lugha rasmi.

### Tathmini ya kipindi ca 2

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali kuhusu mambo muhimu waliyojifunza katika sehemu ya matumizi ya lugha pamoja na kusikiliza na kuzungumza. Maswali yake yacunguze uwezo wa wanafunzi wa kutumia msamiati unaojitokeza katika mazungumzo kati ya Mama na Baba; kubaini namna ya kutumia simu ya mkononi; kujadili kuhusu madhara ya kutumia simu za mkononi pamoja na umuhimu wa kutumia simu hizo katika uwanja wa teknolojia ya habari na mawasiliano.

## Kipindi cha 3: Sarufi (Hali ya kuomba, tungo yakinishi)

**a) Malengo ya somo**

- Kubaini msamiati wa hali ya kuomba;

- Kutumia msamiati wa hali ya kuomba katika tungo yakinishi;
- Kutunga sentensi sahihi katika hali ya kuomba tungo yakinishi.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Vifaa vya darasani kama vile: *madaftari, kalamu, rula* n.k.;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu ca Mwanafunzi, ukurasa 146;*
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Mwalimu atafute vifaa vitakavyoweza kurahisisha uelewa wa wanafunzi katika somo hili kama vile: madaftari, kalamu, rula pamoja na combo ca kunasia sauti au breli na kadhalika. Kupitia vifaa hivyo, mwalimu aandae maswali mbalimbali yatakayowacocea wanafunzi kutambua matumizi ya hali ya kuomba katika mawasiliano ya kila siku pamoja na matumizi yao katika sentensi sahihi.

Mwalimu atambue wakati mwafaka wa kuweka hadharani vifaa alivyovileta au alivyowaomba wanafunzi darasani. Wanafunzi walio na matatizo mbalimbali katika kuelewa na kufahamu haraka yale wanayofundishwa darasani au wale walio na kiwango ca cini katika ujifunzaji wao wataweza kufaidika kutokana na matumizi ya vifaa mbalimbali katika somo hili. Ikiwa kuna wanafunzi wasio na uwezo wa kuona, ni vyema mwalimu awaombe wao wenyewe kuvigusa vifaa vilivyopo wakivitolea maelezo na wale ambao hawana uwezo wa kusikia wavionyeshe kwa kuvigusa huku wakiandika maelezo yao ubaoni.

Ili kuyatimiza malengo yake katika somo hili, ni vyema mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli ya wanafunzi iliyopendekezwa katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 146.

**d) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi ca hapo awali. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa. Wanafunzi waeleze kuhusu aina mbalimbali za simu za mkononi, matumizi ya simu hizi, madhara yao pamoja na umuhimu wao katika kufanikisha mawasiliano.

### 17.5 Sarufi: Hali ya kuomba, tungo yakinishi

Katika hatua hii, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya watatu watatu na awaombe wasome sentensi zilizo kitabuni mwao huku wakicunguza matumizi ya neno '*tafadhali*'. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua na kuelewa matumizi ya neno '*tafadhali*' katika sentensi walizopewa pamoja na maongezi ya kila siku. Wanafunzi wasome sentensi walizopewa kwa makini kisha mwalimu awaelekeze katika kutumia neno '*naomba*' badala ya neno '*tafadhali*'. Wanafunzi washirikishwe katika kujadili ugunduzi wao.

Kupitia mifano ya sentensi iliyopo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua msamiati ambao hutumika katika hali ya kuomba ambao ni maneno kama vile: *tafadhali, naomba, nisaidie* n.k.

Ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wamepata ufahamu wa kutosha katika matumizi ya msamiati wa hali ya kuomba, mwalimu awaombe wafanye zoezi la 3 ambapo wanatakiwa kutunga sentensi tano sahihi katika hali ya kuomba, tungo yakinishi.

### Tathmini ya kipindi ca 3

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali yake yacunguze uwezo wa wanafunzi wa kutumia kwa usahihi msamiati wa hali ya kuomba kama vile: *tafadhali* na *naomba* katika sentensi sahihi na pia katika maongezi yao ya kila siku.

**Maelezo muhimu kwa mwalimu**

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kufahamu kuwa:

- ***Faksi*** ni kifaa cha kutuma taarifa kwa njia ya kielektroni kwa kutumia simu. Taarifa yenyewe pia huitwa faksi. Huhusisha matumizi ya umeme. Faksi ni aina ya barua au ujumbe unaotumwa kwa njia ya mashine inayoitwa faksi. Maelezo machache yanayofafanua ujumbe pekee hutumika.
- ***Simu ya mkononi*** ni simu inayofanya kazi kwa mfumo wa kielektroniki na ambayo huwezesha mawasiliano kwa njia ya mawimbi. Mtu anaweza kutembea nayo na kuipokea akiwa mahali popote. Simu hii huwa haijaunganishwa na nyanya wala nyuzi zozote. Mtu anayepiga simu anaitwa ***mpigaji simu***. Mtu anayepigiwa simu anaitwa ***mpokeaji wa simu***. Mtu anayehakikisha kuwa mawasiliano yanafanyika katika chumba cha ubadilishanaji simu anaitwa ***opareta***.
- Simu ya mkononi pia huitwa ***rununu***.
- Msamiati wa adabu ambao hutumika kuomba mtu akutendee hisani fulani ni kama vile: ***tafadhali, naomba, nisaidie*** n.k.

## 17.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Kwa wanafunzi wenye kiwango ca cini katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge sentensi tano sahihi kwa kutumia maneno au vifungu vya maneno vifuatavyo pamoja na msamiati wa hali ya kuomba.

**Kwa mfano: *simu***

*Tafadhali nipe hiyo simu yangu.*

1. simu
2. arafa
3. teknolojia
4. bofya vidude
5. intaneti

### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe maneno waliyopewa katika hali ya kuomba.

***Kwa mfano:***

1. ***Tafadhali*** *nieleze maana ya* ***teknolojia****.*
2. ***Naomba*** *unitumie* ***arafa*** *hii kwa baba yangu.*
3. ***Tafadhali*** *msaidie babu* ***kubofya vidude*** *vya simu yake.*

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango ca juu ca uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe waandike aya moja ya maelezo kuhusu madhara ya kutumia simu za mkononi.

**Kwa mfano:**

Mimi nimefanya utafiti ili kubaini madhara ya simu za mkononi kwa binadamu. Simu hizi zinapatikana kila mahali na asilimia kubwa ya Wanyarwanda wanazitumia. Kupitia simu za mkononi, mtu anaweza kulaghaiwa na kuibiwa mali na pesa zake. Walaghai humdanganya mtu kuwa wamemtumia pesa kwenye simu yake na kumpigia wakimwomba awarudishie pesa hizo. Iwapo alikuwa na pesa zake kwenye simu yake na ajaribu kuwarudishia pesa hizo wanazodai basi atajipata amedanganywa.

*Watu wengi pia huweza kutazama filamu cafu na zisizokubalika kupitia kwa simu zao za mkononi hivyo kuathiri maadili yao hasa vijana wengi.*

# 17.7 Majibu

**Zoezi la makundi, ukurasa 142**

Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi kwa kurejelea micoro iliyopo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 142.

**Kwa mfano:**

*Micoro hii inaonyesha aina mbalimbali za simu za mkononi.*

**Maswali ya ufahamu, ukurasa 143 - 144**

1. Baba na Mama
2. Kwa sababu mazungumzo hayo yanahusu kifaa ca kiteknolojia (simu) na namna ya kukitumia kifaa hico.
3. Simu ya mkononi/rununu
4. Kutuma arafa au ujumbe na kupiga simu kwa watu mbalimbali. (*Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi kuhusu matumizi ya simu.*)
5. Mama hajaelewa kutumia simu aliyonunuliwa.
6. Hakuna mitambo ya kunasia mawimbi ya kutumika kwenye simu. Simu hiyo ikianguka cini inaweza kupasuka kiwambo cake na isitumike tena.
7. Ni maarifa ya Sayansi na matumizi yake katika mitambo, vyombo na zana katika viwanda, kilimo au mawasiliano. (*Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi.*)
8. Asante, pole, tafadhali, nashukuru n.k. (*Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.*)

**Zoezi la msamiati, ukurasa 144**

Mwalimu atathmini maelezo ambayo wanafunzi watatoa kuhusu msamiati waliopatana nao katika usomaji wa kifungu walicopewa. Ahakikishe kuwa msamiati huu ulitumika kwenye kifungu ca mazungumzo waliyosoma.

***Kwa mfano:***

1. ***teknolojia*** - maarifa ya Sayansi na matumizi yake katika mitambo, vyombo na zana katika viwanda, kilimo au mawasiliano
2. ***sebuleni*** - cumba ca nyumbani ambapo wageni hupokelewa kwa mazungumzo

**Zoezi la 17.1, ukurasa 144**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi walizopewa.

***Kwa mfano:***

1. *Baba alininunulia **simu ya mkononi** kama zawadi.*
2. ***Teknolojia** imerahisisha mawasiliano kwa kiwango kikubwa.*
3. *Simu yangu ya **kubofya vidude** imepotea.*
4. *Nitamwandikia mwalimu wangu wa darasa **arafa** nikimwomba radhi kwa kutofika shuleni.*
5. *Kalisa **atampigia** Neza simu ili kumfariji.*
6. *Nilisoma habari za intaneti kwa **kugusa** kwenye **kiwambo** ca simu ya mama.*
7. ***Kamera** ya simu yangu imeharibika.*
8. *Nitapata habari kuhusu magari kwenye **intaneti**.*

**Zoezi la 17.2, ukurasa wa 145**

1. caji
2. watisapu, fesibuku
3. kunasia mawimbi
4. arafa

**Zoezi la matumizi ya lugha, ukurasa 145**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi. Sharti yawe sahihi kisarufi na yahusu vyombo vya mawasiliano walivyopewa.

***Kwa mfano:***

i) Vyombo vya mawasiliano vilivyopo ni: simu ya mkononi, tarakilishi, simu ya ofisini na mashine ya faksi.

ii). Vyombo hivi hutumiwa kwa ajili ya kuwasiliana na watu katika maeneno mbalimbali. Simu ya mkononi huweza kutuma arafa au kutumika kumpigia mtu na kuzungumza moja kwa moja. Simu ya ofisini hutumika kumpigia mtu mwingine na mkazungumza moja kwa moja. Tarakilishi huwezesha mawasiliano kwa kutuma baruapepe, kupitia kwa watisapu na fesibuku. Faksi hutumika kutuma jumbe za haraka kwa kutumia mashine ya faksi.

iii) Vyombo hivi vyote huwezesha mawasiliano ya haraka.

iv) Vyombo hivi hutumia umeme ili kufanya kazi. Kwa hivyo, watu wasiokuwa na umeme hawawezi kuvitumia. Tarakilishi huhitaji intaneti hivyo watu wasio na intaneti hawawezi kuitumia. Simu ya mkononi huhitaji kuwa na pesa kwa ajili ya kuwasiliana.

**Zoezi la sarufi 17.5B, ukurasa146**

1. Naomba unipigie simu unapofika nyumbani.
2. Naomba uimbe wimbo wa taifa.

3. Naomba uceze mcezo wa miguu.
4. Naomba mpike mihogo kwa kuku.
5. Naomba uzungumze lugha ya Kiswahili sanifu pekee.

**Zoezi la 17.3, ukurasa 146**

Mwalimu atathmini sentensi zitakazotungwa na wanafunzi. Sharti sentensi hizo ziwe sahihi kisarufi na ziwe katika hali ya kuomba, wakati uliopo.

***Kwa mfano:***

1. *Tafadhali ingia garini twende nyumbani.*
2. *Tafadhali zungumza na mgeni aliye sebuleni.*
3. *Naomba unipe kalamu yangu.*
4. *Naomba muimbe wimbo huo tena.*
5. *Tafadhali washa taa ya cumbani mwako.*

# Somo la 18: Matumizi ya tarakilishi

## Kipindi cha 4: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati

### a) Malengo ya somo

- Kusoma kwa usahihi kifungu ca habari kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;
- Kubaini msamiati unaohusiana na matumizi ya tarakilishi.

### b) Vifaa vya kujifunza

- Micoro au pica za aina mbalimbali za tarakilishi;
- Aina mbalimbali za tarakilishi halisi;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 147-149;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia, n.k.).

### c) Maandalizi ya somo

Somo hili ni mwendelezo wa somo lililotangulia ambapo lengo kuu la mwalimu ni kuwasaidia na kuwaelekeza wanafunzi katika kufahamu matumizi ya vyombo mbalimbali vya habari na mawasiliano. Kwa hivyo, mwalimu aandae vifaa mbalimbali vinavyohitajika katika somo hili kama vilivyoorodheshwa hapo juu. Iwapo shule husika ina maabara ya tarakilishi, basi mwalimu anaweza kuwapeleka wanafunzi wake kwenye maabara hayo ili wanafunzi wajifundishe wakiwa na tarakilishi halisi. Kwa kufanya hivi, wanafunzi watapata uelewa wa haraka kuhusiana na somo hili la matumizi ya tarakilishi.

### d) Utaratibu wa somo

#### Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi na awaulize maswali kuhusu somo lililopita. Wanafunzi wajibu maamkizi pamoja na maswali ya mwalimu wao. Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi wasahihishe zoezi walilopewa katika kipindi ca hapo awali ili aweze kuendelea na somo jipya.

## 18.1 Kusoma na ufahamu: Kifungu kuhusu matumizi ya tarakilishi

Mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa kimya kifungu ca habari walicopewa katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 147-148 huku wakiandika msamiati mpya wanaokutana nao. Wanafunzi wasome kwa kimya pamoja na kuandika msamiati huo mpya. Baadaye, mwalimu acunguze ikiwa wanafunzi wote wamesoma kama walivyoambiwa. Kwa hivyo, mwalimu aulize maswali mbalimbali kuhusu kifungu ca habari walicokisoma. Kwa mfano, anaweza kuuliza maswali yafuatayo: *Ni faida gani tunazopata kutokana na matumizi ya tarakilishi?* Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kuonyesha kuwa wamesoma na kukielewa kifungu husika. Kwa mfano, *matumizi ya tarakilishi yamewafanya watu wengi kupata ujuzi wa kiteknolojia, kuweza kuwasiliana na watu duniani kote, kuhifadhi mazingira yetu kwa kupunguza matumizi ya karatasi* na kadhalika.

Baada ya kupata pica ya uelewa wa jumla wa wanafunzi kuhusu kifungu ca habari walicokisoma, mwalimu awaombe tena wasome kwa sauti, kwa usahihi na kwa kuzingatia matumizi ya alama za vituo vinavyopatikana katika kifungu hico. Ni vyema mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa kwa lengo la kutambua herufi, silabi na sentensi zilizopo.

## 18.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu matumizi ya tarakilishi

Katika hatua hii ya tatu, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya watatu watatu ili waweze kujadiliana kuhusu msamiati mpya waliokutana nao. Mwalimu awaombe wazingatie matumizi ya msamiati huo katika kifungu ca habari walicokisoma na watumie kamusi pale wanapoihitaji. Wanafunzi wajadiliane kama walivyoelekezwa na mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi pale wanapotatizika. Hatimaye, mwalimu awaombe wajibu maswali katika zoezi la 18.1 la msamiati ambapo watajigawa katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kucunguza sentensi zilizopo ili waweze kutunga sentensi zao kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mistari.

Wanafunzi watunge sentensi zao kwa kuzingatia jinsi maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi walizopewa yalivyotumika katika kifungu ca habari walicokisoma. Mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika na awashirikishe wanafunzi wote kusahihisha zoezi hilo mara moja wanapomaliza kujadiliana katika makundi yao. Hivyo basi, mwalimu aombe kila kundi liandike sentensi zao ubaoni na wanafunzi wengine wazicunguze na watoe mcango wao kuzikubali au kuzikataa na kuzisahihisha.

Kupitia kwa zoezi lililotolewa kwa wanafunzi katika sehemu hii ya msamiati,

mwalimu ahakikishe kwamba wamepata ujuzi ainasafu wa elimu kuhusu fedha, mazingira, mabadiliko ya hali ya hewa na mwendelezo na hata utamaduni wa kiusanifishaji kwa kucunguza na kutunga sentensi zao wenyewe.

**Tathmini ya kipindi ca 4**

Katika hatua hii, mwalimu ahitimishe kwa kuwauliza wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu mambo muhimu waliyojifunza kuhusiana na matumizi ya tarakilishi. Wanafunzi pia waulizwe maswali kuhusu msamiati unaohusiana na matumizi ya tarakilishi.

## Kipindi cha 5: Matumizi ya lugha

**a) Malengo ya somo**

- Kutambua msamiati wa kiteknolojia unaohusu tarakilishi;
- Kujadili kuhusu watisapu na fesibuku;
- Kufahamu matumizi ya baruapepe;
- Kueleza madhara na faida za kutumia tarakilishi.

**b) Vifaa vya kujifunza**

- Micoro au pica za tarakilishi mbalimbali;
- Tarakilishi halisi zenye kuwezesha matumizi ya watisapu na fesibuku;
- Simu zenye kuwezesha matumizi ya watisapu;
- Barua pepe zilizoandikwa na kujibiwa;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 150;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Mwalimu aandae maswali ya kuelekeza wanafunzi katika ujifundishaji wa somo hili kuhusu matumizi ya tarakilishi, watisapu, fesibuku pamoja na baruapepe. Mwalimu ahakikishe pia kwamba ana vifaa mwafaka vya kufundishia somo hili kama vilivyoorodheshwa hapo juu. Mwalimu anaweza kufundishia somo hili katika maabara ya tarakilishi iwapo shule husika ina maabara hayo. Hili litawawezesha wanafunzi kuweza kuzitumia tarakilishi hizo na kuelewa vyema matumizi yake mbalimbali kwa njia halisi zaidi.

## d) Utaratibu wa somo

### Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake na kuwauliza maswali kuhusu somo lililopita. Wanafunzi wajibu maamkizi pamoja na maswali ya mwalimu wao. Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi wasahihishe zoezi walilopewa katika somo lililopita ili aweze kuendelea na somo hili jipya. Wanafunzi wasahihishe zoezi hilo.

### 18.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

Baada ya haya, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanne wanne na kuwaelekeza kuambatanisha kwa usahihi micoro waliyopewa pamoja na sentensi walizopewa katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 150. Zoezi hili litawawezesha wanafunzi kufahamu matumizi ya watisapu, fesibuku pamoja na baruapepe kwa kutumia tarakilishi au simu ya mkononi. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika majadiliano haya kwenye makundi yao. Wanafunzi waelezane jinsi watisapu au fesibuku zinavyotumika katika mawasiliano, Pia, wajadiliane kuhusu madhara na faida za njia hizi za mawasiliano.

Pia, mwalimu awaelekeze wanafunzi kufahamu namna ya kuandika baruapepe kwa kutumia simu ya mkononi au tarakilishi, jinsi ya kufungua akaunti ya kibinafsi na namna ya kujibu barua pepe anazoandikiwa.

Ili kufanikisha malengo ya somo katika sehemu hii, mwalimu awaombe wanafunzi wafanye zoezi la makundi lililo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 150 ambapo wanafunzi wanatakiwa wajigawe katika makundi ya wanafunzi wanne wanne kisha wajadiliane kuhusu: *maana ya tarakilishi, njia za mawasiliano kupitia kwa tarakilishi ambazo wanafahamu, faida za tarakilishi kwa watumizi pamoja na madhara ya tarakilishi kwa watumizi.*

Katika mawasilisho yao, ni vyema mwalimu awaombe wanafunzi wengine wabainishe makosa yanayofanywa na wenzao ili kukuza uwezo wao wa usuluhishaji wa matatizo na utawala binafsi kwa kulenga kuboresha mawasiliano kati yao kwa lugha rasmi.

### Tathmini ya kipindi ca 5

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kwa kurejelea msamiati mahususi waliojifunza kuhusu matumizi ya tarakilishi, watisapu, fesibuku pamoja na barua pepe. Hivyo basi, vifaa halisi, micoro na pica zilizotumiwa kujifundishia somo hili zitumiwe kucunguza iwapo wanafunzi

wanaweza kurejelea msamiati maalum unaohusiana na matumizi ya tarakilishi kwa ujumla.

## Kipindi cha 6: Kusikiliza na kuzungumza

**a) Malengo ya somo**

- Kujadili kuhusu faida za mradi wa tarakilishi kwa kila mtoto ncini Rwanda;
- Kutambua kasoro za mradi wa tarakilishi kwa kila mtoto;
- Kutoa mapendekezo ya kuboresha mradi wa tarakilishi kwa kila mtoto;
- Kujadili madhara na faida za watisapu, barua pepe na fesibuku.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Micoro au pica za vipakatalishi;
- Tarakilishi halisi zenye kuwezesha matumizi ya watisapu na fesibuku;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 151;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Mwalimu ahakikishe amewagawa wanafunzi katika makundi yanayotakikana. Mwalimu aandae somo hili kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu faida na kasoro za mradi wa tarakilishi kwa kila mtoto ncini Rwanda.

Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kufundishia somo hili ili kuwaelekeza wanafunzi ipasavyo wakati wa kushiriki katika kujadili maswali waliyopewa katika makundi yao.

**d) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi ca 5. Wanafunzi wajibu maswali waliyoulizwa. Mwalimu atumie vifaa alivyovileta kutanguliza funzo hili.

### 18.4 Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano

Baada ya haya, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu ambapo kila kundi litapewa muda wa kujadili maswali yaliyo kwenye *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 151. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika shughuli ya kujadili kuhusu mradi wa tarakilishi kwa kila mtoto ncini Rwanda. Wanafunzi wajadiliane kuhusu mradi huo kwa pamoja. Baada ya kumaliza majadiliano yao katika makundi yao, mwalimu amwombe mwanafunzi mmoja mmoja kutoka katika kila kikundi ajitokeze mbele ya darasa na awasomee wanafunzi wenzake mambo waliyojadili katika kikundi cao. Wanafunzi wengine wasikilize kwa makini mawasilisho ya wanafunzi hao na waandike kasoro na mafanikio yanayojitokeza katika mazungumzo yao ili baadaye waweze kutoa mcango wao kwa kuboresha mazungumzo yao katika mawasilisho na majadiliano mengine.

Mwalimu acunguze jinsi wanafunzi wanavyojadiliana na awaelekeze katika kusahihisha matamshi yao na kutunga sentensi kamili zenye uzito wa mawazo. Ni vyema mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamepata uwezo wa kiubunifu na kiugunduzi pamoja na tafakuri tunduizi kwa kudumisha pia uwezo wao wa kuwasiliana katika lugha rasmi.

### Tathmini ya kipindi ca 6

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mepesi yenye kucunguza uwezo wa wanafunzi wa kudhihirisha uelewa wa faida na kasoro za mradi wa tarakilishi kwa kila mtoto ncini Rwanda.

## Kipindi cha 7: Sarufi (Hali ya kuomba, tungo kanushi)

### a) Malengo ya somo

- Kubaini msamiati wa hali ya kuomba;
- Kutumia msamiati wa hali ya kuomba katika tungo kanushi;
- Kutunga sentensi sahihi katika hali ya kuomba tungo kanushi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Vifaa vya darasani kama vile: *madaftari, kalamu, rula* n.k.;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu ca Mwanafunzi, ukurasa 151-152;*

- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### c) Maandalizi ya somo

Mwalimu atumie vifaa ambavyo alivitumia kufundishia kipindi ca 3 hapo awali kuhusiana na hali ya kuomba, tungo yakinishi kama vile: madaftari, kalamu, rula pamoja na combo ca kunasia sauti au breli na kadhalika. Kupitia vifaa hivyo, mwalimu aandae maswali mbalimbali yatakayowakumbusha wanafunzi matumizi ya hali ya kuomba, tungo yakinishi katika mawasiliano ya kila siku na katika sentensi sahihi.

Mwalimu atambue wakati mwafaka wa kuweka hadharani vifaa alivyovileta au alivyowaomba wanafunzi walete darasani. Wanafunzi walio na matatizo mbalimbali katika kuelewa na kufahamu haraka yale wanayofundishwa darasani au wale walio na kiwango ca cini katika ujifunzaji wao wataweza kufaidika kutokana na matumizi ya vifaa mbalimbali katika somo hili. Ikiwa kuna wanafunzi wasio na uwezo wa kuona, ni vyema mwalimu awaombe wao wenyewe kuvigusa vifaa vilivyopo wakivitolea maelezo na wale ambao hawana uwezo wa kusikia wavionyeshe kwa kuvigusa huku wakiandika maelezo yao ubaoni.

Ili kuyatimiza malengo yake katika somo hili, ni vyema mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli ya wanafunzi iliyopendekezwa katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 151.

### d) Utaratibu wa somo

### Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi ca 3 hapo awali kuhusiana na hali ya kuomba, tungo yakinishi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa. Wanafunzi waeleze kuhusu msamiati unaotumika wakati mtu anapoomba kufanyiwa jambo fulani au anapoomba kupewa kitu fulani.

### 18.5 Sarufi: Hali ya kuomba, tungo kanushi

Katika hatua hii, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanne wanne na awaombe wasome sentensi zilizo kitabuni mwao huku wakicunguza matumizi ya maneno '*tafadhali*' na '*naomba*'. Mwalimu awaelekeze wanafunzi

katika kutambua na kuelewa matumizi ya maneno '*tafadhali*' na '*naomba*' katika sentensi walizopewa pamoja na maongezi ya kila siku. Wanafunzi wasome sentensi walizopewa kwa makini kisha mwalimu awaelekeze katika kutumia maneno '*tafadhali*' na '*naomba*'. Wanafunzi washirikishwe katika kujadili ugunduzi wao.

Baada ya haya, mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kukanusha sentensi walizopewa. Wanafunzi waelekezwe katika kufahamu kuwa katika tungo kanushi, sentensi zilizotumia nafsi mbalimbali za Kiswahili hubadilika na kutumia kikanushi *'-si-'* ili kuashiria ukanushi wake. Mwalimu awatumie wanafunzi wenyewe kwa wenyewe kudhihirisha hali hii ya kuomba katika tungo kanushi. Mwanafunzi mmoja anaweza kuomba apewe kitu fulani na mwanafunzi mwingine naye aombe asipewe kitu hico. Kwa mfano:

- *Naomba unipe gazeti hilo.*
- *Naomba usinipe gazeti hilo.*

Ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wamepata ufahamu wa kutosha katika matumizi ya msamiati wa hali ya kuomba katika tungo kanushi, mwalimu awaombe wafanye zoezi la 2 ambapo wanatakiwa kutunga sentensi sahihi katika hali ya kuomba tungo kanushi kwa kutumia msamiati waliopewa.

### Tathmini ya kipindi ca 7

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali yake yacunguze uwezo wa wanafunzi wa kutumia kwa usahihi msamiati wa hali ya kuomba katika tungo kanushi katika sentensi sahihi na pia katika maongezi yao ya kila siku.

**Maelezo muhimu kwa mwalimu**

***Tarakilishi*** ni chombo cha mawasiliano ambacho hufanana na runinga na hutumia intaneti. Tarakilishi huhifadhi na kuchanganua taarifa zilizoingizwa pamoja na kuongoza mitambo mbalimbali.

## 18.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu awasaidie wanafunzi wenye kiwango ca cini katika ujifunzaji wao kwa kuwaomba wageuze sentensi zifuatazo kutoka tungo yakinishi hadi katika tungo kanushi.

***Kwa mfano:***

***Tungo yakinishi:*** *Tafadhali safisha cumba cangu.*

***Tungo kanushi:*** *Tafadhali usisafishe cumba cangu.*

1. Naomba uwashe tarakilishi hiyo.
2. Tafadhali mpigie mama yako simu.
3. Tafadhali nipakulie cakula kidogo.
4. Naomba uniandikie arafa fupi.
5. Tafadhali zungumza kwa sauti ya cini.

### Majibu ya zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga, ahakikishe kuwa sentensi hizo ni sahihi na kuwa zimehusisha hali ya kuomba, tungo kanushi. Yaani:

1. Naomba usiwashe tarakilishi hiyo.
2. Tafadhali usimpigie mama yako simu.
3. Tafadhali usinipakulie cakula kidogo.
4. Naomba usiniandikie arafa fupi.
5. Tafadhali usizungumze kwa sauti ya cini.

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango ca juu ca uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge sentensi kumi sahihi katika hali ya kuomba, tungo kanushi.

### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi na ziwe katika hali ya kuomba, tungo yakinishi na tungo kanushi.

**Kwa mfano:**

1. *Tafadhali imba wimbo huo tena.* - *Tafadhali usiimbe wimbo huo tena.*
2. *Naomba uketi kwenye kiti hico.* - *Naomba usiketi kwenye kiti hico.*

## 18.7 Majibu

### Zoezi la makundi, ukurasa 147

Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi kwa kurejelea micoro iliyopo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 147.

**Kwa mfano:**

*Mcoro wa kwanza unaonyesha msicana ambaye ni mlemavu lakini anafahamu kutumia tarakilishi. Mcoro wa pili unaoanyesha tarakilishi yenyewe.*

**Majibu ya ufahamu, ukurasa 149**

1. Kuwawezesha watoto kupata ujuzi wa kiteknolojia. Watoto watapata majibu ya maswali yao mengi kutoka kwenye mtandao. Itakuwa rahisi kupata maana za maneno, maelezo na taarifa muhimu kuhusu mada yoyote kutoka kwenye mtandao n.k. (*Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.*)
2. Tarakilishi imecangia katika kuyatunza mazingira kwa kupunguza matumizi ya karatasi nyingi. Kiwango ca masomo kimeimarika kwani wanafunzi wanaweza kujisomea kwa kufanya utafiti wao. Pia, kiwango ca ujuzi na maarifa ca mtu binafsi kimeimarika.
3. Kompyuta
4. Kweli. Kwa sababu mtandao huwaleta pamoja watu wengi katika harakati ya kutafuta habari kuhusu mambo fulani au kuwasiliana. Ni rahisi kuelewa utamaduni wa wanajamii wengine na pia kushirikiana na kutangamana nao kwa kupitia mtandao kwa sababu watu wanaweza kutafuta habari muhimu kwenye mtandao kuhusu lugha, mavazi, vyakula na sherehe zao.
5. Tarakilishi huimarisha kiwango ca ujuzi na maarifa ca mtu binafsi kutokana na mambo mengi anayoyasoma kutoka kwenye mtandao. Wanafunzi wanaomaliza masomo wana mbinu mahususi ambazo zinawawezesha kufanya kazi kwa ukakamavu na kwa kujiamini wapatapo ajira.
6. Manufaa ya tarakilishi/Umuhimu wa tarakilishi
7. Teknolojia imerahisisha shughuli za kielimu, imewezesha mawasiliano kwa njia ya haraka, imeimarisha ucumi na shughuli za kibiashara za nci, imeleta utangamano baina ya wananci na imerahisisha usafiri wa watu na bidhaa. (*Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.)*
8. Kusambaza taarifa na pica cafu kupitia fesibuku hali ambayo huwafedhehesha wazazi na watoto au wafanyakazi na wajiri wao, wahalifu na walanguzi wa dawa za kulevya hutumia mtandao kuuza dawa za kulevya na kusambaza habari za kigaidi, propaganda na vitisho au uhalifu. Watu wengi wamelaghaiwa pesa na wengine kuuawa hasa wanawake kupitia kwa shughuli za mtandaoni.
9. Tarakilishi inawezesha mawasiliano kupitia fesibuku na baruapepe. Mtandao nao umerahisisha kuelewa utamaduni wa wanajamii wengine na pia kushirikiana na kutangamana nao.
10. Madhara na umuhimu wa kutumia:
    a. ***Fesibuku*** imewezesha mawasiliano hivi kwamba mtu anaweza kutuma na kupokea pica, video na pia arafa kwa haraka, mtu anaweza kutangaza bidhaa zake ili kupata wanunuzi na ni njia rahisi ya kuhifadhi na kusambaza

taarifa kwa haraka. Fesibuku ina madhara kama vile: kusambaza taarifa na pica cafu kupitia kwa fesibuku, hali ambayo huwafedhehesha wazazi na watoto au wafanyakazi na wajiri wao. Wahalifu na walanguzi wa dawa za kulevya hutumia mtandao wa fesibuku kuuza dawa za kulevya na kusambaza habari za kigaidi, propaganda na vitisho au uhalifu. Watu wengi wamelaghaiwa pesa na wengine kuuawa hasa wanawake kupitia kwa mtandao.

b. ***Baruapepe*** ni njia ya haraka ya kupata ujumbe na kupokea majibu, huhifadhi wakati na ni nafuu kuliko kuandika barua ya kawaida. Baruapepe inahitaji umeme ili kutumika, haiwezekani iwapo hakuna mtandao na ni sharti wenye kutuma na kupokea wawe na anwani zilizosajiliwa mtandaoni.

c. ***Watisapu*** ni njia ya haraka ya kutuma na kupokea jumbe. Upungufu wake ni kwamba, bila ya simu inayowezesha matumizi yake, mawasiliano hayatatimia na pia ina gharama ya juu kwa kuwa ni sharti kununua bandali za kuwezesha matumizi ya watisapu.

**Zoezi la msamiati, ukurasa 149**

Mwalimu atathmini maelezo ya msamiati ambayo wanafunzi watatoa. Sharti msamiati huo uwe umetumika katika kifungu walicokisoma.

***Kwa mfano:***

1. ***mapendekezo*** - mawazo yanayotolewa kwa watu ili yajadiliwe na kutolewa maoni
2. ***mtandao*** - mfumo wa mawasiliano wa kielektroniki unaopitia katika kompyuta ambao watu huutumia kupata taarifa

**Zoezi la 18.1, ukurasa 149**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi na zihusishe msamiati uliokolezwa rangi.

***Kwa mfano:***

1. *Matumizi ya simu na tarakilishi ni matokeo ya **teknolojia**.*
2. *Mama ameninunulia **tarakilishi** mpya.*
3. *Nilipata habari kuhusu matumizi ya baruapepe kwenye **mtandao**.*
4. ***Mradi** wa kuwapa wanafunzi tarakilishi utaanza mwaka ujao.*
5. *Nina **kamusi** kwenye simu yangu.*
6. *Nilisoma **tamaduni** za watu katika kitabu ca Historia.*
7. *Wanyarwanda **hutangamana** katika shughuli za Umuganda.*

8. *Nilifungua* ***akaunti*** *ya* ***fesibuku*** *jana.*
9. *Kayitesi alinitumia video ya kufurahisha kwenye* ***watisapu****.*
10. *Nitajibu* ***baruapepe*** *ya kaka yangu leo jioni.*

**Zoezi la makundi, ukurasa 150**

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi. Sharti maelezo hayo yajibu maswali yaliyo kitabuni mwao.

**Kwa mfano:**

*1. Tarakilishi ni kifaa ca kielektroni ambaco huhifadhi na kucanganua taarifa zilizoingizwa pamoja na kuongoza mitambo mbalimbali.*

*2. Njia za mawasiliano kupitia kwa tarakilishi ni: fesibuku na baruapepe.*

*3. Watumizi wa tarakilishi huweza kutuma na kupokea jumbe kwa haraka, hutunza mazingira dhidi ya matumizi ya karatasi nyingi na pia huimarisha kiwango cao ca ujuzi na maarifa.*

*4. Tarakilishi ina madhara mengi kwa sababu huweza kusambaza taarifa na pica cafu kupitia kwa fesibuku hali ambayo huwafedhehesha wazazi na watoto au wafanyakazi na waajiri wao. Wahalifu na walanguzi wa dawa za kulevya hutumia mtandao kuuza dawa za kulevya na kusambaza habari za kigaidi, propaganda na vitisho au uhalifu.*

**Zoezi la kusikiliza na kuzungumza, ukurasa 151**

Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi yao kisha awaelekeze kushiriki katika majadiliano kwa kuzingatia maswali yaliyo kwenye vitabu vyao. Mwalimu atathmini hoja ambazo wanafunzi watatoa katika majadiliano yao.

**Zoezi la sarufi, hali ya kuomba, ukurasa 151**

Sentensi katika A ziko katika hali yakinishi ilhali sentensi katika B ziko katika hali kanushi.

**Zoezi la 18.2, ukurasa 152**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe msamiati waliopewa.

***Kwa mfano:***

1. *Tafadhali usitumie* ***mtandao*** *wa intaneti darasani.*
2. *Naomba usiitupe* ***simu ya mkono*** *uliyopewa.*

3. *Tafadhali usisakure kwenye **intaneti** masuala nyeti.*
4. *Tafadhali usiiuze **kompyuta** ya marehemu.*
5. *Tafadhali usitumie pesa za kununua **televisheni**.*
6. *Naomba usiifungue akaunti yangu ya **fesibuku**.*
7. *Tafadhali usinitumie video kwenye **watisapu**.*
8. *Tafadhali usisahau kujibu **baruapepe** ya mwalimu.*

**Zoezi la 18.3, ukurasa 152**

**Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.**

1. Tafadhali usinunue televisheni nyingine.
2. Naomba usinitengenezee simu yangu.
3. Naomba usininunulie bandali za intaneti.
4. Tafadhali mtoto huyo asitumie tarakilishi yangu.
5. Naomba usiniandikie baruapepe kesho asubuhi.

# Somo la 19: Redio na runinga

## Kipindi cha 8: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati

**a) Malengo ya somo**

- Kusoma kwa usahihi kifungu ca habari kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;
- Kutambua msamiati unaohusu matumizi ya redio na runinga;
- Kutambua umuhimu na madhara ya redio na runinga.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Micoro au pica za redio na runinga;
- Redio na runinga halisi;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 153-155;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Somo hili linahusisha kifungu ca habari kuhusu matumizi ya redio na runinga. Mwalimu aandae vifaa vitakavyohitajika kufunzia somo hili kama vilivyobainishwa hapo juu. Mwalimu anaweza kuandaa masimulizi kuhusu vipindi fulani fulani vya redio na pia vya runinga ambayo atawasomea wanafunzi darasani. Masimulizi haya yatamsaidia sana mwalimu katika kuwapa wanafunzi msingi wa kuweza kujadili kuhusu matumizi ya redio na runinga.

Katika kufanikisha somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila zoezi linalohusika.

**d) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake na kuwauliza maswali kuhusu somo lililopita. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu wao. Pia wanafunzi wajibu maswali waliyoulizwa na mwalimu wao. Baadaye, mwalimu acukue fursa hii kuwaomba wanafunzi wasahihishe zoezi walilopewa wakati wa somo lililopita

ili waweze kuendelea na somo jipya. Baada ya haya, mwalimu awacangamshe wanafunzi wake kwa kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu pica na mcoro ulio katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 153. Kwa mfano mwalimu anaweza kuuliza: *Mnaona nini kwenye mcoro na pica hizi?* Mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kuhusu namna ya kujibu maswali waliyoulizwa kwa kuwapa kitangulizi kama vile *"mimi ninaona..."* Kwa mfano: *Mimi ninaona redio.* Katika hatua hii, ni lazima mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kupata ujuzi kuhusu tafakuri tunduizi huku akiwasaidia kuwasiliana kwa lugha rasmi na sahihi.

### 19.1 Kusoma na ufahamu: Kifungu kuhusu matumizi ya redio na runinga

Mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa kimya kifungu ca habari kuhusu matumizi ya redio na runinga huku wakiandika msamiati mpya wanaopatana nao. Hivyo basi, wanafunzi wasome kwa kimya pamoja na kuandika msamiati huo mpya. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wamesoma na kuelewa kama walivyoambiwa, mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu kifungu ca habari kilicopo. Kwa mfano, anaweza kuuliza swali lifuatalo: *Umuhimu wa redio ni upi?* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu swali la mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika kifungu hico. Kwa mfano: *Kupitia kwa redio tunaweza kupata matangazo ya kila aina*.

Baada ya kupata pica ya uelewa wa jumla wa wanafunzi kuhusu kifungu ca habari kinacohusika, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa sauti kifungu hico. Wanafunzi wasome kwa sauti kama walivyoambiwa na mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa kwa lengo la kutambua herufi, silabi na sentensi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kujibu maswali ya kifungu ca habari walicosoma. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote.

Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali hayo huku akitoa maelezo yake kwa kutilia mkazo pale ambapo wanafunzi wanatatizika.

### 19.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu matumizi ya redio na runinga

Mwalimu atoe maelekezo kuhusu namna ya kutafuta maana ya msamiati mpya ulioorodheshwa na wanafunzi wakati wa kusoma kifungu ca habari kilicopo. Mwalimu awaombe wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kujadiliana kuhusu msamiati huo. Wanafunzi wazingatie matumizi ya msamiati huo katika kifungu kilicopo. Wanafunzi wanaweza kujadili msamiati huo huku wakitumia kamusi pale panapohitajika. Mwalimu azunguke darasani huku akiwasaidia wanafunzi na kuwaelekeza pale wanapotatizika.

Hatimaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi kufanya zoezi la 19.1 la msamiati kwa kuwafafanulia kile kinacotakiwa kutimizwa katika zoezi hilo. Mwalimu awaombe wanafunzi kucunguza maana ya maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi walizopewa huku akiwatolea mifano. Wanafunzi wajibu zoezi hilo kama walivyoelekezwa na mwalimu na kulisahihisha mara moja wanapolimaliza.

Isitoshe, ni lazima mwalimu azingatie kwamba wanafunzi wanatakiwa kurejelea matumizi ya msamiati husika katika kifungu ca habari walicokisoma ili kuelewa zaidi.

**Tathmini ya kipindi ca 8**

Mwalimu alenge kutambua ikiwa ujifundishaji umefanywa kwa namna ya kuridhisha. Kwa hivyo, apime uwezo wa wanafunzi kupitia maswali mbalimbali kuhusiana na utambuzi wa matumizi ya redio na runinga, matumizi ya msamiati waliojifunza katika sentensi fupifupi na hata matumizi ya msamiati huo katika maongezi yao nje ya darasa. Mwalimu awazoeshe wanafunzi wake kunyosha mkono kila wakati mwanafunzi anapotaka kuuliza au kujibu swali kwa kuonyesha mienendo ya kuwa na adabu shuleni.

## Kipindi cha 9: Matumizi ya lugha

**a) Malengo ya somo**

- Kujadili vipindi vya redio vyenye mafundisho mema;
- Kujadili vipindi vya runinga vyenye mafundisho mema;
- Kufahamu madhara na faida za redio na runinga.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Micoro au pica za redio na runinga;
- Redio na runinga halisi;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 155-156;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### c) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu matumizi ya lugha kuhusiana na vipindi mbalimbali katika redio na runinga pamoja na mafundisho ambayo wanafunzi huyapata kupitia vipindi hivyo. Mwalimu aandae vifaa atakavyohitaji katika ufundishaji wa somo hili ili wanafunzi wapate uelewa unaofaa. Mwalimu anaweza kuandaa kwa kuandika au kurekodi vipindi kadhaa vya redio na runinga ambavyo anaweza kuwasimulia wanafunzi au kuwawekea wakasikiliza.

Ili kufanikisha somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa amewagawa wanafunzi katika makundi yanayotakiwa kwa kila zoezi husika.

### d) Utaratibu wa somo

### Utangulizi

Mwalimu aanze kipindi hiki kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kuhusiana na somo lililopita kuhusu matumizi ya redio na runinga. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofunzwa katika kipindi kilicotangulia.

### 19.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watano watano kisha wajadiliane kuhusu vipindi kadha wa kadha vya redio pamoja na vya runinga. Wanafunzi waelezane vipindi wanavyopenda, watangazaji wanaowapenda pamoja na sababu zao za kupenda vipindi hivyo na watangazaji hao waliowataja. Pia, wanafunzi wajadili kuhusu madhara na faida za redio na runinga. Mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao. Baada ya muda mfupi wa majadiliano, mwalimu anaweza kuwacagua wanafunzi kadhaa kutoka katika makundi mbalimbali wawasomee wenzao waliyojadili katika makundi yao.

Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kuelewa madhara na faida za redio na runinga. Majadiliano katika makundi yatasaidia kuelewa jambo hili.

Hatimaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kufanya zoezi la 2 ambapo wanahitajika kutafsiri msamiati wa teknolojia ulio katika lugha ya Kiingereza hadi katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano:

| **Kiingereza** | **Kiswahili** |
|---|---|
| • *Mobile phone* | *simu ya mkononi (rununu)* |

- *Sms (short message service)* *arafa*
- *Email* *baruapepe*
- *Laptop* *kipakatalishi*
- *Mouse (computer)* *kipanya (tarakilishi)*

**Tathmini ya kipindi ca 9**

Mwalimu ahitimishe somo hili kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali haya yatamsaidia mwalimu kutambua iwapo wanafunzi wamefahamu matumizi ya redio na runinga pamoja na madhara na faida za vyombo hivi vya habari na mawasiliano.

Mwalimu pia awaulize wanafunzi maswali mepesi ya kubaini iwapo wanafunzi wana uwezo wa kutafsiri msamiati wa lugha ya Kiingereza hadi katika lugha ya Kiswahili.

## Kipindi cha 10: Kusikiliza na kuzungumza

**a) Malengo ya somo**

- Kuigiza utangazaji wa redio;
- Kuigiza utangazaji wa runinga;
- Kufahamu umuhimu wa redio na runinga.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Redio na runinga halisi;
- Wanafunzi wenyewe;
- Watangazaji halisi;
- Micoro au pica za vituo vya utangazaji mbalimbali;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 156;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Mwalimu ahakikishe kuwa amewagawa wanafunzi wake katika makundi ya wanafunzi yanayotakikana. Mwalimu anaweza kupanga mapema safari ya kuwapeleka wanafunzi wake katika kituo kimoja ca redio au runinga ili wajionee wenyewe mambo yanavyofanyika huko. Mwalimu pia anaweza kupanga kuwaalika watangazaji halisi darasani na kuwapa wanafunzi fursa ya

kuwasikiliza moja kwa moja, ana kwa ana. Mwalimu aandae somo kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu utaratibu wa utangazaji katika vituo vya redio na runinga pamoja na madhara na faida za vyombo hivi vya habari.

### d) Utaratibu wa somo

### Utangulizi

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi kilicotangulia. Wanafunzi wajibu maswali waliyoulizwa. Mwalimu atumie vifaa alivyoandaa kutanguliza funzo hili.

### 19.4 Kusikiliza na kuzungumza: Maigizo

Katika sehemu hii, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watano watano kisha awaelekeze jinsi ya kuigiza namna habari au vipindi mbalimbali hutangazwa katika redio na runinga. Mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika.

Baada ya maigizo ya wanafunzi, mwalimu awateue wanafunzi kadhaa kutoka kwa kila kikundi ili waigize namna ya kutangaza habari au vipindi mbalimbali mbele ya wanafunzi wenzao. Mwalimu ahakikishe kuwa anakosoa makosa ya kimatamshi pindi yanapofanyika katika utangazaji wa wanafunzi.

Kupitia kwa maigizo haya, wanafunzi watapata uwezo wa kuwasiliana kwa lugha rasmi na ujasiri wa kuzungumza mbele ya watu. Wanafunzi pia wanaweza kugundua talanta walizo nazo kupitia maigizo haya ya utangazaji wa habari na vipindi mbalimbali.

### Tathmini ya kipindi ca 10

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mepesi yenye kucunguza uwezo wa wanafunzi wa kushiriki katika shughuli za utangazaji wa habari na vipindi mbalimbali vya redio na hata runinga.

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mepesi ya kubaini iwapo wametambua madhara na faida za redio na runinga pamoja na vipindi vilivyo na mafundisho mema. Pia, wanafunzi wahimizwe kuepuka kusikiliza au kutazama vipindi visivyo na mafundisho mema kwao katika umri wao mdogo.

## Kipindi cha 11: Sarufi (Hali ya kuamrisha, tungo yakinishi)

**a) Malengo ya somo**

- Kubaini msamiati wa hali ya kuamrisha;
- Kutumia msamiati wa hali ya kuamrisha katika tungo yakinishi;
- Kutunga sentensi sahihi katika hali ya kuamrisha, tungo yakinishi.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Vifaa vya darasani kama vile: *madaftari, kalamu, rula* n.k.;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu ca Mwanafunzi, ukurasa 156;-157*
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Mwalimu atafute vifaa vitakavyoweza kurahisisha uelewa wa wanafunzi katika somo hili kama vile: *madaftari, kalamu, rula pamoja na combo ca kunasia sauti au breli* na kadhalika. Kupitia kwa vifaa hivyo, mwalimu aandae maswali mbalimbali yatakayowacocea wanafunzi kutambua matumizi ya hali ya kuamrisha katika mawasiliano ya kila siku pamoja na matumizi yake katika sentensi sahihi.

Mwalimu atambue wakati mwafaka wa kuweka hadharani vifaa alivyovileta au alivyowaomba wanafunzi walete darasani. Wanafunzi walio na matatizo mbalimbali katika kuelewa na kufahamu haraka yale wanayofundishwa darasani au wale walio na kiwango ca cini katika ujifunzaji wao wataweza kufaidika kutokana na matumizi ya vifaa mbalimbali katika somo hili. Ikiwa kuna wanafunzi wasio na uwezo wa kuona, ni vyema mwalimu awaombe wao wenyewe kuvigusa vifaa vilivyopo wakivitolea maelezo na wale ambao hawana uwezo wa kusikia wavionyeshe kwa kuvigusa huku wakiandika maelezo yao ubaoni.

Ili kuyatimiza malengo yake katika somo hili, ni vyema mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli ya wanafunzi iliyopendekezwa katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 156.

**d) Utaratibu wa somo**

## Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi ca hapo awali ca sarufi kuhusu hali ya kuomba, tungo yakinishi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa. Wanafunzi waeleze kuhusu msamiati unaotumika katika hali ya kuomba (tungo yakinishi) pamoja na umuhimu wao katika kufanikisha mawasiliano.

## 19.5 Sarufi: Hali ya kuamrisha, tungo yakinishi

Katika hatua hii, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na awaombe wasome sentensi zilizo kitabuni mwao huku wakicunguza matumizi ya msamiati wa kuonyesha hali ya kuamrisha. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua na kuelewa matumizi ya maneno mbalimbali ambayo hutumiwa kwa nia ya kutoa amri fulani katika sentensi walizopewa pamoja na maongezi yao ya kila siku. Wanafunzi wasome sentensi walizopewa kwa makini kisha mwalimu awaelekeze katika kutunga sentensi zao zilizo katika hali ya kuamrisha, tungo yakinishi. Wanafunzi washirikishwe katika kujadili ugunduzi wao.

Kupitia mifano ya sentensi iliyopo, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kutambua jinsi maneno yanavyoweza kutumika ili kuonyesha hali ya kuamrisha.

Ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wamepata ufahamu wa kutosha katika matumizi ya msamiati wa hali ya kuamrisha, mwalimu awaombe wafanye zoezi la 3 ambapo wanatakiwa watunge sentensi sahihi katika hali ya kuamrisha tungo yakinishi.

## Tathmini ya kipindi ca 11

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali yake yacunguze uwezo wa wanafunzi wa kutumia kwa usahihi maneno mbalimbali kwa njia ya kuonyesha hali ya kuamrisha (tungo yakinishi) katika sentensi sahihi na pia katika maongezi yao ya kila siku.

**Maelezo muhimu kwa mwalimu**

- Kitendo cha kutoa maagizo ya kufanyika kwa tendo fulani huitwa ***kuamrisha***.

***Kwa mfano:***

1. ***Nenda ukalale!***

Katika sentensi hii, kuna agizo la mzungumziwa kuamrishwa aende akalale.

2. ***Njoo hapa!***

Katika sentensi hii, kuna agizo la mzungumziwa kuamrishwa aende aliko mzungumzaji.

## 19.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu awasaidie wanafunzi wenye kiwango ca cini katika ujifunzaji wao kwa kuwaomba wageuze sentensi zifuatazo kutoka hali ya kuomba, tungo yakinishi hadi hali ya kuamrisha, tungo yakinishi

***Kwa mfano:***

***Hali ya kuomba (tungo yakinishi):*** *Tafadhali safisha cumba cangu.*
***Hali ya kuamrisha (tungo yakinishi):*** *Safisha cumba cangu!*

1. Naomba uwashe redio yenu.
2. Tafadhali mpikie nyanya cai.
3. Tafadhali nipe maji ya kunywa.
4. Naomba univue viatu vyangu.
5. Tafadhali kimbia upesi umsaidie mama kazi.

### Majibu ya zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

1. Washa redio yenu!
2. Mpikie nyanya cai!
3. Nipe maji ya kunywa!
4. Nivue viatu vyangu!
5. Kimbia upesi umsaidie mama kazi!

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango ca juu ca uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge sentensi kumi sahihi katika hali ya kuamrisha, tungo yakinishi.

**Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi na ziwe katika hali ya kuamrisha, tungo yakinishi.

***Kwa mfano:***

1. *Nenda sokoni haraka!*
2. *Njoo hapa sasa hivi!*

# 19.7 Majibu

**Zoezi la makundi, ukurasa 153**

Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi kwa kurejelea mcoro uliopo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 153.

**Kwa mfano:**

*Mcoro wa kwanza unaonyesha watu wa familia wakitazama runinga sebuleni. Micoro mingine inaonyesha aina mbalimbali za runinga na redio.*

**Maswali ya ufahamu, ukurasa 154**

1. Kupitia redio na runinga binadamu huweza kupata habari kuhusu yanayoendelea katika maeneo mbalimbali, kuburudishwa kupitia kwa muziki, kujifundisha lugha na fasihi, kusambaza utamaduni, n.k. (*Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.*)
2. Kupitia kwa vipindi vyenye nyimbo na ngoma mbalimbali, mashairi na vipindi vya kielimu kwa wanafunzi wa shule na vyuo.
3. Mtangazaji, produsa, matangazo, mtazamaji, msikilizaji, n.k. (*Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.*)
4. Hizi ni habari kutoka nje ya nci husika.
5. Matangazo ya kibiashara, matangazo ya micezo, taarifa za habari, matangazo ya tanzia, n.k. (*Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.*)
6. Yeye hupitisha ujumbe kwa sauti na kwa kuonekana hadi kwa msikilizaji na mtazamaji.
7. Msikilizaji ni mtu anayetega sikio lake ili kusikiliza ujumbe kupitia kwa kituo ca redio. Mtazamaji husikiliza na kutazama pica zinazohusiana na habari zinazotangazwa.
8. *Redio Maria Rwanda, Redio Flash, Redio Isango Star,* n.k. (*Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.*)

9. Habari potovu zinaweza kupeperushwa na kuwaathiri wananci, watoto huweza kutazama filamu cafu kwenye runinga na hivyo kuathiri maadili yao, uigaji wa mavazi na mitindo ya watu maarufu jambo ambalo huathiri maadili ya kijamii, wanafunzi kupoteza muda mwingi wakitazama runinga jambo ambalo huathiri masomo yao pamoja na ufanyaji wa kazi.
10. Redio hupitisha ujumbe kwa kutumia sauti pekee ilhali runinga hupitisha ujumbe kwa sauti pamoja na pica.

**Zoezi la msamiati, ukurasa 155**

Mwalimu atathmini maelezo yatakayotolewa na wanafunzi kuhusu msamiati waliopatana nao katika kifungu ca habari walicosoma.

***Kwa mfano:***

1. ***runinga -*** combo kinaconasa pica, sauti na maandishi kutoka kwenye kituo kimoja ca mawasiliano na kuziwasilisha kwa mtangazaji katika sehemu nyingine mbalimbali
2. ***matangazo -*** habari zinazotolewa kwa watu wengi kwa njia ya redio au televisheni

**Zoezi la 19.1A, ukurasa 155**

Mwalimu atathmini maelezo yatakayotolewa na wanafunzi kuhusu msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi walizopewa katika vitabu vyao.

***Kwa mfano:***

1. ***runinga*** - combo kinaconasa pica, sauti na maandishi kutoka kwenye kituo kimoja ca mawasiliano na kuziwasilisha kwa mtangazaji katika sehemu nyingine mbalimbali
2. ***habari*** - ujumbe unaopitishwa kwa njia ya sauti au pica
3. ***hewani*** - angani
4. ***mtangazaji*** - mtu ambaye hupitisha ujumbe kwa sauti na kwa kuonekana hadi kwa msikilizaji na mtazamaji
5. ***mawimbi*** - mapigo ya sauti yanayosafiri hewani
6. ***matangazo*** - habari zinazotolewa kwa watu wengi kwa njia ya redio au televisheni
7. ***watazamaji*** - watu ambao husikiliza na kutazama pica zinazohusiana na habari zinazotangazwa
8. ***mkuu wa redio*** - mtu ambaye jukumu lake ni kuhakikisha kuwa kuna mpangilio, sera na utaratibu unaofaa wa kuandaa na kurusha matangazo hewani
9. ***vipindi*** - jambo fulani ambalo hutendeka kwa wakati maalum

### Zoezi la 1B, ukurasa 155

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe msamiati walioueleza katika zoezi la 1A hapo juu.

***Kwa mfano:***

1. *Mimi hupenda kutazama **runinga** jioni.*
2. *Mwalimu alitushauri kusikiliza **habari** za micezo kwenye kituo ca redio.*
3. *Matangazo ya mcezo wa kandanda yatapeperushwa **hewani** leo jioni.*
4. ***Mtangazaji** wa leo ni mwanamume.*
5. *Baba alilazimika kusikiliza kituo ca redio ambaco **mawimbi** yake ya utangazaji yalisikika vyema.*
6. ***Matangazo** ya kisiasa yalikamilika mapema asubuhi.*
7. ***Watazamaji** wa taarifa za habari walikasirishwa na kisa ca mbwa kugongwa na gari.*
8. ***Mkuu wa redio** amemkumbusha mtangazaji kujitambulisha kila wakati.*
9. *Kuna **vipindi** vya kufundishia lugha na utamaduni katika runinga.*

### Zoezi la matumizi ya lugha, ukurasa 155

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi yanayotakikana kisha awaelekeze katika namna ya kuendeleza majadiliano yao kuhusiana na matumizi ya redio na runinga pamoja na vipindi na watangazaji wanaowapenda. Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi.

### Zoezi la 19.2, ukurasa 156

1. Website – wavuti/tovuti
2. Internet – intaneti
3. Computer – tarakilishi/kompyuta
4. WhatsApp – watisapu
5. Facebook – fesibuku
6. Mouse – kipanya
7. Television – televisheni/runinga

### Zoezi la kusikiliza na kuzungumza, ukurasa 156

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi yanayotakiwa kisha awaelekeze katika kuigiza namna ya kutangaza habari au vipindi mbalimbali katika runinga na redio. Mwalimu atathmini maigizo ya wanafunzi. Lugha ya Kiswahili sanifu itumiwe.

**Zoezi la 19.3, ukurasa wa 157**

Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi. Sharti zihusishe maneno waliyopewa katika hali yakinishi kwa njia ya kuamrisha. Kwa mfano:

1. Mwambie Neza aniandikie baruapepe!
2. Njoo utengeneze tarakilishi yangu!
3. Nataka ujibu simu yangu!
4. Nitatuma arafa nikiamka!
5. Mwambie atufundishe teknolojia!
6. Ninataka kusikiliza redio!
7. Tazama runinga hii!
8. Utasoma fesibuku kesho!
9. Fungua watisapu na utume video!
10. Nitanunua gazeti moja tu!

# Somo la 20: Barua kwa mhariri

## Kipindi cha 12: Kusoma ufahamu na kujifunza msamiati

### a) Malengo ya somo

- Kusoma kwa usahihi kifungu ca habari kwa utambuzi wa herufi, silabi, maneno na sentensi;
- Kufahamu kuhusu uandishi wa barua kwa mhariri;
- Kutambua maana ya msamiati mpya kutokana na kifungu husika.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Magazeti yenye barua kwa mhariri mbalimbali;
- Mifano ya barua kwa mhariri zilizoandikwa;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 158-160;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia, n.k.).

### c) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu uandishi wa barua kwa mhariri. Kifungu kilico katika *Kitabu ca Mwanafunzi* ukurasa 158-159 kinatoa maelezo kuhusu barua kwa mhariri kwa kurejelea barua hizi huandikwa na akina nani na huandikwa kwa sababu gani. Sifa za barua kwa mhariri zimeangaziwa katika kifungu hiki. Mwalimu aandae mapema vifaa vitakavyomsaidia katika ufundishaji wa somo hili kama vilivyoorodheshwa hapo juu.

### d) Utaratibu wa somo

#### Utangulizi

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu atangulize somo hili kuhusu uandishi wa barua kwa mhariri kwa kuwauliza wanafunzi maswali mepesi ya kuwacangamsha. Maswali kama vile: *Je, umewahi kusoma barua kwa mhariri katika gazeti? Je, unamfahamu mtu ambaye amewahi kuandika barua kwa mhariri katika gazeti?* n.k. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika majadiliano haya. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu.

Baadaye, mwalimu aendelee na somo kwa kuwaomba wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu watazame mcoro na pica zilizo kwenye *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 158. Mwalimu awaulize wanafunzi maswali kuhusu mcoro na pica hizo. Kwa mfano: *Mnaona nini kwenye mcoro na pica hizi?* Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kujibu maswali waliyoulizwa kwa kuwapa kitangulizi kama vile *"Mimi ninaona..."* Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu. Kwa mfano, "*Mimi ninaona gazeti*. Katika sehemu hii, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi wake ili wapate ujuzi kuhusu tafakuri tunduizi, ubunifu na ugunduzi kwa kuwaonyesha micoro husika huku wanafunzi nao wakifikiri na kugundua kile kinacoendelea au kinacoonekana katika micoro hiyo.

## 20.1 Kusoma na ufahamu: Kifungu kuhusu barua kwa mhariri

Mwalimu aombe wanafunzi katika makundi ya watatu watatu wasome kwa kimya kifungu ca habari kuhusu uandishi wa barua kwa mhariri kilico katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 158-159. Wanafunzi wasome kwa kimya kifungu hico huku wakitambua na kuandika msamiati mpya wanaopatana nao. Hatimaye, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu kifungu walicosoma ili kuhakikisha kuwa wamekisoma na kukielewa. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuwauliza: *Barua kwa mhariri huhusu nini?* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma kutoka kwenye kifungu hico. Kwa mfano wanafunzi wanaweza kujibu: *Barua kwa mhariri huhusisha masuala yanayoathiri watu katika kiwango ca kitaifa au hata kimataifa*. Baada ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wamesoma kwa kimya kifungu kilicopo na kukielewa, mwalimu awaombe wanafunzi wasome tena kwa sauti kifungu hico kwa kuhakikisha kuwa wanatamka maneno kwa namna inayofaa. Mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa.

Baadaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kujibu maswali ya ufahamu waliyopewa. Mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika.

Hatimaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali hayo ya ufahamu huku akitoa maelezo pale ambapo wanafunzi wanatatizika. Mwalimu awasaidie wanafunzi wenye matatizo ya kuelewa msamiati uliotumika katika kifungu hico.

## 20.2 Ujifunzaji wa msamiati kuhusu barua kwa mhariri

Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kuwaomba wajadili maana za msamiati mpya ambao walipatana nao katika

usomaji wa kifungu walicopewa. Wanafunzi waeleze maana ya msamiati husika kwa kuzingatia jinsi ulivyotumiwa katika kifungu ca habari walicokisoma. Mwalimu awaombe wanafunzi watumie kamusi ya Kiswahili pale wanapoihitaji. Mwalimu azunguke darasani akiwaelekeza wanafunzi wanaopata taabu katika kuitumia kamusi au kufafanua maana ya msamiati husika.

Baadaye, mwalimu aombe wanafunzi kucunguza msamiati uliopigiwa mstari katika sentensi walizopewa katika zoezi la 20.1 kisha watunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo. Ni vyema mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia na kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika. Baada ya wanafunzi hawa kukamilisha zoezi walilolipewa, mwalimu awaombe wanafunzi kusahihisha kwa pamoja mazoezi hayo ya msamiati.

Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wameelewa msamiati uliokuwa mpya kwao, mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi wataje msamiati ambao hawakuelewa maana yake ili ujadiliwe tena kwa pamoja darasani kulingana na matumizi yake katika kifungu walicosoma. Ni vyema mwalimu azingatie kwamba utunzi wa sentensi za wanafunzi ndio utakaomfahamisha iwapo wanafunzi wamepata ujuzi unaotakikana katika tafakuri tunduizi, suluhisho kwa matatizo na mawasiliano kwa lugha rasmi na sahihi.

**Tathmini ya kipindi ca 12**

Mwalimu ahitimishe funzo hili kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali hayo yaegemee hasa katika kucunguza iwapo wanafunzi wanaweza kutaja sifa za barua kwa mhariri, namna ya kuandika barua kwa mhariri na masuala ambayo watu huweza kuyaandikia barua kwa mhariri pamoja na kutumia msamiati mpya waliojifunza katika maongezi yao hata nje ya darasa.

## Kipindi cha 13: Matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza

### a) Malengo ya somo

- Kujadili kuhusu uandishi wa barua kwa mhariri;
- Kujadili kuhusu mfano wa barua kwa mhariri waliyowahi kusoma;
- Kuandika barua kwa mhariri.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Magazeti yenye barua kwa mhariri mbalimbali;
- Mifano ya barua kwa mhariri zilizoandikwa;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 160-161;
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**c) Maandalizi ya somo**

Somo hili linahusu matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza kwa kurejelea uandishi wa barua kwa mhariri. Mwalimu aandae mifano ya barua kwa mhariri zilizoshughulikia masuala mbalimbali kwa ajili ya kufundishia somo hili. Mwalimu anaweza kuleta darasani magazeti mbalimbali yenye barua kadhaa kwa mhariri. Ikiwezekana zaidi, mwalimu anaweza kumwalika mhariri mmoja wa gazeti lolote kuja kuwazungumzia wanafunzi kuhusiana na uandishi wa barua kwa mhariri. Ili kufanikisha somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa amewagawa wanafunzi katika makundi yanayotakikana kwa kila zoezi husika.

**d) Utaratibu wa somo**

**Utangulizi**

Mwalimu aanze kipindi hiki kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kuhusiana na somo lililopita. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofunzwa katika kipindi ca hapo awali.

**20.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano**

Mwalimu aombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya watatu watatu kisha wajadili kuhusu barua kwa mhariri ambayo wamewahi kusoma kwa kuwaeleza wenzao:

1. *Barua hiyo ilikuwa imecapishwa katika gazeti gani?*
2. *Barua hiyo ilikuwa imeandikwa na nani?*
3. *Barua hiyo ilikuwa inahusu nini?*
4. *Walijifunza nini kutokana na barua hiyo?*

Mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao. Baada ya muda mfupi wa majadiliano mwalimu anaweza kuwacagua wanafunzi kadhaa kutoka katika makundi mbalimbali waeleze

kuhusu: *barua kwa mhariri ambazo wamewahi kusoma, barua hizo ziliandikwa na nani na zilikuwa zinahusu nini* mbele ya wanafunzi wengine na kuwaomba wanafunzi waelezane ugunduzi wao. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kuelewa namna ya kuandika barua kwa mhariri.

Majadiliano katika makundi yatasaidia kuelewa somo hili. Wanafunzi waelekezwe katika kuelewa utaratibu wa kuandika barua kwa mhariri.

Mwalimu awahimize wanafunzi wafanye mazoezi zaidi kuhusu namna ya kuandika barua kwa mhariri katika makundi yao. Baada ya kupata uzoefu, mwanafunzi anaweza kuandika barua kwa mhariri kwa kujitegemea.

## 20.4 Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano

Katika sehemu hii, mwalimu awaelekeze wanafunzi, katika makundi ya wanafunzi watano watano, wafanye zoezi la kuandika barua kwa mhariri kuhusu mada yoyote watakayocagua. Mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi wanaopata matatizo katika makundi yao. Baada ya kukamilisha zoezi hili la kuandika barua kwa mhariri, mwalimu ateue mwanafunzi mmoja mmoja kutoka katika kila kikundi ili awasomee wenzake barua kwa mhariri waliyoandika. Sharti waeleze:

1. Barua inahusu nini?
2. *Barua imeandikwa na nani na kwa lengo gani?*
3. Je, b*arua imefuata mtindo wa kuandika barua kwa mhariri?*

Baadaye, wanafunzi wafanye zoezi la kuandika barua kwa mhariri kwa kucagua mada yoyote kwa kujitegemea.

## Tathmini ya kipindi ca 13

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali haya yatamsaidia mwalimu kutambua iwapo wanafunzi wanaweza kutaja mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa barua kwa mhariri.

Maswali yabainishe iwapo wanafunzi wanaweza kuandika barua kwa mhariri kwa kuzingatia utaratibu unaofaa na kwa kujitegemea.

## Kipindi cha 14: Sarufi (Hali ya kuamrisha, tungo kanushi)

### a) Malengo ya somo

- Kubaini msamiati wa hali ya kuamrisha;
- Kutumia msamiati wa hali ya kuamrisha katika tungo kanushi;
- Kutunga sentensi sahihi katika hali ya kuamrisha, tungo kanushi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Vifaa vya darasani kama vile: *madaftari, kalamu, rula* n.k.;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu ca Mwanafunzi,* ukurasa 161-162*;*
- Combo ca kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### c) Maandalizi ya somo

Mwalimu atafute vifaa vitakavyoweza kurahisisha uelewa wa wanafunzi katika somo hili kama vile: *madaftari, kalamu, rula pamoja na combo ca kunasia sauti au breli* na kadhalika. Kupitia kwa vifaa hivyo, mwalimu aandae maswali mbalimbali yatakayowacocea wanafunzi kutambua matumizi ya hali ya kuamrisha katika mawasiliano ya kila siku pamoja na matumizi yake katika sentensi sahihi.

Mwalimu atambue wakati mwafaka wa kuweka hadharani vifaa alivyovileta au alivyowaomba wanafunzi walete darasani. Wanafunzi walio na matatizo mbalimbali katika kuelewa na kufahamu haraka yale wanayofundishwa darasani au wale walio na kiwango ca cini katika ujifunzaji wao wataweza kufaidika kutokana na matumizi ya vifaa mbalimbali katika somo hili. Ikiwa kuna wanafunzi wasio na uwezo wa kuona, ni vyema mwalimu awaombe wao wenyewe kuvigusa vifaa vilivyopo wakivitolea maelezo na wale ambao hawana uwezo wa kusikia wavionyeshe kwa kuvigusa huku wakiandika maelezo yao ubaoni.

Ili kuyatimiza malengo yake katika somo hili, ni vyema mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli ya wanafunzi iliyopendekezwa katika Kitabu ca Mwanafunzi.

### d) Utaratibu wa somo

## Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi ca hapo awali ca sarufi kuhusu hali ya kuamrisha, tungo yakinishi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa. Wanafunzi waeleze kuhusu maneno yanayotumika katika hali ya kuamrisha (tungo yakinishi) pamoja na madhara yake wakati mwingine katika mawasiliano.

## 20.5 Sarufi: Hali ya kuamrisha, tungo kanushi

Katika hatua hii, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya watatu watatu na awaombe wasome sentensi zilizo kitabuni mwao huku wakicunguza matumizi ya maneno ya kuonyesha hali ya kuamrisha. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kutambua na kuelewa matumizi ya maneno mbalimbali ambayo hutumiwa kwa nia ya kutoa amri fulani katika sentensi walizopewa pamoja na maongezi yao ya kila siku. Wanafunzi wasome sentensi walizopewa kwa makini kisha mwalimu awaelekeze katika kutunga sentensi zao zilizo katika hali ya kuamrisha tungo yakinishi. Wanafunzi washirikishwe katika kujadili ugunduzi wao.

Kupitia mifano ya sentensi iliyopo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua jinsi maneno yanavyoweza kutumika ili kuonyesha hali ya kuamrisha.

Baada ya haya, mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kukanusha sentensi walizopewa. Wanafunzi waelekezwe kufahamu kuwa katika tungo kanushi, sentensi zilizotumia nafsi mbalimbali za Kiswahili hubadilika na kutumia kikanushi *'-si-'* ili kuashiria ukanushi wake. Mwalimu awatumie wanafunzi wenyewe kwa wenyewe kudhihirisha hali hii ya kuamrisha katika tungo kanushi. Mwanafunzi mmoja anaweza kuamrisha mwanafunzi mwingine afanye kitendo fulani na mwanafunzi mwingine naye aamrishe kitendo hico kisifanyike.

***Kwa mfano:***

- *Nenda ukalale!*
- *Usiende kulala!*

Ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wamepata ufahamu wa kutosha katika matumizi ya maneno ya kuamrisha katika tungo kanushi, mwalimu awaombe wafanye zoezi la 2 ambapo wanatakiwa wakanushe sentensi walizopewa katika hali ya kuamrisha.

### Tathmini ya kipindi ca 14

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali yake yacunguze uwezo wa wanafunzi wa kutumia kwa usahihi maneno mbalimbali kwa njia ya kuonyesha hali ya kuamrisha (tungo kanushi) katika sentensi sahihi na pia katika maongezi yao ya kila siku.

**Maelezo muhimu kwa mwalimu**

Barua ambayo huandikwa na kutumwa kwa mhariri wa gazeti fulani kuhusu suala lolote linaloathiri jamii na baada ya utathmini kuchapishwa kwenye gazeti huitwa ***barua kwa mhariri***.

Barua ya aina hii:

- Hutaja jina la mhariri wa gazeti husika.
- Huwa fupi na yenye ujumbe mahususi.
- Huangazia masuala muhimu sana katika jamii.
- Hutumia lugha sanifu na rahisi kueleweka na wasomaji wote.

### 20.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu awasaidie wanafunzi wenye kiwango ca cini katika ujifunzaji wao kwa kuwaomba wageuze sentensi zifuatazo kutoka hali ya kuamrisha tungo yakinishi hadi hali ya kuamrisha tungo kanushi.

***Kwa mfano:***

***Hali ya kuamrisha (tungo yakinishi):*** *Fagia cumba cenu!*
***Hali ya kuamrisha (tungo kanushi):*** *Usifagie cumba cenu!*

1. Washa tarakilishi yako!
2. Pika cakula cako pekee!
3. Nipe sabuni ya kufulia nguo!
4. Amka uende shuleni!
5. Tembea upesi!

### Majibu ya zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

1. Usiwashe tarakilishi yako!
2. Usipike cakula cako pekee!
3. Usinipe sabuni ya kufulia nguo!

4. Usiamke kwenda shuleni!
5. Usitembee upesi!

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango ca juu ca uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge sentensi kumi sahihi katika hali ya kuamrisha, tungo yakinishi na tungo kanushi.

### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi na ziwe katika hali ya kuamrisha, tungo yakinishi na tungo kanushi.

***Kwa mfano:***

1. *Nenda dukani sasa hivi! – Usiende dukani sasa hivi!*
2. *Njoo hapa karibu na mimi! – Usije hapa karibu na mimi!*

## 20.7 Majibu

### Zoezi la makundi, ukurasa 158

Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi kwa kurejelea mcoro uliopo katika *Kitabu ca Mwanafunzi*, ukurasa 158.

**Kwa mfano:**

Mcoro wa kwanza unaonyesha mzee anayesoma gazeti (huenda anasoma barua kwa mhariri). Micoro mingine inaonyesha aina mbalimbali za magazeti yanayopatikana ncini Rwanda.

### Maswali ya ufahamu, ukurasa 159

1. Barua kwa mhariri huwa na:
    - Mada ambayo huhusu masuala yanayofahamika na yanowaathiri watu pakubwa;
    - Jina la mhariri;
    - Mtindo wa barua rasmi.
2. Mutoni K.
3. BARUA KWA MHARIRI KUTOA PONGEZI KWA KUCAPISHA MAONI YA WASOMAJI WA GAZETI.
4. Mwandishi anaeleza madhara ya utumiaji wa dawa za kulevya na anadai kuwa dawa za kulevya husababisha vijana kuvurugika kiakili, wasicana kunajisiwa na wengine kuambukizwa magonjwa hatari.

5. Kwa sababu kitengo ca barua kwa mhariri hutoa maoni na hisia za wasomaji wa gazeti husika na kuhusu masuala mbalimbali.
6. *Rwanda Times, The Rwanda Focus, Umuseke* n.k. (*Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.*)
7. Dawa za kulevya huharibu afya ya watumiaji, husababisha vifo vya watumiaji, vijana wa kike hujipata wamenajisiwa kwa sababu ya kutojielewa na kutofahamu lolote baada ya kutumia dawa za kulevya, kupata mimba zisizotarajiwa na kupata magonjwa ya zinaa.
8. Kwa kujihusisha na shughuli za kujiendeleza kimaisha kama vile: biashara na masomo. (*Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.*)

**Zoezi la msamiati, ukurasa wa 160**

Mwalimu atathmini maelezo ya msamiati ambayo wanafunzi watatoa. Sharti msamiati huo uwe waliopatana nao katika kifungu walicokisoma.

***Kwa mfano:***

***gazeti*** - mkusanyiko wa karatasi zilizocapwa ndani mwake kukiwa na habari, makala na matangazo

**Zoezi la 20.1, ukurasa 160**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe msamiati ulioelezwa katika zoezi la msamiati hapo juu.

***Kwa mfano:***

1. *Kuna **magazeti** mengi kwenye maktaba ya shule yetu.*
2. *Nitamwandikia mhariri **barua** wiki ijayo.*
3. *Nilikutana na **wasomaji** wengi wa gazeti la Rwanda Times.*
4. *Kuna **habari** kuhusu misitu yetu kwenye gazeti hili.*
5. *Gazeti la kesho **litacapisha masuala** kuhusu umuhimu wa elimu.*
6. ***Mada** ya barua kwa mhariri itahusu magonjwa ya zinaa.*
7. *Nitakuwa **mhariri** baada ya masomo yangu.*
8. *Barua rasmi hufananishwa na **barua kwa mhariri**.*
9. ***Dawa za kulevya** ni hatari kwa afya yetu.*
10. ***Mustakabali** wa elimu humu ncini ni tofauti sana.*

**Zoezi la kuandika, ukurasa 160**

Mwalimu atathmini barua ambazo wanafunzi wataandika. Sharti ziwe na muundo halisi wa barua kwa mhariri na ziwe sahihi kisarufi.

***Kwa mfano:***

*Kwa mhariri,*

*Heko kwa juhudi zako za kuipa lugha ya Kiswahili nafasi katika gazeti lako. Kupitia juhudi zako za kucapisha mashairi na nyimbo za Kiswahili kwenye gazeti, nci yetu imeona umuhimu wa kufundisha Kiswahili shuleni na hata katika vyuo. Kuanzia mwaka uliopita, Kiswahili kinafundishwa kama somo mojawapo ya masomo mengi katika mtaala wetu.*

*Kutokana na somo la Kiswahili, watu wengi wamepata ajira kama walimu wa Kiswahili na wengine kuwa watafsiri. Kiswahili ni lugha nzuri sana na inawaleta pamoja watu kutoka mataifa mbalimbali katika kanda ya Afrika Mashariki na Kati. Tumeshuhudia mikutano mingi sana na makongamano ambayo huendeshwa kwa lugha ya Kiswahili. Mbali na hayo, tunapata burudani kutokana na nyimbo za Kiswahili. Lica ya nyimbo hizi kutupa burudani, hutuelimisha kwa mawaidha ambayo huwa ndiyo maudhui katika nyimbo hizi. Kuna nyimbo ambazo hutoa historia ya Waswahili. Nyimbo nyingine hutupatia asili na hali za kimaisha za Waswahili na Waafrika kwa ujumla. Ama kweli, Kiswahili kitukuzwe!*

*Julia Ndiza*

**Zoezi la 20.2, ukurasa 162**

1. Usikimbie dukani kununua sukari!
2. Usinipe hiyo redio ya Kamana!
3. Usije hapa!
4. Usile cakula hico haraka!
5. Usifagie nyumba hii yote!
6. Usimpeleke mgonjwa huyu hospitalini!
7. Usiendeshe gari hilo polepole!
8. Usitembee upesi!

**Zoezi la 20.3, ukurasa wa 162**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe vitenzi walivyopewa katika hali kanushi ya kuamrisha.

***Kwa mfano:***

1. *Usilie ilhali wewe ndiwe mwenye makosa!*
2. *Mwambie Femina asicague matunda yaliyooza!*
3. *Usiandike ukutani kwa kutumia kaa!*
4. *Usitoroke kwa kuwa nimekuona!*
5. *Mtoto mkorofi asimdanganye mwalimu!*

**Majibu ya tathmini ya mada ya 5**

**Zoezi la 1, ukurasa 163**

1. Redio
2. Kipakatalishi
3. Baruapepe
4. Intaneti
5. Watisapu
6. Gazeti
7. Mhariri
8. Mtangazaji

**Zoezi la 2, ukurasa wa 163**

Mwalimu atathmini usahihi wa majibu ya wanafunzi.

1. Madhara ya:
   a. **Redio:** huweza kutangaza habari potovu na ikisikilizwa kwa sauti ya juu kwa muda mrefu, huweza kudhuru masikio ya msikilizaji.
   b. **Runinga:** baadhi ya filamu zinazoonyeshwa huigwa na huenda zikawa za kuwapotosha watu kimaadili hasa vijana.
2. Faida na umuhimu wa:
   a. **Tarakilishi:** hurahisisha mawasiliano kupitia kwa fesibuku na baruapepe na pia huwezesha utafiti kwenye mtandao wa intaneti. Madhara yake ni kuwa, watu huweza kutumia tarakilishi ili kupata habari au video potovu kwenye mtandao zinazoweza kudhuru maadili ya wanajamii.
   b. **Simu ya mkono:** huwezesha upokeaji na upigaji wa simu kwa haraka ili kuwasiliana, hurahisisha kutuma na kupokea pica, video na muziki kupitia kwa mtandao wa watisapu. Madhara yake ni kwamba: huwa ni ghali na huhitaji bandali na caji ili kutumia.
3. i) redio ii) tarakilishi
   iii) gazeti iv) simu ya mkono

**Zoezi la 3, ukurasa 164**

a) Tafadhali msisome taarifa ya habari.
b) Tafadhali msiace siasa mbaya.
c) Tafadhali tusimwombe Mungu wetu.
d) Tafadhali msilinde wanyamapori wetu.
e) Tafadhali tusiishi vyema na majirani.

**Zoezi la 4, ukurasa 164**

Mwalimu atathmini usahihi wa majibu ya wanafunzi.

***Kwa mfano:***

1. Faida za arafa ni kuwa: ujumbe hutumwa na kupokelewa kwa haraka, ujumbe hujibiwa kwa haraka, hurahisisha mawasiliano kwa sababu ya matumizi ya ufupisho wa ujumbe hivyo basi kuhifadhi wakati.
2. Upungufu wa arafa: hutumika tu na watu ambao wana uwezo wa kusoma, ni ghali kwa sababu inahitaji hela ili kutuma ujumbe na majibu huenda yakacelewa iwapo simu ya mpokeaji wa habari itakuwa imezima kwa sababu ya kukosa caji.

**Zoezi la 5, ukurasa 164**

1. Tafadhali zima televisheni.
2. Tafadhali watumie baruapepe.
3. Tafadhali washa redio kunaponyesha.
4. Tafadhali hifadhi arafa niliyokutumia kwenye simu hiyo.

**Zoezi la 6, ukurasa 164**

a. Tafadhali kateni miti ovyo.
b. Tafadhali zuieni ugonjwa wa Ukimwi.
c Tafadhali mkiceza hamtakuwa wagonjwa.
d. Tafadhali tupelekeni tulikotoka.
e. Tafadhali aniandikie barua akifika nyumbani.

## MAREJELEO


BAKITA (2015); *Kamusi Kuu ya Kiswahili;* Longhorn Kenya Ltd; Nairobi, Kenya.

Mbaabu I. (1992); *Sarufi ya Kiswahili*; Longman; Nairobi, Kenya.

Mdee J.S. , Njogu K., na Shafi A. (2011) *Kamusi ya Kiswahili ya Karne ya 21*; Longhorn Kenya Ltd; Nairobi, Kenya.

Ntawiyanga S., Sanja L. na Kinya J. M. (2015); *Kiswahili kwa Shule za Rwanda*, Kidato cha 1; Longhorn Kenya Ltd; Nairobi, Kenya.

Ntawiyanga S. na Kinya J. M. (2015); *Kiswahili kwa Shule za Rwanda*, Kidato cha 2; Longhorn Kenya Ltd; Nairobi, Kenya.

TUKI (2009); *Stadi za Lugha ya Kiswahili*; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

Waihiga G. na Wamitila K. W. (2013); *Chemchemi za Kiswahili*, kidato cha 3; Longhorn Kenya Ltd; Nairobi, Kenya.

Waihiga G. na Wamitila K. W. (2013); *Chemchemi za Kiswahili*, kidato cha 2; Longhorn Kenya Ltd; Nairobi, Kenya.

Waihiga G. na Kagwa F. M. (2003); *Darubini ya Kiswahili*; Phoenix Publishers; Nairobi, Kenya.